https://www.path-2-happiness.com/sw

سواحيلي

Njia yenye kufikisha kwenye furaha

Dr. A. S. Bahammam

Islam kingdom
Chapa ya kwanza 1435 - 2014

Njia yenye kufikisha kwenye furaha
Dr. A. S. Bahammam

https://www.path-2-happiness.com/sw

الطريق إلى السعادة
The Path to Happiness

happiness.com -٢ -www.path

Njia yenye kufikisha kwenye furaha

Fikra zenye kukupeleka kwenye njia iliyonyooka…njia ya furaha

Dr. A. S. BAHAMMAM

٢٠١٤- ١٤٣٥ Chapa ya kwanza

بسم الله الرحمن الرحيم

https://www.path-2-happiness.com/sw

الطريق إلى السعادة

The Path to Happiness

www.path-2-happiness.com

Utangulizi

Kuhimidiwa ni kwa Mola wa Ulimwengu kisha swala na salamu ni kwa Mtume wetu Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) pamoja na familia na sahabu zake. Ama baada ya hayo: Nilikuwa natafuta kitabu kinachoelezea Uislamu kwa njia ya kisasa kinacho afikiana na hali zetu za sasa, kwa njia nyepesi yenye kunufaisha Waislamu na wasiokuwa Waislamu. Kitabu chenye kutegemea misingi wala hakipunguzwi na mambo ya kileo, kitabu kinachotoa taarifa ya Uislamu kama ni safari ya fikra, mantiki, ustaarabu na ya kisomi kufikia kwenye furaha, safari isiyokuwa na kasoro kutoka katika vyanzo vyake vya asili wala kisicho mbali na maneno ya wanazuoni wa Magharibi na Mashariki waliokuwa mashuhuri kuhusu Uislamu. Pamoja na kuwa vilivyopo vina mengi na kheri nyingi ndani yake, na mimi nimejifunza mengi ndani yake, isipokuwa nilipendezwa kukusanya yote yaliyotangulia; ndio haya yaliyomo kwenye kitabu hiki kilicho mbele yenu, ambacho nakikusanya kuliko kukitunga, kimekusanywa kutoka katika vyanzo na njia mbali mbali; ili kuifahamisha dini hii kwa njia za kisasa zaidi.

Ili kuthibitisha kuwa ni njia ya furaha, njia ya kisomi, ustaarabu, njia ya utukufu na karama -hakukuwa na njia zaidi kuliko bora kuelezea dini hii kwa maneno ya Allah ambayo hayajiwi na batili mbele yake au nyuma yake, na kwa ushahidi na dalili kutoka kwa baadhi ya wenye akili wasiokuwa Waislamu, ili athari ienee na upeo wa msomaji muadilifu upanuke.

Kwa hiyo tukapenda kukurudisha kwenye asili, na tuzame pamoja nawe kwenye mantiki ya kiakili, tutakuongoza kwa kauli za wanafalsafa na wana fikra, kisha baada ya hapo tutapita pamoja katika majaribio ya viongozi na watu wenye hekima na busara, watu mashuhuri katika safari ya utafiti wa furaha na njia yake.

Ni msafara wa kiistaarabu wa kifikra pamoja na furaha na njia zake za kuifikia, ni msafara unaoingia ndani ya nafsi kama vile nyakati na historia inavyopita, na kuangalia mbele, katika kufahamu aina nyingi za mifumo mingi sana, kila moja ikidai kuwa inamiliki njia ya kuelekea kwenye furaha. Tunayofanya ni kwa ajili ya miongozo ya Nafsi na kumzingatia kila mtu, na hivyo kukwea katika msafara wa matarajio ya jamii na umati mbali mbali na Umma katika kufahamu njia ya furaha.

Kuwa pamoja nasi ujionee vigezo halisi vya kuchagua njia na kuijua, bali kuichagua na kuitathmini….Ni msafara wa kufahamu njia ya kuelekea kwenye furaha….njia ya maadili, elimu, ustarabu, rehema na karama. Je, unaijua njia hii?! Je ungependa kuijua?!

Dr.Abdullah bin Salim Bahammam.

https://www.path-2-happiness.com/sw

الطريق إلى السعادة
The Path to Happiness

NJIA IKO WAPI?!

https://www.path-2-happiness.com/sw

Yaliyomo

NJIA IKO WAPI?!

Watu wote wanatafuta furaha, njia iko wapi?!

Je, ni Njia ya Kumkana Mungu au Njia ya Dini?

Kuna maswali ambayo bado yanahitaji majibu

Majibu yawe vipi?

Dalili ni zipi?

Dalili za uungu wa Allah ta’ala

NJIA IKO WAPI?!

Watu wote wanatafuta furaha, njia iko wapi?!

Watu wote wanatafuta furaha, hivyo basi njia iko wapi?! Kila mtu kwa njia yake nyepesi anatafuta furaha, pamoja na tofauti mbalimbali za watu kuhusu madhehebu yao, kabila zao, utaifa wao, misingi yao ya kimaadili, malengo yao, ila wote kwa pamoja wanaafikiana katika lengo moja; nayo ni; kutafuta furaha na utulivu.

Utakapomuuliza mtu yeyote: Kwa nini unafanya hivi? Na kwa nini umefanya vile? Atajibu: Nataka furaha!! Awe amesema hivyo moja kwa moja au kwa maana yake.

Kama ni hivyo ni nini furaha, na tunawezaje kuifikia?!

Furaha ni hisia za utulivu inayoendelea, yenye raha, tumaini na shangwe, hisia hizi hutokea kwa matokeo ya hisia ya mambo matatu yenye kudumu, nayo ni; wema wa dhati ya mtu, wema wa maisha ya mtu, na wema wa mwisho wa mtu.



Furaha kwa mkabala

"Huenda ukasimamia jambo lisilokuletea furaha lakini hakuna furaha bila ya kusimamia jambo."

Benjamin Disraeli

Waziri Mkuu wa zamani wa Uingereza.

Furaha ipo karibu sana na sisi

"Tunaitafuta furaha mara nyingi lakini ipo karibu yetu, kama vile tunavyotafuta miwani iliyopo machoni mwetu."

Tolstoy

Mwanafasihi wa Urusi

Kuhusu mambo haya matatu mtu huanza kujiuliza mwenyewe, na maswali yanaongezeka na kuwa makubwa kila akikua, wala mtu huyo hapati furaha hadi aweze kujibu maswali yake yanayomjia mara kwa mara akilini, miongoni mwa maswali hayo ni:-

-Nani mwenye kuumiliki ulimwengu huu na kuufanya atakavyo?

-Ni nani aliyeniumba na kuumba ulimwengu huu ulionizunguka?

-Mimi ni nani? Nimetoka wapi? Kwa nini nimeumbwa? Mwisho wangu uko wapi.

Pindi mwamko wa mwanadamu unapozidi katika nafsi yake na katika maisha yake, maswali haya huzidi kumsumbua akilini mara kwa mara, kwenye fikra zake na roho yake, wala hapati utulivu wowote na furaha hadi zipate majibu yake na kutuliza nafsi yake.

Njia zimekuwa nyingi
Mungu ni mmoja

"Ikiwa hujui unakwenda wapi, basi njia zote zitakupeleka huko."

Lewis Carol
Mwana Hisabati

Je, ni Njia ya Kumkana Mungu au Njia ya Dini?

Watu huanza kufikiria kujibu maswali yaliyotangulia, kuna njia mbili; Njia ya kwanza ni ile ya kumkana Mungu, na ya kuwa ulimwengu ni maada.

Njia ya pili ni ile ya kumuamini Mungu kuwa ni Muumba wa kila kitu; na matokeo yake ni kujitokeza kwa maswali mengi miongoni mwake ni:-

-Je, inawezekana ulimwengu ukapatikana wenyewe tokea hapo mwanzo kutokana na maingiliano yaliyokuja ghafla bila kupangiwa muda.

-Je, inaingia akilini kuwa ghafla hii ya bahati nasibu isiyokuwa na mpangilio wowote ndio imeupata ulimwengu huu ulioratibiwa vizuri?!!

-Je, alichofikia mwanadamu tokea apatikane katika historia nzima ni zao la ukuzi au ndio huo ughafla wa bahati nasibu?!! Na ya kuwa sisi ni unyoya katika pepo yenye kuugeuza geuza kwa hali hiyo hiyo ya ghafla na fujo?!!



Ainisha Muelekeo wako

“Kwa hakika ulimwengu unakunjua njia kwa ajili ya mwenye kujua anakokwenda.”

Ralph Waldo Emerson
Mwanafalsafa wa Kimarekani



-Je, mwanadamu ndio Mungu aliyepanga sheria, nae ni Muumba mbunifu, naye ni kila kitu, na nyuma yake hamna kitu kingine?

-Je, yaliyokuwa nyuma ya maumbile katika mambo ya ghaib. Je ni mazigazi ambayo yanapaswa kupotea mbele ya wasio kuwa na Dini na Ulimwengu wa maada?.

-Je, mwanadamu ni maada tu asiyekuwa na mazingatio yoyote, au ni kuwa asili yake ilikuwa ni nyani aliyeendelea kwa kupita muda?

Ni aina gani maada ya ambayo inaweza kumuumba mwanadamu mwenye sifa hizi za hali ya juu, na mengi bora matukufu, aliyeumbwa kwa mengi ya kushangaza?!

Na je asiyekuwa nacho anaweza kutoa?!

-Je, dunia ndio lengo la mwanadamu na mwisho wa kimbilio lake, hakuna mazingatio kwa yaliyosemwa na dini mbali mbali kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa kuwepo nguvu nyingine zisizokuwa mwanadamu, au maisha mengine yasiokuwa maisha haya?

Allah Ta’ala amesema kuhusu kufikiri kwa watu hao. {Na walisema: Hapana ila huu uhai wetu wa duniani - twafa na twaishi, na hapana kinacho tuhiliki isipo kuwa dahari. Lakini wao hawana ilimu ya hayo, ila wao wanadhani tu.} [45:24],

Kuhusu wale waliokataa na kupinga Allah Ta’ala amesema, {Na wakazikataa kwa dhulma na kujivuna, na hali ya kuwa nafsi zao zina yakini nazo. Basi angalia ulikuwaje mwisho wa mafisadi!} [27:14].



Einstein
Mwanazuoni wa Fizikia

Elimu na Dini

“Mimi si amini ya kuwa elimu yapasa igongane na dini katika hali ya kawaida. Kwa hakika ninaona kuna uhusiano na fungamano baina yao. Hivyo basi mnasema kuwa elimu bila ya dini ni kama vile mtu aliyepooza mguu. Na dini bila ya elimu ni kipofu kila kimoja ni muhimu. Zinatakiwa zifanye kazi pamoja mkono kwa mkono. Inaelekea kwangu kuwa Yule ambae hatofurahishwa na ukweli katika elimu na dini ni kama mtu aliyekufa.”

https://www.path-2-happiness.com/sw

Newton
Mwanafalsafa wa Uingereza

Ulahidi (Kumkana Mungu)... ni aina ya Upumbavu

"Kumkana Mungu ni aina ya Upumbavu: Ninapoangalia utaratibu wa jua ninaona kuwa ardhi imekaa sehemu inayostahiki kutoka kwenye jua, ambayo inayoiwezesha kupata kiasi cha kutosha cha joto na mwanga, na hii bila ya shaka halijatokea ghafla."

Kwa hakika wapinga dini (walahidi) wanakiri udhaifu wao kamilifu kuhusu

kujua siri ya uwepo wa uhai kwa kiumbe chochote; vyovyote awavyo, awe ni mdogo kwa umbile au mkubwa, na wanakiri kuwa hawawezi kurejesha roho kwa mtu kama imefika kooni, kama ni hivyo ipo wapi ile maada wanayoiona kuwa ndio iliyopata na kuwepo ndani ya ulimwengu huu?!

Ni maada gani iliyotumika katika kupatisha ulimwengu huu?!

Na kwa nini wasiweze kuifikia ili kurejesha roho baada ya kiwiliwili kuwa maada isiyo na uhai wowote?.

Ikiwa kinachosemwa na hawa wanaopinga uwepo wa Mwenyezi Mungu ni sahihi iweje basi binadamu wote wakakubaliana kuheshimu dini kiasi hiki.

Kinachosemwa na hawa wapinzani wa Mwenyezi Mungu ya kuwa dini ni ndoto na mambo tu ya kufikirika?!

Kama ni hivyo kwa nini Mitume katika zama zao waliweza kubakisha mafundisho yao hai katika mioyo ya watu, wakati ambapo fikra mbali mbali za watu zimesahaulika, bali si hivyo tu, zimechuja baada ya kupita muda pamoja na njia mbali mbali za kuvutia zinazotumiwa na watu na ufasaha wao?!

Inawezekana vipi kutofautisha baina ya matendo ya kheri na yale ya shari? Bali ni kitu gani ambacho kinaweza kumkataza na kumzuia jambazi kuekeleza ujambazi wake? Na kitu gani kinaweza kufanya moyo wa



Plato
Mwanafalsafa wa Kigiriki (Kiyunani)

Ni nzuri yenye kufuata mfumo maalumu

"Kwa hakika Ulimwengu ni dalili katika uzuri na nidhamu wala hilo haliwezi kuwa ni matokeo ya sababu ya Itifaki, bali ni umbile la mwenye akili mwenye kukusudia kheri na kupanga kila kitu kwa makusudio na hekima."

tajiri kumhurumia fukara? Na kipi kinaweza kumzuia mwizi na mtu mwenye kughushi, haini na mlevi wa

mihadarati..wote hawa kipi kinachoweza kuwazuia kutekeleza matamanio yao?

Kwa hakika jamii za wakana Mungu zinaishi pamoja kama vile makundi ya mbwa mwitu yanayoishi kati ya wenye kudhulumu, wabinafsi, wenye kujipendelea, mapenzi ya matamanio yao na mengineyo; na hivyo basi ukanaji wa Mungu ni sababu kubwa ya tabu azipatazo mwanadamu, ufakiri, kuzidi kwa chuki, hofu na wasiwasi, amesema Allah Mtukufu: {Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu.} [20:124].

Ukanaji Mungu ni fikra batili ambavyo akili, mantiki wala maumbile hayakubali, ni fikra batili inayopingana na elimu; na ndio maana wanazuoni wengi wamewapinga, kama ambavyo inakwenda kinyume na mantiki, kwani fikra yake imesimamia kuwa katika maisha haya hakuna mantiki, bali ni suala la ghafla na bahati nasibu tu ndio iliyouanzisha ulimwengu huu mzuri, wala hakuna maumbile maalum yaliyouanzisha; maumbile sahihi ni yale yanayomlingania mtu kuwa na dini hata kwa wale wanaojidai kuwa hawaamini: {Na wakazikataa kwa dhulma na kujivuna, na hali ya kuwa nafsi zao zina yakini nazo. Basi angalia ulikuwaje mwisho wa mafisadi!} [27:14].

Furaha ya Kweli

“Hivi sasa ninaishi katika uhalisia na sio katika haiba ile ya udanganyifu ambayo tunaishi katika maisha yetu ya sasa. Maada, matumizi yetu, na maingiliano yetu na jinsia nyingine pamoja na matumizi ya mihadarati. kwa kudhania kuwa hivi ndivyo vinavyotupa furaha lakini kwa sasa nimeona Ulimwengu uliojaa furaha na uliojitosheleza kwa upendo, matarajio na amani.

Lauren Booth

Mwanaharakati wa haki za binaadamu wa Uingereza

KUNA MASWALI AMBAYO BADO YANAHITAJI MAJIBU

Bila elimu mwanadamu anakuwa si mwenye kufahamu majibu ya maswali haya, wala elimu za kisasa hazijaweza kujibu maswali haya; kwani kadhia hizi zinaingia katika mzunguko wa dini; na kwa ajili hiyo riwaya zimekuwa nyingi na ushirikina na simulizi zimekuwa nyingi katika maswali haya; jambo ambalo linazidisha babaiko kwa mwanadamu na kumtia hofu.

Wala mwanadamu hawezi kusimama kujibu majibu yenye kutosheleza kwa maswali hayo ila atakapoongozwa na Allah katika njia sahihi ambayo itamfikisha katika wema, amani na utulivu na kwenye furaha na raha.

Kadhia hizi na maswali haya hayaelezwi na kufafanuliwa na mfano wake ila kwenye dini mbali mbali; kwa sababu kadhia hizi huchukuliwa na kuzingatiwa kuwa ni katika elimu za mambo ya ghaibu, na dini iliyokuwa sahihi ndio ambayo inajipwekesha na haki na kauli ya kweli; kwa sababu ni kutoka kwa Allah ambaye amewapelekea wahyi Mitume wake, amesema Allah Ta'ala: {…Sema: Hakika uwongofu wa Mwenyezi Mungu ndio uwongofu…}[2:120]

Na kauli yake Allah: {…Sema: Hakika uwongofu ni uwongofu wa Mwenyezi Mungu…} [3:73]

Hivyo basi imekuwa ni lazima kwa mwanadamu kuikusudia dini ya haki, kujifunza na kuiamini; ili babaiko hili na shaka limuondoke, na aelekee katika njia iliyonyooka, njia ya furaha na ya tumaini.



Ifanye furaha kuwa ni lengo lako

"Ukitaka kuwa mwenye furaha: Unganisha furaha na lengo na sio na mtu au na kitu."

Einstein
Mwanazuoni wa Fizikia

MAJIBU YAWE VIPI?!

Allah amesema: {Na kwa yakini tumemuumba mtu kutokana na asli ya udongo. Kisha tukamjaalia awe tone ya mbegu ya uzazi katika kalio madhubuti. Kisha tukaiumba tone kuwa damu iliyo ganda, na tukaiumba damu kuwa pande la nyama, kisha tukaliumba pande la nyama kuwa mifupa, na mifupa tukaivika nyama. Kisha tukamfanya kiumbe mwengine. Basi ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbaji. Kisha hakika nyinyi baada ya hayo mtakufa. Kisha hakika nyinyi Siku ya Kiyama mtafufuliwa.} [23:12-16].

Hivyo basi mwisho wa kimbilio letu ni kufafanuliwa na kurudi kwetu kwa Allah Ta'ala, kwa maana hiyo maumbile haya hayakuwa ni mchezo (Mwenyezi Mungu Ametukuka dhidi ya kufanya mchezo) bali yalikuwa yenye hekima kubwa, Allah amesema: {Je! Mlidhani ya kwamba tulikuumbeni bure na ya kwamba nyinyi kwetu hamtarudishwa?} [23:115].

Hiyo basi Allah hakuuumba mwanadamu na majini kwa mchezo, bali amewaumba kwa kumuabudu yeye peke yake tu bila kumshirikisha na yeyote, kumuabudu yeye tu kwa mtazamo mpana kwa kufanya yote ayapendayo Allah Ta'ala na kuridhika katika aliyoyafaradhisha, na swala, na dhikri na kuimarisha ardhi, na kuwanufaisha watu; Allah amesema: {Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi.} [51:56]

Watu wote wanarejea na kukimbilia kwake tu, pamoja na marejeo yote ni kwake; Allah amesema: {…Na marejeo ni kwa Mwenyezi Mungu...} [3:28].

Yakini inaondosha mchezo katika maisha ya watu, na kuwapa maana ya maisha yao, na furaha katika mioyo na roho zao Allah amesema: {Au wao wameumbwa pasipo kutokana na kitu chochote, au ni wao ndio waumbaji? Au wao wameziumba mbingu na ardhi? Bali hawana na yakini. } [52:35-36]

Descartes

Mwanafalsafa wa Kifaransa

Muumba wa Kila Kitu

"Mimi nipo: Basi ni nani aliyenileta na ni aliyeniumba?, Mimi sijajiumba; hapana budi kuwepo na Muumba, na Muumba huyu hapana budi awe wajibu wa uwepo. Asiyehitaji uwepo wa mwingine aliyemleta, au mwenye kuhifadhi uwepo wake, Mungu huyu anapasa kusifika kwa sifa zote za uzuri Muumba huyu ni Allah mwanzilishi wa kila kitu."

https://www.path-2-happiness.com/sw

Mwanadamu anaposhindwa kujua siri ya Ulimwengu huu, na kuanza kufikiria viumbe wa Allah, ardhi, nyota, sayari mbali mbali, mfuatano wa usiku na mchana, uhai na mauti, na yote aliyoyaweka Allah katika Ulimwengu huu…. Mwanadamu akifanya hivyo anafahamu kwa yakini kwa maumbile yake ya asili (fitra) kuwa yupo mtukufu na mkubwa aliyeipata ulimwengu huu ambaye ndie mwenye nguvu zaidi kumshinda yeye, ambaye yeye binadamu anastahiki kunyenyekea kwake, kumuabudu, kutarajia thawabu zake na kuhofia adhabu zake.

Vivyo hivyo tafakuri hii katika hayo humfanya mtu kumkubali Muumba Mtukufu Adhwimu, mwenye uwezo na mwenye hekima, na ya kuwa Maada haikuwa chochote isipokuwa kiumbe miongoni mwa viumbe wake vimetokea baada ya kuwa havikuwepo hapo kabla.

Mola huyu, mwenye hekima, mwenye uwezo ambaye amewajulisha waja wake na nafsi yake, na akawasimamishia alama na ishara za kuwepo kwake na dalili mbali mbali na fafanuzi mbali mbali, ambaye Yeye Allah anajitosha dhidi ya yote hayo (naye mwenyewe amejisifu kwa sifa kamilifu) sifa ambazo zinabainisha na kuthibitisha uwepo wake, Uungu wake, na Uola wake kwa sheria za mbinguni, na umuhimu wa kiakili na maumbile ya asili ya kitabia, na umma mbali mbali zikakubaliana katika hilo.

Jibu lenye kutosheleza

"Historia ya dini kwa ujumla, na historia ya Tawhid haswa hutudhihirishia kuwa kumuamini Allah peke yake ni jibu tosha la kipekee la kila swali kuhusu ya Ulimwengu na ubinadamu na lengo la uwepo wao, haiwezekani maisha ya mwanadamu\yakawa na lengo ila Allah peke yake. Na kila ibada na dini kwa mwanadamu lengo lake ni asili ni iwe mtu anajua au hajui –humpelekea katika kumuamini Mungu mmoja."



Cardinal Koenig
Raisi wa Maaskofu wa Austria

DALILI NI ZIPI?

1. Kuwa Allah Ndiye Muangalizi wa yaliyomo katika ubunifu wa Uumbaji

-Je, huoni Ulimwengu huu Mkubwa na yaliyomo katika mbingu na ardhi?!

-Je, umefikiria hata siku moja kuhusu Uumbaji wa mbingu na yaliyomo katika sayari?!

-Je, hukuwahi kuwa na mazingatio katika ardhi ile na vilivyomo ndani yake katika mito, bahari, mabonde na milima?!

-Je, uratibu huu uliopangwa vizuri kwa ubunifu na ufanisi wa hali ya juu haujakufurahisha?.

-Je, ni nani aliyeumba Ulimwengu huu na ukawa katika hali hii ya ubunifu wa hali ya juu iliyopangiliwa kwa mpangilio wa juu kabisa na kupambwa katika umbile hili lenye muujiza kiasi cha kuwa ni alama na ishara ya ukamilifu, na katika isiyokuwa na mfano uliotangulia?!

-Je, ameiumba nafsi yake?! Au katika Ulimwengu huu kuna Muumba mwenye uwezo? Allah amesema: {Hakika katika kuumbwa mbingu na ardhi na kukhitalifiana usiku na mchana ziko Ishara kwa wenye akili, Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima na wakikaa kitako na wakilala, na hufikiri kuumbwa mbingu na ardhi, wakisema: Mola wetu Mlezi! Hukuviumba hivi bure. Subhanaka, Umetakasika! Basi tukinge na adhabu ya Moto.} [3:190-191].

Je, haijawahi kukupitia akilini mwako siku moja kuhusu kuumbwa kwako? Allah amesema: {Na pia katika nafsi zenu - Je! Hamwoni?} [51:21]





Mungu ni Kweli

"Utakapofikiri kwa kina; Sayansi itakulazimisha kuamini kuwepo kwa Mungu."

Lord Kelvin

Mwanafizikia wa Scotland

Sasa ni vipi alivyoumbwa mwanadamu? Allah amesema: {Au wao wameumbwa pasipo kutokana na kitu chochote, au ni wao ndio waumbaji? Au wao wameziumba mbingu na ardhi? Bali hawana na yakini. } [52:35-36]

Na kama hakuumbwa hapo kabla alipokuwa si kitu, (achilia mbali kwamba wao hawakujiumba na kuumba nafsi zao, bali hawakuumba mbingu na ardhi), hakuna shaka yoyote kuwepo kwa Muumba wa Ulimwengu huu na vyote vilivyomo, nae si mwigine bali ni Allah Mtukuka, cha kushangaza mno ni ile hali wanaopinga kuwepo kwa Allah muumba, mwenye kusawiri kila kitu baada ya ishara zote na dalili mbali mbali!!

2. FITRA (MAUMBILE ASILI)

Kwa hakika viumbe wako katika fitra ya kukiri uwepo wa Allah Ta'ala bila ya shaka yoyote ile, kama vile ambavyo anavutika katika kupenda kheri na kuchukia mambo mabaya, bali bila ya shaka kukiri kwao uwepo wa muumba ni katika mambo makubwa yaliyomo na kudumu kwenye fitra kiasi cha kutohitaji dalili yoyote au uthibitisho wowote ule, Allah amesema: {Basi uelekeze uso wako sawasawa kwenye Dini - ndilo umbile la Mwenyezi Mungu alilo waumbia watu. Hapana mabadiliko katika uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo Dini iliyo nyooka sawa. Lakini watu wengi hawajui. } [30:30]

Na Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) naye akasema: «Hakuna mtoto anayezaliwa ila huzaliwa katika fitra» (Bukhari na Muslim)."

Hisia za Kimaumbile

"Mungu ambae tunajisalimisha kwa uwepo wake, haishii kwenye Ulimwengu wa Mada, wala hisia zetu dhaifu haziwezi kumdiriki (kumpata), na katika hilo ni mchezo kujaribu kuthibitisha uwepo wake kwa kutumia sayansi: kwa sababu Mungu mwenyewe huchukua duara lisilokuwa duara lake finyu lenye ukomo. Kwa hakika imani ya kuwepo Mwenyezi Mungu ni katika mambo mahususi ambayo yanaota katika hisia ya mwanadamu na dhamira yake na kukua katika mzunguko (duara) wa uzoefu wake binafsi."

Robert Morris Page

Mwanasayansi

https://www.path-2-happiness.com/sw

3. MAKUBALIANO YA UMMAH

Ummah mbali mbali zimeshakubaliana tokea zamani kunasibisha maumbile na uumbaji wa Ulimwengu huu kwa Allah Ta'ala hivyo kukawepo makubaliano–yaliyodumu ya kuwa Allah Ta'ala ndie muumba wa Ulimwengu huu bila ya mshirika, hivyo Ummah wote hauwezi kuacha kuzingatia kuwepo Muumba wa Mbingu na Ardhi, au Mruzuku asiyekuwa Allah Mtukuka, bali pindi wanapoulizwa kuhusu hayo hukiri (pamoja na ushirikina wao) ule Uungu wa Allah Ta'ala. Amesema Yeye mwenye shani; {Na ukiwauliza; Nani aliye umba mbingu na ardhi na akafanya jua na mwezi kuti'ii amri yake? Bila ya shaka, watasema: Mwenyezi Mungu. Wapi basi wanako geuzwa? Mwenyezi Mungu humkunjulia, na humdhikishia, riziki amtakaye katika waja wake. Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.} [29: 61-63]

Na akasema vile vile: {Na ukiwauliza: Nani aliye ziumba mbingu na ardhi? Bila ya shaka watasema: Kaziumba Mwenye nguvu, Mjuzi} [43:9]

Ama hali ya watu kumkana Mwenyezi Mungu na kukufuru kwao Allah Ta'ala (kama ilivyotangulia kuelezea) ni hali ya kujitenga, yaani ni hali ya kujitenga wafuasi wake wa fikra hii ya kumkana Allah na kundi la watu wenye akili, na kukadhihirika kufeli kwa fikra hiyo katika uhalisia wake.

Imani ya Mungu ni maumbile (Fitra)

"Akili zinazokuwa katika hali ya kawaida kwa watoto zinawafanya kuelekea katika kumuamini Mungu Muumba, badala ya makuzi ambayo sio ya kawaida ya akili za binadamu na ugumu wa kukubali na kudhibiti."

Justin Barret

Mtafiti katika chuo kikuu cha Oxford

4. USHAHIDI WA AKILI

Kwa nyongeza ya yaliyotangulia katika dalili na ushahidi mbali mbali yakuwepo kwa Allah na Uungu wake; basi akili ya mtu ni miongoni mwa dalili kuwa ya kuwa Uumbaji huu wa Ulimwengu katika hali hii haiwezekani kabisa kuwa imejiumba yenyewe; yaani kiumbe kilichotokea tu na kuzuka na bila ya shaka yoyote kuwa kila chenye kuzuka hakikosi mzushaji.

Swali lenye kujitokeza hapa; ni mara ngapi umepata dhiki au msiba au lawama, umeelekea kwa nani? Umenyenyekea kwa nani? Nani umemuomba akuondoshee dhara yako na kufariji humumi na huzuni zako?! Allah Ta'ala amesema: {Na taabu inapo mfikia mtu humwomba Mola wake Mlezi naye ameelekea kwake. Kisha akimpa neema kutoka kwake, husahau yale aliyo kuwa akimwitia zamani, na akamfanyia Mwenyezi Mungu washirika ili apoteze watu njia yake. Sema: Starehe na ukafiri wako kwa muda mchache. Kwani hakika wewe utakuwa miongoni mwa watu wa Motoni.}[39:8]

Katika aya nyinginezo Allah amesema, {Yeye ndiye anaye kuendesheni bara na baharini. Hata mnapo kuwa majahazini na yakawa yanakwenda nao kwa upepo mzuri wakaufurahia, upepo mkali ukawazukia, na yakawajia mawimbi kutoka kila upande, na wakaona wamesha zongwa, basi hapo humwomba Mwenyezi Mungu kwa kumsafishia niya: Ukituokoa na haya bila ya shaka tutakuwa miongoni mwa wanao shukuru. Lakini akisha waokoa, mara wanafanya jeuri tena katika nchi bila ya haki. Enyi watu! Jeuri zenu zitakudhuruni wenyewe. Hii ni starehe ya maisha ya dunia tu. Kisha marejeo yenu ni kwetu, na hapo tutakuambieni mliyo kuwa mkiyatenda.}[10:22-23]

Kuwa Mwenye Akili

"Je, inawezekana mwenye akili kupima au kuamini kuwa mada tupu ya akili na hekima imejitengeneza yenyewe kwa kubahatisha tu"?!

John Cleveland Cothran

Profesa wa Sayansi katika Chuo Kikuu cha Dolth

Na amesema vile vile, {Na wimbi linapo wafunika kama wingu, wao humwomba Mwenyezi Mungu kwa kumsafia dini. Lakini anapo waokoa wakafika nchi kavu, wapo baadhi yao huenda mwendo wa sawa. Wala hazikanushi Ishara zetu ila aliye khaini kafiri mkubwa.}[31:32].

DALILI ZA UUNGU WA ALLAH TA'ALA

Maumbile sahihi na akili zilizotua zinakiri kuwa Ulimwengu huu una Mola, na Viumbe hivi vina Muumba; na vimethibitisha kuwepo kwa Uungu wake na ya kuwa Yeye ni Mmoja katika Uungu na Uola wake, hana mshirika katika Uungu wake, na dalili zake ni nyingi na zipo wazi, miongoni mwazo ni:

1. haiwezekani kuwepo na Miungu wawili katika Ulimwengu huu?!!

Lau kwamba kungekuwepo na miungu

Falsafa na Dini

Falsafa kidogo inamsogeza mtu kwenye kumpinga Mungu. Ama kubobea katika Falsafa humrudisha mtu kwenye dini."

Francis Becon

Mwanafalsafa wa Uingereza

wawili (kwa ajili ya mjadala tu) swali litabakia: Vipi kama watapingana na kila mmoja kuekeleza matakwa yake?!! Mmoja akataka jambo na mwingine atake kinyume chake?!

haiwezekani ila mmoja kuwa juu ya mwingine, na hahesabiwi mwingine kuwa ni mnyonge au dhaifu, Je, mnyonge anaweza kuwa ni Mungu?!! Na kubakia Mungu kuwa ni mmoja tu, Allah Mtukuka amesema: {Mwenyezi Mungu hana mwana yeyote, wala hanaye mungu mwengine. Inge kuwa hivyo basi kila mungu angeli chukua alivyo umba, na baadhi yao wangeli washinda wengine. Mwenyezi Mungu ameepukana na sifa wanazo msifu. Mjuzi wa siri na dhaahiri, na ametukuka juu ya hayo wanayo mshirikisha nayo.}[23:91-92].

Cha kushangaza ni mtu kumuabudu asiye na uwezo wala nguvu, hana umiliki wa mbingu na ardhi, hawezi kuumba chochote, hamiliki chochote katika nafasi yake mbali ya kuwamilikisha wengine –madhara au manufaa, mauti wala uhai wala ufufuo Allah Ta'ala

Hakuna Mungu ila Allah

"Sikiza, Ee Israeli; Bwana, Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja.." (6:4).

Agano la Kale (Torati)

https://www.path-2-happiness.com/sw



Herschel

Mwanafalsafa na Mtaalamu wa sayari wa Uingereza

Upekee wa Mungu

"Kila wigo wa elimu unapopanuka huongezeka dalili na uthibitisho wa uwepo wa hekima ya Muumba mwenye uwezo usio na mipaka na wanazuoni wa ardhi, taasisi mbali mbali, sayansi ya mazingira halisi na hesabu hujitahidi katika tafiti na ugunduzi wao kila chenye kulazimu ili kuanzisha hekalu la elimu ili kunyanyua neno la Muumba."

amesema: {Ametukuka aliye teremsha Furqani kwa mja wake, ili awe mwonyaji kwa walimwengu wote. Ambaye ni wake ufalme wa mbingu na ardhi, wala hakuwa na mwana, wala hakuwa na mshirika katika ufalme, na akaumba kila kitu na akakikadiria kwa kipimo. Na wamechukua badala yake miungu ambayo haiumbi chochote, bali hiyo inaumbwa, haijimilikii nafsi zao madhara wala manufaa, wala haimiliki mauti, wala uhai, wala kufufuka.} [25:1-3].

Vinginevyo kama jambo ndilo kama wasemavyo washirikiana kuwa pamoja na Allah kuna miungu ambao huabudiwa ili kumkurubisha kwake aombewe basi hao waabudiwa wanamuabudu na wanajikurubisha kwake na kutafuta kwao wasila na ukuruba, Allah Ta'ala amesema: {Sema: Lau kuwa wangeli kuwa pamoja naye miungu mingine kama wasemavyo, basi wangeli tafuta njia ya kumfikia Mwenye Kiti cha Enzi. Subhanahu Wa Taa'la, Ametakasika na Ametukuka juu kabisa na hayo wanayo yasema. }[17:42-43],

Bali Yeye ni Allah mmoja Mkusudiwa, ambaye hakuzaa wala kuzaliwa wala hafanani na chochote.

Hawa wenye kuabudiwa hawamiliki chochote wala hawawezi; Allah amesema: {Sema: Waite mnao wadaia kuwa ni badala ya Mwenyezi Mungu. Hawamiliki hata uzito wa chembe hichi katika mbingu wala ardhi. Wala hawana ushirika wowote humo. Wala Yeye hana msaidizi miongoni mwao. Wala uombezi mbele yake hautafaa kitu, isipo kuwa kwa aliye mpa idhini.} [34:22-23]



Yaani, Waambie washirikina wanaomshirikisha Allah na viumbe vingine ambao hawanufaishi wala hawadhuru, ambao hawana uwezo na, pamoja na udhaifu uliopo lakini bado wanashikamana nao, wabainishie ubatili wa ibada zao; Waombeni hao wanaodai kumshirikisha Allah, kama kweli maombi yenu yanawafaeni, kwani hakika kuna sababu za udhaifu na kushikamana kwao, na kutoweza kujibu dua kutoka popote, kama ni hivyo hawamiliki chochote; hawamiliki hata udogo wa mdudu chungu mbinguni wala ardhini kwa kujitenga au kwa kushirikiana katika hilo. Na Miungu ile ambao mnadai wapo mbinguni na ardhini ambayo mnamshirikisha kwayo Allah haina uwezo wa kumiliki chochote kile, si kidogo wala kingi. Miungu ile ya kishirikina haina ufalme wala ushiriki, labda isemwe: Huenda wakawa ni wasaidizi wa mfalme, na mawaziri wake, hivyo basi maombi yao huenda yakawa na manufaa; (kwa sababu Mfalme ana haja nao) basi atawatekelezea haja zao kwa wale waliokuwa nao karibu; na hilo Allah Ta'ala amelikana daraja hili kwa kusema: {ana nini}; yaani Allah ni mmoja Mtenza nguvu {miongoni mwao.} Yaani: kwa waabudiwa {msaidizi} yaani msaada na waziri ambao humsaidia katika ufalme wake na mipango yake.

Mwenye kuuangalia Ulimwengu huu na mwenendo wake ataona mpango uliopangika kwa utaratibu wa hali ya juu; na hii ni dalili ya kuwa kuna mwenye kuiendesha naye ni Mungu mmoja Mzuri Mwenye uwezo, amesema Ta'ala: {Na Mungu wenu ni Mungu mmoja tu, hapana mungu ila Yeye. Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu. Hakika katika kuumbwa kwa mbingu na ardhi, na kukhitalifiana usiku na mchana, na marikebu ambazo hupita baharini kwa viwafaavyo watu, na maji anayo yateremsha Mwenyezi Mungu kutoka mbinguni, na kwa hayo akaihuisha ardhi baada ya kufa kwake, na akaeneza humo kila aina ya wanyama; na katika mabadiliko ya pepo, na mawingu yanayo amrishwa kupita baina ya mbingu na ardhi, bila shaka zimo Ishara kwa watu wanao zingatia. } [2:163-164].

Je, utaratibu huu haukuwa ukienda mwaka mzima wala haiharibiki wala kusimama sekunde moja jambo ambalo lingeharibu ulimwengu huu tulionao, yote hayo makadirio yake yako kwa Allah, Je, utaratibu haukuwa kutoka kwa Muumba mpangaji wa mambo mmoja, asiye na mshirika?! Je, hii si dalili ya wazi ya kutowezekana uwepo Uungu zaidi ya mmoja kwa mtu mwenye akili?! Allah Ta'ala amesema: {Lau wangeli kuwamo humo miungu wengine isipo kuwa Mwenyezi Mungu basi bila ya shaka hizo mbingu na ardhi zingeli fisidika. Subahana 'Llah Ametakasika Mwenyezi Mungu, Bwana wa A'rshi (Kiti cha Enzi), na hayo wanayo yazua.} [21:22].

Yaani lau katika mbingu na ardhi kungekuwa na miungu wawili basi yangeharibika na kuharibika yaliyomo kwa viumbe, kwa hakika ulimwengu huu (kama inavyoonekana) katika ukamilifu utakavyokuwa katika islahi na kufuata utaratibu ambao hauna kasoro wala aibu yoyote, wala katazo, wala upinzani na hii inathibitisha kuwa mpangaji wake ni mmoja, na Mola ni mmoja na Mungu ni mmoja lau kama kungekuwa na wapangaji wawili na Mola wawili au zaidi ya hao; basi utaratibu wake ungeharibika, na nguzo zake zingebomoka basi bila ya shaka zingezuiana na kupingana, na kama mmoja wao angetaka kupanga kitu na mwingine hataki hilo, basi ingeshindikana wote kufanikiwa katika matakwa yao, na kufanikiwa kwa matakwa ya mmoja bila ya mwingine ni uthibitisho wa udhaifu wa mwingine, na kutokuwa na uwezo, na kukubaliana kwao na kuafikiana kwao katika jambo moja katika mambo yote ni jambo lisilowezekana; hivyo basi yapasa kwa mmoja mwenye nguvu na uwezo apate muradi wake peke yake bila ya kuzuiwa wala kupingwa na huyu ndie Allah Mmoja Pekee Mwenye nguvu na uwezo.

https://www.path-2-happiness.com/sw

Lengo Kuu

"Ulimwengu huu umedhihiri kwetu kwa hali hii ambayo haijaacha kitu chochote cha kubahatisha, bali kila sehemu katika sehemu zake kuelekea kwenye lengo. Lengo hilo linaelekea kwenye lengo kuu kabisa kuliko hilo. Hivyo ndivyo inavyofikia katika lengo la mwisho."



Plato

Mwanafalsafa wa Kigiriki

Manabii wa wateule wote tokea zama za Adam ('Alayhi Salaam), hadi Nuuh, Ibrahim, Musa, Issa na Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) nao ni watu walioepushwa na madhambi ya nafsi zao na wenye akili angavu na kauli ya ukweli na amana ya kufikishana uongofu juu ya kumpwekesha Allah Ta'ala na kuwa Yeye ndiye Hapana Mungu ila Allah, Allah amesema: {Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia ya kwamba hapana mungu isipo kuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu. } [21:25]

Na akasema vile vile kumsifu Nuhu ('Alayhi Salaam) {Tulimpeleka Nuhu kwa kaumu yake, naye akasema: Enyi kaumu yangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu. Nyinyi hamna Mungu ila Yeye. Hakika mimi ninakukhofieni adhabu ya Siku iliyo kuu} [7:59]

Na akasema kuhusu Issa ('Alayhi Salaam) {Na hali Masihi mwenyewe alisema: Enyi Wana wa Israili! Muabuduni Mwenyezi Mungu, Mola wangu Mlezi na Mola wenu Mlezi. Kwani anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu atamharimishia Pepo, na mahala pake ni Motoni. Na walio dhulumu hawatakuwa na wa kuwanusuru.}[5:72]

Na akamuamrisha Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) awaambie watu wake: {Sema: Hakika imefunuliwa kwangu ya kwamba hakika Mungu wenu ni Mungu Mmoja tu. Je! Mmesilimu?} [21:108]

Hivyo basi ni jambo la msingi kwa wenye akili nzuri kufuata Mtume wao, na kumpwekesha Allah Ta'ala na kumuamini Yeye Mola wao mlezi na Mungu wao, ili wapate furaha ya duniani na ya Akhera, Allah Ta'ala amesema: {Mwenye kutenda mema, mwanamume au mwanamke, naye akawa ni Muumini, tutamhuisha maisha mema; na tutawapa ujira wao kwa bora ya waliyo kuwa wakiyatenda.} [16:97].

https://www.path-2-happiness.com/sw

Bwana Mmoja

“Wewe umeonyeshwa haya, ili upate kujua ya kuwa BWANA ndiye Mungu, hapana mwingine ila yeye” (Kumbukumbu la Torati) 4:35).
“Mimi ni BWANA, wala hapana mwingine zaidi yangu mimi hapana Mungu.” (Isaya 45:5).

Kwa hakika matendo mema pamoja na imani malipo yake ni maisha mazuri katika ardhi hii, sio lazima yawe ni yenye neema sana au utajiri wa mali, bali inaweza kuwa hivyo au isiwe hivyo, na maisha yanaweza kuwa mazuri lakini mtu bila ya kuwa na mali au utajiri; Katika maisha kuna mambo mengi ambayo sio mali wala utajiri, bali baadhi ya mambo ambayo mtu katika maisha yake anayafurahia, ni kama:-

i-Mawasiliano ya mtu na Mola wake, kumuamini na kuwa na utulivu na ulezi wake na stara yake, na kuridhiwa naye.

ii-Kuna suala la afya ya mtu na utulivu wake, kuridhika na kupata baraka, kuishi katika nyumba na mapenzi katika mioyo.

iii-Kuna suala la mtu kufurahi kwa kufanya kwake matendo mema na athari yake katika dhamira yake, na katika maisha yake, Na hayakuwa mali katika maisha ya mwanadamu isipokuwa ni kipengele kimoja tu katika pambo katika maisha yake: {Mali na wana ni pambo la maisha ya dunia. Na mema yanayo bakia ni bora mbele ya Mola wako Mlezi kwa malipo, na bora kwa matumaini.} [18:46].

Itakapokuwa moyo wa mwanadamu unaungana na kitu kilichokuwa kitukufu zaidi na chenye kubaki zaidi kwa Allah Ta’ala basi wakati huo maisha ya mtu huyo yanakuwa na maana nyingine, na furaha hali kadhalika inakuwa na maana nyingine katika maisha.

Mwanadamu huyo akikataa ila kuipa mgongo, basi atakuwa ameiridhia nafsi yake njia nyingi za tabu na balaa ambazo kupata mara kwa mara bila kukatika, na huenda mtu huyo akawa ameridhia nafsi yake njia nyingi za tabu na shida na mashaka anaelea hapo bila kuacha, Allah Ta’ala amesema:

Mungu Mmoja

“Ndipo Yesu alipomwambia, Nenda zako, Shetani, kwa maana imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake.” (Mathayo 4:10, Luka 4:8).
“Na uzima wa milele ndio huu, wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.” (Yohana 17:3).

Agano Jipya (Injili)

http[illegible]m/sw



Dalili ya Furaha

"Sikujua furaha hapo kabla. Tokea nianze kusoma Qur-aan nami nilijiuliza hali ninashangaa, kwanini watu wanakwenda bila muongozo kwenye dunia hii hali ya kuwa dalili na mwanga ipo mbele yao."?!

Cat Stephens (Kwa sasa Yusuf Islam

Aliyekuwa Muimbaji wa Uingereza

{Basi yule ambaye Mwenyezi Mungu anataka kumhidi humfungulia kifua chake kwa Uislamu. Na anaye taka apotee hukifanya kifua chake kina dhiki, kimebana, kama kwamba anapanda mbinguni. Namna hivi Mwenyezi Mungu anajaalia uchafu juu ya wasio amini.} [6:125],

Atakaye mpwekesha Mwenyezi Mungu mmoja bila ya kumshirikisha basi mtu huyo atakuwa na moyo uliofunguka na raha na utulivu.

Ama yule aliyempoteza anaufanya moyo wake una dhiki, tabu na kero, Allah atulinde, naye ni mfano wa aliyeamini na kumpwekesha Allah pekee, na yule ambae amemshirikisha Mwenyezi Mungu na kupotea, Mwenyezi Mungu ametoa mfano mwingine; aliposema: {Mwenyezi Mungu amepiga mfano wa mtu mwenye mabwana washirika wanao gombana, na wa mtu mwengine aliye khusika na bwana mmoja tu. Je! Wako sawa katika hali zao? Alhamdulillahi, Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu! Lakini wengi wao hawajui.} [39:29].

https://www.path-2-happiness.com/sw

Mtu mshirikina ni kama vile mtu anamilikiwa na idadi ya watu wenye tabia mbaya nao wanashindana, mmoja anamwambia njoo, na mwingine anamwambia kaa, na mtu wa tatu anamwambia simama; mtu huyu anababaika katika jambo lake hana raha ya kiwiliwili wala hana raha ya dhamira yake au nafsi yake, na mwenye kumpwekesha Allah ni kama vile mtu aliyehusika na bwana mmoja tu, angemwamrisha na kumkataza ni mtu mmoja tu, Je, watu hawa wawili wanalingana?! Alhamdulillah, shukran na himidi ni zake Allah pekee, na kusifiwa kuzuri ni kwake, na kuwa Yeye hapana Mola isipokuwa Yeye tu, ama wale ambao hawafahamu wanaishi maisha ya taabu na migongano ya ndani na yanayosuhubiana nayo miongoni mwa tabu na kero na sononeko na babaiko, mgongano na kujiuwa.

Kujiua na Dini

Wataalamu wawili kutoka katika Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) Dr. Jos Manuel na Mtafiti Alesandra Fishman wameainisha uhusiano kati ya kujiua na Dini anayofuata mtu, matokeo yalikuwa kama ifuatavyo: Katika utafiti wao wa kisayansi uliohifadhiwa katika marejeo ya Umoja wa Mataifa.
A global perspective in theepidemiology of suicide



https://www.path-2-happiness.com/sw

الطريق إلى السعادة
The Path to Happiness

Kuumbwa kwa Ulimwengu na Mwanadamu... Hekima, Kukirimiwa na Lengo

Yaliyomo

Kuumbwa kwa ulimwengu na Mwanadamu... Hekima, Kukirimiwa na Lengo

Je, umewahi kufikiria Umbile la Ulimwengu?!

Hekima ya kuumbwa kwaulimwengu

Kuumbwa na kukirimiwa kwamwanadamu

Mwanamke kukirimiwa sawa na mwanamume

Hekima ya kuumbwa kwa

mwanadamu

Baada ya hapo ewe mwanadamu…

Kuumbwa kwa Ulimwengu na Mwanadamu... Hekima, Kukirimiwa na Lengo

Je, umewahi kufikiria Umbile la Ulimwengu?!

Kwa hakika tafakuri ya Viumbe vya Allah ni moja ya njia nyingi ambazo zinampelekea mtu katika imani, huzidisha yakini kwa mwanadamu, na kumtambulisha kwa ukubwa wa Muumba na upeo wa elimu na hekima yake, Allah Ta'ala Ndie aliyeumba mbingu na ardhi kwa haki, hakuziumba kwa batili wala kwa mchezo wala hakuumba hivi hivi bila ya lengo. Allah Ta'ala amesema: {Mwenyezi Mungu ameumba mbingu na ardhi kwa Haki. Kwa hakika katika hayo ipo Ishara kwa Waumini.}[29:44].

Katika ulimwengu huu kuna viumbe kiasi gani ambao hawahesabiki! Unadhani wameumbwa kwa hekima ipi?!

Katika Ulimwengu huu kuna alama na dalili mbali mbali ambazo zinaonyesha kwa uwazi uwezo wa Allah Ta'ala na elimu mambo leo inaendelea kuvumbua na kutafiti dalili na alama mbali mbali ambazo zina mfanya mwanadamu ahisi utukufu wa Muumba huyu.

Lau mtu akifikiri kwa undani zaidi kwa Ulimwengu huu na yaliyomo katika Viumbe vya Allah atayakinisha ukamilifu wa yakini kuwa Ulimwengu huu

Ewe Mola Wangu!

"Nilipoona baadhi ya picha za anga za hivi karibuni jibu langu la kwanza lilikuwa ni kupiga mayowe nikisema Ewe Mola wangu! Kazi imezaa matunda. Kwa ujumla wake katika umri wangu hicho ni kitu cha kuvutia!!!"

Dr. Paul Murdin

Professor wa Mambo ya Unajimu Chuo Kikuu cha Cambridge

umeumbwa kwa uwezo usio na ukomo kwa ufanisi wa hali ya juu kabisa, na aliyeumba ni Mungu Mwenye hekima, mwenye uwezo, Mjuzi amepima na akaufanyia uzuri kipimo chake.

Inatosha kufahamu kwa kuzingatia ya kuwa ndani ya Ulimwengu huu na mbingu zake na sayari na nyota zake na yaliyomo kama vile ardhi yetu, bahari, mito, ardhi, milima, wanyama, na miti ambayo imeumbwa na Allah na ambayo haikuwepo hapo kabla ili ipate hisia ni kiasi gani uwezo wa Allah, elimu yake na hekima yake, Allah Ta'ala amesema: {Je! Hao walio kufuru hawakuona kwamba mbingu na ardhi zilikuwa zimeambatana, kisha Sisi tukazibabandua? Na tukajaalia kwa maji kila kilicho hai? Basi je, hawaamini? Na tukaweka katika ardhi milima iliyo thibiti ili isiwayumbishe, na tukaweka humo njia pana ili wapate kuongoka. Na tukaifanya mbingu kuwa dari iliyo hifadhiwa, lakini wanazipuuza Ishara zake. Na Yeye ndiye aliye umba usiku na mchana na jua na mwezi, vyote katika anga vinaogelea. } [21:30-33].

Na pindi mwenye akili anapofikiria katika viumbe wa Allah, mtu anakuwa anafahamu kwa elimu ya yakini kuwa yaliyo katika Ulimwengu huu yanamuabudu Mola wake; kila kiumbe chake kinamsabihi kwa himidi zake Allah, Allah Ta'ala amesema: {Viliomo mbinguni na viliomo katika ardhi vinamtakasa Mwenyezi Mungu, Mfalme, Mtakatifu, Mwenye nguvu, Mwenye hikima.}[62:1]

Na kusujudu kwa utukufu wake, Amesema Allah Ta'ala {Je! Huoni kwamba vinamsujudia Mwenyezi Mungu viliomo mbinguni na viliomo katika ardhi, na jua, na mwezi, na nyota, na milima, na miti, na wanyama, na wengi miongoni mwa watu. Na wengi imewastahiki adhabu. Na anaye fedheheshwa na Mwenyezi Mungu hana wa kumhishimu. Hakika Mwenyezi Mungu hutenda apendayo.} [22:18].

Vivyo hivyo, viumbe hivi vinamsabihi Allah Ta'ala na kumswalia, Allah amesema: {Je! Huoni kwamba Mwenyezi Mungu vinamtakasa vilivyomo katika mbingu na ardhi, na ndege wakikunjua mbawa zao? Kila mmoja amekwisha jua Sala yake na namna ya kumtakasa kwake. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyajua wayatendayo.}[24:41],

Hivyo basi muumini ataona kuwa Ulimwengu wote huenda na kutembea kama vile ni msafara mmoja katika muelekeo mmoja kwa Allah, hivyo basi pia atakwenda kwa furaha kwa muelekeo huu mzuri uliobarikiwa na maisha yake na utulivu wa roho yake.

Miongoni mwa dalili za Uungu

"Kuona kwangu sayari yetu ilikuwa ni ishara (maono) ya kiungu."

Edgar Mitchell
Wa sita katika wanaanga waliokwenda mwezini

Huu ni Uumbaji wa Mungu!!

"Kuona jambo hili kutambadilisha mwanadamu, na kumfanya mtu kuthamini viumbe vya Mungu na kumpenda Mungu." Akizungumzia kuhusu Ulimwengu.

James Irwin
Mwanaanga

Mungu Kumkirimu Mwanadamu.

Uislamu ambao ni kanuni ya Mwenyezi Mungu tunauona ukiwa ni wazi katika mazingira yanayotuzunguka; Kwa maamrisho pekee ya Mwenyezi Mungu, milima, bahari, sayari, nyota zinakwenda na kuongoka katika mapito yake (mzunguko wake). Vivyo hivyo kila atom katika ulimwengu huu (hata viumbe visivyokuwa hai) ila mwanadamu amevuliwa (anaondolewa) katika kanuni hii; kwani Mwenyezi Mungu amempa uhuru wa kuchagua; kwa hiyo anaweza kujisalimisha kwa amri ya Allah au akaweka kanuni zake mwenyewe na kwenda katika dini yake ambayo anairidhia, kwa masikitiko njia ya pili ina vizuizi vikubwa."

Deborah Potter

Mwanahabari wa Kimarekani

https://www.path-2-happiness.com/sw

Hekima ya kuumbwa kwa ulimwengu

1. Dalili ya Kumpwekesha Allah Ta'ala.

Kwa hakika Ulimwengu huu mpana na yaliyomo ndani yake katika viumbe na miujiza ni ushahidi mkubwa wa utukufu wa uwezo wa Allah Ta'ala na ukamilifu wa maumbile yake na hii ni dalili ya kumpwekesha Allah Ta'ala, na kuwa hana Mola asiyekuwa yeye wala Mungu asiyekuwa Yeye, Allah Ta'ala amesema: {Na katika Ishara zake ni kuwa kakuumbeni kwa udongo. Kisha mmekuwa watu mlio tawanyika kote kote. Na katika Ishara zake ni kuwa amekuumbieni wake zenu kutokana na nafsi zenu ili mpate utulivu kwao. Naye amejaalia mapenzi na huruma baina yenu. Hakika katika haya bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanao fikiri. Na katika Ishara zake ni kuumba mbingu na ardhi, na kutafautiana ndimi zenu na rangi zenu. Hakika katika hayo zipo Ishara kwa wajuzi. Na katika Ishara zake ni kulala kwenu usiku na mchana, na kutafuta kwenu fadhila zake. Hakika katika haya bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanao sikia. Na katika Ishara zake hukuonyesheni umeme kwa kukutieni khofu na tamaa. Na hukuteremshieni maji kutoka mbinguni, na kwa hayo huifufua ardhi baada ya kufa kwake. Hakika katika hayo zipo Ishara kwa watu wanao zingatia. Na katika Ishara zake ni kuwa mbingu na ardhi zimesimama kwa amri yake. Kisha atakapo kuiteni mwito mmoja tu, hapo mtatoka kwenye ardhi. Na vyake Yeye vilivyo mbinguni na katika ardhi. Vyote vinamt'ii Yeye.} [30:20-26]

Katika aya nyingine amesema: {Sema: Alhamdu Lillahi! Kuhimidiwa ni kwa Mwenyezi Mungu! Na amani ishuke juu ya waja wake alio wateuwa. Je! Mwenyezi Mungu ni bora, au wale wanao washirikisha naye? AU NANI yule aliye ziumba mbingu na ardhi, na akakuteremshieni maji kutoka mbinguni, na kwa hayo tukaziotesha bustani zenye kupendeza? Nyinyi hamna uwezo wa kuiotesha miti yake. Je! Yupo mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Bali hao ni watu walio potoka. Au nani yule aliye ifanya ardhi mahali pa kutua, na akajaalia ndani yake mito, na akaweka milima? Na akaweka baina ya bahari mbili kiziwizi? Je! Yupo mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Bali wengi wao hawajui. Au nani yule anaye mjibu mwenye shida pale anapo mwomba, na akaiondoa dhiki, na akakufanyeni warithi wa ardhi? Je! Yupo mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Ni machache mnayo yazingatia. Au nani yule anaye kuongoeni katika giza la bara na bahari, na akazipeleka pepo kuleta bishara kabla ya rehema zake? Je! Yupo mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Ametukuka Mwenyezi Mungu juu ya wanao washirikisha naye. Au nani anaye uanzisha uumbaji, kisha akaurejesha? Na nani anaye kuruzukuni kutoka mbinguni na kwenye ardhi? Je! Yupo mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Sema: Leteni hoja zenu kama nyinyi ni wasema kweli.} [27:59-64].

https://www.path-2-happiness.com/sw

2. Ulimwengu kudhalilishwa kwa ajili ya Mwanadamu:

Mwenyezi Mungu amemuacha huru mwanadamu na kuabudu vitu; na hivyo kujaalia vyote vilivyomo katika ardhi hii vikiwa vimedhalilishwa kwa ajili ya mwanadamu kama ni fadhila na takrima kwake kutoka kwa Allah peke yake; kwa lengo la kufanikisha uimarishaji wa ardhi, ukhalifa, na zaidi ni kukamilisha utekelezaji wa ibada ndani yake, na kudhalilishwa hapa ina maana mbili: kudhalilishwa kwa ajili ya kumfahamu Allah, fadhila zake, ukarimu na utukufu wake. Na kudhalilishwa kwa maana ya kumkirimu mwanadamu na kunyanyua hadhi yake ukilinganisha na vile vilivyodhalilishwa kwake; Allah Ta'ala amesema: {Na amefanya vikutumikieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi, vyote vimetoka kwake….} [45:13]

Na amesema vile vile Allah mtukufu: {Mwenyezi Mungu ndiye aliye ziumba mbingu na ardhi, na akateremsha maji kutoka mbinguni. Na kwa hayo akatoa matunda kuwa ni riziki yenu. Na akafanya yakutumikieni majahazi yanayo pita baharini kwa amri yake, na akaifanya mito ikutumikieni. Na akalifanya jua na mwezi kwa manufaa yenu daima dawamu, na akaufanya usiku na mchana kwa manufaa yenu. Na akakupeni kila mlicho muomba. Na mkihisabu neema za Mwenyezi Mungu hamwezi kuzidhibiti. Hakika mwanaadamu ni dhaalimu mkubwa, mwenye kuzikufuru neema.} [14:32-34]

Miongoni mwa dalili za Utume.

"Vipi Muhammad (mtu asiyesoma yaliyoandikwa) ambaye amekulia katika jamii ya Jaahiliya amejua miujiza ya Ulimwengu ambayo imeelezwa na Qur-aan Tukufu. Ambayo hadi hivi sasa sayansi inaendelea kuyatafiti?! Hapana shaka basi maneno haya kuwa ni maneno Mwenyezi Mungu Aliyetukuka.

Deborah Potter
Mwanahabari wa Kimarekani



3. Huenda Mkayakinisha kukutana na Mola wenu:

Hakika katika umbile la mbingu na ardhi (tuache suala la kuumbwa kwa mwanadamu) ni uthibitisho ulio wazi kuhusu ufufuo baada ya kifo, je, haikuwa suala la kurejesha maumbile ni rahisi na mepesi zaidi kuliko kuumba mara ya kwanza?! Allah Ta'ala amesema: {Na Yeye ndiye anaye anzisha uumbaji, kisha ataurudisha mara nyengine. Na jambo hili ni jepesi zaidi kwake….}[30:27]

Bali kwa hakika kuumbwa mbingu na ardhi ni kukubwa kuliko maumbile ya mwanadamu, Allah Ta'ala amesema: {Bila ya shaka kuumba mbingu na ardhi ni kukubwa zaidi kuliko kuwaumba watu. Lakini watu wengi hawajui.} [39:57]

Na Allah Mtukufu akasema: {Mwenyezi Mungu aliye ziinua mbingu bila ya nguzo mnazo ziona, ametawala kwenye Ufalme wake, na amefanya jua na mwezi yamt'ii, kila kimoja kinakwenda kwa kiwango maalumu. Anayapanga mambo, na anazipambanua Ishara ili mpate kuwa na yakini kukutana na Mola wenu Mlezi.} [13:2].

Haki ni Moja

"Kuangalia aina hii ya kiumbe wala usimuamini Mwenyezi Mungu hilo kwangu mimi ni jambo lisilowezekana ….Hili limezidisha imani yangu. Natamani pawepo na maneno yenye kuelezea tukio hili.

John Glenn

Mwanaanga wa kwanza wa Kimarekani



Uko wapi ndani ya Ulimwengu huu.

"Picha hii ni ya mkusanyiko mkubwa wa sayari (galaxies) Sehemu yake ndogo huwakilisha sayari na njia zake ni zaidi ya 1,000,000,000,000 ya jua. Na jua ni kubwa kuliko ardhi kwa mara 1,300,000, na ardhi ni kubwa kuliko nyumba yako (kwa mfano ukubwa wa nyumba yako ni mita 500)kwa mara 1,020,144,000,000 na nyumba yako ni kubwa kuliko wewe mwenyewe kwa mara ngapi."?!'

https://www.path-2-happiness.com/sw



Tone katika Bahari

"Hadi hivi sasa nyota kubwa iliyoumbuliwa ni VY Canis Majoris iko mbali nasi kwa masafa ya miaka elfu tano ya mwanga na ni kubwa kuliko jua kwa 9,261, 000,000 yaani 9 Bilioni na mara 261 milioni!! Na jua ni kubwa kuliko ardhi yetu kwa mara 1,300,000.

Kuumbwa na kukirimiwa kwa mwanadamu

Pamoja na utukufu wa umbile la mbingu na ardhi isipokuwa ni kwamba Mwenyezi Mungu amemdhalilishia hilo mwanadamu na kujaalia vitu hivyo kudhalilika kwake: Pamoja na utukufu wa umbile la mbingu na ardhi isipokuwa ni kwamba Mwenyezi Mungu amemdhalilishia hilo mwanadamu na kujaalia vitu hivyo kudhalilika kwake: {Na amefanya vikutumikieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi, vyote vimetoka kwake….} [45:13];

Na hilo ni kwa kumkirimu yeye mwanadamu na kumfadhilisha yeye kuliko viumbe vingine vyote, Allah Ta'ala amesema: {Na hakika tumewatukuza wanaadamu, na tumewapa vya kupanda nchi kavu na baharini, na tumewaruzuku vitu vizuri vizuri, na tumewafadhilisha kwa fadhila kubwa kuliko wengi miongoni mwa tulio waumba.} [17:70]

Allah amemuumba mwanadamu na kumjulisha kisa cha kuumbwa kwa Adam na kukirimiwa, kisha kumteremsha kutoka peponi kushuka ardhini kwa wasiwasi wa shetani na dhambi zake, kisha kutubia kwake, Allah amesema: {Na hakika tulikuumbeni, kisha tukakutieni sura, kisha tukawaambia Malaika: Msujudieni Adam. Basi wakasujudu isipo kuwa Iblisi, hakuwa miongoni mwa walio sujudu. Mwenyezi Mungu akasema: Nini kilicho kuzuia kumsujudia nilipo kuamrisha? Akasema: Mimi ni bora kuliko yeye. Umeniumba kwa moto, naye umemuumba kwa udongo. Akasema: Basi teremka kutoka humo! Haikufalii kufanya kiburi humo. Basi toka! Hakika wewe u miongoni mwa walio duni. Akasema: Nipe muhula mpaka siku watakapo fufuliwa. Akasema: Utakuwa miongoni mwa walio pewa muhula. Akasema: Kwa kuwa umenihukumia upotofu, basi nitawavizia katika Njia yako Iliyo Nyooka. Kisha

nitawazukia mbele yao na nyuma yao na kuliani kwao na kushotoni kwao. Wala hutawakuta wengi wao wenye shukrani. Akasema: Toka humo, nawe umekwisha fedheheka, umekwisha fukuzwa. Hapana shaka atakaye kufuata miongoni mwao, basi nitaijaza Jahannam kwa nyinyi nyote. Na wewe, Adam! Kaa wewe na mkeo katika Bustani hii, na kuleni humo mpendapo. Wala msiukaribie mti huu, mkawa katika wale walio dhulumu. Basi Shet'ani aliwatia wasiwasi ili kuwafichulia tupu zao walizo fichiwa, na akasema: Mola Mlezi wenu hakukukatazeni mti huu ila msije mkawa Malaika, au msije mkawa katika wanao ishi milele. Naye akawaapia: Kwa yakini mimi ni miongoni wa wanao kunasihini. Basi akawateka kwa khadaa. Walipo uonja ule mti, tupu zao zilifichuka na wakaingia kujibandika majani ya Bustanini. Mola wao Mlezi akawaita: Je, sikukukatazeni mti huo, na kukwambieni ya kwamba Shet'ani ni adui yenu wa dhaahiri? Wakasema: Mola wetu Mlezi! tumejidhulumu nafsi zetu, na kama hutusamehe na kuturehemu, hakika tutakuwa katika wenye kukhasirika. Akasema: Teremkeni! Mtakuwa nyinyi kwa nyinyi maadui. Na kwenye ardhi itakuwa ndio makao yenu na starehe yenu mpaka ufike muda. Akasema: Humo mtaishi, na humo mtakufa, na kutoka humo mtatolewa.} [7:11-25]

Mwenyezi Mungu amempa mwanadamu sura nzuri kabisa, kisha akampulizia roho yake, hivyo mwanadamu akatokea katika umbile zuri kabisa anasikia na kuona na kutembea na kuzungumza: {…Basi ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbaji.} [23:14]

Na akamfundisha kila anachohitaji kukifahamu na akampa sifa na vipawa ambavyo hakumpa kiumbe mwingine kama vile: Akili, Elimu, ubainifu, kuongea, umbile, sura nzuri, umbile lililokirimiwa na kiwiliwili cha kati na kati, na kuweza kupokea elimu mbalimbali na kutumia dalili kwa fikra na kuongoza katika tabia njema na sifa nzuri kabisa na akamkirimu na kumfadhilisha kuliko viumbe vingi; katika mandhari ya kukirimiwa hivi kwa mwanadamu iwe kwa mwanamume au mwanamke.

https://www.path-2-happiness.com/sw

Binadamu wote ni sawa.

"Watu wote huzaliwa huru wakiwa sawa katika utukufu na haki, na wamepewa akili na dhamira. Na ni juu yao kuamiliana baadhi yao kwa wengine kwa roho ya udugu.

Mada ya kwanza katika tangazo la kimataifa la haki za binadamu.

-Hakika Allah amemuumba mwanadamu kwa mkono wake tokea kuumbwa kwake wakati wa kuumbwa kwa Adam ('Alayhi Salaam); na huu ni utukufu na kukirimiwa hakuna utukufu zaidi ya huu; Allah Ta'ala amesema:

{Mwenyezi Mungu akamwambia: Ewe Iblisi! Kipi kilicho kuzuia kumt'ii yule niliye muumba kwa mikono yangu? Je! Umejiona mkubwa, au umekuwa katika wakuu kweli?} [38:75]

-Hakika Allah Ta'ala amemuumba mwanadamu katika umbile zuri; Allah amesema, {Bila ya shaka tumemuumba mtu kwa umbo lilio bora kabisa.} [95:4]

Na akasema vile vile: {…na akakupeni sura, na akazifanya nzuri sura zenu. Na marudio ni kwake} [64:3].

-Mwenyezi Mungu Mtukufu amemkirimu mwanadamu huyu wa kuamrisha Malaika wake kumsujudia Adam, Baba wa wanadamu, aliposema Allah Ta'ala: {Na pale tulipo waambia Malaika: Msujudieni Adam. Wakamsujudia isipo kuwa Iblisi….} [17:61].

-Allah Ta'ala amemkirimu mwanadamu huyu na akamneemesha kwa akili, kufikiria, kusikia, kuona na hisia nyingine za fahamu, Allah Ta'ala amesema: {Na Mwenyezi Mungu amekutoeni matumboni mwa mama zenu, hali ya kuwa hamjui kitu, na amekujaalieni masikio na macho na nyoyo ili mpate kushukuru.} [16:78].

-Allah Ta'ala alimpulizia roho; na hapo ndipo daraja lake likawa la juu, Allah akasema: {Na nitakapo mkamilisha na kumpulizia roho inayo tokana nami, basi muangukieni kwa kumt'ii.} [38:72]

https://www.path-2-happiness.com/sw

Na huu ni ukarimu mkubwa alioupata mwanadamu; na ndipo ilipopasa mwanadamu kuheshimiwa kama mwanadamu, sasa iweje mwanadamu huyu amfanyie uadui yule aliyempulizia roho Allah Ta'ala.?!!

Allah Ta'ala akamfanya kuwa ni Khalifa katika ardhi, na sio Malaika au Jini; Allah akasema: {Na pale Mola wako Mlezi alipo waambia Malaika: Mimi nitamweka katika ardhi Khalifa (mfwatizi), wakasema: Utaweka humo atakaye fanya uharibifu humo na kumwaga damu, hali sisi tunakutakasa kwa sifa zako na tunakutaja kwa utakatifu wako? Akasema: Hakika Mimi nayajua msiyo yajua.} [2:30]

Na huu ni utukufu mkubwa ambao Malaika hawakuupata ambao hawamuasi Allah alichowaamuru, na ambao daima wapo katika kumdhukuru, kumtakasa na kumtukuza Allah Ta'ala.

Ujumbe wetu

"Allah ametutuma kuwatoa watokao kwenye kuabudu watu kuelekea kwenye kumuabudu Allah. Na kutoka katika mashaka ya dunia kuelekea kwenye upana wake, na kutoka kwenye dhuluma ya dini kwenda kwenye uadilifu wa Uislamu"

Ribi'l bin 'Amir

Miongoni mwa sahaba wa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam)

-Allah Ta'ala amemdhalilishia mwanadamu huyu yote yaliyomo hapa ulimwenguni kwa mbingu zake na ardhi yake, na yaliyomo baina yake na ndani yake katika jua, mwezi, nyota na sayari. Allah Ta'ala amesema: {Na amefanya vikutumikieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi, vyote vimetoka kwake. Hakika katika hayo zimo Ishara kwa watu wanao fikiri. } [45:13],

-Kuwa Allah Ta'ala amemkomboa mwanadamu na amemuacha huru na utumwa wowote kwa kiumbe chochote (kingine) kadiri ya ubora wake au ukubwa wake, na hicho ni kilele cha uhuru aliokuwa nao mwanadamu; kwa jinsi alivyohamishwa kutoka katika kunyenyekea kwa mwanadamu na kumuabudu mwanadamu mwenzake hadi kumuabudu Allah Ta'ala, na kuabudu huku kwa ajili ya Allah ndio kilele cha uhuru dhidi ya kumuabudu asiyekuwa Yeye. Na hii ndio maana Allah akakataa kuwepo kwa wakala baina yake na waja wake; kwani kuna baadhi ya watu wamejiwekea na kuzusha wakala baina ya mwanadamu na Mola wake na wengine kwa hilo wamepewa

sifa ya Uungu. Allah amemkirimu mwanadamu kwa sababu hakuna wakala baina yake na Mola wake, Allah amesema: {Wamewafanya makuhani wao na wamonaki wao kuwa ni marabi badala ya Mwenyezi Mungu, na pia Masihi bin Maryamu. Na wala hawakuamrishwa isipo kuwa wamuabudu Mungu Mmoja, hapana mungu ila Yeye. Subhanahu, Ametakasika na hayo wanayo mshirikisha nayo.} [9:31].

-Kumkomboa mwanadamu kutokana na khofu ya mustakbali na kukata tamaa, nayo ni kwa kupitia kuamini kwa hukumu (majaliwa) na kudura pamoja na kufuata sababu zote za kimaisha za kimaada; hivyo basi imani ya majaliwa na kudura ndio inayomfanya mwanadamu muumini katika hali ya usalama na amani, na katika hali ya utukufu na hisia ya karama na kuondokana na kero na huzuni au masikitiko yaliyopita madamu hakufanya mapungufu katika kuchukua na kutumia sababu mbali mbali. Kwa sababu yote ni kutoka kwa Allah, Allah Ta'ala amesema¨ {Hautokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila umekwisha andikwa katika Kitabu kabla hatujauumba. Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi.} [57:22],

Imani hii inamfanya mwanadamu kuwa katika mizani nzuri ya nafsi na utulivu mkubwa wa kweli; ambapo misiba haimuathiri wala haimfanyi kuwa muoga au mwenye huzuni kama ambavyo neema mbalimbali na furaha haimfanyi kuwa ni jeuri, mwenye kujiona na kujivuna

-Akili ya mwanadamu kuheshimiwa; Allah Ta'ala ameipa thamani kubwa sana akili ya mwanadamu pamoja na fikra zake Ameamuru kuangalia na kuchukua mazingatio, na kajaalia swala la kufikiria kuhusu kuumbwa kwa mbingu na ardhi na kusimamisha hoja na dalili mbali mbali kuwa ni faradhi; Allah Ta'ala amesema: {Sema: Angalieni yaliomo mbinguni na kwenye ardhi! Na Ishara zote na maonyo hayawafai kitu watu wasio amini.} [10:101]

Hakuna mtu wa Kati

"Kuna jambo muhimu: Nalo kutokuwepo mtu wa kati baina ya mja na Mola wake. Na hili ndilo walilolipata wenye akili za kitendaji."

Etienne Denier

Mchoraji na Mwanafikra wa Kifaransa

Kadhalika Allah ameamuru akili ya mwanadamu iheshimiwe, kutunzwa, kuangaliwa vizuri, kuifanyisha kazi, kuishughulisha, na kutoyagandisha kwa njia ya kufuata mambo kibubusa na kutumia kasumba tu; Hakuna kukalifishwi ila kwa kutumia akili, kama vile ambavyo Mwenyezi Mungu alivyofanya akili ya mwanadamu kuwa ndio dalili ya kuwepo kwake Yeye Allah na hoja ya upweke wake; bali Allah amewataka wanadamu warejee kwenye akili pale wanapotofautiana; Allah Ta'ala amesema: {…Sema: Leteni ushahidi wenu kama nyinyi ni wasema kweli} [2:111]

Na akaikomboa akili kutokana na kila aina ya upotofu, ushirikina, udajali na kutegemea majini na mfano wa hayo.

-Kuhakikisha na kuthibitisha kuwa kila mwanadamu ana majukumu (wajibu) na atahesabiwa kwa matendo yake, wala hakuna uhusiano wowote na matendo ya mtu mwingine, Allah Ta'ala amesema: {Na mbebaji habebi mzigo wa mwingine…} [35:18]

Na kukirimiwa huku kwa mwanadamu ndani ya Qur-aan; kunafuta ile fikra ya dhambi ya asili, na kumkomboa na kumsafisha mwanadamu kutokana na mazito yake.

Mwanamke kukirimiwa sawa na mwanamume

Kukirimiwa mwanadamu hakukuishia tu kwa mwanamume bila ya mwanamke, au kwa jinsia moja bila ya nyingine, asili ya mwanamke ni sawa na ya mwanamume katika kukirimiwa na kutukuzwa sawa kwa sawa: {…Nao wanawake wanayo haki kwa Sharia kama ile haki iliyo juu yao….} [2:228]

Allah Mtukufu akasema: {Na Waumini wanaume na Waumini wanawake wao kwa wao ni marafiki walinzi….} [9:71],

Wala mwanamke hatofautiani kabisa na mwanamume katika suala la malipo ya akhera, Allah amesema: {Mola Mlezi wao, akayakubali maombi yao akajibu: Hakika sipotezi kazi ya mfanya kazi miongoni mwenu, akiwa mwanamume au mwanamke, kwani ni nyinyi kwa nyinyi….} [3:195],

Na katika aya nyingine, Allah kasema: {Na anaye fanya mema, akiwa mwanamume au mwanamke, naye ni Muumini - basi hao wataingia Peponi wala hawatadhulumiwa hata kadiri ya tundu ya kokwa ya tende.} [4:124]

Allah amemkirimu mwanamke kama mwanadamu pindi alipo mzingatia kuwa ni mwenye kukalifishwa mwenye majukumu

Sawa kwa Sawa

"Chuo kikuu cha Oxford hakijatoa haki sawa baina ya wanafunzi wa kike na wa kiume (katika Michezo na Umoja wa wanafunzi); isipokuwa kwa uamuzi uliotolewa tarehe 21 Julai mwaka 1964."





Muujiza ya kweli

"Ikiwa sisi tutalinganisha misingi ya Qur'ani na misingi ya jamii zote zilizopita; basi tutakuta kuwa Qur-aan ndio itakayokuwa imerikodi maendeleo ndani yake yasiokuwa na ubishi, na haswa haswa kwa munasaba wa Athens na Roma; ambapo mwanamke alikuwa na mapungufu kwa sura thabiti."

Roger Garoudye

Mwanafalsafa wa Kifaransa

kamili kama alivyo mwanaume na ni mwenye kulipwa thawabu na kuadhibiwa kama alivyo mwanaume, hata jukumu la mwanzo kabisa ambalo Mwenyezi Mungu amempa mwanadamu lilikuwa la wote kwa pamoja; yaani mwanamke na mwanaume; pale Allah alipowaambia wanadamu wa mwanzo ambao ni Adamu na mke wake: {Na tulisema: Ewe Adam! Kaa wewe na mkeo katika Bustani, na kuleni humo maridhawa popote mpendapo, lakini msiukaribie mti huu tu; mkawa katika wale walio dhulumu.} [2:35]

Kama ambavyo Allah hakumbebesha mzigo mwanamke kuwa ndiye aliyekuwa sababu ya kumtoa Adam peponi na tabu walizokuwa wakipata au kuendelea kuzipata vizazi vyao baada yao kama ilivyo katika dini nyinginezo, bali Allah amemtaja Adam kuwa ndie mhusika mkuu: {Na hapo zamani tuliagana na Adam, lakini alisahau, wala hatukuona kwake azma kubwa.} [20:115] {Basi wakaula wote wawili, na uchi wao ukawadhihirikia na wakaanza kujibandika majani ya Bustani. Na Adam akamuasi Mola wake Mlezi, na akapotea njia. Kisha Mola wake Mlezi akamteuwa, naye akamkubalia toba yake, naye akamwongoa. } [20:121-122].

Mwanamke katika Sheria za mwanadamu

"Huko Roma kulikuwa na mkutano mkubwa, ukitafiti mambo ya mwanamke. Maamuzi yakatolewa kuwa mwanamke hana roho (nafsi) na kwa sababu ya dosari hii hatarithi maisha ya akhera. Kadhalika mwanamke ni uchafu hapaswi kula nyama, wala kucheka, bali hata kuzungumza, na muda wake wote autumie katika swala, ibada na utumishi. Wakamkataza kufanya yote hayo wakamwekea kufuli la chuma mdomoni mwake; ikawa mwanamke katika familia za juu na za chini anatembea njiani na akienda na kurudi nyumbani kwake na huku mdomoni mwake kukiwa na kufuli. Hii ni mbali na mateso mengine ya kiwiliwili ayapatayo mwanamke huyu kwa kumzingatia kuwa yeye ni nyenzo ya upotoshaji anayotumia shetani kuharibu nyoyo."

Mwanamke mbele yao

Katika sheria za kale za Kihindi tunasoma: Maradhi, mauti, moto, sumu, nyoka na moto vyote hivyo ni bora kuliko mwanamke. Haki ya mwanamke ya kuishi huisha kwa kuisha haki ya mumewe ambae ndie bwana na mmiliki wake. Akiona maiti yake inaungua nae hujitupa kwenye moto ule, vinginevyo ni haki yake kupata laana ya milele.

Hivyo basi katika utu na ubinadamu ni kuwa mwanaume analingana na mwanamke sawa kwa sawa, Allah Ta'ala amesema: {Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamngu zaidi katika nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye khabari. } [49:13]

Hivyo ni kuwa mwanaume anashirikiana na mwanamke na wanafanana au wako sawa kwa sawa katika mambo yafuatayo:-

-Maendeleo ya mtu katika haki maalum za kumiliki: Haiba ya mwanamke ni yenye hadhi na kuheshimiwa kisheria, Allah amempa haki sawa na mwanaume katika Majukumu na utekelezaji wake, amemthibitishia haki yake ya kutumia na kuingia katika mkataba yote; kama haki ya kuuza, haki ya kununua na mfano wake, na haki zote hizi ni za wajibu kutekeleza bila ya kifungo chochote au kizuizi ambacho kitazuia uhuru wake wa kutekeleza, ila vizuizi vile ambavyo vina mzuia mwanaume vile vile, Allah Tabaaraka amesema: {…Wanaume wana fungu katika walio vichuma, na wanawake wana fungu katika walio vichuma…} [4:32],

Kadhalika amempa haki ya kurithi, Allah Ta'ala amesema: {Wanaume wana sehemu katika wanayo yaacha wazazi na jamaa walio karibia. Na wanawake wanayo sehemu katika waliyo yaacha wazazi na jamaa walio karibia. Ikiwa kidogo au kingi. Hizi ni sehemu zilizo faridhiwa.} [4:7]

Na akamfanya mwanamke mbele ya sheria sawa na mwanaume anapopatia au kukosea; Allah amesema: {Na mwizi mwanamume na mwizi mwanamke, ikateni mikono yao, hayo ni malipo ya waliyo yachuma, ndiyo adhabu ya mfano itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima.} [5:38].

-Malipo ya Akhera; Allah amesema: {Mwenye kutenda mema, mwanamume au mwanamke, naye akawa ni Muumini, tutamhuisha maisha mema; na tutawapa ujira wao kwa bora ya waliyo kuwa wakiyatenda.} [16:97]

Urafiki na kunusuriana. Allah amesema: {Na Waumini wanaume na Waumini wanawake wao kwa wao ni marafiki walinzi. Huamrisha mema na hukataza maovu, na hushika Sala, na hutoa Zaka, na humt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hao Mwenyezi Mungu atawarehemu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mtukufu Mwenye nguvu, Mwenye hikima.} [9:72].

Ni Jeuri gani hii?!!!

"Mwanamke kwa mwanamume ni kama mtumwa kwa bwana wake. Au ni kama vile kazi za mikono ukilinganisha na kazi za akili. Au ni kama mfano wa Mshenzi na Myunani. Mwanamke ni mwanamume mpungufu, ameachwa amesimama katika daraja la chini kwenye ngazi ya maendeleo."

Aristotle

Mwanafalsa wa Kigiriki

Mwanamke wa Kifaransa

"Huko Ufaransa moja katika majimbo yake kulifanyika mkutano mwaka 586 mazungumzo yalihusu mwanamke: Je, ni mwanadamu au sio mwanadamu? Hitimisho lilikuwa ni uamuzi wa waliohudhuria kuwa mwanamke ni binadamu, lakini ameumbwa kumuhudumia mwanamume, katika mwezi wa Februari mwaka 1938 ilitolewa kanuni ya kufuta kanuni zingine zilizokuwa zikimkataza mwanamke wa Kifaransa katika baadhi ya matumizi ya mali (baada ya hapo kuruhusu) na kwa mara ya kwanza katika historia ya mwanamke wa Kifaransa aweze kufungua akaunti kwa jina lake katika mabenki.

Haki za Mwanamke Zimemezwa

“Nikageuka, na moyo wangu ulikazwa katika kujua na kupeleleza, na kuitafuta hekima, na maana ya mambo yaliyoko; ili nifahamu ya kuwa uovu ni upumbavu, na upumbavu ni wazimu. Nami nimeona lililo na uchungu kupita mauti; yaani, mwanamke ambaye moyo wake ni mitego na tanzi, na mikono yake ni kama vifungo.” (Mhubiri 7:26

Kitabu Kitakatifu- Agano la kale



Sawa kwa Sawa

“Katika kivuli cha Uislamu mwanamke amerejesha uhuru wake, na akapata hadhi ya juu: Uislamu unawazingatia wanawake kuwa ni ndugu walio sawa na wanaume, na kila mmoja anamkamilisha mwingine, Uislamu umelingania taaluma ya mwanamke na kumzawadia elimu na utamaduni. Kwa hiyo ukampa haki ya kumiliki na uhuru wa kutumia anachomiliki, kama ambavyo umempa haki ya kuvunja mkataba wa ndoa na uhuru wa kufikiri na kujieleza.”

Mona Cluskey

Mwanadiplomasia wa Kijerumani

«Yamekuja maamrisho ya kumhurumia mwanamke na kumfanyia wema; Allah ameharamisha wanawake kuuwawa katika vita, na akaamrisha kukaa pamoja na wanawake wenye hedhi na kufanyia nao uwakala na wakati huo Mayahudi walikuwa wanakataa hilo na kuwatenga na kuwadharau wala hawafanyi nao uwakala hadi watoharike, mwanamke katika zama za Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) walikirimiwa kwa hali ya juu pindi aliposema: “Mbora wenu ni mbora wenu katika familia yake, na mimi ni mbora wenu kwa familia yangu.» (Imepokewa na Tirmidhi, na akasema hadithi hii ni Hassan Sahihi).

«Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) alikasirika pale mwanamke alipopigwa katika zama zake, na kusema: “Mmoja wenu anampiga mke wake kipigo cha mtumwa, kisha jioni humkumbatia» (Al-Bukhari).

«Na wakati kundi la wanawake lilipokuja kuwashitaki waume zao kwa Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasallam); Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) alisema: “Wanawake wengi wamekuja katika nyumba ya Muhammad kuwashitakia waume zao, wao (waume) hawakuwa bora kwao.» (Abu Dawuud).

https://www.path-2-happiness.com/sw

Mwanamke amepewa ambayo hajapewa mwanaume; Allah ameamrisha mama afanyiwe wema zaidi kuliko baba wakati mmoja mtu mmoja alikuja kwa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) akasema: «Ewe Mtume wa Allah ni nani mwenye haki ya kusuhubiana nae –katika riwaya nyingine wema –Mtume akasema: Mama yako, akauliza: Kisha nani? Akasema: Mama yako, akauliza: Kisha nani? Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) akasema: Baba yako.» (Al-Bukhari na Muslim).

Na hivyo Mtume kuyafanya malezi ya watoto wa kike yana ujira mkubwa kuliko malezi ya watoto wa kiume; Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) amesema: «Atakayejaribiwa (kuwa) na wasichana hawa kisha akawafanyia wema, watakuwa sitara yake na moto» (Bukhari na Muslim)

Na akaseme tena Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam):

«Ewe Mola kwa hakika mimi nasikitishwa (kwa kutotolewa) haki za wanyonge wawili; yatima na mwanamke» (Hadithi Hassan, imepokewa na An-Nasai kwa sanad nzuri)

Sheria za Mwanadamu zinadhulumu na ni jeuri

"Mfalme Henry wa nane alitoa kanuni ya kuharamisha mwanamke kusoma kitabu kitakatifu. Kama ambavyo mwanamke alikuwa akihesabiwa katika Sheria za jumla za Kiingereza katika mwaka 1850 kuwa si katika raia wake wala hawakuwa na haki zao binafsi, wala hata haki ya kumiliki nguo zao wala katika mali zao walizopata kwa jasho lao."

Mfalme Henry wa Nane

HEKIMA YA KUUMBWA KWA MWANADAMU

Mwanadamu huyu ambaye Allah amemdhalilishia kila kitu katika Ulimwengu huu na kumkirimu yeye peke yake na kuwaacha viumbe wengine, Allah amemuumba kwa hekima kubwa sana; Allah ameepukana na mchezo na ubatili, Allah amesema: {Hakika katika kuumbwa mbingu na ardhi na kukhitalifiana usiku na mchana ziko Ishara kwa wenye akili, Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima na wakikaa kitako na wakilala, na hufikiri kuumbwa mbingu na ardhi, wakisema: Mola wetu Mlezi! Hukuviumba hivi bure. Subhanaka, Umetakasika! Basi tukinge na adhabu ya Moto.} [190-191]

Kadhalika Allah amezungumzia kuhusu dhana potofu ya makafiri: {Na hatukuziumba mbingu na ardhi na viliomo ndani yao bure. Hiyo ni dhana ya walio kufuru. Ole wao walio kufuru kwa Moto utao wapata.} [38:27]

Allah hakumuumba mwanadamu kwa ajili ya kula, kunywa na kuzaa tu, na kwa mfano huo wawe sawa na wanyama, bali Allah Ta'ala amemkirimu na kumfadhilisha mwanadamu kuliko wengi aliowaumba lakini watu wengi wamekataa na wamekufuru; hivyo wakajifanya hawajui au kukataa hekima ya kweli ya kuumbwa kwao, hamu yao kubwa ikawa ni kustarehe kwa matamanio ya kidunia, na maisha ya watu hawa ni kama vile maisha ya wanyama, bali duni zaidi kuliko wanyama, Allah Ta'ala amesema: {…Na walio kufuru hujifurahisha na hula kama walavyo wanyama, na Moto ndio makaazi yao.} [47:12]

Katika aya zingine Allah amesema: {Waache wale, na wastarehe, na iwazuge tamaa. Watakuja jua.} [15:3]



Kwa Mungu

"Kwa hakika dini na sayansi hupigana katika vita moja dhidi ya shaka, kupinga (dini) na uzushi na sauti yao moja katika vita hivi ni daima itakuwa: Tuelekee kwa Mwenyezi Mungu."

Marx Planck

Mwanzilishi wa nadharia ya Kwanta (Quantum)

Na: {Na tumeiumbia Jahannamu majini wengi na watu. Wana nyoyo, lakini hawafahamu kwazo. Na wana macho, lakini hawaoni kwayo. Na wana masikio, lakini hawasikii kwayo. Hao ni kama nyama howa, bali wao ni wapotofu zaidi. Hao ndio walio ghafilika.} [7:179].

Watu wote wanalazimika kuamini kuwa viungo vyao vimeumbwa kwa hekima, huu ni uoni wa mazingatio kwa mfano masikio kwa ajili ya kusikilizia, na kadhalika…Je, inawezekana sasa viungo vya mwanadamu vikaumbwa kwa hekima halafu mwanadamu mwenyewe akaumbwa bila maana? Au ni kuwa haridhiki kumuitikia Mola wake ambaye amemuumba alipomjulisha hekima ya kuumbwa kwake?!

Hivyo basi ni kwa nini Allah ametuumba? Na kwa nini alitukirimu na kutudhalilishia kila kitu? Ametujulisha hilo Subhaanahu; Allah amesema: {Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi. } [51:56],

Na Allah Mtukufu akasema vile vile: {AMETUKUKA ambaye mkononi mwake umo Ufalme wote; na Yeye ni Mwenye uweza juu ya kila kitu. Ambaye ameumba mauti na uhai ili kukujaribuni ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi. Na Yeye ni Mwenye nguvu na Mwenye msamaha.} [67: 1-2],

Na kinachofahamika kwa watu wenye akili ni kuwa mwenye kutengeneza kitu ndiye mwenye uwezo wa kukielezea hekima yake kuliko mtu mwingine, na kwa Mwenyezi Mungu kuna mifano mikubwa, kwani yeye ndiye aliyemuumba mwanadamu, naye anajua zaidi hekima ya kuumbwa kwake. Ibada hapa ufahamu wake ni mpana mno, mkubwa kuliko Swala, Funga, bali inaingia ndani yake

Hoja yenye nguvu

"Ni vigumu kwa mwanadamu kuleta taswira ya mwanzo wa uhai au kuendelea kwake bila ya kuwepo nguvu yenye kuumba yenye kutawala. Na mimi ninaamini kuwa Wanafalsafa katika tafiti zao za kifalsafa kuhusu maisha wamefumbia macho hoja yenye nguvu kuhusiana na mambo yalio katika Nidhamu (utaratibu) wa ulimwengu huu

Magnus Maclees

Mwanachama wa Chama cha Wanasayansi Uingereza

kuimarisha ardhi yote, Allah Ta'ala anasema: {…Yeye ndiye aliye kuumbeni katika ardhi, na akakuwekeni humo. Basi mwombeni msamaha, kisha mtubu kwake. Hakika Mola wangu Mlezi yupo karibu, anaitikia maombi.} [12:61]

Na maisha yote ya mwanadamu ni ibada kwake Allah amesema: {Sema: Hakika Sala yangu, na ibada zangu, na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote. Hana mshirika wake. Na hayo ndiyo niliyo amrishwa, na mimi ni wa kwanza wa Waislamu.} [6:162-163].



Ibada ni ufahamu mpana

Amesema Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) «Ikisimama kiama na katika mkono wa mmoja wenu kuna mche basi na aoteshe.» (Ahmad). Wakauliza: Ewe Mtume wa Allah Je, mmoja wetu atayaendea matamanio yake kisha atakuwa na ujira? Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) akasema: «Je unaonaje kama angeyaweka katika haramu, Je atapata madhambi? Vivyo hivyo akiweka katika halali atapata nayo ujira.» (Muslim).

Hadithi tukufu

https://www.path-2-happiness.com/sw

BAADA YA HAPO EWE MWANADAMU…

Ikiwa Ulimwengu huu wote umedhalilishwa kwa ajili yako na dalili mbali mbali, alama zake na ushahidi mbele ya macho yako zenye kushuhudia kuwa: Hapana Mola apasaye kuabudiwa ila Allah Peke Yake hana mshirika, na pindi ujuapo Ewe mwanadamu ya kuwa ufufuo kwako na maisha yako na kufufuliwa baada ya kufa kwako ni jepesi mno kuliko kuumbwa kwa mbingu na ardhi, na ya kuwa Allah Ta'ala amekuumba kwa umbo lililo bora, na akakukirimu kwa takrima kubwa, na akakudhalishia Ulimwengu wote kwa ajili yako, sasa ni nini kikudanganyacho na Mola wako Mtukufu (hata ukamuasi)?! Allah amesema: {Ewe Mwanaadamu! Ni nini kikudanganacho na Mola wako Mtukufu Aliyekuumba.} [82:6-8]

Mwishowe wewe ni mwenye kukutana na Mola wako, Allah amesema: {Ewe mtu! Hakika wewe unajikusuru kwa juhudi kumwendea Mola wako Mlezi, basi utamkuta. Ama atakaye pewa daftari lake kwa mkono wa kulia, Basi huyo atahisabiwa hisabu nyepesi, Na arudi kwa ahali zake na furaha. Na ama atakaye pewa daftari lake kwa nyuma ya mgongo wake, Basi huyo ataomba kuteketea. Na ataingia Motoni. } [84:6-12]

Nenda katika njia ya furaha ya duniani na Akhera kwa maisha kwa lengo na hekima ya kuumbwa kwako, na hapo ndipo utakapopata furaha kwa ajili ya maisha yako, na utapata utulivu na kufurahia kukutana na Mola wako baada ya kifo chako.

Ulimwengu wote upo katika kumuabudu Mola wake, viumbe wake wote wanamsabihi na kumhimidi Mola wao, Allah Ta'ala amesema: {…Viliomo mbinguni na viliomo katika ardhi vinamtakasa Mwenyezi Mungu…} [62:1]

Na vinasujudu kwa ukubwa wake: {Je! Huoni kwamba vinamsujudia Mwenyezi Mungu viliomo mbinguni na viliomo katika ardhi, na jua, na mwezi, na nyota, na milima, na miti, na wanyama, na wengi miongoni mwa watu. Na wengi imewastahiki adhabu. Na anaye fedheheshwa na Mwenyezi Mungu hana wa kumhishimu. Hakika Mwenyezi Mungu hutenda apendayo.} [22:18].

Bali viumbe vyote hivi vinaswali kwa ajili ya Mola wake kwa swala inayonasibiana nao, Allah amesema: {Je! Huoni kwamba Mwenyezi Mungu vinamtakasa vilivyomo katika mbingu na ardhi, na ndege wakikunjua mbawa zao? Kila mmoja amekwisha jua Sala yake na namna ya kumtakasa kwake…} [24:41],

Je, inakulaiki wewe kukosa kuhudhuria katika tukio hili lenye kutisha? Baada ya hapo utakuwa ni mwenye kufedheheshwa; amesema kweli Allah Ta'ala: {Je! Huoni kwamba vinamsujudia Mwenyezi Mungu viliomo mbinguni na viliomo katika ardhi, na jua, na mwezi, na nyota, na milima, na miti, na wanyama, na wengi miongoni mwa watu. Na wengi imewastahiki adhabu. Na anaye fedheheshwa na Mwenyezi Mungu hana wa kumhishimu. Hakika Mwenyezi Mungu hutenda apendayo.} [22:18]

https://www.path-2-happiness.com/sw

Je, hawazingatii?!

"Mimi nashangazwa kwa anayeangalia mbinguni na kuona ukubwa wa Uumbaji kisha asimuamini Mungu."

Abraham Linkolin

Raisi wa 16 wa Marekani.

https://www.path-2-happiness.com/sw

الطريق إلى السعادة
The Path to Happiness



JE, MWANADAMU ANA HAJA YA DINI?

https://www.path-2-happiness.com/sw

Yaliyomo

JE, MWANADAMU ANA HAJA YA DINI?

Je, ni lazima kuwa na Dini?

Haja ya dini kwa jamii mbali mbali

Vidhibiti vya dini ya haki

Ni dini ipi tunayohitajia?

JE, MWANADAMU ANA HAJA YA DINI?

Je, ni lazima kuwa na Dini?

Matokeo Imara

"Imani ni matokeo imara na matukufu zaidi katika tafiti za kisayansi."

Einstein
Mwanazuoni wa Fizikia



Mwanadamu kwa hali yoyote hawezi kuishi bila Dini, na kwa sababu mwanadamu ni mtu mwenye tabia ya kuingiliana na watu na hawezi kuishi peke yake huku akijitenga na jamii, nae vile vile katika maumbile yake ni mtu mwenye dini hawezi kuishi maisha ya sawa sawa bila kuwa na dini, swala la mtu kuwa na dini ni suala la kimaumbile na tabia ya asili ya mwanadamu na hakuna dalili kubwa yenye kuthibitisha hilo kuliko ile hali ya mwanadamu kumtegemea Mwenyezi Mungu katika hali ya shida na dharura, Allah Ta'ala amesema, {Na wanapo panda katika marikebu, humwomba Mwenyezi Mungu kwa kumsafia ut'iifu. Lakini anapo wavua wakafika nchi kavu, mara wanamshirikisha.} [29:65]

Kama ambavyo mtu aliyetengeneza mashine ndiye mwenye kufahamu zaidi mahitajio yake vivyo hivyo na muumbaji huwajua zaidi viumbe wake na mahitaji yao, {Asijue aliye umba, naye ndiye Mjua siri, Mwenye khabari? } [67:14]

Na kwa sababu Muumba ni Mrehemu na Ghafuri Mkarimu; amewawekea watu sharia ya Dini ili Nafsi zao zihuishwe na maisha yao yadhibitiwe, Allah Ta'ala amesema, {Enyi mlio amini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele….} [8:24],

Na kwa hilo basi hata yule ambaye anakwenda kinyume na maumbile sahihi na anadai kumkana Allah Ta'ala, wao ni ndani ya Nafsi zao wanajua uongo wa kukana kwao, Allah amesema, {Na wakazikataa kwa dhulma na kujivuna, na hali ya kuwa nafsi zao zina yakini nazo. Basi angalia ulikuwaje mwisho wa mafisadi!} [27:14]

Na huenda hilo likaonekana kwa uwazi zaidi wakati wa zahama na matatizo zaidi, Allah amesema, {Sema: Mwaonaje ikikujieni adhabu ya Mwenyezi Mungu, au ikakufikieni hiyo Saa - mtamwomba asiye kuwa Mwenyezi Mungu, ikiwa nyinyi ni wakweli? Bali Yeye ndiye mtakaye mwomba, naye atakuondoleeni mnacho mwombea akipenda. Na mtasahau hao mnao wafanya washirika wake.} [6:41-42]

Kadhalika katika Surat Zumar amesema: {Na taabu inapo mfikia mtu humwomba Mola wake Mlezi naye ameelekea kwake. Kisha akimpa neema kutoka kwake, husahau yale aliyo kuwa akimwitia zamani, na akamfanyia Mwenyezi Mungu washirika ili apoteze watu njia yake. Sema: Starehe na ukafiri wako kwa muda mchache. Kwani hakika wewe utakuwa miongoni mwa watu wa Motoni. } [39:8].

Wanadamu wote wapo katika maumbile ya asili waliyoumbwa nayo na Allah Ta'ala katika kumuabudu yeye kwa mkono wake kheri na shari kufanya ayatakayo na kuhukumu atakavyo, Allah Ta'ala amesema: {Na ikiwa Mwenyezi Mungu akikugusisha madhara, basi hapana wa kukuondolea hayo ila Yeye. Na ikiwa akikugusisha kheri, basi Yeye ndiye Mwenye uweza wa kila kitu.} [6:17]

Na katika Surat Faatwir amesema: {Rehema ambayo Mwenyezi Mungu anawafungulia watu hapana wa kuizuia. Na anayo izuia hapana wa kuipeleka isipo kuwa Yeye. Naye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima.} [35:2].



Mtu wa Dini na Mgonjwa

"Nakumbuka yale masiku ambayo hakukuwepo na mazungumzo ya watu isipokuwa kuhusu ugomvi baina ya elimu na dini. Mgogoro huu uliisha bila kurejewa, kwani elimu ya sasa ya tiba ya nafsi inatoa habari nzuri kuhusu misingi ya dini. Kwanini?!! Kwa sababu matabibu wa nafsi wamegundua kuwa kuwa imani yenye nguvu na kushikamana na dini na swala hutosheleza kushinda wasiwasi, khofu na msongo wa mawazo na kutibu nusu ya maradhi ambayo tunayoyalalamikia. Hadi Dr. A. A. Bell akasema: "Kuwa mtu mwenye kushikamana na dini hasumbuliwi na maradhi ya nafsi."

Dale Carnegie

Mwandishi wa Kimarekani.

Dale Carnegie
Mwandishi wa Kimarekani

Kuwa Mbobezi

"Mwanafalsafa Francis Becon alisema kweli aliposema, "Falsafa ndogo humpelekea mtu kwenye kumkana Mungu. Ama kubobea katika falsafa humrejesha mtu kwenye dini."

Mwanadamu ana nguvu za aina mbili: Nguvu ya elimu na nguvu ya matakwa yake, na kwa kadiri ya juhudi yake katika kutekeleza nguvu hizo mbili mwanadamu huyo hufikia malango yake aliyojipangia na vivyo hivyo ndivyo mwanadamu apatavyo furaha.

Ama nguvu ya kwanza (nguvu ya elimu) kwa kadiri ya maarifa yake kwa Allah, kwa majina yake na sifa zake, na yanayopasa kwake katika maamrisho na makatazo, kitabia na kimaadili na vipi ilivyo njia ya ukuruba na kuwa juu ya daraja za mwenye kufuata, na yote yenye kupelekea katika elimu ya ndani kuhusu Nafsi za wanadamu na maradhi yake na jinsi ya kuyashinda hayo, na kwa maadui zake na kila chenye kuzuia baina yake na Mola wake, mbali na mtu kukwea daraja za juu za kutakasa tabia yake iwe ya kiungu kiasi cha kupanda juu kufikia roho za juu na hima za juu, mbali kabisa na mambo ya hovyo kwa lengo la kupata maslahi ya kidunia na matamanio yake, kwa kiasi hicho ndio kimada unapokuwa daraja ya uja wa mtu kwa Allah Ta'ala na nafasi yake, bali na furaha yake duniani sembuse ya akhera.



Nguvu hii ya kielimu ndio masurufu na msaada wa nguvu ya matakwa ya mtu, ambayo yatamuongoza katika uongofu pamoja na kuthibiti na kufanya mambo mazuri, Allah Ta'ala amesema: {Enyi mlio amini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele….} [8:24]

Na haya madhehebu ya wakanayo Mungu na Dini yanatangaza kufilisika kwao kwa kutekeleza kwao raha za kiwiliwili sembuse kushibisha mahitajio ya kiroho, madhehebu haya yameshindwa kabisa kumhakishia mwanadamu furaha ya kweli vyovyote watakavyopeana kauli nzuri na kupamba kauli zao kwa ghururi.

Mwanadamu anamuelekea nani katika matatizo yake na misiba yake! Anategemea nguzo imara, anaelekea kwa Allah Ta'ala; penye nguvu, matarajio, subira na kutegemea kwema na kumwachia mambo yote yeye. Allah amesema; {Wale walio amini na zikatua nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndio nyoyo hutua!} [13:28].

Hadi hapo atakapoonja uchungu wa moto kwa dhulma ndipo atakapokuwa na yakini kuwa ulimwengu huu una Mola, na ambaye anamnusuru aliyedhulumiwa hata kama, ni baada ya muda kupita, na ya kuwa kuna siku ya mwisho ambayo kila mmoja atalipwa alichokichuma, na mtu mwema kulipwa mema yake na muovu kulipwa maovu yake na hivyo basi kifua chake kuwa imara kwa tumaini na yakini kwa Allah. Allah Ta'ala amesema: {Je! Aliye yafuata ya kumridhisha Mwenyezi Mungi ni kama yule aliye stahiki ghadhabu ya Mwenyezi Mungu, na makaazi yake yakawa Jahannamu? Napo ni mahala pabaya pa kurejea.} [3:162].



Ukweli Ulio wazi Zaidi

"Utafiti wangu kwa ajili ya kupata shahada ya uzamifu (PhD) ilikuwa kuhusu Malezi na kujenga Ummah. Nimegundua kuwa nguzo za Kiislamu za msingi zimeweka misingi mikuu na kanuni madhubuti ili kurudisha jengo la Ummah kijamii, kiuchumi na kiroho

Dr. Douglas R. Archer

Meya wa Regina

Kushika Dini ni tiba ya Maradhi

"Matabibu wa nafsi wamegundua kuwa imani madhubuti na kushikamana na dini inamtosha kushinda khofu, wasiwasi na msongo wa nafsi na kuponya maradhi haya."

Dale Carnegie
Mwandishi wa Kimarekani.

Tibu mwenyewe nafsi yako.

"Kwa hakika tiba kubwa zaidi ya nafsi ni kumuamini Mwenyezi Mungu."

William James
Mwanazuoni wa Elimu nafsi (Saikolojia) wa Marekani.



Havipo pamoja

"Madhehebu ya Kiyakinifu (unaotanguliza anasa za dunia) siku zote wanathibitisha ambacho wanashirikiana baina ya mwanadamu na mnyama. Wakati ambapo dini inasisitiza kinachotenganisha baina yao."

Alija 'Ali Izetbegovic
Rais wa zamani wa Jamhuri ya Bosnia Herzegovina.

Kinyume na yaliyotangulia; yule ambaye amepoteza maarifa yake kwa Allah Ta'ala na kumuamini basi mtu huyo amepoteza nguvu zake zote, na kadhalika atakuwa amepoteza raha, tumaini na furaha, na atakuwa anaishi baina ya hamu na huzuni, hana utulivu ndani ya nafsi yake, hamu yake kubwa ni kutekeleza na kufanikisha matamanio yake hajui malengo ya maisha yake, wala maana ya kuwepo kwake hapa ulimwenguni. Bali mtu huyu anaishi akibabaika hajui afanye nini, akitafuta furaha, akifuata matamanio yake, lakini anarudi nyuma kiasi cha kuwa ni mnyama au aliyepotea zaidi, Allah Ta'ala amesema: {Au wewe unadhani kwamba wengi wao wanasikia au wanaelewa? Hao hawakuwa ila ni kama nyama hoa tu, bali wao wamepotea zaidi njia.}[25:44],

Na ikitokea mtu huyu kapatwa na msiba basi kuangukia kuwa ni muhanga wa angamizo la nafsi na angaiko na babaiko lake la



ndani, {Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu.} [20:124]

Ni tofauti kubwa sana baina ya mtu mwenye kumjua Mola wake, na kujua ukubwa wake na akajua kinachompasa kwake kwa Mola wake na kuijali kwake kumridhisha Mola wake, akifuata sheria zake, akitii maamrisho yake na kuacha makatazo yake, Na akajua kuwa ni mwenye haja ya kudumu kwa Mola wake katika madogo na makubwa, katika mambo dhalili na matukufu, na

Matabibu wenye kutoa mawaidha



"Kwa hakika matabibu wa nafsi ni watu wenye kutoa mawaidha kwa njia mpya; Kwani wao hawatuhimizi dini kwa sababu ya adhabu ya motoni huko akhera, bali wao hutuusia kushikamana na dini ili tusipate adhabu ile ile ya moto hapa duniani, kama vile moto wa vidonda vya tumbo na msongo wa nafsi na wendawazimu."

Henry Ford

Mwanzilisi wa Shirika la Ford la Magari Marekani





katika kila wakati Allah Ta'ala amesema: {Enyi watu! Nyinyi ndio wenye haja kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kujitosha, Msifiwa.}[35:15].

Na mtu mwingine dhana na mawazo yamemtupa katika taabu na kiza na shida, akipapasa kwa kupepesuka kama vile kipofu hapa na pale, moyo wake ukiwa umejaa shaka na wasiwasi, kila akijaribu kukamata au kushika furaha anajikuta yupo katika mazigazi baada ya mazigazi, na hata akipata ladha za dunia na matamanio yake, na hata akipanda cheo na daraja za juu, Je, mtu atakayemkosa Allah atapata nini? Na atakayempata Allah atakuwa amekosa nini?

Dini ni Maisha

"Dini ni katika vipaji muhimu vya mwanadamu. Tunatosheka kusema kuwa mtu kukosa dini humsukuma kwenye hali ya kukata tamaa kiroho, inamlazimisha kutafuta nguvu ya kidini kwenye sahani zisizomiliki chochote ndani yake."

Arnold J. Toynbee
Mwanahistoria wa Uingereza.

Zama za Babaiko

"Kwa hakika sisi tunaishi katika zama za babaiko, wala hapana shaka kuwa mafanikio ya Sayansi na teknolojia zimemzidishia mwanadamu anasa na starehe lakini kwa upande mwingine haikumuongezea furaha na utulivu bali kinyume chake imemuongezea khofu, babaiko, kukata tamaa na maradhi ya nafsi yamemuondoshea maana nzuri ya maisha haya."

Dr. Rene Dubos

Mwanasayansi aliyepata tuzo ya Nobel



https://www.path-2-happiness.com/sw

Haja ya dini kwa jamii mbali mbali

Hoja yenye kuzungumza

"Kwa hakika kuna uwezekano wa kudhoofika kila kitu tunachokipenda, na kubatilisha uhuru wa matumizi ya akili, elimu, na viwanda, lakini ni muhali kufutika dini, bali itabakia kuwa ni hoja yenye kuzungumza dhidi ya ubatili wa madhehebu ya kiyakinifu (yanayotanguliza dunia na anasa zake) ambayo yanataka kumdhibiti mwanadamu katika dhiki ya uduni katika maisha ya ardhini."

Ernest Renan

Mwanahistoria wa Kifaransa

Philip Hitti

Mwanahistoria wa Kilebanoni

Ikiwa mtu binafsi hana budi awe na dini, basi haja ya jamii mbali mbali kwenye dini ni kubwa zaidi, Dini ni ngao yenye kuikinga jamii; na hiyo ni kwa sababu maisha ya mwanadamu hayasimami isipokuwa kwa kushirikiana na watu wake katika mambo ya kheri: {…Na saidianeni katika wema na uchamngu. Wala msisaidiane katika dhambi na uadui...} [5:2],

Na ushirikiano huu hautimii ila kwa mfumo unaopangilia mahusiano yake, na kuainisha majukumu yake na kudhamini haki zao, mfumo huu hauna budi kutoka kwa yule mpole mwenye ujuzi na elimu kwa anayohitajia mwanadamu, {Asijue aliye umba, naye ndiye Mjua siri, Mwenye khabari?} [67:14]

Kila ambapo mwanadamu anapokwenda kinyume na dini, sheria yake na mfumo wake ndipo jinsi ambapo hupotea na kughibu na kudumbukia katika kiza cha shaka, upotevu, haya, taabu na mateso.

Hakuna katika ardhi yote hii nguvu ambayo ni sawa na nguvu ya dini au mtu kufuata dini katika kudhamini watu kuheshimu mfumo au utaratibu Fulani, na kadhalika kudhamini mshikamano wa jamii

Sheria ya kweli

"Sheria ya Kiislamu haitofautishi baina ya dini na baina ya ambacho ni dunia. Sheria hiyo inaonesha mahusiano ya mwanadamu na Mwenyezi Mungu na wajibu wake kwa Mungu na kuyapanga kama inavyofanya kwa hali ya mahusiano ya mtu kwa ndugu yake mwanadamu. Na amri zote za Allah na makatazo yake –katika yanayofungamana na mambo ya dini na dunia na mengine kwenye Qur-aan na ndani yake pana ayah elfu sita au ziada ya hapo, miongoni mwa hizo ayah elfu ni kuhusu sheria."

Dini haina nafasi ya matamanio

"Tunaona katika sababu ya mapokezi ya kushangaza aliyokutana nayo Muhammad huko Madina, ni kuwa kuingia katika Uislamu kwa watu wa Madina ulianza kwa tabaka la viongozi na lengo ilikuwa ni kutibu fujo ile ambayo ilikumba jamii ya Madina na ikiteseka nayo. Sababu kubwa ni kile walichokipata ndani ya Uislamu, ambayo ni kuwepo kwa nidhamu madhubuti chini ya sheria zilizopangwa. Na matamanio ya watu kuwa chini ya utawala wa kisheria ambao umejitenga na matamanio yao."

Thomas Arnold

Mustashrik (mtaalamu wa mambo ya nchi za mashariki) wa Kiingereza

Ziko wapi akili zenu?!

"Kwa nini mna shaka ya kuwepo kwa Mungu?! Na lau si yeye basi mke wangu angenisaliti, na mtumishi wangu angeniibia."

Voltaire

Mwanafalsafa wa Kifaransa

na utulivu kwa mfumo wake na sababu zote za usalama na siri katika hilo ni kuwa mwanadamu anatofautiana na viumbe vingine kwa kuwa harakati zake na matendo yake ya hiari yanayotawalia uongozi wake kitu ambacho hakitokei katika usikizi wake wala uoni wake, bali ni akida ya kiimani ambayo ina adabisha roho na kutakasa kiwili wili chake na kuifanya kuwa ni mwangalizi wa siri yake kama ambavyo inakuwa ni mwangalizi wa dhahiri yake, {Na ukinyanyua sauti kwa kusema...basi hakika Yeye anajua siri na duni kuliko siri.} [20:7].

Mwanadamu huongozwa na akida iwe ni sahihi au mbovu, akida yake ikitengemaa basi mambo yake yote yatatengemaa, na ikiharibika mambo yake yote yataharibika.

Kwa ajili hiyo dini ndio ikawa dhamana bora zaidi ya kusimamisha miamala baina ya watu katika misingi ya uadilifu na usawa, na hilo likawa ni jambo ambalo halina budi katika jamii, wala hatutokuwa tumekosea tukisema kuwa dini itachukua nafasi ya moyo katika kiwiliwili cha Umma mbali mbali.

Ikiwa dini kwa ujumla inachukua nafasi hii, na leo hii mtu akiangalia ataona dini nyingine na mila mbali mbali ulimwenguni, na kila jamii yenye dini fulani hufurahishwa nayo na hukamatana nayo. Kama hali ndivyo hivyo ilivyo ni dini gani basi ambayo ndio sahihi na ambayo itamthibitishia na kumkamilishia nafsi ya mwanadamu anachotaka kukifikia?! Na ni nini vidhibiti vya dini ya haki?!



Vidhibiti vya dini ya haki

Mara zote kila mwenye itikadi au akida fulani ana yakini timilifu kuwa akida yake ndio itikadi iliyokuwa sahihi zaidi na ya haki kuliko itikadi nyingine, na kila mmoja anatofautiana na mwenye itikadi nyingine kwa kuthibitisha hilo; pale watu wenye itikadi za kibinadamu zilizoharibika au zilizopotea huthibitisha hilo kwa kudai kuwa wamewakuta baba zao wakifanya hivyo na ya kuwa wao huwafuata wao, Allah Ta'ala amesema, {Na kadhaalika hatukumtuma mwonyaji kwenye mji wowote ila watu wake walio deka kwa starehe walisema: Hakika sisi tuliwakuta baba zetu wanashika dini makhsusi, na sisi tunafuata nyayo zao. Akasema (Mwonyaji): Hata nikikuleteeni yenye uwongofu bora kuliko mlio wakuta nao baba zenu? Wakasema: Sisi tunayakataa tu hayo mliyo tumwa.} [43:23-24]

Na aya nyingine amesema, {Na wanapo ambiwa: Fuateni aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu; wao husema: Bali tutafuata tuliyo wakuta nayo baba zetu. Je, hata ikiwa baba zao walikuwa hawaelewi kitu, wala hawakuongoka? Na mfano wa walio kufuru ni kama mfano wa anaye mpigia kelele asiye sikia ila wito na sauti tu -- ni viziwi, mabubu, vipofu, kwa hivyo hawaelewi} [2:170-171]

Na hutoa dalili ya msimamo wao huu kwa kufuata kibubusa bila ya kutumia akili au kufikiria, au kuthibitisha kwa kutumia habari za uongo au zenye makosa, zenye kugongana ambazo hazina dalili juu ya ukweli wake, na bila ya shaka haifai kutolea hoja au dalili kwa dini hizi na mila mbali mbali.

Na kwa sababu haki ni moja sio nyingi, ni muhali itikadi zote hizo kuwa ni sawa, na ni muhali zote hizo kuwa sahihi katika wakati mmoja, la sivyo usawa ungekuwa unapingana, na hili halikubaliki kwa akili iliyosalimika: {…Na lau kuwa imetoka kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu bila ya shaka wangeli kuta ndani yake khitilafu nyingi.} [4:82].

Kama ni hivyo basi dini sahihi ni ipi? Ni vidhibiti gani ambavyo vinaweza kuhukumu kuwa moja ya itikadi hii ni ya kweli na nyingine isiyokuwa hiyo si ya kweli?!

Vidhibiti hivi ni:-

Kwanza: Dini iwe ni kutoka kwa Mungu, yaani kutoka kwa Allah Ta'ala na hiyo iwe imekuja kupitia kwa Malaika miongoni mwa Malaika kwa Mtume ili nae afikishe kwa waja wa Allah; kwa sababu dini ya haki ni dini ya Allah aliyeumba Ulimwengu huu, na Allah Ta'ala ndiye ambaye analipa na kuwahesabu viumbe Siku ya Kiama kwa dini ambayo amewateremshia, Allah amesema: {Hakika Sisi tumekuletea wahyi wewe kama tulivyo wapelekea wahyi Nuhu na Manabii walio kuwa baada yake. Na tulimpelekea wahyi Ibrahim na Ismail na Is-haka na Yaakub na wajukuu zake, na Isa na Ayub na Yunus na Harun na Suleiman, na Daud tukampa Zaburi. Na Mitume tulio kwisha kukuhadithia kabla yake, na Mitume wengine hatukukuhadithia. Na Mwenyezi Mungu alinena na Musa kwa maneno. Mitume hao ni wabashiri na waonyaji, ili watu wasiwe na hoja juu ya Mwenyezi Mungu baada ya kuletewa Mitume. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.} [4:163-165].

Na kulingana na jambo hilo ni kuwa dini yoyote ambayo mtu anajinasibisha nayo na sio

kwa Allah ni dini batili bila ya shaka, na dini ambayo ataiendeleza mwanadamu na kuiongezea ni batili vile vile bila ya chembe ya shaka, wala mwenye kuiendeleza au kuibadilisha ni mwenye kujua yale yanayowafaa watu kuliko Allah muumba: {Asijue aliye umba, naye ndiye Mjua siri, Mwenye khabari?} [67:14]

Upekee wa Mungu mmoja (Tauhidi)

"Hakika ya msingi katika Uislamu ni Tauhidi kuwa Allah ni mmoja na Muhammad ni Mtume wa Allah. Ama ushirikina umewekwa pembeni. Hakuna baba wala mtoto wala mpaka kati ya ambacho ni kitukufu, na ambacho ni cha dunia, au cha Mashariki na kile cha Magharibi kuna ulimwengu mmoja tu na dini moja tu."

Michael Hems
Mwandishi wa Uingereza

Vinginevyo mwenye kuendeleza au kuweka sheria ni Allah Muumba mwenye kujua kinachowafaa viumbe vyake, ametakasika Allah kwa hilo: {Je, wanataka dini isiyo kuwa ya Mwenyezi Mungu, na hali kila kilichomo mbinguni na katika ardhi kimesilimu kwa kumt'ii Yeye kikipenda kisipende, na kwake Yeye watarejeshwa?} [3:83]

Na Allah akasema tena, {La! Naapa kwa Mola wako Mlezi! Hawataamini mpaka wakufanye wewe ndiye muamuzi katika yale wanayo khitalifiana…} [4:65].

Pili: Dini hiyo iwalinganie watu kumuabudu Allah Ta'ala na kuharamisha ushirikina; hivyo basi Da'wah katika tawhidi ndio msingi wa da'wah ya Mitume yote, na ushirikina na upagani ndio ambayo inakwenda kinyume kabisa na maumbile sahihi ya mwanadamu na akili zilizoongoka, Allah Ta'ala amesema: {Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia ya

kwamba hapana mungu isipo kuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu} [21:25]

Na kila Mtume alisema maneno yafuatayo kwa watu wake: {…Muabuduni Mwenyezi Mungu. Nyinyi hamna Mungu ila Yeye. Hakika mimi ninakukhofieni adhabu ya Siku iliyo kuu.} [7:59],

Na kwa hilo basi dini yoyote ambayo itakiri ushirikina, au kumshirikisha Nabii au Malaika au walii au mtu au jiwe pamoja na Allah, basi dini hiyo ni batili, kwani ibada ni kwa Allah pekee hana mshirika pamoja nae, na upagani na ushirikina ni upotevu ulio dhahiri, na kila dini hata kama ikiwa kutoka kwa Allah na ikaingizwa ndani yake ushirikina basi dini hiyo vile vile ni batili, Allah Ta'ala ametupigia mfano; aliposema, {Enyi watu! Unapigwa mfano, basi usikilizeni. Hakika wale mnao waomba badala ya Mwenyezi Mungu, hawatoumba hata nzi ijapo kuwa watajumuika kwa hilo. Na nzi akiwapokonya kitu hawawezi kukipata kwake. Amedhoofika kweli huyo mwenye kutaka na mwenye kutakiwa. Hawakumuadhimisha Mwenyezi Mungu anavyo stahiki kuadhimishwa. Hakika Mwenyezi Mungu bila ya shaka ni Mwenye kushinda.} [22:73-74].

Uumbaji wa Mwenyezi Mungu

"Kwa hakika watoto wadogo wana muelekeo uliotangulia wa kumuamini Mungu. Kwani wao huzingatia kuwa kila kilicho katika Ulimwengu huu kimeumbwa kwa sababu. Hata kama tukiwatupa watoto peke yao kisiwani na wakaishi wenyewe bila shaka watamuamini Mwenyezi Mungu."

Justin Barret

Mtafiti wa Chuo Kikuu cha Oxford

https://www.path-2-happiness.com/sw



Ugonjwa wa Upotofu

"Elimu ni dawa ya sumu ya upotofu"

Adam Smith
Mwanafalsafa wa Scotland

Tatu: Dini hiyo iafikiane na maumbile sahihi, Allah amesema: {Basi uelekeze uso wako sawasawa kwenye Dini - ndilo umbile la Mwenyezi Mungu alilo waumbia watu. Hapana mabadiliko katika uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo Dini iliyo nyooka sawa. Lakini watu wengi hawajui.} [30:30],

Na maumbile sahihi ni kila ambacho Allah amempa mwanadamu na ikawa kwake ni sehemu ya maumbile yake, kwani haiwezi kuwa dini ambayo haifai maumbile ya mwanadamu, vinginevyo basi Muumba asingekuwa na uwezo wa kuweka sheria ya dini, na jambo hii ni muhali na la kishirikina.

Nne: Dini hiyo iafikiane na akili sahihi; kwa sababu dini sahihi ni sheria ya Allah na akili sahihi ni maumbile aliyoyaumba Allah, na ni muhali sheria ya Allah na maumbile yake kugongana, Allah amesema: {Je! Hawatembei katika ardhi ili wapate kuwa na nyoyo zao za kuzingatia, au masikio ya kusikilia? Kwani hakika si macho yanayo pofuka, lakini zinazo pofuka ni nyoyo ziliomo vifuani.} [22:46]

Na Akasema, {Hakika katika mbingu na ardhi ziko Ishara kwa Waumini. Na katika umbo lenu na katika wanyama alio watawanya zimo Ishara kwa watu wenye yakini. Na kupishana usiku na mchana, na riziki anayo iteremsha Mwenyezi Mungu kutoka mbinguni, na kwayo akaifufua ardhi baada ya kufa kwake, na mabadiliko ya upepo, ni Ishara kwa watu wenye akili. Hizi Aya za Mwenyezi Mungu tunakusomea kwa haki; basi hadithi gani watakayo iamini baada ya Mwenyezi Mungu na Aya zake?} [45:3-6]

Hivyo basi haiswihi kuwa dini ya kweli imejaa upotevu na migongano kiasi tunapata baadhi yake ni tofauti kabisa na nyingine, na huu ni mgongano wa akili sahihi, hivyo basi haiwezi kuamrisha kisha ikaja amri nyingine inayogongana nayo, wala isiharamishe jambo au kuiruhusu kwa kundi maalumu kisha kulihamisha kwa kundi jingine, au kutofautisha baina ya vyenye kufanana au kuvikusanya baina ya vyenye kugongana,

Allah Ta'ala amesema,{Hebu hawaizingatii hii Qur'ani? Na lau kuwa imetoka kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu bila ya shaka wangeli kuta ndani yake khitilafu nyingi.} [4:82]

Bali ni lazima iwe imejengwa kwa dalili nyingi mbali mbali zilizo wazi, Allah amesema: {…Leteni ushahidi wenu kama nyinyi ni wasema kweli.} [2:111]

Leteni Hoja Zenu

"Mwenye busara ni Yule anayejenga Imani yake juu ya Hoja."

David Hume
Mwanafalsafa wa Scotland

Mtu na tabia zake

"Mtu asiye na tabia njema ni mnyama amaeachwa huru katika ulimwengu huu."

Albert Camus
Mwanafalsafa wa Kifaransa

Tano: Dini hiyo ilingane na tabia nyema na matendo mema, Allah amesema: {Sema: Njooni nikusomeeni aliyo kuharimishieni Mola wenu Mlezi. Nayo ni kuwa, msimshirikishe Yeye na chochote. Na wazazi wenu wafanyieni wema. Wala msiwauwe watoto wenu kwa sababu ya umasikini. Sisi tunakuruzukuni nyinyi na wao. Wala msikaribie mambo machafu, yanayo onekana, na yanayo fichikana. Wala msiuwe nafsi ambayo Mwenyezi Mungu ameharimisha kuiuwa, ila ikiwa kwa haki. Hayo amekuusieni ili myatie akilini. Wala msiyakaribie mali ya yatima ila kwa njia ya wema kabisa, mpaka afikilie utu-uzima. Na timizeni vipimo na mizani kwa uadilifu. Sisi hatumkalifishi mtu ila kwa kadiri ya uwezo wake. Na msemapo semeni kwa uadilifu ingawa ni jamaa. Na ahadi ya Mwenyezi Mungu itekelezeni. Hayo amekuusieni ili mpate kukumbuka. Na kwa hakika hii ndiyo Njia yangu Iliyo Nyooka. Basi ifuateni, wala msifuate njia nyingine, zikakutengeni na Njia yake. Haya amekuusieni ili mpate kuchamngu.} [6:151-153]

Na Allah akasema, {Hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha kufanya uadilifu, na hisani, na kuwapa jamaa; na anakataza uchafu, na uovu, na dhulma. Anakuwaidhini ili mpate kukumbuka.} [16:90]

https://www.path-2-happiness.com/sw

Haisihi dini ambayo italingania uongo au mauaji au dhulma au wizi au kuhaka na kupora na kufanya uasi au mfano wa hayo.

Sita: Itengeneze mahusiano kati ya Mwanadamu na Muumba wake, na mahusiano ya viumbe kwa viumbe, Allah amesema, {Hamuabudu badala yake ila majina tu mliyo yapanga nyinyi na baba zenu. Mwenyezi Mungu hakuyateremshia hayo uthibitisho wowote. Hapana hukumu ila ya Mwenyezi Mungu tu. Yeye ameamrisha msimuabudu yeyote isipo kuwa Yeye tu. Hiyo ndiyo Dini Iliyo Nyooka. Lakini watu wengi hawajui.} [12:40]

Hivyo basi inapasa dini hiyo kutengeneza majukumu ya mwanadamu kwa Mola wake, kadhalika itengeneze mahusiano ya viumbe na watu, Allah amesema: {Muabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na chochote. Na wafanyieni wema wazazi wawili na jamaa na mayatima na masikini na jirani wa karibu na jirani wa mbali, na rafiki wa ubavuni na mpita njia, na walio milikiwa na mikono yenu ya kulia….} [4:36].

Saba: Dini hiyo imuheshimu mwanadamu na imkirimu wala isitofautishe baina ya wafuasi wake kwa tofauti zozote zile ziwe za kijinsia, rangi au kabila; kigezo cha kufadhilishwa na ubora ni kile anachokipata mwanadamu kutoka katika kazi yake, elimu na ucha-Mungu, Allah amesema: {Na hakika tumewatukuza wanaadamu, na tumewapa vya kupanda nchi kavu na baharini…} [17:70]

Kuwa Mwanahalisi

"Mtazamo halisi katika maisha na ushauri wa kweli na kulingania kwenye hisani, huruma na mguso wa kheri wa kibinadamu, haya na mengineyo ni katika dondoo ambazo kwangu zilikuwa ni dalili kubwa za ukweli wa dini ya Uislamu."

Jul

Mustashrik wa Kidenimaki



Tabia njema zinakupa raha

"Ninachokifahamu kuwa tendo zuri ulifanyalo linalotokana na tabia njema ni lile linalokufanya baada ya hapo uhisi raha, na tabia mbaya baada ya kulifanya unapojisikia vibaya"

Ernest Hemingway

Mwandishi wa Kimarekani

Na akasema vile vile, {Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamngu zaidi katika nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye khabari.} [49:13].

Nane: Dini hiyo imuelekeze mwanadamu katika njia sahihi isiyokuwa na kombo, na njia hiyo iwe ni tiba kwa mwanadamu na iwe nuru na muongozo wao, Allah amesema akielezea kuhusu majini baada ya kusikiliza kwao Qur-aan wakiambizana, {Wakasema: Enyi kaumu yetu! Sisi tumesikia Kitabu kilicho teremshwa baada ya Musa, kinacho sadikisha yaliyo kuwa kabla yake, na kinacho ongoza kwenye Haki na kwenye Njia Iliyo Nyooka.}[46: 30],

Na akasema Allah, {Na tunateremsha katika Qur'ani yaliyo ni matibabu na rehema kwa Waumini. Wala hayawazidishii madhaalimu ila khasara.} [17:82]

Nayo ni nuru na muongozo wa watu ambao unawaongoza watu kutoka kwenye dhuluma za ujinga (ujahili) na upotevu kwenda kwenye Nuru ya utiifu na furaha katika nyumba zote mbili, Allah amesema: {Enyi Watu wa Kitabu! Amekwisha kujieni Mtume wetu anaye kufichulieni mengi mliyo kuwa mkiyaficha katika Kitabu, na anaye samehe mengi. Bila shaka imekujieni kutoka kwa Mwenyezi Mungu nuru na Kitabu kinacho bainisha.} [5:15]

Urithi bora

"Miongoni mwa mambo muhimu ambayo Uislamu umeyarithisha Ulimwengu huu ulioendelea ni kanuni zake za dini ambazo zinaitwa Sheria. Kwa hakika sheria ya Kiislamu ni kitu cha pekee katika mlango wake, ni jumla za amri za kiungu ambazo zinaratibu maisha ya kila Muislamu katika Nyanja zote, nazo zinakusanya hukumu maalumu kuhusu ibada na mambo mengine ya kidini, kama ambayo inakusanya misingi ya kisiasa na kanuni zake mbali mbali."

Joseph Sachacht
Mustashrik wa Kijerumani

Na Akasema Allah tena, {Hapana kulazimisha katika Dini. Kwani Uwongofu umekwisha pambanuka na upotofu. Basi anaye mkataa Shet'ani na akamuamini Mwenyezi Mungu bila ya shaka amekamata kishikio madhubuti, kisicho vunjika. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua. Mwenyezi Mungu ni Mlinzi wa walio amini. Huwatoa gizani na kuwaingiza mwangazani. Lakini walio kufuru, walinzi wao ni Mashet'ani. Huwatoa kwenye mwangaza na kuwaingiza gizani. Hao ndio watu wa Motoni, na humo watadumu.} [2:256-257].



Hakuna Usawa

"Aina mbaya zaidi ya kukosekana usawa ni kujaribu kusawazisha kati ya vitu visivyo sawa."

Aristotle
Mwanafasafa wa Kigiriki

Mtake Msaada Mwenyezi Mungu

"Pengine ingewezekana kuokoa maelfu ya wanaoadhibika kwa kupiga makelele katika hospitali za wendawazimu, lau wao wangeomba ulinzi wa Mwenyezi Mungu badala ya wao wenyewe kuingia kwenye mapigano na Nafsi zao bila ya msaada wala muokozi."

Dale Carnegie
Mwandishi wa Kimarekani

Ni dini ipi tunayohitajia?

Ni dini ipi ambayo tunaweza kuipitishia vigezo vya dini ya haki iliyotangulia?

Tunaweza kugawa dini mbali mbali kulingana na vyanzo vyake katika makundi mawili:

-Dini za Ardhi au za Wanadamu, sio za mbinguni wanadamu wanaziainisha na kuziendeleza wao wenyewe, sio zilizoshuka kutoka kwa Allah Ta'ala; dini hizi ni kama vile Ubudha, Uhindu, Umajusi na upagani, hizi ni dini ambao zipo mbali kabisa na dini ya kweli, dini hizi zinatokana na matamanio ya mwanadamu; {Je! Umemwona aliye fanya matamanio yake kuwa ndiye mungu wake, na Mwenyezi Mungu akamwacha apotee pamoja na kuwa ana ujuzi, na akapiga muhuri juu ya masikio yake, na moyo wake, na akambandika vitanga machoni mwake? Basi nani atamwongoa huyo baada ya Mwenyezi Mungu? Hamkumbuki?} [45:23]

Sio dini kutoka kwa Mungu, bali dini za matamanio ya watu, hivyo basi utaona kuwa dini hizi zimejaa uzushi, udajali, matabaka na migongano, Allah Ta'ala amesema, {…Na lau kuwa imetoka kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu bila ya shaka wangeli kuta ndani yake khitilafu nyingi.} [4:82].

Lakini Mwenyezi Mungu ni mmoja

"Watafiti wametaabika wakiwa wanahesabu idadi ya miungu ya dini za wanadamu: Idadi ya miungu ya Wamisri wa kale ni zaidi ya miungu mia nane, na idadi ya miungu ya Kihindu ni zaidi ya miungu elfu kumi, na mfano wa ushirikina huu kwa Wagiriki na Wabudha, na mengine miongoni mwa dini za watu za ardhini."

https://www.path-2-happiness.com/sw

-Dini za Mbinguni kutoka kwa Allah, kama vile Uyahudi, Ukristo na Uislamu, na watu wenye dini hizi Muumba aliwaelekeza dini yao na kuridhia, Allah amesema, {Amekuamrisheni Dini ile ile aliyo muusia Nuhu na tuliyo kufunulia wewe, na tuliyo wausia Ibrahim na Musa na Isa, kwamba shikeni Dini wala msifarikiane kwayo. Ni magumu kwa washirikina hayo unayo waitia. Mwenyezi Mungu humteua kwake amtakaye, na humwongoa kwake aelekeaye.} [42:13]

Bila shaka dini nyingi za ardhini ni kundi kubwa la fikra mbali mbali na mkusanyiko wa wanadamu waliochagua katika yanayonasibiana na matamanio yao, lakini baada ya muda mfupi mwanadamu akagundua kuwa haifai, kwa hivyo wao wakajaribu kuziendeleza, na wao hali kadhalika kuendelea katika kupotea, sifa za dini hizi za ardhini (watu) ni hizi zifuatazo:-

Sheria ya kweli

“Nimefahamu na kudiriki kuwa anachohitaji mwanadamu ni sheria ya mbinguni inayoweka haki na kuondosha batili.”

Tolstow

Mwanafasihi wa Kirusi

Ushirikina: Kila siku wanatengeneza Mungu mpya, Mungu wao anatengenezwa na mikono yao, wala hawafikiri kutokuwezekana kuwepo Mungu pamoja na Allah vinginevyo wangepigana au kugongana, Allah amesema: {Mwenyezi Mungu hana mwana yeyote, wala hanaye mungu mwengine. Inge kuwa hivyo basi kila mungu angeli chukua alivyo umba, na baadhi yao wangeli washinda wengine. Mwenyezi Mungu ameepukana na sifa wanazo msifu. Mjuzi wa siri na dhaahiri, na ametukuka juu ya hayo wanayo mshirikisha nayo.} [23:91-92]

Utabaka: Dini za ardhi zimesimama katika matabaka na kuwafanya watu kuwa watumwa; kwani watu wameweka kwa ajili yao wenyewe na sio wengine; ili wafanikiwe katika lengo lao na wawafanye wengine kuwa watumwa, Allah amesema: {Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni

kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamngu zaidi katika nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye khabari.} [49:13]

Na Mwenyezi Mungu akawakataza watu kuangaliana vibaya kwa kusema, {Enyi mlio amini! Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao, wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao. Huenda hao wakawa bora kuliko wao} [49:11],

Hivyo basi kwa Mwenyezi Mungu hakuna fadhila au hakuna ubora wa mweupe kwa mweusi, wala kwa ukoo fulani ukilinganisha na mwingine wala kaumu fulani dhidi ya kaumu nyingine. Ama dini za ardhi (zilizoundwa na watu) zinasimama kwa misingi ya tabaka.

Kwenda kinyume na maumbile (fitra): Dini za ardhi zinakwenda kinyume na maumbile sahihi ya mwanadamu, zinasimamia katika kumbebesha mwanadamu asiyoyaweza, zipo kinyume na mazingira, na tabia ya mwanadamu, akili sahihi, kwani wafuasi wake wamekuwa mbali na njia ilionyooka na wakabadilisha, Allah amesema: {Basi uelekeze uso wako sawasawa kwenye Dini - ndilo umbile la Mwenyezi Mungu alilo waumbia watu. Hapana mabadiliko katika uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo Dini iliyo nyooka sawa. Lakini watu wengi hawajui.} [30:30]

Tabaka za Kijeuri

"Mgawanyiko wa kitabaka katika dini ya Kihindu uko kama ifuatavyo: Tabaka la weupe; Hili ni tabaka la watu wa dini na wanazuoni. Tabaka la Wekundu; linakusanya maamiri na wanajeshi. Tabaka la Manjano: linakusanya wakulima na wafanya biashara. Tabaka la Weusi linahusisha mafundi mikono na viwanda. Ama tabaka la tano ambalo linafahamika kuwa ni tabaka la watu duni (Untouchable-tabaka la chini kabisa) linahusisha wenye kazi duni. Na tabaka za juu linatumikisha matabaka ya chini na matabaka ya chini yanahudumia matabaka ya juu."

https://www.path-2-happiness

Uzushi: Ni itikati au fikra iliyosimama juu ya mawazo matupu bila ya uwepo wa sababu za kiakili, au za kimantiki au za kielimu, na dini nyingi za ardhini zina uzushi usiokuwa na dalili yoyote au hoja, wala uzushi haujengwi ila kwa uzushi wenyewe, amesema kweli Allah: {… Sema: Leteni hoja zenu kama nyinyi ni wasema kweli.} [27:64].

Migongano: Hizi ni dini ziliojaa migongano, kila kundi linasimama katika kupinga kundi jingine na huziendeleza fikra hizi pinzani, Allah amesema: {…Na lau kuwa imetoka kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu bila ya shaka wangeli kuta ndani yake khitilafu nyingi.} [4:82]

Ama dini za mbinguni ni neema kutoka kwa Allah ambazo Mwenyezi Mungu amewapa wanadamu ili awaongoze na kuwamulikia njia yake na kuwasimamishia hoja juu yake na kuwaepusha, upotofu, ushirikina, kwenda kinyume na maumbile (fitra) na akili kwa kuwatuma Mitume wafikishe ujumbe kutoka kwa Mola wao: {Mitume hao ni wabashiri na waonyaji, ili watu wasiwe na hoja juu ya Mwenyezi Mungu baada ya kuletewa Mitume. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.} [4:165].

https://www.path-2-happiness.com/sw

Migongano ya Kibudha

"Mabudha wanakana Mungu na wanadai (au baadhi yao) kuwa Budha ni mtoto wa Mungu, na wanapinga roho na wanaamini kuwa roho ya marehemu huingia katika mwili wa mtu mwingine."

https://www.path-2-happiness.com/sw

الطريق إلى السعادة
The Path to Happiness

MITUME NA MANABII

https://www.path-2-happiness.com/sw

Yaliyomo

MITUME NA MANABII

JE, WATU WANA HAJA NA MITUME?

UKWELI WA UTUME NA UJUMBE WAKE

DALILI ZA UTUME

MISINGI YA DA'WAH YA MITUME

HISTORIA YA ULUL-'AZM

https://www.path-2-happiness.com/sw

MITUME NA MANABII

JE, WATU WANA HAJA NA MITUME?

Mwenyezi Mungu ameumba viumbe wake katika umbile (fitra) sahihi, na akawawekea akili ili waweze kupambanua baina ya haki kwenye batili, na kwa sababu akili za wanadamu zina mapungufu na udhaifu, matamanio na maslahi, bali na migongano ndani yake.

Katika hali hiyo wanachokiona baadhi ya watu kuwa ni kizuri na wema wengine wanaweza kukiona kuwa kibovu, bali hata mtu mmoja anaweza kubadilika rai yake kwa kubadilika kwa zama na mahali, pamoja na kuwa akili hizo haziwezi kudiriki kilichojificha katika hali halisi katika elimu mbali mbali, kadhalika hawezi kudiriki muradi wa Muumba, maamrisho yake na makatazo yake, mbali na kuwa mwanadamu hawezi kupokea kutoka kwa Allah moja kwa moja, Allah amesema: {Na haikuwa kwa mwanaadamu kwamba Mwenyezi Mungu amsemeze ila kwa Wahyi (Ufunuo), au kwa nyuma ya pazia, au kumtuma Mjumbe. Naye humfunulia ayatakayo kwa idhini yake. Hakika Yeye ni Mtukufu, Mwenye hikima.} [42:51]

Hivyo basi Allah akachagua viumbe vyake bora zaidi miongoni mwa Mitume na Manabii ili wawe mabalozi wazuri baina yake Yeye Allah na waja wake, Allah amesema: {Mwenyezi Mungu huteuwa Wajumbe miongoni mwa Malaika na miongoni mwa watu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona.} [22:75],

Ili wawaongoze watu katika kumuabudu Yeye, na wawaondoshe kwenye dhuluma za kiza na kuwapeleka katika uongofu wa Nuru, ili watu wasiwe na

https://www.path-2-happiness.com/sw

hoja kwa Allah baada ya kupelekewa Mitume –Allah amesema: {Mitume hao ni wabashiri na waonyaji, ili watu wasiwe na hoja juu ya Mwenyezi Mungu baada ya kuletewa Mitume. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.} [4:165].

Hivyo basi suala la kutuma Mitume kwa watu likawa ni jambo kubwa la neema kwa watu kutoka kwa Allah; ili awafundishe kinachowafaa na kinachowatakasa, Allah amesema: {Hakika Mwenyezi Mungu amewafanyia wema mkubwa Waumini vile alivyo waletea Mtume aliye miongoni mwao wenyewe, anaye wasomea Aya zake, na anawatakasa, na anawafunza Kitabu na hikima, ijapo kuwa kabla ya hapo walikuwa katika upotovu ulio wazi.} [3:164].

Kwa hakika neema kubwa kutoka kwa Allah ni kuwatumia watu Mitume, na Mtume huyo kuwa {miongoni mwao},

neema hii inaonekena dhahiri na wazi kuwa Mtume huyu ametumwa na Allah akizungumza na watu kwa maneno matukufu ya Allah Ta'ala, akizungumza na watu kuhusu dhati ya Allah na sifa zake na kuwaeleza ukweli wa Uungu na sifa zake, mbali mbali, kisha akawalingania katika yale yatakayofanya maisha yao yawe mazuri, na awaongoze katika kitakachofaa mioyo yao na hali zao mbali mbali, na kuwalingania na kuwaita katika Pepo ambayo upana wake ni mbingu na ardhi, huu ni ukarimu mkubwa wa neema hii, fadhila hii na utoaji huu? Bali huwatoharisha na huwanyanyua na huwasafisha, husafisha mioyo yao na fikra zao na hisia zao, na husafisha nyumba zao, heshima zao na Swala zao, na hutoharisha maisha yao, jamii zao, na mifumo yao, na huwasafisha wao na uchafu wa ushirikina, upagani na upotofu na masimulizi potofu, na yale ambayo yanapatikana katika maisha haya katika minasaba mbali mbali na desturi mbovu zisizofaa kwa mwanadamu na maana ya utu wake.

Kuwa mtu Usio na Makuu

"Hata katika kilele cha utukufu wake Muhammad alidumu katika hali yake, alikuwa akichukia anapoingia sehemu yenye kundi la watu wakamsimamia au kupitiliza katika kumkaribisha."

Washington Irving
Mwanadiplomasia na mwanafasihi wa Kimarekani

Vivyo hivyo kuwasafisha na uchafu wa maisha ya kijaahiliya, na uchafu ulioenea katika hisia za watu, katika itikadi zao na ufahamu wao wa mambo mbali mbali.

Ujahilia ni Ujahilia, na kila ujahilia una uchafu wake, haijalishi huo ujahilia uko wapi kulingana na zama na mahali, pale ambapo nyoyo za watu zikaepuka na akida ya kiungu inayohukumu muono wao katika sharia ambayo inatokana na akida hii-ambayo ndio itakayohukumu maisha yao basi bila shaka kitakachokuwepo hapa kitakuwa ni Ujahilia katika sura zake mbali mbali, na hapana budi kumuokoa mwanadamu na Ujahilia huu iwe ujahilia huu ni wa zama hizi au wa zama za kale, Ujahiia ndio huo huo, Ujahilia uwe ni ule wa zamani au wa leo hii-sifa zote za Jaahiliya zitapatikana kwenye sifa zile za Ujahilia wa zamani katika upande wa tabia (Akhlaq) na wa kijamii, na utaweka malengo ya maisha ya mwanadamu na hali kadhalika upeo wake (mwisho wake)! Pamoja na kuwa ufunguzi wa elimu za maendeleo na makubwa ya kielimu na viwanda na teknolojia: {…ijapo kuwa kabla ya haya walikuwa katika upotofu ulio dhaahiri.} [62:2]

Upotevu katika mtazamo na itikadi, na upotevu katika malengo ya maisha ni upotevu katika desturi na mifumo, na (tabia), ni upotofu katika nidhamu (mfumo) ni upotevu katika jamii na tabia.

Wanadamu ni Wanyama wanapokataa Dini

Katika takwimu katika moja ya vyuo vikuu nchini Marekani ambavyo yaliandikwa katika kitabu (Amerika ina swali au haiswali) ya David Parton kuwa:

-Asilimia themanini 80% ya wanawake Marekani hubakwa mara moja katika maisha yao!!

-Idadi ya wanawake wenye kubakwa kila siku ni zaidi ya wasichana 19000. Matokeo ya hilo ni kuwa kiasi cha asilimia thelathini 30% ya wasichana huko Marekani ima hupata mimba au hutoa mimba au kujifungua katika umri wa miaka kumi na nne.

-Asilimia sitini na moja (61%) za ya hali ya kubakwa ilikuwa kwa wasichana chini ya miaka kumi na nane.

-Asilimia 29% ya ubakaji ilikuwa kwa watoto chini ya miaka kumi na moja

David Parton

Mwandishi wa Kimarekani



UKWELI WA UTUME NA UJUMBE WAKE

Miongoni mwa hekima ya Allah Ta'ala ni kuwa kila Mtume ni miongoni mwa jinsi ya watu anaowatumia Mtume, Allah amesema: {Nasi hatukuwatuma kabla yako ila watu wanaume tulio wapa Wahyi (Ufunuo)….} [16:43]

Na azungumze kwa lugha ya watu wake ili wafahamu maneno yake, na maana yake, Allah amesema: {Na hatukumtuma Mtume ila kwa ulimi wa kaumu yake ili apate kuwabainishia. Basi Mwenyezi Mungu humuacha akapotea amtakaye, na akamwongoa amtakaye. Naye ni Mtukufu Mwenye nguvu na Mwenye hikima.} [14:4]

Mitume wote husafika kwa utimilifu wa akili na usalama wa fikra zao, na ukweli na uaminifu wa kupokea amana za watu na kuhifadhi, na kuepushwa na dhambi ambayo huharibu mwenendo wa mwanadamu, na viwili wili

https://www.path-2-happiness.com/sw

vyao kuepushwa na vinavyochukiza na macho kutazama, Allah ametakasa nafsi zao na tabia zao, wao ni watu wakamilifu zaidi kwa tabia, na wenye nafsi zilizotakaswa zaidi na mikono yenye ukarimu. Allah Ta'ala amekusanya kwao tabia njema kama alivyokusanya kwao uvumilivu, elimu, usamehevu, ukarimu, ushujaa na uadilifu; kiasi cha kupambanuka katika tabia hizi baina ya watu wao, Mitume ni watu bora zaidi katika viumbe vyake, Mwenyezi Mungu amewachagua kubeba ujumbe na kufikisha amana, Allah amesema: {…Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi kuliko wote kujua wapi anaweka ujumbe wake….} [6:124]

Na akasema: {Hakika Mwenyezi Mungu alimteuwa Adam na Nuhu na ukoo wa Ibrahim na ukoo wa Imran juu ya walimwengu wote.} [3:33]

Na akasema kuhusu Issa ('Alayhi salaam): {Na pale Malaika walipo sema: Ewe Maryamu! Hakika Mwenyezi Mungu anakubashiria (mwana) kwa neno litokalo kwake. Jina lake ni Masihi Isa mwana wa Maryamu, mwenye hishima katika dunia na Akhera, na miongoni mwa walio karibishwa (kwa Mwenyezi Mungu). Naye atazungumza na watu katika utoto wake na katika utuuzima wake, na atakuwa katika watu wema.} [3:45-46],

Na Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) alijulikana kwa watu wake kama "Mkweli mwaminifu." Kabla ya kuteremshwa kwa utume, na Mola wake akamsifu kwa: {Na hakika wewe una tabia tukufu.} [68:4].

Hawa Mitume na Manabii pamoja na sifa alizowasifu nazo Allah Ta'ala miongoni mwa sifa tukufu, ila wao ni watu yanawafika yanayowafika watu wote, wao wanasikia njaa, wanaugua, wanalala, wanakula, wanaoana na wanakufa, Allah amesema: {Na hakika Sisi tulikwisha watuma Mitume kabla yako, na tukajaalia wawe na wake na dhuriya….} [13:38],

Na akasema Mtukuka: {Kwa hakika wewe utakufa, na wao watakufa.}[39:30]

Na akasema kuhusu Mtume wake Muhammad: {…Na ukaficha nafsini mwako aliyo taka Mwenyezi Mungu kuyafichua…} [33:37].

Na katika hali hiyo huenda wakateswa, au wakauwawa, au wakafukuzwa kwenye miji yao, Allah amesema: {Na walipo kupangia mpango walio kufuru wakufunge, au wakuuwe, au wakutoe. Wakapanga mipango yao, na Mwenyezi Mungu akapanga yake. Na Mwenyezi Mungu ndiye mbora wa mipango.} [8:30]

Lakini mwisho wake wao kupata ushindi duniani na akhera.

DALILI ZA UTUME

Mitume na Manabii ambao Allah amewatuma kwa waja wake ni lazima Allah awasimamishie hoja na dalili zinazobainisha ukweli wa Da'wah yao, yenye kuhakikisha kuwa wao ni Mitume wa Allah ili hoja isimame kwa watu, na kusiwe na udhuru kwa kutowasadikisha na kuwatii, Allah amesema: {Kwa hakika tuliwatuma Mitume wetu kwa dalili waziwazi} [57:25].

Miongoni mwa dalili muhimu sana katika hizo ni:

Allah anawapa Mitume na Manabii kwa aya mbali mbali na miujiza, ambayo Allah huipitisha katika mikono ya Mitume na Manabii wake katika mambo ambayo yanavunja mazoea ya kawaida ya kimaumbile ambazo mwanadamu hawezi kufanya, mfano wa hayo ni alama ya Musa ('Alahyi Salaam) pale fimbo yake ilipogeuka kuwa nyoka, Allah amesema: {Na nini hicho kilichomo mkononi mwako wa kulia, ewe Musa? Akasema: Hii ni fimbo yangu; naiegemea na ninawaangushia majani kondoo na mbuzi wangu. Tena inanifaa kwa matumizi mengine. Akasema: Itupe, ewe Musa! Akaitupa. Mara ikawa nyoka anaye kwenda mbio. Akasema: Ikamate, wala usiogope! Tutairudisha hali yake ya kwanza. Na uambatishe mkono wako kwenye ubavu. Utatoka mweupe pasipo kuwa na madhara yoyote. Hiyo ni ishara nyengine. Ili tukuonyeshe baadhi ya ishara zetu kubwa. } [20:17-23]

Na alama ya Issa ('Alahyi Salaam) alipokuwa akiponya mbalanga na ukoma kwa idhini ya Allah, katika ndimi ya Mariam Allah amesema akimbashiria Issa: {Maryamu akasema: Mola wangu Mlezi! Vipi nitampata mwana na hali hajanigusa mwanaadamu? Mwenyezi Mungu akasema: Ndivyo vivyo hivyo, Mwenyezi Mungu huumba apendacho. Anapo hukumu jambo, huliambia: Kuwa! Likawa. Na atamfunza kuandika na Hikima na Taurati na Injili. Na ni Mtume kwa Wana wa Israili kuwaambia: Mimi nimekujieni na Ishara kutoka kwa Mola Mlezi wenu, ya kwamba nakuundieni kwa udongo kama sura ya ndege. Kisha nampuliza anakuwa ndege kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na ninawaponesha vipofu wa tangu kuzaliwa na wakoma, na ninawafufua maiti kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na ninakwambieni mnacho kila na mnacho weka akiba katika nyumba zenu. Hakika katika haya ipo Ishara kwenu ikiwi nyinyi ni wenye kuamini. Na ninasadikisha yaliyo kuwa kabla yangu katika Taurati, na ili nikuhalalishieni baadhi ya yale mlio harimishiwa, na nimekujieni na Ishara kutokana na Mola Mlezi wenu. Kwa hivyo mcheni Mwenyezi Mungu na nit'iini mimi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mola wangu Mlezi na ni Mola wenu Mlezi. Basi muabudni Yeye. Hii ndiyo Njia Iliyo Nyooka. } [3:47-51]

Na alama kubwa kwa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) ambayo ni Qur-aan, pamoja na yeye kutokusoma

kilichoandikwa, Allah amesema: {Sema: Wangeli kusanyika watu na majini ili walete mfano wa hii Qur'ani basi hawaleti mfano wake, hata wakisaidiana wao kwa wao. Na hakika tumewaeleza watu katika hii Qur'ani kwa kila mfano. Lakini watu wengi wanakataa isipo kuwa kukanusha tu.} [17:88 -89].

Na aya nyinginezo kuhusu Mitume na Manabii.

Na kwa kufuatilia na kusoma aya na miujiza ambayo Allah Ta'ala amewapa Mitume na Manabii wake tunaona zinaingia katika mambo matatu: Elimu, uwezo na kujitosha (utajiri) hivyo basi kutoa habari kuhusu mambo ya ghaibu yaliyopita na yajayo; kama vile Issa ('Alahyi Salaam) alivyowaambia watu wake chakula watakachokula na watakachohifadhi katika majumba yao-na Mtume wetu Muhammad kuelezea kuhusu Umma zilizotangulia na kuwajulisha kuhusu mitihani mbali mbali na dalili za Kiama ambazo zitakuja baadae–yote hayo yanatokana na elimu, na kubadilika fimbo kuwa nyoka, na kuponya mbalanga na ukoma, na kufufua watu na Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) kuepushwa na madhambi, na katika mlango wa kudura, na kumlinda kwa aliyetaka kumdhuru, Allah amesema: {Ewe Mtume! Fikisha uliyo teremshiwa kutoka kwa Mola wako Mlezi. Na ikiwa hukufanya hayo basi hukufikisha ujumbe wake. Na Mwenyezi Mungu atakulinda na watu. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi watu makafiri.} [5:67], Mambo haya matatu: elimu, uwezo, na kujitosha (utajiri), ambayo miujiza inarejea haifai



Muujiza wa Milele

"Kwa hakika miujiza ya Manabii waliomtangulia Muhammad katika uhalisia ilikuwa ni miujiza ya wakati maalumu. Ambapo tunaweza kuiita Qur-aan muujiza wa milele: kwani taathira yake ni yenye kudumu na kuendelea. Ni rahisi kwa muumini katika zama na mahali popote kuona muujiza huu kwa kusoma tu katika kitabu cha Mwenyezi Mungu. Katika muujiza huu tunapata sababu ya kuenea kwa kasi kwa Uislamu. Kuenea ambako sababu yake wazungu hawaifahamu; kwa sababu hawajui Qur-aan, au ni kwa sababu hawaifahamu ila kupitia kwenye tafsiri ambazo hazinufaishi kwenye maisha achilia mbali kuwa si sahihi."

Etienne Denier

Mchoraji na Mwanafikra wa Ufaransa



kuwa katika sura ya ukamilifu ila kwa Allah Ta'ala.

1. Bishara ya Manabii waliotangulia kwa Manabii wanaofuatia:

Katika dalili za ukweli wa utume ni manabii waliotangulia kutabiri kuja kwa manabii wanaofuatia, Allah amechukua ahadi na mkataba (Mithaqi) ya kila Mtume ya kuwa lau akimtuma Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalam) katika maisha yake watamuamini, Allah Ta'ala amesema: {Na pale Mwenyezi Mungu alipo chukua ahadi kwa Manabii: Nikisha kupeni Kitabu na hikima, kisha akakujieni Mtume mwenye kusadikisha mliyo nayo, ni juu yenu mumuamini na mumsaidie. Akasema: Je, mmekiri na mmekubali kushika agizo langu juu ya hayo? Wakasema: Tumekubali. Akasema: Basi shuhudieni, na Mimi ni pamoja nanyi katika kushuhudia.} [3:81].

2. MTAZAMO KATIKA HALI ZA MANABII

Manabii na Mitume walikuwa wakiishi na kuchanganyika na watu wao na kuamiliana pamoja nao; na hivyo kuwa rahisi kwa watu kujua nyendo zao, na kujua ukweli wao, hivyo basi pale walipomtuhumu Maryam na mwanae Mtume wa Allah Issa ('Alahyi Salaam) Allah alidhihirisha ukweli wao, Allah amesema: {Akenda naye (mwanawe) kwa jamaa zake amembeba. Wakasema: Ewe Maryamu! Hakika umeleta kitu cha ajabu! Ewe dada yake Harun! Baba yako hakuwa mtu muovu, wala mama yako hakuwa kahaba. Akawaashiria (mtoto). Wakasema: Vipi tumsemeze aliye bado mdogo yumo katika mlezi? (Mtoto) akasema: Hakika mimi ni mtumwa wa Mwenyezi Mungu. Amenipa Kitabu, na amenifanya Nabii. Na amenijaalia ni mwenye kubarikiwa popote pale niwapo. Na ameniusia Sala na Zaka maadamu ni hai, Na nimtendee wema mama yangu. Wala hakunifanya niwe jeuri, mwovu. } [19:27-33].

Ukristo wa Kweli

"Kwa hakika dini ya Ukristo ambayo Muhammad alitaka kuirejesha kwenye asili yake safi kama ambavyo Masihi mwenyewe alivyoibashiri inakwenda kinyume na mafundisho ya siri ambayo ameyatangazwa Paulo na makosa makubwa aliyoyaingiza yaliwagawa sana wakristo.
Matarajio ya Muhammad na hamu yake ni kuwa baraka ya dini ya Ibrahim isiwe kwa watu wake peke yake tu, bali ienee kwa watu wote. Hivyo basi dini yake ya kati kwa kati ikawaongoza na kuwastaarabisha watu milioni nyingi na kama sio dini hii wengi wangeendelea kuzama katika ushenzi na ndio maana wakaupata udugu huu kupitia dini hii ya Kiislamu."

Laitner
Mustashrik kwa Kiingereza

Hivyo ndivyo Issa alivyozungumza utotoni. Makureishi walikuwa wakimuita Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) kabla ya kutimilizwa kwake kuwa ni 'Mkweli Mwaminifu; na hiyo ni kutokana na ukweli wake na uaminifu wake, Qur-aan imeelekeza hilo; ili kutoa dalili ya ukweli wa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) kwa sababu maisha yake binafsi yalikuwa ni dalili kubwa, Allah amesema, {Sema: Mwenyezi Mungu angeli taka nisingeli kusomeeni, wala nisingeli kujuvyeni. Kwani nalikwisha kaa nanyi umri mzima kabla yake! Basi, je! Hamzingatii?} [10:16].

3. MUONO WA DA'WAH YA MTUME

Miongoni mwa dalili za utume na kuafikiana Da'wah ya Mtume katika misingi yake pamoja na misingi ya Da'wah ya Mitume na Manabii wote, hivyo Mtume analingania kwenye Tawhid ya Allah Ta'ala: kwani hili ndilo lengo ambalo kwa ajili yake Mwenyezi Mungu ameumba na kutuma Mitume,

Allah amesema: {Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia ya kwamba hapana mungu isipo kuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu.} [21:25]

Na akasema: {Na waulize Mitume wetu tulio watuma kabla yako: Je! Tulifanya miungu mingine iabudiwe badala ya Rah'mani?} [43:45]

Akasema: {Na kwa hakika kwa kila umma tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Mwenyezi Mungu, na muepukeni Shetani. Basi kati yao wapo alio waongoa Mwenyezi Mungu. Na kati yao wapo ambao ulio wathibitikia upotovu. Basi tembeeni katika ardhi, muangalie ulikuwaje mwisho wa wanao kanusha.} [16:36]

Na katika yote haya ndio iliyokuwa da'wah ya Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) Mtume alikuwa ni sawa na wanadamu wengine ila alifadhilishwa na kukirimiwa na Wahyi, Allah amesema: {Sema: Mimi ni mwanaadamu kama nyinyi. Ninaletewa Wahyi kwamba Mungu wenu ni Mungu Mmoja. Mwenye kutaraji kukutana na Mola wake Mlezi basi naatende vitendo vyema, wala asimshirikishe yeyote katika ibada ya Mola wake Mlezi.} [18:110],

Hivyo basi hawezi kulingania ufalme au uraisi, Allah Ta'ala amesema: {Sema: Mimi sikwambiini kuwa ninazo khazina za Mwenyezi Mungu. Wala sijui mambo yaliyo fichikana. Wala sikwambiini kuwa mimi ni Malaika. Mimi sifuati ila yanayo funuliwa kwangu. Sema: Je, wanakuwa sawa, kipofu na mwenye kuona. Basi hamfikiri?} [6:50]

Ushahidi wa Kweli

"Hakuna siku Muhammad ambavyo alijinasibisha na Uungu au nguvu yoyote ya kustaajabisha. Kinyume chake alikuwa na pupa juu ya maandiko, kuwa yeye alikuwa ni Mtume tu wa Mwenyezi Mungu amemtengeneza kufikishia watu WAHYI.

Rom Landau

Mkosoaji wa Uingereza

https://www.path-2-happiness.com/sw

Wala hawawaulizi watu ujira wa Da'wah yake atoayo Allah amezungumza akiwaelezea Mitume yake Nuuh, Huud Swalah, Luut na Shu'ayb kuwa waliwaambia kaumu yake: {Na sikutakini juu yake ujira, kwani ujira wangu hauko ila kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote. } [26:109] {Kadhalika katika aya zifuatazo vile vile} [26:127, 145, 164 na 180]

Na Muhammad akawaambia watu wake: {Sema (Ewe Mtume): Sikuombeni ujira juu ya haya, wala mimi si katika wadanganyifu.} [38:86]

Kujivua kwa ajili ya Mungu

"Pamoja na kuwa Muhammad alikuwa ni bwana katika Bara Arabu: Hakufikiria lakabu, wala hakushughulika kuyakuza, bali aliendelea kuwa katika hali yake akitosheka kuwa yeye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na kuwa yeye ni Mtumishi wa Waislamu: Husafisha nyumba yake mwenyewe na hushona viatu vyake kwa mkono wake, alikuwa ni mtu mwema na mkarimu kama vile mapito ya upepo, Hakusudiwi na fukara yoyote wala mtu dhalili ila atampa alichonacho, na alichonacho kilikuwa ni kidogo kisicho mtosha yeye mwenyewe.".

Lady Evelin Cobbold

Mwanamama wa Kiingereza

4. NUSURA YA ALLAH NA KUUNGWA KWAO MKONO:

Katika dalili za ukweli wa manabii na waliotumwa vile vile ni Allah kuwanusuru na kuwahifadhi; itaingiaje akilini mtu adai utume au unabii nae ni muongo katika Da'wah yake, halafu baada ya hapo Allah atawalie kumnusuru,

kumuhifadhi, kumuunga mkono na kueneza Da'wah yake, bali hilo halitoshi wala hamteremshii adhabu yake!! Allah amesema: {Wala msiseme uwongo, kwa kuropokwa na ndimi zenu: Hichi halali, na hichi haramu - mkimzulia uwongo Mwenyezi Mungu. Hakika wanao mzulia uwongo Mwenyezi Mungu hawatafanikiwa.} [16:116] Na akasema Mtukuka, {Na lau kama angeli tuzulia baadhi ya maneno tu, Bila ya shaka tungeli mshika kwa mkono wa kulia, Kisha kwa hakika tungeli mkata mshipa mkubwa wa moyo!} [69:44 -46].

Mimi ni mwanadamu kama nyinyi

"Ama kwa hakika Muhammad haiba halisi ya historia, bila yeye Uislamu usingeweza kupanuka na kuongezeka… wala hakusita hata mara moja kusema kuwa yeye ni binadamu kama wengine mwisho wake ni mauti, na kuwa yeye anatafuta msamaha na maghufira (kufutiwa dhambi) kwa Mwenyezi Mungu. Hata kabla ya kifo chake alitaka kusafisha dhamira yake kwa kila kosa dogo alilolifanya. Akasimama mara moja akihutubia: "Enyi Waislamu, kama nitakuwa nimempiga yeyote huu hapa mgongo wangu mtu alipize kisasi chake, au nimemnyang'anya mali yake basi mali yangu ni miliki yake."

Henry Serouya

Mustashrik wa Kifaransa



https://www.path-2-happiness.com/sw

MISINGI YA DA'WAH YA MITUME

Da'wah ya Mitume yote imewafikiana katika misingi maalumu; msingi wa da'wah ya Mitume ni mmoja, Allah Ta'ala amesema: {Amekuamrisheni Dini ile ile aliyo muusia Nuhu na tuliyo kufunulia wewe, na tuliyo wausia Ibrahim na Musa na Isa, kwamba shikeni Dini wala msifarikiane kwayo…} [42:13];

Na ndio maana dini ya Mitume yote ikawa ni moja, Allah amesema, {Enyi Mitume! Kuleni vyakula vizuri na tendeni mema. Hakika Mimi ni Mjuzi wa mnayo yatenda. Na kwa yakini huu Umma wenu ni Umma mmoja, na Mimi ni Mola wenu Mlezi, basi nicheni Mimi.} [23:51-52],

Pamoja na sheria zake kutofautiana, Allah amesema, {Kila mmoja katika nyinyi tumemwekea sharia yake na njia yake} [5:48],

Na lau sheria zingetokea kuwa kinyume na misingi ile basi ingetokea katika hekima, maslahi na huruma, bali ni muhali kuja kinyume na aliyokuja nayo, Allah amesema: {Na lau kuwa Haki ingeli fuata matamanio yao, basi zingeli haribika mbingu na ardhi na waliomo ndani…} [23:71],

Na katika kadhia mbalimbali ambazo Mitume wameafikiana na katika ujumbe wake mbali mbali ni:- -Kumuamini Allah, Malaika wake, kitabu chake, Mitume wake, Siku ya Mwisho, na Qadar kheri na shari yake, Allah Mtukuka amesema: {Mtume ameamini yaliyo teremshwa kwake kutoka kwa Mola Mlezi wake, na Waumini vile vile. Wote wamemuamini Mwenyezi Mungu, na Malaika wake, na Vitabu vyake na Mitume wake. Hatutafautishi baina ya yeyote katika Mitume wake, na (Waumini) husema: Tumesikia na tumet'ii. Tunakutaka maghfira Mola Mlezi wetu! Na marejeo ni kwako.} [2:285].

Amri ya kumuabudu Allah Peke Yake bila ya kumshirikisha yeye na chochote na kumtakasa na kuwa na mke na mtoto, mfano na kuabudu masanamu, Allah Mtukuka amesema: {Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia ya kwamba hapana mungu isipo kuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu} [21:25]

Vivyo hivyo amri ya kufuata njia yake, na kutofuata njia tofauti, na kutekeleza ahadi, na kupima sawa sawa kwa kilo na mizani na wema kwa wazazi wawili na uadilifu baina ya watu na ukweli katika kauli na amali, na kuharamisha maovu yaliyodhihiri na yaliyojificha na uovu na kudhulumu, na kuharamisha kuua watoto, na kuua nafsi pasina haki, na kukataza riba na kula mali ya mayatima, na kukataza ubadhirifu na kiburi na kula mali za watu kwa batili. Imani ya siku ya mwisho; kila mtu ana elimu ya yakini kuwa kuna siku ambayo atakufa, lakini nini baada ya kifo chake? Je, ni mwenye furaha au huzuni? Na kila Mitume na Manabii walifikisha na kuwaambia watu wao kuwa watafufuliwa na kulipwa malipo yao, ikiwa kheri basi atalipwa kheri na ikiwa shari atalipwa shari, na jambo hili la kufufuliwa na kuhesabiwa-akili zilizo salimika zinalikubali, na kuungwa mkono na sheria za Mwenyezi Mungu, kwa hakika Muumba mwenye uwezo, mwenye elimu, mwenye hekima ametakasika kuumba viumbe hivi hivi kwa mchezo na bila ya lengo na kuwaacha hivi hivi tu. Allah amesema, {Na hatukuziumba mbingu na ardhi na viliomo ndani yao bure. Hiyo ni dhana ya walio kufuru. Ole wao walio kufuru kwa Moto utao wapata.} [38:27]

Bali amewaumba viumbe wake kwa hekima kubwa, na kwa lengo tukufu zaidi, Allah amesema, {Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi} [51:56]

Si laiki kwa (Mwenyezi) Mungu huyu mwingi wa hekima kuwafanya sawa wenye kutii na waasi na wale wenye kumfuata na kumuasi Allah amesema, {Je! Tuwafanye walio amini na wakatenda mema kama wafanyao uharibifu katika nchi? Au tuwafanye wachamngu kama waovu?} [38:28];

Hivyo basi ilikuwa ni ukamilifu wa hekima yake na ukubwa wa kudura yake Yeye Allah kuwalipa waja wake kwa matendo yao Siku ya Kiama; hivyo basi mwema atapewa thawabu na atamuadhibu mkosaji, Allah amesema:

{…ili awalipe kwa uadilifu wale walio amini na wakatenda mema. Na walio kufuru, wao watapata vinywaji vinavyo chemka, na adhabu chungu kwa sababu ya walivyo kuwa wakikufuru.} [10:4];

Hivyo basi ni wepesi kiasi gani kuhuisha watu kwa ajili ya kuhesabiwa kwao baada ya mauti, si ndio yeye (Subhaanahu wa Ta'ala) aliyeumba Mbingu na Ardhi?! Na Yeye Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) ameumba viumbe bila mfano uliotangulia, Je, hawezi kurudi kuumba mara nyingine?! Allah amesema: {Je! Hawaoni ya kwamba Mwenyezi Mungu, aliye ziumba mbingu na ardhi, na hakuchoka kwa kuziumba, kuwa ni Muweza wa kuwafufua wafu? Kwani? Hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu.} [46:33]

Na akasema Mtukuka: {Kwani aliye ziumba mbingu na ardhi hawezi kuwaumba mfano wao? Kwani! Naye ndiye Muumbaji Mkuu, Mjuzi.} [36:81]

Kwa hiyo mwenye kuweza kuanzisha kitu mwanzoni ana uwezo wa kukirejesha tena, Allah amesema: {Na Yeye ndiye anaye anzisha uumbaji, kisha ataurudisha mara nyengine. Na jambo hili ni jepesi zaidi kwake. Naye ndiye mwenye mfano bora katika mbingu na ardhi. Na Yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima.} [30:27];

Misingi Misafi

"Uislamu sio dini mpya kutoka kwa Muhammad, lakini ilipoanza kusambaa ardhini baada ya kupita miaka mia sita ya kupaishwa mbinguni kwa masihi. WAHYI wa pili ulianza kushuka, ulikuwa ni ule ule unaounga dini za mbinguni na kuzirejesha kwenye asili yake safi. Mitume wote waliotumwa na Mwenyezi Mungu walikuwa Waislamu na ujumbe wao ulikuwa ni mmoja daima."

Deborah Potter

Mwanahabari wa Kimarekani

Bali ilishatokea kufufuliwa kwa wafu katika maisha haya ya duniani kwa idhini ya Mwenyezi Mungu mbele ya Nabii Ibrahim ('Alahyi Salaam), {Na alipo sema Ibrahim: Mola wangu Mlezi! Nionyeshe vipi unavyo fufua wafu. Mwenyezi Mungu akasema: Kwani huamini? Akasema: Hasha! Lakini ili moyo wangu utue. Akamwambia: Twaa ndege wane na uwazoeshe kwako, kisha uweke juu ya kila kilima sehemu, kisha wete, watakujia mbio. Na ujue kwamba hakika Mwenyezi Mungu ni Mtukufu Mwenye nguvu, na Mwenye hikima.} [2:260]

Na ilitokea hivyo hivyo kwa Issa ('Alahyi Salaam) kwa idhini ya Mwenyezi Mungu Allah amesema, {Na pale Mwenyezi Mungu atapo sema: Ewe Isa bin Maryamu! Kumbuka neema yangu juu yako, na juu ya mama yako, nilipo kutia nguvu kwa Roho Takatifu, ukazungumza na watu katika utoto na utuuzimani. Na nilivyo kufunza kuandika na hikima na Taurati na Injili. Na ulipo tengeneza udongo sura ya ndege, kwa idhini yangu, kisha ukapuliza ikawa ndege kwa idhini yangu; na ulipo waponesha vipofu na wakoma kwa idhini yangu; na ulipo wafufua wafu kwa idhini yangu; na nilipo kukinga na Wana wa Israili ulipo wajia na hoja zilizo wazi, na wakasema walio kufuru miongoni mwao: Haya si lolote ila ni uchawi mtupu!} [5:110]

Tawhidi halisi

"Mtume wa Waarabu Muhammad kwa sauti kutoka kwa Mola wake, amewaita waabudu masanamu, wafuasi wa Ukristo na Uyahudi yaliyopotoka kwenye dini safi ya Tawhidi, na hivyo kuridhia kuingia katika mgogoro mkubwa pamoja na makundi mengine ya watu ambayo yanampeleka mtu katika kumshirikisha Muumba na miungu mingine."

Laura VecciaVaglieri

Mustashrik wa Kitaliano

https://www.path-2-happiness.com/sw

HISTORIA YA ULUL-'AZM

Watu walikuwa katika uongofu na wakatofautiana, Allah akatuma Mitume, ili awafundishe watu na awaonye:

{Yeye ndiye aliye mpeleka Mtume kwenye watu wasio jua kusoma, awasomee Aya zake na awatakase, na awafunze Kitabu na hikima, ijapo kuwa kabla ya haya walikuwa katika upotofu ulio dhaahiri} [62:2]

Lakini watu wakagawanyika kulingana na da'wah ya Mitume katika makundi mawili; kundi lililokubali (lililosadikisha) Mitume na kuamini, na kundi lililokadhibisha Mitume na kuwakana na kile walichokuja nacho, waliwakadhibisha kwa ujeuri; {Watu wote wa likuwa ni umma mmoja. Mwenyezi Mungu akapeleka Manabii wabashiri na waonyaji. Na pamoja nao akateremsha Kitabu kwa Haki, ili kihukumu baina ya watu katika yale walio khitalifiana. Na wala hawakukhitalifiana ila wale walio pewa Kitabu hicho baada ya kuwafikia hoja zilizo wazi, kwa sababu ya uhasidi baina yao. Ndipo Mwenyezi Mungu kwa idhini yake akawaongoa walio amini kwendea haki katika mambo waliyo khitalifiana. Na Mwenyezi Mungu humwongoa amtakaye kwenye Njia Iliyo Nyooka.} [2:213]

Na walikadhibisha kwa kiburi na kufuata matamanio yao, {…Basi kila walipo kufikieni Mitume kwa yale ambayo hayapendwi na nafsi zenu, mlijivuna; wengine mkawakanusha, na wengine mkawauwa.} [2:87].

Allah Ta'ala ameamrisha Mitume wote waaminiwe, {Semeni nyinyi: Tumemuamini Mwenyezi Mungu na yale tuliyo teremshiwa sisi, na yaliyo teremshwa kwa Ibrahim na Ismail na Is-hak na Yaakub na wajukuu zake, na waliyo pewa Musa na Isa, na pia waliyo pewa Manabii wengine kutoka kwa Mola wao Mlezi; hatutafautishi baina ya yeyote katika hao, na sisi tumesilimu kwake.} [2:136],

https://www.path-2-happiness.com/sw

Na akawaahidi watakaoamini Mitume kupata furaha, na uokozi hapa duniani na akhera, na akawakamia watakaokufuru na kuupa mgongo kupata khasara na tabu hapa duniani kabla ya kesho akhera, Allah amesema,

{Na atakaye fanya urafiki na Mwenyezi Mungu na Mtume wake na walio amini, basi hakika kundi la Mwenyezi Mungu ndilo lenye kushinda.} [5:56]

Na akasema vile vile:

{Wale walio amini na zikatua nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndio nyoyo hutua! Wale walio amini na wakatenda mema watakuwa na raha na marejeo mazuri.} [13:28-29]

Na akasema kwa wale waliokufuru Mitume:

{Msiwadhanie walio kufuru kwamba watashinda katika nchi. Na makaazi yao ni Motoni, na hakika ni maovu kweli marejeo yao} [24:57].

Kila Mtume alikuwa na adui zake, Allah amesema:

{Na kadhaalika tumemfanyia kila Nabii maadui mashet'ani wa kiwatu, na kijini, wakifundishana wao kwa wao maneno ya kupamba-pamba, kwa udanganyifu. Na angeli penda Mola wako Mlezi wasingeli fanya hayo. Basi waache na wanayo yazua.} [6:112],

Kisha waliokadhibisha waliwafanyia jeuri Mitume na kuwafanyia uadui, na wakawafanyia istihzai na kuwadharau, Allah amesema:{Na hakuwafikia Mtume ila walimkejeli.} [15:11]

Na akasema Mtukuka:{Na hawajii Nabii yeyote ila walikuwa wakimkejeli.} [43:7]

Na akasema Mtukuka: {Na hakika Mitume walio kabla yako walifanyiwa kejeli, lakini walio wafanyia kejeli wakaja kuzungukwa na yale yale waliyo kuwa wao wanayafanyia kejeli.} [6:10]

Na hali kadhalika wakawatishia kuwafukuza na kuwatoa katika miji yao, au warudi katika dini zao, Allah amesema, {Na walio kufuru wakawaambia Mitume wao: Tutakutoeni katika nchi yetu, au mrudi katika mila yetu. Basi Mola wao Mlezi aliwaletea wahyi: Hakika tutawaangamiza walio dhulumu!} [14:13],

Vitisho hivyo vikafikia kiasi cha kuwauwa, {…Na kila taifa lilikuwa na hamu juu ya Mtume wao wamkamate….} [40:5],

Yaani kumuuwa, kiasi cha miongoni mwao kuuwa Mitume wao, {…Basi kila walipo kufikieni Mitume kwa yale ambayo hayapendwi na nafsi zenu, mlijivuna; wengine mkawakanusha, na wengine mkawauwa} [2:87],

Mwenyezi Mungu baada ya hapo akawaangamiza waliokadhibisha na akadhihirisha dini ya Mitume, kama alivyosema Allah Ta'ala: {Mwenyezi Mungu ameandika: Hapana shaka Mimi na Mtume wangu tutashinda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye kushinda.} [58:21]

Na akasema Mtukuka: {Na bila ya shaka neno letu lilikwisha tangulia kwa waja wetu walio tumwa. Ya kuwa wao bila ya shaka ndio watakao nusuriwa.} [37:171-172]

Na Allah aliokoa Mitume wake wote, kama Allah alivyosema: {Na tukawaokoa wale walio amini na walio kuwa wanamchamngu.} [27:53]

Na akasema vile vile: {Na tukawaokoa walio amini na wakawa wanamcha-mngu.} [41:18]

Na kila Mtume aliyekwenda kwa watu wake na kulazimiana na

Marcel Boisard
Mwanafikra wa Kifaransa

Kutoka katika taa moja.

"Hakukuwepo ndani ya ujumbe wa Muhammad kubatilisha yaliyoteremshwa kabla yake; bali ni kusadikisha upungufu uliovikumba vitabu vya mbinguni kama vile; kubadilisha na kuvunja sheria, na ukalazimishwa kusafisha mafundisho ya Mitume waliyotangulia katika kila kosa. Hivyo kupanuka ndani yake na kuenea kwake: ili iwafae wanadamu wote katika kila zama na mahali."

yanayonasibiana nao kutengeneza maisha yao na kuwatakasa; Basi ambaye atakadhibisha Mtume mmoja, ni kama vile amewakadhibisha Mitume wote, yule ambae hamuamini Issa ('Alahyi Salaam) basi kihakika hatokuwa amemwamini Musa ('Alahyi Salaam), na Muhammad akafuta ujumbe wa Issa ('Alahyi Salaam) Allah amesema:

{Na tumekuteremshia wewe, kwa haki, Kitabu hichi kinacho sadikisha yaliyo kuwa kabla yake katika Vitabu na kuyalinda. Basi hukumu baina yao kwa aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamanio yao ukaacha Haki iliyo kujia….} [5:48]

Kwa hivyo basi ambaye hatomuamini Muhammad kihakika hatakuwa amemuamini Issa ('Alahyi Salaam). Na kuwa ni lazima kuwe Mtume wa mwisho kwa ajili ya watu wote na mahali pote, na sio kwa muda maalumu au fulani, vinginevyo Walimwengu wangepotea na kuangamia bila ya kuwepo msaada wa Wahyi kutoka kwa Muumba wa Ardhi na Mbingu. Hivyo basi Muhammad akawa ndiye Mtume wa mwisho Allah amesema,

{Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na Mwisho wa Manabii, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu} [33:40]

https://www.path-2-happiness.com/sw

NI IPI HISTORIA YA MANABII NA MITUME AMBAYO NDIO HISTORIA YA WANADAMU?

Tunaanzia pale Allah alipotaka kumuumba mwanadamu mpaka kumtoa Adam Peponi na kuteremka ardhini, {Na pale Mola wako Mlezi alipo waambia Malaika: Mimi nitamweka katika ardhi Khalifa (mfwatizi), wakasema: Utaweka
a uharibifu humo na kumwaga damu, hali sisi tunakutakasa
tunakutaja kwa utakatifu wako? Akasema: Hakika Mimi
ua. Na akamfundisha Adam majina ya vitu vyote, kisha
va Malaika, na akasema: Niambieni majina ya hivi ikiwa
Wakasema: Subhanaka, Wewe umetakasika! Hatuna ujuzi
yo tufunza Wewe. Hakika Wewe ndiye Mjuzi Mwenye
Ewe Adam! Waambie majina yake. Basi alipo waambia
a: Sikukwambieni kwamba Mimi ninajua siri za mbinguni
inayajua mnayo yadhihirisha na mliyo kuwa mnayaficha?
ulipo waambia Malaika: Msujudieni Adam, wakamsujudia
isipo kuwa Iblis, alikataa na akajivuna na akawa katika
afiri. Na tulisema: Ewe Adam! Kaa wewe na mkeo katika
ani, na kuleni humo maridhawa popote mpendapo, lakini
karibie mti huu tu; mkawa katika wale walio dhulumu.
ni Shet'ani aliwatelezesha hao wawili na akawatoa katika
vo kuwamo, na tukasema: Shukeni, nanyi ni maadui nyinyi
nyinyi. Katika ardhi yatakuwa makaazi yenu na starehe kwa
a. Kisha Adam akapokea maneno kwa Mola wake Mlezi,
Mola wake Mlezi alimkubalia toba yake; hakika Yeye ndiye
Mwingi wa kukubali toba na Mwenye kurehemu. Tukasema: Shukeni nyote; na kama ukikufikieni uwongofu utokao kwangu, basi watakao fuata uwongofu wangu huo haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika. Na wenye kukufuru na kuzikanusha ishara zetu, hao ndio watakao kuwa watu wa Motoni, humo watadumu.} [2:30-39].

Hatutofautishi baina yao.

"Qur-aan tukufu ni kitabu cha pekee ambacho kinakiri uwepo wa vitabu vingine kutoka mbinguni. Wakati ambapo tunaona vitabu vyote hivyo kila kimoja kinakataa vingine."



Bashir Shaad

Mhubiri wa India.

Kisha baada ya hapo watu wakaupa mgongo uongofu na haki, ndipo alipotuma Mitume wake, Mitume wakafuatana pamoja na sheria zao; {Amekuamrisheni Dini ile ile aliyo muusia Nuhu na tuliyo kufunulia wewe, na tuliyo wausia Ibrahim na Musa na Isa, kwamba shikeni Dini wala msifarikiane kwayo.} [42:13]

Kisha wakafuatana Mitume wa Allah kutokea Idriss hadi Nuhu, Ibrahim, Ismail, Musa, Issa na Muhammad (Swalawatu Llahi Wasalamuhu alayhim jami'an). Allah ametutajia visa vyao na kutujulisha habari zao, hapa tutataja kidogo kuhusu visa vya baadhi yao; kwani visa vyao vimejaa mazingatio kwa wenye akili, Allah Ta'ala amesema: {Kwa hakika katika hadithi zao limo zingatio kwa wenye akili. Si maneno yaliyo zuliwa, bali ni ya kusadikisha yaliyo kabla yake, na ufafanuzi wa kila kitu, na ni uwongofu na rehema kwa kaumu yenye kuamini} [12:111];

Miongoni mwa visa hivyo ni:-

1. NUUH ('Alayhi salaam)

Watu wake hapo kabla walikuwa ni waumini, wakimuabudu Allah peke yake, wakiamini Siku ya Mwisho, na wakifanya mambo mema, watu wale akafa, watu wakahuzunika kwa wema wao na tabia zao njema wakatengeneza picha zao (Wakawapa majina yafuatayo: Wadda, Yaaghutha,Yaa'uqa, Nasra, watu wakavutika na picha zile na…) wakafanya ndio alama za wale watu wema waliokufa miongoni mwao, watu wa mjini wakatukuza picha zile, wakikusudia kuwatukuza wafu wale muda ukapita wale watu wazima wakafa na kubaki watoto na kuwa wakubwa, wakawa wanaongezea namna mbali mbali za kutukuza, na kunyenyekea mbele zao, picha na sura

zile zikawa na nafasi kubwa katika mioyo ya watu wale, ama kizazi cha pili kilichofuatia wakawa wamejiwekea sheria ya kuabudu sura zile na kusema kuwa ile ni miungu inabidi wayasujudie na kunyenyekea mbele yake; wakawa wanayaabudu, wengi wakapotea kwa kufanya hivyo.

Baada ya hapo Allah akawatumia watu wale Mtume Nuhu (‘Alahyi Salaam); ili awaelekeze njia (iliyonyooka), na kuwakataza kuabudu masanamu, na kuwaelekeza kumuabudu Allah Ta’ala, Nuhu (‘Alahyi Salaam) akaenda kwa kaumu yake… {…Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu. Nyinyi hamna mungu asiye kuwa Yeye…} [23:23]

Wakamkadhibisha, na hawakumkubali, akawaonya na kuwatahadharisha adhabu ya Allah Ta’ala. Akasema: {Hakika mimi ninakukhofieni adhabu ya Siku Kubwa.} [26:135],

Wakasema: {Wale watukufu katika kaumu yake wakasema: Hakika sisi tunakuona wewe umo katika upotofu ulio dhaahiri.} [7:60],

Nuhu akawajibu: {Akasema: Enyi watu wangu! Mimi simo katika upotofu, lakini mimi ni Mtume nitokaye kwa Mola Mlezi wa viumbe vyote. Nakufikishieni Ujumbe wa Mola Mlezi wangu, na ninakunasihini; na ninayajua kwa Mwenyezi Mungu msiyo yajua nyinyi.} [7:61-62]

Watu wakashangazwa na maneno ya Nuhu, wakawa wanasema. Wewe ni mtu kama sisi, utakuwaje Mtume kutoka kwa Allah? Na ambao wamekufuata ni kundi la watu dhaifu na watu wa chini, kisha hamna ubora kutushinda sisi, si katika mali wala katika vyeo, na sisi tunadhania kuwa mnadanganya katika madai yenu haya, baadhi ya kaumu wakawaambia wengine: {…Huyu si chochote ila ni mtu tu kama nyinyi. Anataka kujipa ubora juu yenu. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu amependa basi yakini angeli teremsha Malaika. Hatukusikia haya kwa baba zetu wa zamani. Huyu si lolote ila ni mtu mwenye wazimu…} [23:24-25]

Baadhi yao wakahamasisha wengine kuabudu masanamu yao: {Na wakasema: Msiwaache miungu yenu, wala msimwache Wadda wala Suwaa’ wala Yaghutha, wala Yau’qa, wala Nasra.} [71:23].

Nuhu (‘Alayhi salaam) akawaambia: {Je, mnastaajabu kukujieni mawaidha yanayotoka kwa Mola Mlezi wenu kwa njia ya mtu aliye ni mmoja katika nyinyi, ili akuonyeni…} [7:63]

Na baada ya hapo Nuhu akawachukulia kwa upole na ulaini, lakini watu waliendelea na inadi yao, na akawalingania wakati wote mpaka akasema: {Akasema: Ee Mola wangu Mlezi! Hakika mimi nimewaita watu wangu usiku na mchana, Lakini wito wangu haukuwazidisha ila kukimbia. Na hakika mimi kila nilipo waita ili upate kuwaghufiria, walijiziba masikio yao kwa vidole vyao, na wakajigubika nguo zao, na wakakamia, na wakatakabari vikubwa mno! } [71:5-7]

Akawalingania katika kila njia iliyowezekana: {Tena niliwaita kwa uwazi, Kisha nikawatangazia kwa kelele, tena nikasema nao kwa siri.} [71: 9-10],

Wengine wakajiundia nyudhuru duni kwa kusema: {Wakasema: Je! Tukuamini wewe, hali wanao kufuata ni watu wa chini?} [26:111]

Nuhu akawajibu kwa upole na ulaini na kuwakumbusha: {Akasema: Nayajuaje waliyo kuwa wakiyafanya?} [26:112]

Kisha akawaambia: {Hisabu yao haiko ila kwa Mola wao Mlezi, laiti mngeli tambua!} [26:113]

Hoja ikakamilika, udhuru ukakatika, na da'wah ikaendelea takriban karne Kisha Nuhu akasema tena: {Wala mimi si wa kuwafukuza Waumini.} [26:114],

Na, {na mimi sitawafukuza walio amini} [11:29].

Ujumbe wa Mwisho.

"Muhammad ni Mtume aliyeleta Uislamu; na hivyo kuwa kipengele cha mwisho katika mnyororo wa Mitume ambao wamebeba ujumbe mkubwa."

Pro. Rolf Baron

Profesa wa Vyuo Vikuu vya Austria

Vipi nitawafukuza watu ambao wameniamini, wamenihami na wamenisaidia kutangaza da'wah?! Kisha akawaambia: {Na enyi watu wangu! Ni nani atakaye nisaidia kwa Mwenyezi Mungu nikiwafukuza hawa? Basi je, hamfikiri?} [11:30], {Mimi si cho chote ila ni Mwonyaji wa dhaahiri shaahiri.} [26:115].Ninawaonya watu sawa kwa sawa, bila kutofautisha kati ya mtukufu na mnyonge, tajiri na fukara, mkubwa na mdogo na mweupe na mweusi…, watu walipokatikiwa na hoja na kushindwa kujibu dalili za Nuhu, wakawa wanamtisha kumpiga mawe: {Wakasema: Ikiwa huachi, ewe Nuhu, bila ya shaka utapigwa mawe.} [26:116].

Nuhu alipokuwa na yakini kuwa hawakubali maelezo yoyote (mantiki), wala hawaongoki, alinyenyekea kwa Allah amuokoe dhidi ya watu wale wenye inadi, {Akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika watu wangu wamenikanusha.} [26:117]

{Basi hukumu baina yangu na wao kwa hukumu yako, na uniokoe mimi na walio pamoja nami, Waumini.} [26:118]

Pamoja na kuwa Nuhu alikuwa akihofisha kaumu yake na adhabu ya Allah, pindi watakapong'ang'ania ukafiri, baadhi yao walimjibu kwa kejeli: {…Basi tuletee hayo unayo tuahidi, ukiwa miongoni mwa wasemao kweli.} [11:32],

Nuhu akawajibu: "Jambo hili halipo katika mikono yangu": {Akasema: Mwenyezi Mungu atakuleteeni akipenda…} [11:33], {Wala nasaha yangu haikufaini kitu nikitaka kukunasihini…} [11:34].

Allah akamteremshia Wahyi: {…Hataamini yeyote katika watu wako ila wale walio kwisha amini. Basi usisikitike kwa waliyo kuwa wakiyatenda.} [11:36],

kumi, Nuhu alikata tamaa, akamuomba Mola wake, kwa kusema: {Na Nuh'u akasema: Mola wangu Mlezi! Usimwache juu ya ardhi mkaazi wake yeyote katika makafiri! Hakika ukiwaacha watawapoteza waja wako, wala wao hawatazaa ila waovu makafiri.} [71:26-27].

Allah akamteremshia Wahyi wa kutengeneza Meli (Safina): {Tukampa wahyi: Unda jahazi mbele ya macho yetu na uwongozi wetu!...} [23:27]

Akaanza kutengeneza: {Na akawa anaunda jahazi, na kila wakipita wakuu wa kaumu yake wakimkejeli….} [11:38]

Nuhu akawa anawajibu kwa adabu na upole: {…Yeye akasema: Ikiwa nyinyi mnatukejeli na sisi tunakukejelini kama mnavyo tukejeli.} [11:38]

Kisha akiwaonya kwa adhabu ya Allah: {Nanyi mtakuja jua ni nani itakaye mfikia adhabu ya kumhizi, na itakaye mteremkia adhabu ya kudumu.} [11:39]

Na akafanya kazi kwa bidii, hadi alikamilisha kutengeneza Safina.

Kisha Allah akamuamrisha Nuhu kubeba katika safina ile wale walioamini pamoja nae, na kila chenye roho jozi mbili: {Hata ilipo kuja amri yetu, na tanuri ikafoka maji, tulisema: Pakia humo wawili wawili, dume na jike, kutoka kila aina, na ahali zako, isipo kuwa wale ambao imekwisha wapitia hukumu; na watu walio amini. Na hawakuamini pamoja naye ila wachache tu.} [11:40]

Akawabeba wote walioamini pamoja nae jozi mbili mbili, {Na akasema: Pandeni humo kwa Bismillahi, Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, kwenda kwake na kusimama kwake. Hakika Mola wangu Mlezi ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu.} [11:41].

Kiburi na uharibifu wa Historia.

"Katika karne ya kati Wakristo katika maandishi yao walianza kugawa watu kwa misingi ya kikabila na kitaifa kama ilivyotajwa katika agano la kale (Mwanzo) na kuongeza ugawaji wa tabaka jipya: Ikawa ni itikadi iliyoenea kuwa watu wa dini na makasisi wanatokana na kizazi cha Shemu. Wapiganaji wanatokana na kizazi cha Yafith. Mafukara wanatokana na kizazi cha Hamu watoto wa Nuhu ('Alayhi Salaam). Ilifikia kuwa katika mwaka 1964 kumpeleka Senata wa Marekani Robert Byrd kutoka mji wa Virginia ya Magharibi kutumia kisa cha Nuhu kama sababu ya kubaki sera ya ubaguzi katika Marekani.

Nuhu alipopanda na walioamini kwenye Safina pamoja nae, na akachukuwa wanyama, kila mmoja katika mahali pake, mbingu ikaanza kunyesha mvua kubwa, chemchem za ardhi zikaanza kububuja maji mengi: {Basi tukaifungua milango ya mbingu kwa maji yanayo miminika. Na tukazipasua ardhi kwa chemchem, yakakutana maji kwa jambo lilio kadiriwa. Na tukamchukua kwenye safina ya mbao na kamba .Ikawa inakwenda kwa nadhari yetu, kuwa ni malipo kwa alivyo kuwa amekanushwa.} [54:11-14]

Nuhu akamuona mwanae ambae hakuamini pamoja nae akiwa anataka kukimbia ili asizame akamuita: {…Ewe mwanangu! Panda pamoja nasi, wala usiwe pamoja na makafiri} [11:42]

Lakini mtoto alikataa imani, na akakataa nasaha za baba yake, alimjibu Nuhu kwa kusema: {Akasema: Nitakimbilia mlimani unilinde na maji….} [11:43]

Nuhu akamuonea huruma mtoto wake huku akisema: {(Nuhu) akasema: Leo hapana wa kulindwa na amri ya Mwenyezi Mungu ila aliye mrehemu mwenyewe...} [11:43],

Hapo hapo: {…Na wimbi likawatenganisha, akawa katika walio zama} [11:43]

Nuhu akamsikitikia mwanae, na kunyenyekea kwa Allah amuokoe mwanae. Allah alimuahidi kuwaokoa watu wake, Nuhu (‘Alayhi salaam) akasema: {…Ee Mola Mlezi wangu! Hakika mwanangu ni katika ahali zangu, na hakika ahadi yako ni haki. Na Wewe ni Mwenye haki kuliko mahakimu wote.} [11:45].

Allah ambae alimuahidi kuwaokoa watu wake (familia yake) waliokuwa wema, alisema: {Akasema: Ewe Nuhu! Huyu si katika ahali zako. Mwendo wake si mwema….} [11:46],

Katika dini hakuna kuwepo mtu wa kati, huyo si katika watu wako, haitamnufaisha kuwa ni mwanao madamu hakumuamini Allah wala kumpwekesha.

Baada ya maji kufurika kila sehemu, na kila kafiri kuangamia: {Na ikasemwa: Ewe ardhi! Meza maji yako…} [11:44]

Na maji yalioyotoka chini ya ardhi kusita. Allah aliteremshaWahyi, {…Na Ewe mbingu! Jizuie...} [11:44]

na simama kunyesha mvua; mvua ikasimama: {…Basi maji yakadidimia chini…} [11:44]

Hilo ni jabali ambalo safina ilitia nanga juu yake, na Wahyi ukateremka kwa Nuhu ('Alayhi salaam): {…Ewe Nuhu! Shuka kwa salama itokayo kwetu, na baraka nyingi juu yako na juu ya watu walio pamoja nawe…} [11:48]

Nuhu akateremka kutoka katika Safina, na wakataremka waumini waliokuwa pamoja nae, wakajenga mji, na kupanda miti na wakawaacha wanyama waliokuwa nao, na ardhi ikaanza kuimarishwa na watu kuzaana na kuenea.

Mitume kudharauliwa.

Nuhu akaanza kuwa mkulima, akapanda mizabibu; akanywa divai, akalewa; akawa uchi katika hema yake. Hamu, baba wa Kanaani, akauona uchi wa baba yake, akawaeleza ndugu zake wawili waliokuwa nje. Shemu na Yafethi wakatwaa vazi, wakalitanda mabegani mwao wote wawili, wakaenda kinyumenyume, wakaufunika uchi wa baba yao; na nyuso zao zilielekea nyuma, wala hawakuuona uchi wa baba yao. Nuhu akalevuka katika ulevi wake, akajua mwana wake mdogo alivyomtendea. Akasema, Na alaaniwe Kanaani; Atakuwa mtumwa kabisakwa ndugu zake." (Mwanzo: 9:20-25) na hivyo akawabariki Shemu na Yafethi.
Katika tafsiri ya andiko hili Talmud Baabli imetaja. Kitabu Sanhadrin uk. 70 kuwa Kanaani au Hamu aligombana na Nuhu na kumfanyia maovu!! Kamwe haiwezekani kwa Nabii Mtukufu kufanya hivyo.

2. IBRAHIM ('Alayhi salaam)

Ibrahim ('Alahyi Salaam) Mtume wa Tawhidi, hilo linadhihiri katika Historia yake; hivyo ndio maana Allah akamsifu kwa kusema: {Hakika Ibrahim alikuwa mfano mwema, mnyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu, mwongofu, wala hakuwa miongoni mwa washirikina.} [16:120];

Ibrahim aliishi pamoja na kaumu ya washirikina, bali baba yake alikuwa mmoja wa wanaoabudu masanamu na mmoja miongoni mwa wanaoyatengeneza na kuyaabudu, Ibrahim akaanza kujadiliana na baba yake pamoja na kaumu yake: {Na pale Ibrahim alipo mwambia baba yake, Azar: Unayafanya masanamu kuwa ni miungu? Hakika mimi nakuona wewe na watu wako mmo katika opotofu ulio wazi.} [6:74]

Na akapinga yaliyokuwa kwa kaumu yake kwa hoja madhubuti ushirikina wao na akawa anaangalia katika alama na dalili za kuwepo kwake Allah Ta'ala: {Na ulipo muingilia usiku akiona nyota, akasema: Huyu ni Mola Mlezi wangu. Ilipo tua akasema: Siwapendi wanao tua.} [6:76];

Yaani: kuzama kwa nyota: {akasema: Siwapendi wanao tua. Alipo uona mwezi unachomoza…} [6:76-77],

Yaani: Kuchomoza kutoka kwenye upeo wa macho, na akaona baadhi ya watu wakiyaabudu: {…alisema: Huyu ndiye Mola Mlezi wangu…} [6:77].

Akapinga matendo yao, huku akistaajabia ibada zao!! Aliitumia fursa hiyo: {…Ulipotua…} [6:77];

Yaani kupotea chini ya upeo wa macho, alielekea kwa watu wake na kuwaambia: {…akasema: Kama Mola Mlezi wangu hakuniongoa, nitakuwa katika kaumu walio potea. …Na alipo liona jua linachomoza} [6:77-78],

Na akawaona watu wakinyenyekea mbele yake: {…akasema: Huyu ndiye Mola Mlezi wangu. Huyu mkubwa kuliko wote….} [6:78]

Akapinga matendo yao!! Akashangazwa ni kwa nini wamefanya jua kuwa Mungu wao?! {…Lilipo tua…} [6:78],

Na kupotea machoni, aliwaelekea watu wale ambao walikuwa wakiiabudia, akawaambia: {…alisema: Enyi watu wangu! Mimi simo katika hayo mnayo fanyia ushirikina. … Hakika mimi nimeuelekeza uso wangu sawa sawa kwa aliye ziumba mbingu na ardhi, wala mimi si miongoni mwa washirikina.} [6:78-79].

Na alikuwa akimpa sana mawaidha baba yake na kumkataza ushirikina kwa utulivu, adabu na mantiki: {Sema: Nani anaye kulindeni usiku na mchana na Arrahmani Mwingi wa Rehema? Bali wao wanapuuza kumkumbuka Mola wao Mlezi. Au wao wanao miungu watao weza kuwakinga nasi? Hao hawawezi kujinusuru nafsi zao, wala hawatalindwa nasi! Bali tuliwastarehesha hawa na baba zao mpaka umri ukawa mrefu kwao. Je, hawaoni ya kwamba Sisi tunaifikia ardhi tukiipunguza ncha zake? Basi je! Hao ni wenye kushinda? Sema: Mimi nakuonyeni kwa Wahyi. Na viziwi hawasikii wito wanapo onywa.} [21:42-45].

Kwa bahati mbaya jibu la baba yake lilikuwa kali: {(Baba) akasema: Unaichukia miungu yangu, ewe Ibrahim? Kama huachi, basi lazima nitakupiga mawe. Na niondokelee mbali kwa muda!} [19:46].

Jibu la Ibrahim lilikuwa la adabu ya hali ya juu, huruma na upole: {(Ibrahim) akasema: Salamun a'laika! Amani iwe juu yako! Mimi nitakuombea msamaha kwa Mola wangu Mlezi. Hakika Yeye ananihurumia sana. Nami najitenga nanyi na hayo mnayo yaabudu badala ya Mwenyezi Mungu. Na ninamwomba Mola wangu Mlezi; asaa nisiwe mwenye kukosa bahati kwa kumwomba Mola wangu Mlezi.} [19:47-48]

Ibrahim aliendelea kuwalingania watu wake na baba yake kwa Allah na tawhidi yake na kuacha ushirikina, lakini watu wake hawakumuitikia Ibrahim na wakaendeea na ushirikina: {Na watu wake wakamhoji. Akasema: Je, mnanihoji juu ya Mwenyezi Mungu, na hali Yeye ameniongoa? Wala siogopi hao mnao washirikisha naye, ila Mola wangu Mlezi akipenda kitu. Mola wangu Mlezi amekusanya ilimu ya kila kitu. Basi je, hamkumbuki? Na vipi nivikhofu hivyo mnavyo vishirikisha, hali nyinyi hamkhofu kuwa nyinyi mmemshirikisha Mwenyezi Mungu…} [6:80-81],

Na kwa mara nyingine akawaambia: {Alipo mwambia baba yake na kaumu yake: Mnaabudu nini?} [26:70]

Wakamjibu: {Wakasema: Tunaabudu masanamu, daima tunayanyenyekea} [26:71], {Akasema: Je! Yanakusikieni mnapo yaita? Au yanakufaeni, au yanakudhuruni?}[26:72-73],

Likawa jibu la kipumbavu ambalo halitumii akili wala mantiki, kwa kuiga tu: {Wakasema: Bali tumewakuta baba zetu wakifanya hivyo hivyo.}[26:74]

Akawajibu kwa kutumia tawhidi halisi kwa hoja na akili na busara: {Je! Mmewaona hawa mnao waabudu- Nyinyi na baba zenu wa zamani? Kwani hakika hao ni adui zangu, isipo kuwa Mola Mlezi wa walimwengu wote. Ambaye ndiye aliye niumba, na Yeye ndiye ananiongoa, Na ambaye ndiye ananilisha na kuninywesha. Na ninapo ugua ni Yeye ndiye anaye niponesha. Na ambaye atanifisha, na kisha atanihuisha. Na ambaye ndiye ninaye mtumai kunisamehe makosa yangu Siku ya Malipo. Mola wangu Mlezi! Nitunukie hukumu na uniunganishe na watendao mema. Na unijaalie nitajwe kwa wema na watu watakao kuja baadaye. Na unijaalie katika warithi wa Bustani za neema. Na umsamehe baba yangu, kwani hakika alikuwa miongoni mwa wapotovu.}[26:75-86].

https://www.path-2-happiness.com/sw

Ilipofika sikukuu ya kaumu ile, mfalme pamoja na watu wake walikwenda uwanjani jangwani; ili watekeleze na kusherehekea sikukuu huko, Ibrahim hakutoka pamoja nao; walipondoka: "Nao wakamwacha, wakampa kisogo. Basi akaiendea miungu yao kwa siri, akaiambia: Mbona hamli? Mna nini hata hamsemi? Kisha akaigeukia kuipiga kwa mkono wa kulia. " [37:90-93],

Waliporudi wakakuta miungu yao imevunjwa, watakuwaje ni Miungu ambayo haiwezi kujitetea! Walikuja upesi: "Wakasema: Nani aliye ifanyia haya miungu yetu? Hakika huyu ni katika walio dhulumu. Wakasema: Tumemsikia kijana mmoja akiwataja. Anaitwa Ibrahim. Wakasema: Mleteni mbele ya macho ya watu, wapate kumshuhudia! Wakasema: Je! Wewe umeifanyia haya miungu yetu, ewe Ibrahim? " [21:59-62],

Akawajibu kwa hoja kubwa: {Akasema: Bali amefanya hayo huyu mkubwa wao. Basi waulizeni ikiwa wanaweza kutamka.} [21:63]

Wakawa wadogo mbele ya hoja ile: {Basi wakajirudi nafsi zao, wakasema: Hakika nyinyi mlikuwa madhaalimu! Kisha wakarejea kwenye ule ule upotovu wao wakasema: Wewe unajua kwamba hawa hawesemi.} [21:64-65]

Akawajibu kwa hoja kubwa yenye nguvu: {Akasema: Basi nyinyi mnawaabudu asiye kuwa Mwenyezi Mungu wasio kufaini kitu wala kukudhuruni? Aibu yenu nyinyi na hivyo mnavyo viabudu badala ya Mwenyezi Mungu! Basi nyinyi hamtii akilini?} [21:66-67]

https://www.path-2-happiness.com/sw

Wakataka kulipa kisasi baada ya kukosa hoja, mantiki na dalili: {Wakasema: Mchomeni moto, na muinusuru miungu yenu, ikiwa nyinyi ni watendao jambo!} [21:68]

Allah akamuokoa: {Sisi tukasema: Ewe moto! Kuwa baridi na salama kwa Ibrahim! Wao walimkusudia maovu, lakini Sisi tukawafanya wao ndio walio khasiri.} [21:69-70].

Baada ya Allah kumuokoa, akarudi na kujadiliana na mfalme wao: {Hukumwona yule aliye hojiana na Ibrahim juu ya Mola wake Mlezi kwa sababu Mwenyezi Mungu alimpa ufalme? Ibrahim alipo sema: Mola wangu ni yule ambaye huhuisha na kufisha….} [2:258],

Mbele ya hoja hii yenye nguvu iliyo wazi imekuja kuwa jibu la (mfalme) mpumbavu: {…Yeye akasema: Mimi pia nahuisha na kufisha…} [2:258],

Ibrahim hakubishana nae kwenye kuropoka huku, na kutoka katika mjadala huu kuwa anaweza kumuua mtu na kumuacha mtu: {…Ibrahim akasema: Mwenyezi Mungu hulichomozesha jua mashariki, basi wewe lichomozeshe magharibi. Akafedheheka yule aliye kufuru; na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhaalimu.} [2:258]

Udhaifu wa hoja, dalili na mantiki yao ukadhihirika; na baada ya mjadala Ibrahim akataka aone waziwazi namna ambayo Mola wake atahuisha: {Na alipo sema Ibrahim: Mola wangu Mlezi! Nionyeshe vipi unavyo fufua wafu. Mwenyezi Mungu akasema: Kwani huamini? Akasema: Hasha! Lakini ili moyo wangu utue. Akamwambia: Twaa ndege wane na uwazoeshe kwako, kisha uweke juu ya kila kilima sehemu, kisha wete, watakujia mbio. Na ujue kwamba hakika Mwenyezi Mungu ni Mtukufu Mwenye nguvu, na Mwenye hikima.} [2:260].

Allah akamuamrisha Ibrahim pamoja na mwanae Ismail kusafisha nyumba ya Allah ya Makka kutokana na ushirikina na masanamu: {…Na tuliagana na Ibrahim na Ismail: Itakaseni Nyumba yangu kwa ajili ya wanao izunguka kwa kut'ufu na wanao jitenga huko kwa ibada, na wanao inama na kusujudu. Na alipo sema Ibrahim: Ee Mola wangu Mlezi! Ufanye huu uwe mji wa amani, na uwaruzuku watu wake matunda, wale wanao muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Akasema: Na mwenye kukufuru pia nitamstarehesha kidogo, kisha nitamsukumiza kwenye adhabu ya Moto, napo ni pahala pabaya mno pa kurejea. Na kumbukeni Ibrahim na Ismail walipo inyanyua misingi ya ile Nyumba wakaomba: Ewe Mola Mlezi wetu! Tutakabalie! Hakika Wewe ndiye Msikizi Mjuzi. Ewe Mola Mlezi wetu! Tujaalie tuwe ni wenye kusilimu kwako, na pia miongoni mwa vizazi vyetu wawe umma ulio silimu kwako. Na utuonyeshe njia za ibada yetu na utusamehe. Bila shaka Wewe ndiye Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu.} [2:125-128].

Msikiti wa Ibrahim Al-Khalil katika msikiti wa Al-Ibrahimy katika mji wa Al-Khahil huko Palestina.

https://www.path-2-happiness.com/sw

3. MUSA ('Alahyi Salaam)

Bani Israil walikuwa wakisomeshana wenyewe kuhusiana na Mtume Ibrahim ('Alahyi Salaam) kuwa katika kizazi chake atatoka kijana ambae mfalme wa Misri ataangamia kwa mikono yake, utabiri huu ulikuwa ni maarufu kwa Bani Israil. Habari zile zikafika kwa Firauni na maamiri wake walimueleza habari hiyo, hivyo kuamuru kuuwawa kwa wavulana wa Bani Israil kwa kutahadhari na kuwepo kwa kijana huyo. Zama hizo Bani Israil walikuwa wanaishi kwa kuonewa shida na dhuluma kubwa kutoka kwa Firauni: {Hakika Firauni alitakabari katika nchi, na akawagawa wananchi makundi mbali mbali. Akalidhoofisha taifa moja miongoni mwao, akiwachinja watoto wao wanaume na akiwaacha watoto wao wanawake. Hakika yeye alikuwa katika mafisadi.} [28:4]

Allah akataka kuwaneemesha waliodhoofishwa miongoni mwa Bani Israil: {Na tukataka kuwafadhili walio dhoofishwa katika nchi hiyo na kuwafanya wawe waongozi na kuwafanya ni warithi. Na kuwapa nguvu katika nchi, na kutokana na wao kuwaonyesha kina Firauni na Hamana na majeshi yao mambo yale waliyo kuwa wakiyaogopa.} [28:5-6].

Pamoja na Firauni kujihadhari na kukwepa kutopatikana Musa, kiasi cha kuwafanya askari wake wakiwazungukia wenye mimba na wakijua tarehe za kuzaa kwao, hivyo basi alikuwa hazai mwanamke yoyote mtoto wa kiume isipokuwa watamchinja wachinjaji hao muda ule ule, Lakini Allah alitaka kumuoneshe Firauni, Hamana na majeshi yake walichokua wakitahadhari. Pindi mama yake Musa alipozaa: {Tulimfunulia mama yake Musa kwa kumwambia: Mnyonyeshe. Na utakapo mkhofia basi mtie mtoni, na usikhofu wala usihuzunike. Hakika Sisi tutamrudisha kwako na tutamfanya miongoni mwa Mitume.} [28:7]

Hivyo akawa na khofu juu yake, akamuweka katika sanduku la mbao na kumtupa mtoni:{Basi wakamwokota watu wa Firauni, aje kuwa adui kwao na huzuni. Hakika Firauni na Hamana na majeshi yao walikuwa wenye makosa.} [28:8].

Mapenzi ya Musa yakaingizwa moyoni mwa mke wa Firauni: {Na mkewe Firauni alisema: Atakuwa kiburudisho cha macho kwangu na kwako. Msimuuwe! Huenda akatufaa, au tumpange kuwa mwenetu. Wala wao hawakutambua.} [28:9]

Ama mama yake Musa: {Na moyo wa mama yake Musa ukawa mtupu. Alikuwa karibu kumdhihirisha, ingeli kuwa hatukumtia nguvu moyo wake ili awe miongoni mwa Waumini. Naye akamwambia dada yake Musa: Mfuatie. Basi naye akawa anamuangalia kwa mbali bila ya wao kujua.} [28:10-11]

{Na tukamjaalia awakatae wanyonyeshaji wote tangu mwanzo, mpaka dada yake akasema: Je! Nikuonyesheni watu wa nyumba watakao mlea kwa ajili yenu, nao pia watakuwa wema kwake? Basi tukamrudisha kwa mama yake ili macho yake yaburudike, wala asihuzunike. Na ajue ya kwamba ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli, lakini wengi wao hawajui.} [28:12-13].

Musa akakulia katika nyumba ya dhalimu muovu Firauni: {Na Musa alipo fika utu-uzima baraabara, tulimpa akili na ilimu. Na hivi ndivyo tunavyo walipa walio wema. Na akaingia mjini wakati wa kughafilika wenyeji wake, na akakuta humo watu wawili wanapigana - mmoja ni katika wenzake, na mwengine katika maadui zake. Yule mwenzake alimtaka msaada kumpiga adui yake. Musa akampiga ngumi, akamuuwa. Akasema: Hiki ni kitendo cha Shet'ani; hakika yeye ni adui, mpotezaji dhaahiri. Akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika mimi nimejidhulumu nafsi yangu; basi nisamehe. Akamsamehe; hakika Yeye ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu. Akasema: Mola wangu Mlezi! Kwa ulivyo nineemesha, basi mimi sitakuwa kabisa msaidizi wa wakosefu.} [28:14-17].

Lakini baada ya kuua adui yake na adui wa Bani Israil: {Akapambazukiwa mjini asubuhi naye ana khofu, akiangalia huku na huku. Mara yule yule aliye mtaka msaada jana akawa anampigia kelele amsaidie. Musa akamwambia: Hakika wewe ni mgomvi kweli kweli. Basi alipo taka kumshika kwa nguvu yule aliye adui wao wote wawili, akasema: Ewe Musa! Unataka kuniuwa kama ulivyo muuwa mtu jana? Wewe hutaki ila kuwa jabari katika nchi, wala hutaki kuwa miongoni mwa wenye maslaha.. Na akaja mtu kutoka mwisho wa mji akipiga mbio, akasema: Ewe Musa! Wakubwa wanashauriana kukuuwa. Basi toka! Hakika mimi ni katika wanao kupa nasaha. Basi akatoka, naye ana khofu, akiangalia huku na huku. Akasema: Mola wangu Mlezi! Niokoe na watu madhaalimu.} [28:18-21],

Aliondoka Misri na kuelekea Madyan: {Na alipo elekea upande wa Madyana alisema: Asaa Mola wangu Mlezi akaniongoa njia iliyo sawa. Na alipo yafikia maji ya Madyana alikuta umati wa watu wananywesha (wanyama wao), na akakuta karibu yao wanawake wawili wanawazuia wanyama wao. Akasema: Mna nini? Wakasema: Hatunyweshi sisi mpaka wamalize hao wachunga. Na baba yetu ni mzee sana. Basi Musa akawanywesha; kisha akarudi kivulini, na akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika mimi ni mhitaji wa kheri utakayo niteremshia.} [28:22-24].

Wale wasichana wawili wakamwambia baba yao –Nabii wa Allah Shu'ayb – alichokuwa nacho, Nabii wa Allah Shu'ayb ('Alahyi Salaam), akamtuma mmoja wa binti zake kwa Musa ('Alahyi Salaam): {Basi mmoja katika wale wanawake wawili akamjia, naye anaona haya. Akasema: Baba yangu anakwita akulipe ujira wa kutunyweshea….} [28:25].

Musa akafika kwa Shu'ayb ('Alayhima salaam): {…Basi alipo mjia na akamsimulia visa vyake, alisema: Usiogope; umekwisha okoka kwenye watu madhaalimu.} [28:25],

Binti yake mmoja alipoona uaminifu wa Musa ('Alahyi Salaam): {Akasema mmoja katika wale wanawake: Ewe baba yetu! Muajiri huyu. Hakika mbora wa kumuajiri ni mwenye nguvu na muaminifu.} [28:26]

Shu'ayb akamtaka Musa ('Alayhima salaam): {Akasema: Mimi nataka kukuoza mmojawapo katika binti zangu hawa wawili kwa kunitumikia miaka minane. Ukitimiza kumi, khiari yako; lakini mimi sitaki kukutaabisha. Inshallah utanikuta miongoni mwa watu wema. Musa akasema: Hayo yamekwisha kuwa baina yangu na wewe. Muda mmojapo nikiumaliza sitiwi ubayani. Na Mwenyezi Mungu ni Mlinzi juu ya haya tunayo yasema. } [28:27-28].

Musa alipomaliza muda wake alisafiri kwenda kwa watu wake: {Basi alipo timiza muda wake na akasafiri na ahali zake, aliona moto upande wa Mlima T'uri. Akawaambia ahali zake: Ngojeni! Mimi nimeona moto, labda nitakuleteeni kutoka huko khabari au kijinga cha moto ili mpate kuota moto.} [28:29],

Hapo ndipo Allah alipomteremshia Wahyi:



{Basi alipo ufikia aliitwa kutoka ng'ambo ya bonde la kuliani katika eneo lilio barikiwa kutoka kwenye mti: Ewe Musa! Hakika Mimi ni Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote. Na tupa chini fimbo yako. Basi alipo iona ikitikisika kama nyoka, akarudi nyuma wala hakutazama. (Akaambiwa): Ewe Musa! Njoo mbele wala usiogope. Hakika wewe ni miongoni mwa walio salimika. Ingiza mkono wako kwenye mfuko wako, utatoka mweupe pasipo na ubaya. Na jiambatishe mkono wako ukihisi khofu. Basi hizi ni dalili mbili zitokazo kwa Mola wako Mlezi kumpelekea Firauni na wakuu wa umma wake. Hakika hao walikuwa watu mafaasiki.} [28:30-32],

Lakini Musa alimuogopa Firauni kwa sababu alimuua adui yake hapo kabla, na kwa sababu ya fundo lililo kwenye ulimi wake: {Akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika mimi nilimuuwa mtu katika wao, kwa hivyo naogopa wataniuwa. Na ndugu yangu Harun ni fasihi zaidi ulimi wake kuliko mimi. Basi mtume ende nami kunisaidia, ili anisadikishe. Hakika mimi nina khofu watanikadhibisha.} [28:33-34].

https://www.path-2-happiness.com/sw

Akamuomba Allah amfanye ndugu yake Harun, Waziri: {Na nipe waziri katika watu wangu, Harun, ndugu yangu. Kwake yeye niongeze nguvu zangu. Na umshirikishe katika kazi yangu. Ili tukutakase sana. Na tukukumbuke sana. Hakika Wewe unatuona. Akasema: Hakika Umepewa maombi yako, ewe Musa! } [20:29-36].

Walipokwenda kwa Firauni na kumfikishia waliyotumwa katika kumlingania yeye kumuabudu Allah Ta'ala peke yake bila kumshirikisha na chochote na kufungua mateka wa Bani Israil na kuacha kuwakamata, kuwatenza nguvu na kuwanyanyasa na awaache wamuabudu Mola wao watakavyo, na wajishughulishe na kumpwekesha Allah peke yake na kunyenyekea kwake. Firauni akatakabari na kupetuka mipaka na akamuangalia Musa kwa jicho la dharau na kebehi akimwambia: {(Firauni) akasema: Sisi hatukukulea wewe utotoni, na ukakaa kwetu katika umri wako miaka mingi? Na ukatenda kitendo chako ulicho tenda, nawe ukawa miongoni mwa wasio na shukrani? } [26:18-19].

Musa akamjibu: {(Musa) akasema: Nilitenda hayo hapo nilipo kuwa miongoni mwa wale walio potea.} [26:20];

Yaani kabla sijateremshiwa Wahyi na kupewa utume: {Basi nikakukimbieni nilipo kuogopeni, tena Mola wangu Mlezi akanitunukia hukumu, na akanijaalia niwe miongoni mwa Mitume.} [26:21],

Kisha akasema akimjibu Firauni alivyojisifu kumlea na kumfanyia wema:

{Na hiyo ndiyo neema ya kunisumbulia, na wewe umewatia utumwani Wana wa Israili?} [26:22];

Yaani neema hii uliyoitaja ya kwamba ulinifanyia mema na mimi ni mtu mmoja katika Bani Israil na kwa upande wa pili umewatumikisha watu hawa wa Bani Israil kwa ukamilifu na kuwafanya kuwa watumwa katika kukutumikia na kukuhudumia katika shughuli zako. Kisha Firauni akamuulizia Mola ambae Musa anamlingania: {Firauni akasema: Na nani huyo Mola Mlezi wa walimwengu wote?} [26:23],

Likaja jibu linalo kinaisha: {Akasema: Ndiye Mola Mlezi wa mbingu na ardhi, na viliomo baina yao, ikiwa nyinyi ni wenye yakini.} [26:24],

Firauni akaanza kebehi: {(Firauni) akawaambia walio mzunguka: Hamsikilizi?} [26:25],

Musa akaendelea na kulingania watu wote: {(Musa) akasema: Ndiye Mola wenu Mlezi, na Mola Mlezi wa baba zenu wa kwanza.} [26:26],

Firauni akazidisha uovu wake: {(Firauni) akasema: Hakika huyu Mtume wenu aliye tumwa kwenu ni mwendawazimu.} [26:27],

Hata hivyo, Mtume wa Allah Musa hakuacha kadhia yake: {(Musa) akasema: Ndiye Mola Mlezi wa Mashariki na Magharibi na viliomo baina yao, ikiwa nyinyi mnatia akilini.} [26:28],

Dikteta mkubwa mwenye kiburi na kujikweza Firauni aliyekosa hoja na akili na mantiki alianza vitisho: {(Firauni) akasema: Ukimfuata mungu mwengine asiye kuwa mimi, basi bila ya shaka nitakufunga gerezani.} [26:29],

Kama ambavyo kebehi na dharau za Firauni hazikumuondosha Musa katika da'wah yake, hata vitisho vya Firauni havikumfanya kuacha

https://www.path-2-happiness.com/sw

da'wah yake; hivyo alimjibu: {Akasema: Je! Ijapo kuwa nitakuletea kitu cha kubainisha wazi? Akasema: Kilete basi, kama wewe ni katika wasemao kweli. Basi akaitupa fimbo yake, mara ikawa nyoka wa kuonekana dhaahiri. Na akautoa mkono wake, na mara ukawa mweupe kwa watazamao.} [26:30-33],

Firauni akaogopea watu wasije kumuamini (Musa), hivyo akawaambia watu wake: {(Firauni) akawaambia waheshimiwa walio mzunguka: Hakika huyu ni mchawi mtaalamu. Anataka kukutoeni katika nchi yenu kwa uchawi wake. Basi mna shauri gani? Wakasema: Mpe muda yeye na nduguye na uwatume mijini wapigao mbiu ya mgambo. Wakuletee kila mchawi bingwa mtaalamu. " [26:34-37]

Baada ya Firauni kuona hoja zote alifanya jeuri na kukana na kukataa: {Na hakika tulimwonyesha ishara zetu zote. Lakini alikadhibisha na akakataa. Akasema: Ewe Musa! Hivyo umetujia kututoa katika nchi yetu kwa uchawi wako? Basi sisi hakika tutakueletea uchawi kama huo. Basi weka miadi baina yetu na wewe, ambayo tusiivunje sisi wala wewe, mahali patapo kuwa sawa. Akasema: Miadi yenu ni siku ya Sikukuu; na watu wakusanywe kabla ya adhuhuri. Basi Firauni akarudi na akatengeneza hila yake, kisha akaja. } [20:56-60],

Musa akawaogopea kupata adhabu ya Allah: {Musa akamwambia: Ole wenu! Msimzulie Mwenyezi Mungu uwongo, asije akakufutilieni mbali kwa adhabu. Na mwenye kuzua lazima ashindwe!} [20:61];

Hivyo wakatofautiana, baadhi yao wakasema: haya si maneno ya mchawi: {Basi wakazozana kwa shauri yao wenyewe kwa wenyewe, na wakanong'ona kwa siri.} [20:62].

Lakini wao wakarejea, wengi wao wakasema: {Wakasema: Hakika hawa wawili ni wachawi, wanataka kukutoeni katika nchi yenu kwa uchawi wao, na waondoe mila zenu zilizo bora kabisa. Kwa hivyo kusanyeni hila zenu zote, kisha mfike kwa kujipanga safu, na kwa yakini atafuzu kweli kweli leo atakaye

https://www.path-2-happiness.com/sw

shinda.} [20:63-64] {Akasema: Bali tupeni nyinyi! Tahamaki kamba zao na fimbo zao zikaonekana mbele yake, kwa uchawi wao, kuwa zinapiga mbio. } [20:66]

Musa akaogopea wale wachawi wasije wakawafitinisha: {Basi Musa akaingia khofu nafsi yake.} [20:67],

Allah akamteremshia Wahyi; Musa: {Tukasema: Usikhofu! Hakika wewe ndiye utakaye shinda. Na kitupe kilicho katika mkono wako wa kulia; kitavimeza walivyo viunda. Hakika walivyo unda ni hila za mchawi tu, na mchawi hafanikiwi popote afikapo.} [20:68-69], {Nasi tukamfunulia Musa kumwambia: Tupa fimbo yako. Mara ikavimeza vyote vile walivyo vibuni. Kweli ikathibiti na yakabat'ilika waliyo kuwa wakiyatenda.} [7:117-118],

Kwa ghafla (likatokea jambo lisilotarajiwa): {Kwa hivyo walishindwa hapo, na wakageuka kuwa wadogo. Na wachawi wakapoomoka wakisujudu. Wakasema: Tumemuamini Mola Mlezi wa viumbe vyote, Mola Mlezi wa Musa na Haarun.} [7:119-122], {Basi wachawi wakaangushwa wanasujudu. Wakasema: Tumemuamini Mola Mlezi wa Harun na Musa! } [20:70],

Vitisho vya Firauni vikaonekana kama upumbavu: {(Firauni) akasema: Oh! Mnamuamini kabla sijakupeni ruhusa? Hakika yeye ndiye mkubwa wenu aliye kufundisheni uchawi. Basi kwa yakini nitakukateni mikono yenu na miguu yenu kwa kutafautisha. Na nitakutundikeni misalabani katika vigogo vya mitende.... } [20:71],

Jibu lao halikutarajiwa kwa Firauni, na huu ni uthibitisho wa wazi jinsi Imani inavyomfanya aliyeamini: {Wakasema: Haidhuru, kwani sisi ni wenye kurejea kwa Mola wetu Mlezi. Hakika sisi tunatumai Mola wetu Mlezi atatusamehe makosa yetu, kwa kuwa ndio wa kwanza wa kuamini.} [26:50-51].

Firauni akaendelea kuwaudhi waumini; Allah akamuadhibu pamoja na walio nae: {Na hakika tuliwaadhibu watu wa Firauni kwa miyaka (ya ukame) na kwa upungufu wa mazao, ili wapate kukumbuka. Likiwafika jema wakisema: Haya ni haki yetu. Na likiwafika ovu husema: Musa na walio pamoja naye ni wakorofi. Hakika ukorofi wao huo unao wafikia unatoka kwa Mwenyezi Mungu. Lakini wengi wao hawajui. } [7:130-131],

Hawakuamini wala kutubia: {Na wakisema: Hata ukituletea Ishara yoyote

kutuzuga hatuto kuamini. Basi tukawapelekea tufani, na nzige, na chawa, na vyura, na damu, kuwa ni Ishara mbali mbali. Nao wakapanda kiburi, na wakawa watu wakosefu.} [7:132-133],

Walipochoka:

{Na ilipo waangukia adhabu wakasema: Ewe Musa! Tuombee kwa Mola wako Mlezi kwa aliyo kuahidi. Ukituondolea adhabu hii hapana shaka tutakuamini, na tutawaachilia Wana wa Israili wende nawe. Lakini tukiwaondolea adhabu mpaka muda fulani wao waufikie, mara wakivunja ahadi yao.} [7:134-135],

Hawakutekeleza waliyoyaahidi, bali walitengua waliyoyasema:

{Basi tuliwapatiliza, tuka-wazamisha baharini kwa sababu walizikanusha Ishara zetu, na wakaghafilika nazo.} [7:136].

Watu wa Misri walipozama katika ukaidi, ukafiri na inadi yao na kumfuata mfalme wao, na kwenda kinyume na Nabii wao na Mtume wao Musa bin Imran ('Alahyi Salaam), na baada ya Allah kuwasimamishia hoja kubwa na kuwaonesha miujiza, lakini pamoja na yote hayo hawakuacha wala hawakurudi nyuma, na hawakuamini isipokuwa wachache miongoni mwa kaumu ya Firauni.

Ama wachawi wote, na Bani Israil wote, Imami zao zilikuwa za kificho kwa kumuogopa Firauni na dhuluma zake, ujeuri na ubabe wa utawala wake. Mwenyezi Mungu alimteremshia wahyi Musa pamoja na nduguye Harun ('Alahyi Salaam) wajiwekee majumba maalumu miongoni mwao tofauti na nyumba za watu wa Firauni; ili wawe katika matayarisho ya kuhama pindi watakapoamrishwa ili waweze kufahamiana nyumba zao, na ili wamuabudu Allah huko:

{Na tukampelekea Musa na ndugu yake wahyi huu: Watengenezeeni majumba watu wenu katika Misri na zifanyeni nyumba zenu ndio mwahali mwa ibada, na wabashirie Waumini.} [10:87].

Kisha Allah akamteremshia Wahyi mja wake Musa:

{Na tulimuamrisha Musa kwa wahyi: Nenda na waja wangu wakati wa usiku. Kwa hakika mtafuatwa. } [26:52],

Jibu la Firauni likawa:

{Basi Firauni akawatuma mijini wapiga mbiu za mgambo. (Wakieneza): Hakika hawa ni kikundi kidogo. Nao wanatuudhi. Na sisi ni wengi, wenye kuchukua hadhari.} [26:53-56],

Na Allah akataka:

{Basi tukawatoa katika mabustani na chemchem, Na makhazina, na vyeo vya hishima, Kadhaalika; na tukawarithisha hayo Wana wa Israili.} [26:57-59]

Wakawafuata Bani Israil:

{Basi wakawafuata lilipo chomoza jua. } [26:60],

Walipofika kwa Bani Israil:

{Na yalipo onana majeshi mawili haya, watu wa Musa wakasema: Hakika sisi bila ya shaka tumepatikana! } [26:61],

Lakini jibu la Musa lilikuwa limejaa tumaini la Allah, kumjua na kumtegemea yeye Allah Ta'ala:

{(Musa) akasema: Hasha! Hakika yu pamoja nami Mola wangu Mlezi. Yeye ataniongoa!} [26:62],

Baada ya hapo hidaya ya Allah na rehma zake zikateremka:

{Tulimletea wahyi Musa tukamwambia: Piga bahari kwa fimbo yako. Basi ikatengana, na kila sehemu ikawa kama mlima mkubwa. Na tukawajongeza hapo wale wengine. Tukawaokoa Musa na walio kuwa pamoja naye wote. Kisha tukawazamisha hao wengine. Hakika bila ya shaka katika hayo ipo Ishara; lakini wengi wao si katika wenye kuamini. Na kwa hakika Mola wako Mlezi ndiye Mwenye nguvu Mwenye kurehemu.} [26:63-68].

Katika wakati huu mgumu wenye kutisha:

{Tukawavusha bahari Wana wa Israili, na Firauni na askari wake wakawafuatia kwa dhulma na uadui!...} [10:90],

Hapa ndipo Firauni alipoyakinisha mauti na kuangamia:

{…Hata Firauni alipo kuwa anataka kuzama akasema: Naamini kuwa hapana mungu ila yule waliye muamini Wana wa Israili, na mimi ni miongoni mwa walio nyenyekea} [10:90],

Lakini alishachelewa; kwani mauti yalishamdiriki: {Ala! Sasa? Na hali uliasi kabla yake na ukawa miongoni mwa mafisadi! } [10:91],

Mwenyezi Mungu akatimiza neema yake kwa Bani Israil kwa kumuangamiza adui yao na walipovuka bahari: {Na tukawavusha bahari Wana wa Israili, wakafika kwa watu wanao abudu masanamu yao. Wakasema: Ewe Musa! Hebu tufanyie na sisi miungu kama hawa walivyo kuwa na miungu….} [7:138];

Yaani ombi la mjinga baada ya neema ya kuokolewa na Allah dhidi ya Firauni na majeshi yake: {…Musa akasema: Hakika nyinyi ni watu msio jua kitu. Hakika haya waliyo nayo watu hawa yatakuja angamia, na hayo waliyo kuwa wakiyafanya yamepotea bure.} [7:138-139],

Kisha Musa akaenda katika kiaga na Mola wake: {Tulimuahidi Musa masiku thalathini na tukayatimiza kwa kumi; ikatimia miadi ya Mola wake Mlezi masiku arubaini. Na Musa akamwambia nduguye Haarun: Shika mahala pangu kwa watu wangu na utengeneze wala usifuate njia ya waharibifu. } [7:142],

Allah akazungumza na Musa na akamfanya mahsusi kwa maneno yake na ujumbe wake: {(Mwenyezi Mungu) akasema: Ewe Musa! Mimi nimekuteuwa wende kwa watu na Ujumbe wangu na maneno yangu. Basi chukua niliyo kupa na uwe katika wanao shukuru.} [7:144]

Na akamneemesha kwa mawaidha na Taurati ambayo ndani yake kuna hukumu za Allah: {Na tukamuandikia katika mbao kila kitu, mawaidha na maelezo ya mambo yote. (Tukamwambia): Basi yashike kwa nguvu na uwaamrishe watu wako wayashike kwa ubora wake. Nami nitakuonyesheni makaazi ya wapotofu.} [7:145],

Kiaga ilipotimia, na Mola wake akampa Musa Taurati, Musa alirudi kwa watu wake na akawakuta: {Na baada yake watu wa Musa walimfanya ndama kutokana na mapambo yao (kumuabudu), kiwiliwili tu kilicho kuwa na sauti. Hivyo, hawakuona kuwa hawasemezi wala hawaongoi njia? Wakamuabudu, na wakawa wenye kudhulumu. Na walipo juta na wakaona ya kwamba wamekwisha potea, walisema: Ikiwa Mola wetu Mlezi hakuturehemu na akatusamehe, bila ya shaka tutakuwa miongoni mwa walio khasiri.} [7:148-149],

Ikawa ni habari yenye kuumiza sana kwa Musa: {Na alipo rudi Musa kwa watu wake, naye amekasirika na kuhuzunika, alisema: Ni maovu yalioje mlio nifanyia nyuma yangu! Je, mmeitangulia amri ya Mola wenu Mlezi? Na akaziweka chini zile mbao, na akamkamata kichwa ndugu yake akimvutia kwake. (Haarun) akasema: Ewe mwana wa mama yangu! Hakika hawa watu wamenidharau, na wakakaribia kuniuwa. Basi usiwafurahishe maadui juu yangu, wala usinifanye pamoja na watu madhaalimu. (Musa) akasema: Mola Mlezi wangu! Nisamehe mimi na ndugu yangu, na ututie katika rehema yako. Nawe ni Mwenye kurehemu kushinda wote wenye kurehemu.} [7:150-151],

Kisha akaongea na Saamiriy aliyetengeneza ndama yule, akasema: {(Musa) akasema: Ewe Msamaria! Unataka nini?} [20:95]

Akamjibu: {Akasema: Niliona wasiyo yaona wao, nikashika gao katika unyao wa Mtume. Kisha nikalitupa. Na hivi ndivyo ilivyo nielekeza nafsi yangu.} [20:96];



Jibu la Musa likawa jibu lenye nguvu lenye kukata hoja zote za kumshirikisha Allah: {(Musa) akasema: Basi ondoka! Na kwa yakini utakuwa katika maisha ukisema: Usiniguse. Na hakika una ahadi kwako isiyo vunjwa. Na mtazame huyo mungu wako uliye endelea kumuabudu - Sisi kwa hakika tutamchoma moto, kisha tutamtawanya baharini atawanyike. Hakika Mungu wenu ni Allah, Mwenyezi Mungu, tu. Hapana Mungu isipo kuwa Yeye. Ujuzi wake umeenea kila kitu. } [20:97-98],

Kisha Musa akaenda nao kuelekea ardhi tukufu, baada ya kuchukua mbao (za maandiko):{Na Musa ilipo mtulia ghadhabu aliziokota zile mbao. Na katika maandiko yake mna uwongofu na rehema kwa wanao mwogopa Mola wao Mlezi.} [7:154],

Baadhi ya Bani Israil walikuwa hawakubali yaliyomo katika Taurati; Allah akanyanyua Jabali juu yao: {Na pale tulipo unyanyua mlima juu yao ukawa kama kwamba ni kiwingu kilicho wafunika, na wakadhani kuwa utawaangukia, (tukawaambia): Kamateni kwa nguvu tuliyo kupeni, na yakumbukeni yaliyomo ndani yake ili mpate kumcha Mungu.} [7:171],

Hivyo wakachukua pamoja na kuwa kuna uongofu kwao na rehema kwa kuogopea jabali lisije kuwaangukia, wakaendelea kuwafanyia maudhi Bani Israil pamoja na Mtume wao Musa ('Alahyi Salaam). Basi mara moja wakauwa mtu, na mtu yule alikuwa ni Bani Israil tajiri, mtoto wa nduguye alimpitia usiku na akamchinja! Wakatofuatiana na kutuhumiana na kila mmoja akajitetea, wakamfuata Mtume wao Musa ('Alayhi salaam), na kumwambia kwa jeuri na adabu mbovu; ikiwa wewe Musa ni nabii basi muulize Mola wako! Allah akamuamrisha Musa: Ewe Musa waamrishe Bani Israil wachinje ng'ombe, kisha wachukue kiungo chake wampige nacho maiti; nami nitamuhuisha kwa idhini yangu; hivyo maiti Yule atazungumza na kumtaja aliyemuua, Allah amesema: {Na mlipo muuwa mtu, kisha mkakhitalifiana kwayo, na Mwenyezi Mungu ni mwenye kuyatoa hayo mliyo kuwa mkiyaficha. Tukasema: Mpigeni kwa kipande chake (huyo ng'ombe). Ndivyo hivi Mwenyezi Mungu huwahuisha wafu; na anakuonyesheni Ishara zake ili mpate kufahamu.} [2:72-73],

As-Samiry – Mtengeneza Ndama wa Sanamu.

Haiwezekani Mtume wa Allah Harun kuwa ndie aliyetengeneza ndama na kulingania ushirikina: Mitume wote walikuwa ni walinganizi wa Tawhid. Atakayenukuu yasiyokuwa hayo amepotoka, mfano wa hayo yaliyokuja:

"Harun akawaambia: Zivunjeni pete za dhahabu zilizo katika masikio ya wake zenu, na wana wenu, na binti zenu, mkaniletee. Watu wote wakazivunja pete za dhahabu zilizo katika masikio yao, wakamletea Haruni. Akaipokea mikononi mwao akaitengeneza kwa patasi, akaifanya iwe sanamu ya ndama kwa kuiyeyusha; na wakasema, Hiyo ndiyo miungu yako, Ee Israeli, iliyo kutoka katika nchi ya Misri." (Kutoka: 32/2-4). Agano la kale.

Musa akasema: Chinjeni ng'ombe, na wangemchukua ng'ombe yeyote ingetosha lakini kutokana na maudhi yao Allah akasema kwa ulimi wa Musa: {Na Musa alipo waambia watu wake: Hakika Mwenyezi Mungu anakuamrisheni mchinje ng'ombe. Wakasema: Je! Unatufanyia mzaha? Akasema: Audhubil lahi! Najikinga kwa Mwenyezi Mungu nisiwe miongoni mwa wajinga. } [2:67]

Watu wakajibu: {Wakasema: Tuombee kwa Mola wako Mlezi atupambanulie ni ng'ombe gani?...} [2:68]

Walikazania nae Allah akawakazania: {…Akasema: Hakika Yeye anasema kwamba ng'ombe huyo si mpevu, wala si kinda….} [2:68]

Sio mkubwa mzee wala mdogo: {…Akasema: Hakika Yeye anasema kwamba ng'ombe huyo si mpevu, wala si kinda, bali ni wa katikati baina ya hao. Basi fanyeni mnavyo amrishwa.} [2:68]

Wakajifunga zaidi: {Wakasema: Tuombee kwa Mola wako atupambanulie nini rangi yake?...} [2:69],

Allah hakuwauliza rangi na hakuwawekea sharti maalumu: {…Akasema: Yeye anasema, kuwa ng'ombe huyo ni wa manjano, na rangi yake imekoza, huwapendeza wanao mtazama.} [2:69],

Wakakusanyika katika baraza maalum, kisha wakarudia maneno yao: {Wakasema: Tuombee kwa Mola wako Mlezi atupambanulie ni yupi? Hakika tunaona ng'ombe wamefanana. Na kwa yakini, Inshaallah, Mwenyezi Mungu akipenda, tutaongoka. } [2:70],

https://www.path-2-happiness.com/sw

Allah akawajibu: {Akasema: Yeye anasema: Kuwa huyo ni ng'ombe asiye tiwa kazini kulima ardhi wala kumwagia maji mimea, mzima, hana baka. Wakasema: Sasa umeleta haki. Basi wakamchinja, na walikaribia kuwa wasifanye hayo.} [2:71],

Wakatafuta katika miji na vijiji vya Bani Israil, kijiji hadi kijiji; wakampata ng'ombe huyu kwa tabu na taklifu kubwa na kwa thamani ghali mno; wakamchinja na hawakuwa wakitaka hilo, wakampiga maiti ambaye wametofautiana ni nani aliyemuua kwa sehemu ya kiungo cha ng'ombe yule; maiti Yule akaamka kwa kutetema na hasira; akaamka akiwa hai kutoka kaburini kwake kwa idhini ya Allah akiwa amesimama, Musa akamuuliza: Ni nani aliyekuuwa? Akasema: Huyu hapa: {Tukasema: Mpigeni kwa kipande chake (huyo ng'ombe). Ndivyo hivi Mwenyezi Mungu huwahuisha wafu; na anakuonyesheni Ishara zake ili mpate kufahamu.} [2:73].

Walipofika katika ardhi tukufu, waliwakuta watu wenye nguvu (majabari): {Na pale Musa alipo waambia watu wake: Enyi watu wangu! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilizo juu yenu, alipo wateuwa Manabii kati yenu, na akakufanyeni watawala, na akakupeni ambayo hakuwapa wowote katika walimwengu. Enyi watu wangu! Ingieni katika nchi takatifu ambayo Mwenyezi Mungu amekuandikieni. Wala msirudi nyuma, msije mkawa wenye kukhasirika. Wakasema: Ewe Musa! Huko wako watu majabari. Nasi hatutaingia huko mpaka wao watoke humo. Wakitoka humo hapo tutaingia.} [5:20-22], {Wakasema: Ewe Musa! Sisi hatutaingia humo kamwe maadamu wao wamo humo. Basi nenda wewe na Mola wako Mlezi mkapigane. Sisi tutakaa hapa hapa.} [5:24];

Allah akawakosoa kwa udhaifu wao, na akawaadhibu kwa upotofu na kuacha kwao jihadi na kwenda kinyume na Mtume wao, Musa akasema: {Akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika mimi similiki ila nafsi yangu na ndugu yangu. Basi tutenge na hawa watu wapotovu. } [5:25],

Allah Mtukuka akamuitikia: {(Mwenyezi Mungu) akasema: Basi nchi hiyo wameharimishiwa muda wa miaka arubaini, watakuwa wakitanga-tanga katika ardhi. Basi wewe usiwasikitikie watu wapotovu. } [5:26],

Wakawa wanatembea katika ardhi bila malengo usiku na mchana, asubuhi na jioni.

4. ISSA BIN MARYAM (‘Alayhi salaam).

Baba yake Maryam (‘Alahyi Salaam) alikuwa ni ‘Imran, mja miongoni wa waja wa Bani Israil, alitokana na kizazi cha Dawud (‘Alahyi Salaam), katika nyumba ya wacha-Mungu, mama yake Maryam alikuwa hashiki mimba, akatamani kupata mtoto; akaweka nadhiri kwa Allah kuwa akipata mimba atamtoa mwanae wakfu kuitumikia dini na msikiti mtukufu (yaani mpenzi katika nyumba tukufu):

{Alipo sema mke wa Imran: Mola wangu Mlezi! Nimekuwekea nadhiri kilichomo tumboni mwangu kuwa wakfu; basi nikubalie. Hakika Wewe ndiye Mwenye kusikia na Mwenye kujua. Basi alipo mzaa alisema: Mola wangu Mlezi! Nimemzaa mwanamke - na Mwenyezi Mungu anajua sana aliye mzaa - Na mwanamume si sawa na mwanamke. Na mimi nimemwita Maryamu. Nami namkinga kwako, yeye na uzao wake, uwalinde na Shet’ani aliye laaniwa.} [3:35-36];

Allah akamkubalia mama yake Maryam nadhiri yake:

{Tena Mola wake Mlezi akampokea kwa mapokeo mema na akamkuza makuzo mema…} [3:37]

Katika sura nzuri na mandhari ya furaha na njia ya waja wema wenye furaha; na hivyo basi Allah akasema: {…na akamfanya Zakariya awe mlezi wake…} [3:37]

Allah akamneemesha kwa mlezi wake ni nabii vile vile, inasemwa kuwa alikuwa ni mume wa mama yake mdogo au mume wa dada yake: {…Kila mara Zakariya alipo ingia chumbani kwake alimkuta na vyakula. Basi alimwambia: Ewe Maryamu! Unavipata wapi hivi? Naye akasema: Hivi vinatoka kwa Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu humruzuku amtakaye bila ya hisabu.} [3:37]

Ukarimu na utawala wa Allah kwake yeye, hivyo Mola wake akamkirimu, kumchagua, kumtoharisha, kumkamilisha na kumuamrisha kumuabudu: {Na angalia pale Malaika walipo sema: Ewe Maryamu! Kwa hakika Mwenyezi Mungu amekuteuwa, na akakutakasa, na akakutukuza kuliko wanawake wote. Ewe Maryamu! Mnyenyekee Mola Mlezi wako na usujudu na uiname pamoja na wainamao.} [3:42-43],

Kisha Allah alipotaka Maryam amzae Issa ('Alahyi Salaam) alijitenga na watu wake: {Na mtaje Maryamu katika Kitabu, pale alipo jitenga na jamaa zake mahali upande wa mashariki; Na akaweka pazia kujikinga nao. Tukampelekea Roho wetu, akajifananisha kwake sawa na mtu.} [19:16-17]

Maryam akaogopa, akimdhania kuwa anataka kumfanyia uovu: {(Maryamu) akasema: Hakika mimi najikinga kwa Mwingi wa Rehema aniepushe nawe, ukiwa ni mchamngu. (Malaika) akasema: Hakika mimi ni mwenye kutumwa na Mola wako Mlezi ili nikubashirie tunu ya mwana aliye takasika.} [19:18-19],

Maryam akashangaa: {Akasema: Nitampataje mwana hali mwanaadamu yeyote hajanigusa, wala mimi si kahaba?} [19:20].

Yule mjumbe akamwambia hii ni hukumu ya Allah, na Mwenyezi Mungu amekufanya kuwa aya (dalili) na jambo hilo ni jepesi kwake: {(Malaika) akasema: Ndio hivyo hivyo! Mola wako Mlezi amesema: Haya ni mepesi kwangu! Na ili tumfanye kuwa ni Ishara kwa watu, na Rehema itokayo kwetu, na hilo ni jambo lilio kwisha hukumiwa.} [19:21],

Kwa hiyo katika ambayo Mwenyezi Mungu ameyataka ni ishara ya kuzaliwa kwa Issa ('Alahyi Salaam) kutoka kwa mama aliyetoharika ambae hakuzini au kufanya maovu na bila ya kuwa na baba (hii ni rehema

kutoka kwa Allah na utekelezaji wa hukumu ya Allah Ta'ala. Hivyo kuzaliwa Issa ('Alahyi Salaam) kukawa ni muujiza, miongoni mwa miujiza na aya miongoni mwa aya zake, mfano wake katika hilo ni mfano wa kuumbwa Adam bila baba:

{Hakika mfano wa Isa kwa Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa Adam; alimuumba kwa udongo kisha akamwambia: Kuwa! Basi akawa. Hii ni kweli itokayo kwa Mola wako Mlezi. Basi usiwe miongoni mwa wanao fanya shaka.} [3:59-60].

Aliposhika mimba alijiweka mbali na watu wake: {Basi akachukua mimba yake, na akaondoka nayo mpaka mahali pa mbali. } [19:22]

Uzazi ukamjia: {Kisha uchungu ukampeleka kwenye shina la mtende; akasema: Laiti ningeli kufa kabla ya haya, na nikawa niliye sahaulika kabisa!} [19:23],

Na hapa ndipo kulipotokea muujiza mwingine kwa Nabii wa Allah (Issa ('Alahyi Salaam): {Pakatangazwa kutoka chini yake: Usihuzunike! Hakika Mola wako Mlezi amejaalia chini yako kijito kidogo cha maji! Na litikise kwako hilo shina la mtende, utakuangushia tende nzuri zilizo mbivu. Basi kula, na kunywa, na litue jicho lako. Na pindi ukimwona mtu yeyote basi sema: Hakika mimi nimeweka nadhiri kwa Mwenyezi Mungu ya kufunga; kwa hivyo leo sitasema na mtu.} [19:24-26],

Na aliporejea kwa watu wake, kukutana nao kulikuwa kubaya kwa Maryam mwenye kutoharika mwenye

Manabii ni watu bora zaidi.

"Baadhi ya yaliyopotoshwa juu ya Mitume ya Allah na manabii inataja kuwa walilewa, au kuangukia katika uzinifu, au kuamrisha kuwa watu ni yote hayo ni upotofu mbayo haifai na hailingani na watu wenye tabia za juu mbali ya kuwa wao ni watu waliokuwa bora zaidi…. Wao ni Manabii wa Allah, katika hayo ni yale yaliyokuja – katika Taurati kuhusu Dawudi ('Alayhi Salaam) (Samweli (2) 11/2-26) na kutoka kwa Yoshua bin Nuun (mwana wa Nuni) ('Alayhi Salaam) (Yoshua 6/24) na kutoka kwa Musa ('Alayhi Salaam) (Hesabu:31/14-18) Musa ('Alayhi Salaam), na mengine mengi yasiyokuwa hayo hayafai Mtume wa Allah."

kujihifadhi: {Akenda naye (mwanawe) kwa jamaa zake amembeba. Wakasema: Ewe Maryamu! Hakika umeleta kitu cha ajabu! Ewe dada yake Harun! Baba yako hakuwa mtu muovu, wala mama yako hakuwa kahaba. } [19:27-28],

Nae hakuwajibu, bali: {Akawaashiria (mtoto)….} [19:29],

Wakachukizwa wakasema: {… Wakasema: Vipi tumsemeze aliye bado mdogo yumo katika mlezi?} [19:29], {(Mtoto) akasema: Hakika mimi ni mtumwa wa Mwenyezi Mungu. Amenipa Kitabu, na amenifanya Nabii. Na amenijaalia ni mwenye kubarikiwa popote pale niwapo. Na ameniusia Sala na Zaka maadamu ni hai, Na nimtendee wema mama yangu. Wala hakunifanya niwe jeuri, mwovu. Na amani iko juu yangu siku niliyo zaliwa, na siku nitakayo kufa, na siku nitakayo fufuliwa kuwa hai.} [19:30-33],

Lakini kundi moja la Mayahudi halikuamini, wakamtuhumu Al-Twahira kwa uzushi mkubwa: {Na pia kwa kufuru zao na kumsingizia kwao Maryamu uwongo mkubwa} [4:156],

Wakamtuhumu Al-Twahira kwa uzinifu, Allah akamkosha na tuhuma ile, na akamuelezea Maryam kuwa: {Na mama yake ni mwanamke mkweli.} [5:75];

Muumini wa Unabii na ujumbe wa Issa ('Alahyi Salaam).

Allah akamneemesha Mtume wake na mja wake Issa ('Alayhi salaam) na mama yake: {Na pale Mwenyezi Mungu atapo sema: Ewe Isa bin Maryamu! Kumbuka neema yangu juu yako, na juu ya mama yako, nilipo kutia nguvu kwa Roho Takatifu, ukazungumza na watu katika utoto na utuuzimani. Na nilivyo kufunza kuandika na hikima na Taurati na Injili…} [5:110],

Na akamtia nguvu kwa miujiza na alama: {…Na ulipo tengeneza udongo sura ya ndege, kwa idhini yangu, kisha ukapuliza ikawa ndege kwa idhini yangu; na ulipo waponesha vipofu na wakoma kwa idhini yangu; na ulipo wafufua wafu kwa idhini yangu; na nilipo kukinga na Wana wa Israili ulipo wajia na hoja zilizo wazi, na wakasema walio kufuru miongoni mwao: Haya si lolote ila ni uchawi mtupu! Na nilipo wafunulia Wanafunzi kwamba waniamini Mimi na Mtume wangu, wakasema: Tumeamini na shuhudia kuwa sisi ni Waislamu.} [5:110-111],

Kisha ni kuwa Al-Hawariyyuun (wafuasi wake) walimtaka Issa ('Alayhi salaam) amuombe Mola wake awateremshie chano cha kula kutoka mbinguni, Allah kasema: {Wanafunzi walipo sema: Ewe Isa bin Maryamu! Je, Mola wako Mlezi anaweza kututeremshia chakula kutoka mbinguni?...} [5:112],

Issa akawaogopea kutoshukuru kwao: {…Akasema: Mcheni Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi ni Waumini. Wakasema: Tunataka kukila chakula hicho, na nyoyo zetu zitue, na tujue kwamba umetuambia kweli, na tuwe miongoni mwa wanao shuhudia.} [5:112-113],

Kwa hiyo akamuomba Mola wake: {Akasema Isa bin Maryamu: Ewe Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wetu! Tuteremshia chakula kutoka mbinguni ili kiwe Sikukuu kwa ajili ya wa mwanzo wetu na wa mwisho wetu, na kiwe ni Ishara itokayo kwako. Basi turuzuku, kwani Wewe ndiye mbora wa wanao ruzuku. Mwenyezi Mungu akasema: Hakika Mimi nitakuteremshieni hicho. Lakini yeyote katika nyinyi atakaye kanya baadae, basi hakika Mimi nitampa adhabu nisiyopata kumpa yeyote katika walimwengu.} [5:114-115],

Hata hivyo baadhi ya walioteremshiwa walikufuru.

Ama Mayahudi katika Bani Israil waliomkadhibisha Nabii wa Allah Issa ('Alayhi salaam) kule kukufuru kwao na kukadhibisha kwao na vitimbi vyao viliendelea kwa Isa ('Alahyi Salaam): {Na Makafiri walipanga mipango na Mwenyezi Mungu akapanga mipango, na Mwenyezi Mungu ndiye mbora wa wenye kupanga.} [3:54],

Allah akamjulisha kuhusu vitimbi vyao, na jinsi ambavyo Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) atamuokoa kutokana nao:

{Pale Mwenyezi Mungu alipo sema: Ewe Isa! Mimi nitakufisha, na nitakunyanyua kwangu, na nitakutakasa na wale walio kufuru, na nitawaweka wale walio kufuata juu ya wale walio kufuru, mpaka Siku ya Kiyama. Kisha marejeo yenu yatakuwa kwangu, nikuhukumuni katika yale mliyo kuwa mkikhitalifiana.} [3:55],

Issa anasisitiza katika Injili kuwa Mungu ni mmoja.

"Na mmojawapo wa waandishi akafika, akawasikia wakisemezana naye, akatambua ya kuwa amewajibu vema, akamwuliza, Katika amri zote ni ipi iliyo ya kwanza? Yesu akamjibu, Ya kwanza ndio hii, Sikia, Israeli, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja; nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote." (Marko Mtakatifu 12:28-35). Huu ni usia wa kwanza.

Na walipoendelea kuvunja ahadi, vitimbi, ukafiri wao, na jaribio lao la kuuwa manabii wa Allah na kumtuhumu Al-Twahira Maryam ('Alayha salaam) kwa uzushi Allah alisema: {Basi kwa sababu ya kuvunja kwao ahadi zao, na kuzikataa kwao ishara za Mwenyezi Mungu, na kuwauwa kwao Manabii bila ya haki, na kusema kwao: Nyoyo zetu zimefumbwa; bali Mwenyezi Mungu amezipiga muhuri kwa kufuru zao, basi hawaamini ila kidogo tu - Na pia kwa kufuru zao na kumsingizia kwao Maryamu uwongo mkubwa, Na kwa kusema kwao: Sisi tumemuuwa Masihi Isa, mwana wa Maryamu, Mtume wa Mwenyezi Mungu…} [4:155-157]



https://www.path-2-happiness.com/sw

Lakini Allah alimuokoa dhidi yao: {…nao hawakumuuwa wala hawakumsalibu ….} [4:157]

Bali walimuua aliyefanana nae: {…bali walifananishiwa tu. Na hakika walio khitalifiana katika haya wamo katika shaka nayo. Wao hawana ujuzi nayo wowote, ila ni kufuata dhana tu. Wala hawakumuuwa kwa yakini. Bali Mwenyezi Mungu alim- tukuza kwake, na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.} [4:157-158],

Allah akamuokoa Mtume wake Issa ('Alayhi salaam) na kumnyanyua kwake:

{Na hawi katika Watu wa Kitabu ila hakika atamuamini yeye kabla ya kufa kwake. Naye Siku ya Kiyama atakuwa shahidi juu yao.} [4:159].

Issa katika Uislamu

"Nilipousoma Uislamu nilipata sura nyingine tofauti za Masihi ('Alayhi Salaam) ambazo ziliingiza katika nafsi yangu athari kubwa."

Frederick Dolamark.

Mkuu wa Maaskofu
Johannesburg.

Huu ndio ukweli wa kisa cha Issa ('Alayhi salaam):

{Huyo ndiye Isa mwana wa Maryamu. Ndiyo kauli ya haki ambayo wanaifanyia shaka. Haiwi kwa Mwenyezi Mungu kuwa na mwana, Subhanahu, Yeye ametakasika! Anapo lihukumia jambo basi huliambia tu: Kuwa! Likawa. } [19:34-35],

Kwa hiyo Allah kabainisha kuwa haifai Yeye kuwa na mtoto; kwa kuwa Yeye ni Muumba wa kila kitu na mmliki wake, na kila kitu kinahitaji na dhalili kwake, na wote mbinguni na ardhini ni waja wake, Yeye ndie Mola wao La ilaha illa Llah; ni Yeye na hakuna Mola mwingine asiyekuwa Yeye.

Injili inakanusha kusulubiwa na inathibitisha Kuinuliwa Mbinguni.

"Basi wakaokota mawe ili wamtupie; lakini Yesu akajificha, akatoka hekaluni." (Yohana 8:59).
"Wakatafuta tena kumkamata; lakini akatoka mikononi mwao." (Yohana 10:39).
"Hili limetokea ili yatimie yaliyokuja kwenye kitabu: Hakuvunja chochote katika mfupa." (Yohana 36:19).
"Huyu Yesu huyu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni." (Matendo ya Mitume 1:11)

https://www.path-2-happiness.com/sw

5. MUHAMMAD (Swala Llahu 'alayhi wasalaam)

Mtume Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) ni mwisho wa mitume na manabii, Issa – ('Alayhi salaam) amewabashiria Bani Israil kuja mtume wa mwisho, Allah amesema: {Na Isa bin Mariamu alipo sema: Enyi Wana wa Israili! Hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu, ninaye thibitisha yaliyo kuwa kabla yangu katika Taurati, na mwenye kubashiria kuja Mtume atakaye kuja baada yangu; jina lake ni Ahmad! Lakini alipo waletea hoja zilizo wazi, walisema: Huu ni uchawi ulio dhaahiri!} [61:6],

Hivyo basi bishara ya Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) ipo katika Taurati na Injili. Allah amesema: {Ambao kwamba wanamfuata huyo Mtume, Nabii, asiye soma wala kuandika, wanaye mkuta kaandikwa kwao katika Taurati na Injili, anaye waamrisha mema na anawakanya maovu, na anawahalalishia vizuri, na ana waharimishia viovu, na anawaondolea mizigo yao na minyororo iliyo kuwa juu yao. Basi wale walio muamini yeye, na wakamhishimu, na wakamsaidia, na wakaifuata nuru iliyo teremshwa pamoja naye - hao ndio wenye kufanikiwa.} [7:157],

Bali Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) amechukua ahadi na mkataba kwa manabii wamuamini Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) na wamnusuru yeye kama atatumwa kwao wakiwa hai, na wawaambie kaumu zao hilo ili habari yenyewe ienee baina ya Ummah zote, Allah

amesema: {Na pale Mwenyezi Mungu alipo chukua ahadi kwa Manabii: Nikisha kupeni Kitabu na hikima, kisha akakujieni Mtume mwenye kusadikisha mliyo nayo, ni juu yenu mumuamini na mumsaidie. Akasema: Je, mmekiri na mmekubali kushika agizo langu juu ya hayo? Wakasema: Tumekubali. Akasema: Basi shuhudieni, na Mimi ni pamoja nanyi katika kushuhudia.} [3:81]

Qur-aan imeashiria bishara hizo, na kuthibitisha ukweli wa Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam), Allah amesema: {Na walio kufuru wanasema: Wewe hukutumwa. Sema: Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi baina yangu na nyinyi, na pia yule mwenye ilimu ya Kitabu} [13:43],

Na katika aya nyingine: {Na hakika bila ya shaka haya yamo katika Vitabu vya kale. Je! Haikuwa kwao ni Ishara kwamba wanayajua haya wanazuoni wa Wana wa Israili? } [26:196-197]

Na akazungumzia kuhusu msimamo wa Ahlul kitab ambao ilipasa kuwa ndio

wa mwanzo na waumini kwa kumjua kwao kama walivyokuwa wakiwajua watoto wao: {Wale tulio wapa Kitabu wanayajua haya kama wanavyo wajua watoto wao; na kuna kikundi katika wao huificha haki na hali wanajua.} [2:146],

Allah Mtukuka amesema: {Na alipo wajia Mtume kutoka kwa Mwenyezi Mungu, mwenye kuthibitisha yale waliyo nayo, kundi moja miongoni mwa wale walio pewa Kitabu lilitupa Kitabu cha Mwenyezi Mungu hicho nyuma ya migongo yao kama kwamba hawajui.} [2:101],

Tabiri zile zikathibitika kwa Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam), na kuwa yeye ndie Mtume ambae Allah amezungumzia kuja kwake, hata hivyo kundi moja miongoni mwao likaficha haki likiwa linajua, na wakiacha yaliyokuja kwenye vitabu vyao vitakatifu nyuma ya migongo yao kama kwamba hawafahamu.

Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) alikuja na Tawhidi: Yaani kumpwekesha Allah peke yake bila kumshirikisha kama walivyo kuja Mitume na Manabii waliotangulia, Allah Mtukuka

amesema: {Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia ya kwamba hapana mungu isipo kuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu.} [21:25],

Kama alivyotumwa kusadikisha Mitume na manabii waliotangulia, bila ya kutofautisha chochote katika kuwaamini wao: {…hatutafautishi baina ya yeyote katika hao…} [2:136],

Bali yule ambae atamsadiki na kumuamini Muhammad bila ya kuamini mtume yoyote au nabii aliokuja ndani ya Qur-aan-basi mtu hakumkubali wala kumuamini Muhammad: {Amekuamrisheni Dini ile ile aliyo muusia Nuhu na tuliyo kufunulia wewe, na tuliyo wausia Ibrahim na Musa na Isa, kwamba shikeni Dini wala msifarikiane kwayo.} [42:13]

Na akatia mkazo kuwa yeye ni mja wa Allah: {Sema: Mimi ni mwanaadamu kama nyinyi. Ninaletewa Wahyi kwamba Mungu wenu ni Mungu Mmoja. Mwenye kutaraji kukutana na Mola wake Mlezi basi naatende vitendo vyema, wala asimshirikishe yeyote katika ibada ya Mola wake Mlezi.} [18:110],

Na Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasalaam) alikuwa ni Umiyyi hasomi wala haandiki (yaliyoandikwa) kama ilivyokuja sifa yake katika vitabu vilivyotangulia ili Ahlul Kitab wamtambue ambao wanajua sifa zake zilizokuja ndani ya vitabu vyao; kama alivyosema Allah (Subhaanahu



Muhammad …Mtume wa Mwisho.

“Kwa sababu Mungu atanipandisha kutoka ardhini na atabadilisha mandhari ya haini hadi kila mmoja wenu atadhania: pamoja na hayo pindi anapokufa mtu muovu mimi nitakuwa katika fedheha muda mrefu Ulimwenguni, lakini kutokana na mimi atakapokuja Muhammad Mtume Mtukufu doa hili litaniondoka.”

Injili ya Barnaba.

wa Ta'ala): {Ambao kwamba wanamfuata huyo Mtume, Nabii, asiye soma wala kuandika, wanaye mkuta kaandikwa kwao katika Taurati na Injili, anaye waamrisha mema na anawakanya maovu, na anawahalalishia vizuri, na ana waharimishia viovu, na anawaondolea mizigo yao na minyororo iliyo kuwa juu yao. Basi wale walio muamini yeye, na wakamhishimu, na wakamsaidia, na wakaifuata nuru iliyo teremshwa pamoja naye - hao ndio wenye kufanikiwa.} [7:157].

Allah alipitisha miujiza ile kwenye mikono yake kama alivyopitisha katika mikono ya Mitume kabla yake – miujiza mingi ilikuwa ni ya kuonekana japokuwa muujiza mkubwa zaidi ulikuwa ni Qur-aan tukufu ambayo na ni yake kuna habari za wa mwanzo na za wa mwisho, ubainifu, uongofu, rehma na bishara: {…Na tumekuteremshia Kitabu hiki kinacho bainisha kila kitu, na ni uwongofu, na rehema, na bishara kwa Waislamu.} [16:89],

Na uoni kwa waumini: {Hizi ni dalili zilizo wazi kwa watu wote, na ni uwongofu, na rehema kwa watu wanao yakinisha.} [45:20],

Mtume Ummiy (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) akawabainishia watu walichotofautiana ndani ya Qur-aan: {Na hatukukuteremshia Kitabu isipo kuwa uwabainishie yale ambayo wanakhitalifiana, na kiwe Uwongofu na Rehema kwa watu wanao amini.} [16:64].

Pamoja na makafiri wa kikureishi kujua ukweli wake na amana yake na kwa sababu tokea mwanzo walimuita 'Mkweli mwaminifu' lakini pamoja na hayo walimkadhibisha, Allah akawapa changamoto wakusanyike wote, watu kwa majini na walete mfano wa Qur-aan hii: {Sema: Wangeli kusanyika watu na majini ili walete mfano wa hii Qur-aani basi hawaleti mfano wake, hata wakisaidiana wao kwa wao.} [17:88],

Wakashindwa pamoja na uwezo wao wa lugha na akawapa changamoto nyingine baada ya kukusanyika walete aya kumi tu mfano wake: {Au wanasema: Ameizua? Sema: Basi leteni Sura kumi zilizo zuliwa mfano wa hii, na waiteni muwawezao badala ya Mwenyezi Mungu, ikiwa mnasema kweli.} [11:13],

Wakashindwa na akawapa changamoto nyingine ya kuleta sura moja inayokaribiana nayo. {Na ikiwa mna shaka kwa hayo tuliyo mteremshia mja wetu basi leteni sura moja ya mfano wake…} [2:23];

Walishindwa pamoja na uwezo wao wa lugha.

Makafiri wa Kikureishi wakaendelea kumkadhibisha; Allah akamuamrisha kusubiri kama walivyosubiri Ulul 'Azm



Injili inayotoa biashara ya Muhammad.

"Itabakia hivi hadi atakapokuja Muhammad Mtume wa Mungu ambaye muda atakapofika atauweka wazi uongo kwa walioamini sheria ya Mungu. Na imekuja katika Isaya: Mimi nimefanya jina lako Muhammad Ewe Muhammad Ewe uliye mtakatifu kutoka kwa Mungu Jina lako lipo milele. Na katika Habakkuki imekuja (3:3-6): "Mungu alikuja kutoka Temami, yeye aliye mtakatifu kutoka mlima Parani. Utukufu wake ukaangaza mbingu kutokana na haiba ya Muhammad, nayo dunia ikajaa sifa yake. Au kama ilivyokuja katika Isaya: Nilichompa sitompa mwingine. Ahmad (jina lingine la Muhammad) anamhimidi Mungu mazungumzo yenye kuja kutoka kwa watu bora duniani: Viumbe watafurahi kwayo na kumtakasa kila kitukufu na kuadhimisha kila sehemu."

injili ya Barnaba

katika mitume na manabii kabla yake: Ibrahim, Nuuh, Musa na Issa ('Alayhi salaam) wote: {Basi subiri, kama walivyo subiri Mitume wenye stahmala kubwa...} [46:35]

Akasubiri na akaendelea na da'wah yake akiwalingania na kuwafundisha maneno yake na maneno ya Muumba wake, Allah akamtosheleza na kumlinda: {Ewe Nabii! Mwenyezi Mungu anakutoshelezea wewe na Waumini walio kufuata.} (8:64), {Je! Mwenyezi Mungu si wa kumtosheleza mja wake?...} [39:36]

Allah akamnusuru kama alivyowanusuru Mitume wengine: {Mwenyezi Mungu ameandika: Hapana shaka Mimi na Mtume wangu tutashinda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye kushinda.} [58:21],

Akasema Mtukuka: {Na bila ya shaka neno letu lilikwisha tangulia kwa waja wetu walio tumwa. Ya kuwa wao bila ya shaka ndio watakao nusuriwa. Na kwamba jeshi letu ndilo litakalo shinda. } [37:171-173], {Hakika bila ya shaka Sisi tunawanusuru Mitume wetu na walio amini katika uhai wa duniani na siku watapo simama Mashahidi} [40:51].

Makafiri wakataka kuzuia ujumbe wake na kuzima nuru yake, lakini Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) akatimiza



Kiigizo Chema na mfano wa juu.

"Nimetafuta katika historia mfano wa juu wa mtu huyu. Nikaupata kwa Nabii Muarabu Muhammad."

Mwandishi na mshairi wa Ujerumani.

Goethe

Uliza na Qur-aan itakujibu.

"Nimesoma Qur-aan nikapata majibu kwa kila swali linalohusu maisha."

Michael Hart.

Mwandishi wa Kimarekani.



Na kwa watu ni Ahmad.

"Hakika ule msemo maarufu wa Kikristo: Utukufu ni kwa Mungu aliye juu. Katika ardhi ni amani, na kwa watu ni furaha. Haikuwa hivi, bali ilikuwa: Utukufu ni kwa Mungu aliye juu na katika ardhi ni amani na kwa watu ni Ahmad."

David Benjamin Kelden

Kiongozi Mkuu wa Wakristo
Mosol-Iraq

neema yake: {Wanataka kuizima nuru ya Mwenyezi Mungu kwa vinywa vyao. Na Mwenyezi Mungu atakamilisha nuru yake ijapo kuwa makafiri watachukia. Yeye ndiye aliye mtuma Mtume wake kwa uwongofu na Dini ya haki ili ipate kuzishinda dini zote, ijapo kuwa washirikina watachukia. } [61:8-9].

Akakamilisha neema yake na kuudhihirisha Uislamu, akatilia mkazo juu ya Tawhidi ya Allah katika dini zote, akakamilisha neema yake kwa wanadamu kwa ujumbe huu na dini hii: {…Leo nimekukamiliishieni Dini yenu, na nimekutimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni UISLAMU uwe ndiyo Dini…} [5:3],

Bali aliihifadhi dini hii, na akaufanya ujumbe huu kubakia hadi Siku ya Kiama: {Hakika Sisi ndio tulio teremsha Ukumbusho huu, na hakika Sisi ndio tutao ulinda.} [15:9];

Kwa hiyo huu ni ujumbe hitimisho wa ujumbe wote: {Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na Mwisho wa Manabii, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu} [33:40],

Nao ni ujumbe wenye kubakia hadi pale ambapo Allah atairithi ardhi hii na waliomo.

Basi ni ujumbe gani huu wenye kubakia kwa hifadhi ya Allah hadi Siku ya Malipo…..?!

Qur-aan ni muujiza.

“Qur-aan inaongoza fikra na kukamata nyoyo, imeshuka kwa Muhammad dalili ya ukweli wake.”

Henri de Castriesry.
Luteni wa zamani wa jeshi la Kifaransa.



https://www.path-2-happiness.com/sw

الطريق إلى السعادة
The Path to Happiness

UJUMBE UNAOBAKIA

https://www.path-2-happiness.com/sw

Yaliyomo

UJUMBE UNAOBAKIA

MIONGONI MWA DALILI ZA UTUME WAKE (Swala Llahu ‘alayhi wasalaam)

UTUME WA MWISHO

REHEMA KWA WALIMWENGU

FURAHA YA MWANADAMU KWA KUTUMWA KWAKE (Swala Llahu ‘alayhi wasalaam)

NI UPI UJUMBE ULIOBAKIA?

UJUMBE ULIOBAKIA NDILO UMBILE LA ULIMWENGU

UJUMBE ULIOBAKIA NI DINI YA MANABII NA MITUME WOTE:

UKAMILIFU WA UJUMBE ULIOBAKIA:

MISINGI YA UWEKAJI SHERIA

SIFA ZA UWEKAJI SHARIA WA KIISLAMU:

SHERIA YA KIISLAMU NA KANUNI ZA WANADAMU…TOFAUTI ZILIZOPO:

VYANZO VYA UISLAMU.

UJUMBE UNAOBAKIA

Kila mwanadamu anapokuwa mbali na uongofu wa mbinguni na ujumbe wa Mitume basi watu hao watagubikwa na kiza, ndio maana akawa anatuma Mtume baada ya Mtume: {Mitume hao ni wabashiri na waonyaji, ili watu wasiwe na hoja juu ya Mwenyezi Mungu baada ya kuletewa Mitume. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.} [4:165];

Hivyo basi Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) hamuadhibu yoyote ambaye hajamtumia Mtume: {…Wala Sisi hatuadhibu mpaka tumpeleke Mtume.} [17:15],

Na baada ya kutumwa kwa Issa ('Alayhi salaam), kisha Allah akamnyanyua jamii mbali mbali ya wanadamu zilisumbuka kwa Ujahilia na upotevu, dhuluma na kiza; hivyo dini za Allah zilikumbwa na mabadiliko ya kuchafuliwa mafundisho yake na baadhi ya waovu wakabadilisha akida yake safi ya tawhidi kwa upagani na ushirikina, na kumfanyia Allah jeuri na kusema juu yake bila ya haki, na kwenda kinyume, na dhati yake, wakati huo hakukuwepo na tofauti yeyote baina ya wapagani na Ahlul Kitabu pamoja na waabudu masanamu katika ibada zao na maisha yao.

Nuru ya tawhidi ikawa imepotea katikati ya msongamano huu mkubwa wa ushirikina na upingaji na kubadilisha na kugeuza maneno ya Allah (Subhaanahu wa Ta'ala), wale waliopewa kitabu wakatupa ahadi na

https://www.path-2-happiness.com/sw



makubaliano (agano), mikataba na maneno ya Allah nyuma ya migongo yao, na hawakuyajali wakaficha haki na kudhihirisha batili, na wakafanya ujasiri katika maharamisho ya Allah, kwa dharau haki za Allah na haki za viumbe, na wakanunua kwa hilo (kuficha kwao) thamani ndogo kwa baadhi tu ya vyeo na mali chache, kama ilivyotokea kwa viongozi wao wenye kufuata matamanio yao, wenye kutanguliza matamanio yao kuliko haki, hivyo basi vita vikaenea na udikteta ukadhihiri, wanadamu wakaishi maisha ya kiza juu ya kiza.

Nyoyo zikapata kiza cha ukafiri na ujinga kutokana na hayo. Tabia zikachafuka, maadili, heshima za watu zikaharibiwa na haki mbali mbali ufisadi ukadhihiri katika nchi kavu na baharini, kiasi cha kuwa lau mtu akiangalia kwa akili yenye kufahamu ataona kuwa wanadamu (wakati ule) walikuwa katika hali ya mauti (Sakarati ya Mauti) na kuwa mwisho wao umekaribia, Allah hakuwataka kuleta maslahi makubwa ya utume ambayo itaondoa tatizo lililopo na kuwapelekea watu katika uongofu ili imuongoze mwanadamu njia yake na kumuongoza katika njia ya sawa…

Hivyo basi Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) katikati ya janga hili lenye kiza katika maisha ya mwanadamu, Allah alimchagua Mtume wake Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) ili awe:

Tukio tukufu.

"Tukio moja tu ni miongoni mwa matukio yenye faida zaidi katika historia ya mwanadamu nalo si jingine bali ni kudhihiri kwa Uislamu."

George Sarton

Mhadhiri katika Vyuo Vikuu vya Washington na Havard.

Na akamtuma pamoja naye nuru inayoongoza ambayo inamuokoa mwanadamu dhidi ya upotofu na mashaka yake, hadi Allah alipokamilisha dini hii kwa wanadamu na akatimiza neema yake kwa ukamilifu wake, na Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) akafanya jihadi ili aweze kufikia kwenye haki kwa walimwengu wote: {Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote} [21:107],

Kiasi cha kuonja njia ya furaha, nae (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) katika jihadi yake yote hakuwa anataka chochote katika starehe za dunia, wala hakutaka ujira kwa watu, Allah amesema: {Sema (Ewe Mtume):Sikuombeni ujira juu ya haya, wala mimi si katika wadanganyifu.} [38:86],

Bali Mola wake alimpa khiyari baina ya kuwa Mtume kwa sura ya malaika au Mtume kwa sura ya mwanadamu, Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) akachagua kuwa mja Rasuli. Ikawa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) ni mwanadamu anayeishi kama wanadamu wengine, anasikia njaa kama wanavyosikia maswahaba zake, anaumia na kupata majeraha kama wanavyojeruhiwa, na kufanyakazi pamoja nao, na anajifakharisha kuwa ni mja wa Allah, hivyo Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) anapotaka kumkirimu humsifu kwa uja, "Allah amesema: {Kuhimidiwa ni kwa Mwenyezi Mungu, ambaye amemteremshia mja wake Kitabu, wala hakukifanya kina upogo.} [18:1],

Habari ya Ajabu Zaidi.

"Habari ya kuibuka kwa Uislamu ilikaribia kuwa habari ya ajabu zaidi ambayo historia ya mwanadamu imeandika, kudhihiri kwa Uislamu katika Ummah ambao kabla ya wakati huo ulikuwa hauna utulivu na nchi ilikuwa imeparaganyika. Haikupita muda wa miongo kumi ya kudhihiri kwake Uislamu ulikuwa umeshasambaa nusu ya Ulimwengu ikivunja falme kubwa na kuzitupilia mbali, na kubomoa dini za kale ambazo zimepita zama na vizazi, na hivyo kubadilisha nafsi za umma nyingi na kujenga Ulimwengu mpya wenye nguzo imara nayo ni Ulimwengu wa Uislamu."

Lothrop Stoddard

Mwandishi wa Kimarekani

https://www.path-2-happiness.com/sw

Rehema kwa Walimwengu.

“Maisha ya mfano wa Muhammad. Na nguvu kama nguvu za kuchunguza na kufikiri kwake mambo, jihadi yake, na msimamo wake wa kuondosha upotofu uliokuwa katika Ummah wake na ujahilia wa watu wake na ukali wake wa kupambana na washirikina kunyanyua neno la Mola wake na kufungamana na ujasiri wake katika kuthibitisha nguzo za dini ya Kiislamu. Yote hayo ni dalili kuwa hakukusudia udanganyifu au kuishi katika batili; alikuwa ni mwanafalsafa, khatibu, Mtume, mweka sheria, mwenye kumuongoza binadamu kwenye akili, mwanzilishi wa dini isiyokuwa na udanganyifu. Yeye ni muanzilishi dola ishirini ulimwenguni, na mfunguzi wa nchi ya Kiroho mbinguni. Ni nani aliyepata ukubwa wa Uislamu kama alivyopata yeye!!

Lamartine

Mshairi wa Kifaransa.

Bali alikuwa akitahadharisha watu kuvuka mipaka na kutoa zaidi ya haki yake, amesema Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasalaam): “Msinikweze kama Wakristo walivyomkweza Ibn Maryam, bali mimi ni mja, basi semeni mja wa Allah na Mtume wake.” (Bukhari).

Na kila mwenye kumuona na akamjua atajua ukweli wake na akasoma sira yake atashangazwa

na tabia yake (Swala Llahu 'alayhi wasalaam), kwa nini isiwe hivyo wakati maadui zake walimshuhudia kabla ya marafiki, na makafiri kabla ya Waislamu! Inatosha uthibitisho wa Mola wake aliposema:

{Na hakika wewe una tabia tukufu.} [68:4],

Bali inatosha kuwa Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) alimchagua awe mwisho wa Mitume na manabii, na alipomaliza jukumu lake Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) alimfisha, lakini ujumbe wake ukaendelea kubaki hadi Siku ya Malipo.

Katika wakuu wa watu (Miongoni mwa watu mashuhuri).

"Muhammad alikuwa ni mtu wa pekee katika historia aliyefanikiwa kwa njia bora zaidi katika viwango vyote vya kidini na kidunia. Kwa hakika mkusanyiko (muunganiko) huu wa pekee ambao hauna mfano kwa ajili ya taathiri ya kidini na kidunia pamoja, linamfanya kuwa mtu mwenye haiba tukufu zaidi yenye taathira katika historia ya mwanadamu."

Michael Hart

Mwandishi wa Kimarekani.

MIONGONI MWA DALILI ZA UTUME WAKE (Swala Llahu 'alayhi wasalaam)

Kuwa amelingania kumuabudu Allah Ta'ala peke yake na kuacha kuabudu wasiokuwa yeye, akiafikiana katika hilo na Mitume wote, na atakayelinganisha baina ya aliyokuja nayo Musa, Issa ('Alayhi salaam) na yale aliyokuja nayo Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) miongoni mwa akida sahihi na sheria na hukumu mbali mbali na elimu mbali mbali zenye manufaa atajua na kufahamu kuwa yote hayo yanatoka katika kijaruba kimoja nayo ni taa ya utume.

Hamkanushi isipokuwa ni Mpingaji

"Muhammad ni Mtume wa kweli kwa maana halisi ya neno. Kamwe hatuwezi kukana kuwa Muhammad ndio kiongozi mwenye kuelekeza kwenye njia ya kuokoka."

Hans Kung
Mwanazuoni wa kidini wa Switzerland

Kuwa alidhihirisha miujiza na alama mbali mbali ambazo hazidhihirishwi ila na Mitume ya Allah; kwani Sunnah ya Allah Ta'ala imepita katika mikono ya Manabii waliopita imevunja ada (mazoea) ili iwe ni miujiza kwao, na dalili ya ukweli wao, na nia ya kusimamisha hoja kwa kaumu yao, na miujiza ya kila Mitume ilikuja kwa jinsi ambayo kaumu ya mtume yule ilivyopiga maendeleo katika jambo fulani. Hivyo basi muujiza wa Musa ('Alayhi salaam) ukanasibiana na jinsi kaumu yake ilivyopiga hatua katika fani maalumu; nayo ni fani ya uchawi, Allah kwa miujiza aliompa Musa akabatilisha uchawi wao, na wakashindwa kushindana na Musa katika hilo pamoja na werevu mkubwa na uhodari wa hali ya juu waliokuwa nao katika aina mbalimbali za uchawi. Kaumu ya Issa ('Alahyi Salaam) waliiga maendeleo makubwa katika fani ya utabibu na madawa, Allah akawaponya katika mikono ya Issa ('Alahyi Salaam) katika maradhi yaliyoshindikana

kutibiwa kiasi cha kuwa Allah akawafufua wafu katika mikono ya Issa ('Alahyi Salaam).

Miujiza yote hii ilikuwa ni ya kihisia (yaani yenye kuonekana), imefungamana na mahali na zama maalum, haina sifa ya kilimwengu na kudumu, miongoni mwa miujiza ya Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) ni kama miujiza ile ya kihisia; miongoni mwa miujiza hiyo ni:

Kububujika maji kutoka katika vidole vya Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam).

Chakula kidogo kukifanya kingi kiasi cha kula yeye pamoja na Waislamu wengine walio nae, na kubakia.

Kufanya maji kuwa mengi kiasi cha kunywa jeshi zima na kutawadha.

Gogo kumlilia alipoacha kulitumia katika mimbari.

Jiwe kumsalimu alipokuwa Makkah.

Mti kumnyenyekea yeye.

Changarawe kusabahi katika kiganja chake.

Kuponya magonjwa kwa uwezo wa Allah, na mengineyo,

Qur-aan imerikodi moja katika miujuza ile muujiza wa Israa na Miiraji; Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) alipopelekwa Israa kutoka msikiti wa Masjid Al-Haram Makkah kuelekea Al-Masjidil Aqswaa, kisha akapaishwa Mii'raj kutoka katika msikiti wa Aqswa hadi mbingu ya saba, Allah Ta'ala amesema:

Maneno ya Mwenyezi Mungu.

Nilipomaliza kusoma Qur-aan nikajawa na hisia kuwa hii ndio haki ambayo inakusanya majibu toshelevu kuhusu maumbile na mengineyo. Kadhalika hutupa matukio kwa njia ya mantiki ambayo tunaona yakigongana na vitabu vingine vya dini. Ama Qur-aan inayazungumzia kwa njia nzuri yenye kupendeza ambayo haiachi fursa ya mtu kutia shaka kuwa huu ndio ukweli, na ya kuwa maneno haya bila ya shaka ni ya Mwenyezi Mungu.

Deborah Potter

Mwandishi wa Kimarekani

https://www.path-2-happiness.com/sw

Hazifanani.

"Hakuna mfano wa Uislamu, dini ambayo imetukuza Manabii na Mitume ambao walikuja kabla ya Mtume Mwarabu. Dini hii imewataka waumini wake kuwatukuza watu hawa na kuwaamini. Hakuna dini iliyo sawa na Uislamu katika kuheshimu dini zingine zilizoteremka ambazo zilitangulia katika kuteremka na Wahyi."

Nassry Salhab

Mwanafasihi wa Kilebanoni.

{SUBHANA, Ametakasika aliye mchukua mja wake usiku mmoja kutoka Msikiti Mtukufu mpaka Msikiti wa Mbali, ambao tumevibariki vilivyo uzunguka, ili tumuonyeshe baadhi ya Ishara zetu. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia na Mwenye kuona.} [17:1].

Vivyo hivyo muujiza wa kupasuka kwa mwezi; ambapo Allah Ta'ala amesema: {Saa imekaribia, na mwezi umepasuka!} [54:1],

Na hii ilitokea wakati Makafiri walipomtaka Mtume Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) athibitishe ukweli wake kwa muujiza uliokuwa wazi kabisa, na wakaainisha wazi awapasulie mwezi, na kuahidi kuwa baada ya hapo wataamini, siku hiyo ya tukio ilikuwa ni siku ya mwezi kamili (Badri), yaani: usiku wa siku ya kumi na nne ya mwezi; ambao mwezi unakuwa kwa ukamilifu wake na kwa uwazi zaidi..

Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) akamuomba Mola wake ampe walichokiomba; mwezi ukapasuka mara mbili: nusu ikawa juu ya mlima wa Saffa na nusu nyingine juu ya Jabali Qayqu'aan inayoelekeana nayo, baada ya kupatikana kwa muujiza huu mkubwa washirikina wa Kikureishi hawakuamini, bali waliuzingatia kuwa ni uchawi, na huu ndio mwendo wa wapingaji wa dini ya Allah.

Kwa Ulimi Bainifu wa Kiarabu

"Aya ambazo Muhammad amerudia kuzitaja katika sura hizi tukufu zimeacha mbali nyuma yake kauli za wanadamu fasaha zaidi kama ambavyo inawezekana kuzileta kupitia maandiko yaliyowekwa ambayo yametufikia."

Régis Blachère

Mustashrik wa Kifaransa.

Ni kawaida ya wapingaji pindi haki inapobomoa utawala wao na nuru ya Allah inapofunika upotofu wao, hapo hufanya vitimbi na kusimama mbele yake, ima kwa kupotosha misingi yake au kugeuza hakika zenyewe, kwa dhana ya kuwa hayo yatatosha kumaliza na kuangamiza ukweli wenyewe, Allah amesema: {Na wakiona Ishara hugeuka upande na husema: Huu uchawi tu unazidi kuendelea. Na wamekanusha na wamefuata matamanio yao. Na kila jambo ni lenye kuthibiti.} [68:2-3].

Qur-aan: Ni muujiza mkubwa zaidi, ni wenye kubaki katika karne zote na dahari, nao ni muujiza wa kimaana na kiakili na alama miongoni mwa alama za utume; kwa sababu ni kitabu fasaha zaidi, Allah amemteremshia (Mtume) Ummiyyi (asiyesoma yaliyoandikwa), ikawa ni changamoto kwa watu wenye ufasaha zaidi walete sura moja mfano wa Qur-aan.

Muujiza uliopo kwenye Qur-aan na changamoto yake na hakuna yoyote mwenye kukanusha hayo isipokuwa mwenye kiburi.

Kwa hiyo inashinda kwa ufasaha wake, balagha yake, umbuji, utaratibu na mpangilio wake, na yaliyomo ndani yake miongoni mwa habari zilizopita na zinazokuja,

https://www.path-2-happiness.com/sw

kadhalika sheria na hukumu mbali mbali na maadili ya juu zaidi uongofu, nuru na baraka.

Kama ambavyo miujiza ya kisayansi inayovumbuliwa kila siku inakubaliana na habari za wahyi madamu ni hakika za kisayansi ulimwenguni, ambazo hazikuwa zikifahamika hapo kabla zote hizo ni uthibitisho bayana wa ukweli wa utume wa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam), kama ambavyo sayansi leo hii ilivyovumbua hatua mbali mbali (tofauti) anazopitia kichanga anapokuwa tumboni kwa mama yake na kuwepo kwa kizuizi cha maji baina ya maji tamu na maji chumvi baharini na mifano mingine kama hiyo.

Hata hivyo uthibitisho mkubwa zaidi za kuwa kwake kutoka kwa Allah ni kubakia kwake ikiwa imehifadhiwa zaidi ya karne kumi na nne bila ya kupotoshwa, au kubadilishwa, wala hachoki msomaji wake hata akikariri mara nyingi kwa kuisoma, Allah amesema: {Hakika Sisi ndio tulio teremsha Ukumbusho huu, na hakika Sisi ndio tutao ulinda.} [15:9].

Bali Qur-aan yenyewe imehifadhi akida (itikadi) sahihi ikiwa na sheria kamili ndani yake, na ikasimamisha Umma bora kabisa, hapa inatudhihirikia sisi kuwa muujiza wa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) umekuwa bora tofauti na miujiza ya ndugu zake manabii na Mitume (Swala Llahu

Qur-aan na Sayansi bega kwa bega.

"Nilifanya utafiti kuhusu Qur-aan Tukufu bila ya kuwa na fikra yake yoyote hapo kabla, na bila upendeleo. Lengo ni kutafuta kiwango cha maafikiano kati ya Qur-aan na kinachopatikana katikaelimu leo hii. Nilichokipata ni kuwa Qur-aan haina aya au andiko linaloweza kukosolewa kwa upande wa elimu katika zama hizi."

Maurice Bucaille

Maurice Bucaille

https://www.path-2-happiness.com/sw

Hayo ni Maneno ya Mwenyezi Mungu.

"Mimi sina shaka japo mara moja katika ujumbe wa Muhammad na ninaamini kuwa yeye ni Mtume wa mwisho. Ametumwa kwa watu wote na ujumbe wake umekuja kuhitimisha Wahyi uliokuja katika Torati na Injili. Dalili nzuri kabisa katika hilo ni Qur-aan yenye miujiza. Mimi napinga fikra za Pascal mwanazuoni wa Ulaya mwenye chuki kubwa ya Uislamu na Waislamu isipokuwa fikra moja tu: nayo ni kauli yake: Qur-aan sio katika utunzi wa Muhammad kama ambavyo sio katika utunzi wa Mathayo."

F. Motague

Mwanafikra na Mvumbuzi wa Kifaransa.

'alayhi wasallam) waliotangulia kwa kulinganisha ukubwa wa miujiza ile, pia miujiza ya Mtume Muhammad ni ya watu wote ulimwenguni na wa zama zote na ni muujiza utakao dumu milele.

Changamoto inaendelea kusimama dhidi ya wote wataendelea kushindwa kuleta mfano wa Qur-aan hii, Allah amesema:

{Sema: Wangeli kusanyika watu na majini ili walete mfano wa hii Qur'ani basi hawaleti mfano wake, hata wakisaidiana wao kwa wao.} [17:88].

Kuwa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) alitabiri matukio mbalimbali ulimwenguni na yalitokea kama alivyosema; kama vile Fathi (ufunguzi) ya Shaam, Iraq na Constantinople (uturuki). Hali kadhalika ameelezea kuhusu Ummah mbali mbali zilizopita na hali zao pamoja na manabii na mitume wao, kuanzia Adam ('Alayhi salaam), Nuuh, Ibrahim, Musa na Issa ('Alayhi salaam), kama ambavyo alitabiri matukio ya siku za usoni; na yakatokea kama alivyotabiri na miongoni mwa hayo ni pale Wafursi walipowashinda Warumi, Allah akaeleza kuwa baada ya miaka michache Warumi watawashinda Wafursi, Allah amesema: {Alif Lam Mim (A.L.M.) Warumi wameshindwa, Katika nchi iliyo karibu. Nao baada ya kushindwa kwao watashinda Katika miaka michache. Amri ni ya Mwenyezi Mungu kabla yake na baada yake. Na siku hiyo Waumini watafurahi. Kwa nusura ya Mwenyezi Mungu humnusuru amtakaye. Naye ndiye Mwenye nguvu Mwenye kurehemu. Ni ahadi ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu havunji ahadi yake. Lakini watu wengi hawajui. Wanajua hali ya dhaahiri ya maisha ya dunia, na wameghafilika na Akhera.} [30:1-7],

Na tukio hilo likatokea kama alivyolielezea Allah (Subhaanahu wa Ta'ala).

Manabii ('Alayhi salaam) wametabiri kuja kwa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) kabla ya kuja kwake kwa dahari nyingi wakatoa wasifu wa kutumwa kwake, mji na umma na mataifa mbali mbali na wafalme kumnyenyekea yeye na umma wake na wakataja kuenea kwa dini yake.

Kuwa yeye ni mwisho wa Mitume, na kama asingetumwa basi utabiri wao ungekuwa batili.

Ukweli wa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) na kuthibiti jambo lake katika Taurati na Injili, na baadhi ya watu katika Ahlul kitabu wakati wa kutumwa kwake ambao kasumba haikuwapofusha (kufanya hivyo); kama vile mtawa Bahira, bwana Waraqa bin Nawfal, sahaba Salman Al-Faarisy, aliyekuwa mwanazuoni wa kiyahudi kabla hajasilimu Abdallah bin Salaam na Zaid bin Sa'atah.

Ushindi wake kwa Ummah mbali mbali aliopigana nao ni dalili na alama miongoni mwa alama za utume wake; kwani ni muhali kwa mtu kujidai kuwa ametumwa na Mwenyezi Mungu (nae ni muongo) kisha baada ya hapo Allah ampe ushindi na kumuwezesha kuwashinda maadui, da'wah yake kuenea na kuongezeka kwa wafuasi wake, hilo halitokei ila katika mikono ya Mtume Mkweli.

Ibada yake Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam), ukweli wake, historia yake nzuri, mwendo wake, sheria yake na tabia yake njema, kwani aliyemtengeneza katika adabu hizo ni Mola wake: {Na hakika wewe una tabia tukufu.} [68:4],

Ni tengenezo la Mwenyezi Mungu.

"Katika zama ambazo nchi nyingi zilianguka, nchi ambazo hapo kabla zilikuwa sehemu ya utawala wa –Ufalme wa kale wa Diocletian. Ghafla katika moyo wa majangwa ya Arabia aliibuka mtesi (utesi). Ufalme ule uliochoka ukawa unafuatilia mtesi Yule kama kwamba ni ufalme mpya ambao ulikuwa unaibukia Magharibi. Uadui huu ulikuwa unapanuka siku hadi siku machoni mwa watu. Na ulinzi wa Mwenyezi Mungu ndio ambao daima ulikuwa ukiwaongoza askari wale wakweli na waaminifu kuelekea kwenye jihadi na ushindi mkubwa. Ushindi ule ulipelekea kufunguliwa kwa Syria na Misri, na baada ya hapo ufalme wa Wasasani wakaingia katika mazungumzo na Wakonstantini wakitishiwa na muelekeo ule (wa ushindi wa Waislamu)."

Aldo Mieli

Mustashrik wa Kifaransa.

Kwani sifa hizi tukufu hazikusanyiki isipokuwa kwa Nabii wa kweli.

Njia ya upokeaji wa habari ya Tawaatur ambayo utume wa Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) umenukuliwa pamoja na miujiza yake, mwenye kuangalia kwa makini hali za manabii mbali mbali na kusoma historia zao; atafahamu ufahamu wa yakini kuwa hakuna njia iliyothibitisha utume wa Nabii yoyote ila njia hiyo vile vile imethibitisha utume wa Nabii Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam).

Ukiangalia namna utume wa Musa na Issa ('Alayhima salaam) ulivyonukuliwa, utafahamu kuwa imenukuliwa kwa njia ya Tawaatur, na ndio Tawaatur iliyonukuu utume wa Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) ni tukufu zaidi na yenye kuaminiwa zaidi, kadhalika Tawaatur iliyotumika kunukuu miujiza na alama mbali mbali ni zenye kufanana, bali ya Muhammad ni kubwa zaidi na ni zama za karibuni zaidi; kwa sababu miujiza yake ilikuwa ni mingi zaidi, bali muujiza ulio mkubwa zaidi ni hii Qur-aan ambayo inaendelea kunukuliwa na kupokewa kwa njia za tawaatur kwa njia ya sauti na maandiko.

Kutosoma kwake kilichoandikwa na kutoandika kwake ni dalili ya miujiza yake, Allah alimtumia Mtume wake Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) akiwa hasomi na kuandika na huu ni uthibitisho kuwa Qur-aan tukufu imeshushwa kwake na Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) na ni dalili

kubwa sana na haswa kwa kuwa yeye ameishi pamoja na watu wake miaka mingi sana na lau angekuwa anajua kusoma yaliyoandikwa washirikina wangedai kuwa alichokuja nacho ni katika uvumbuzi wake na katika fikra zake. Allah amesema: {Na namna hivi tumekuteremshia Kitabu (cha Qur'ani). Basi wale tulio wapa Kitabu (cha Biblia) wataiamini (Qur'ani), na miongoni mwa hawa (washirikina) wapo watakao iamini. Na hawazikatai Ishara zetu isipo kuwa makafiri. Na wewe hukuwa kabla yake unasoma kitabu chochote, wala hukukiandika kwa mkono wako wa kulia. Ingeli kuwa hivyo wangeli fanya shaka wavunjifu.} [29:47-48], Kama inavyothibitisha kuwa aliyokuja nayo Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) ni kutoka kwa Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) na sio kutoka kwake mwenyewe (yeye Muhammad), Allah amesema: {Yeye ndiye aliye mpeleka Mtume kwenye watu wasio jua kusoma, awasomee Aya zake na awatakase, na awafunze Kitabu na hikima, ijapo kuwa kabla ya haya walikuwa katika upotofu ulio dhaahiri.} [62:2]

Katika wasifu wa Mtume Umiyyi ambaye anawasomea wasiojua kusoma aya za Allah, yaani Wahyi

https://www.path-2-happiness.com/sw



wake, na kuwatakasa na kuwafundisha kitabu, yaani anawakaririsha hicho, kama ambavyo Mitume walivyokuwa wanawatamkisha Ummah kitabu kwa kuandika na kuwaelimisha hekima ambayo Mitume iliyotangulia imefundisha Ummah zao. Katika wasifu wote huu kuna changamoto kwa muujiza wa Ummiyyi (kutosoma yaliyoandikwa) katika Mtume huyu (Swala Llahu 'alayhi wasalaam), pamoja na kuwa kwake Ummiyyi ameletea Ummah wake faida nyingi ambayo Mitume iliyosoma imewapelekea Ummah zao, hakuna upungufu wowote, hivyo Ummiyyi wenyewe umeibuka kuwa ni muujiza umempatisha sahibu yake yaliyo bora zaidi kuliko waliyoyapa mitume wenye kuandika kama vile Musa ('Alayhi salaam).

Tabia za Utume.

"Kwa hakika mimi nampenda Muhammad: Sababu ni ile tabia yake safi aliyonayo na mawazo na fikra zake. Kwa hakika mtoto huyu wa majangwani alikuwa ni mwanamme mwenye rai huru: Hujitegemea mwenyewe tu wala hajidai yasiyokuwepo, hakuwa mwenye kiburi!! Hata hivyo hakuwa dhalili, akisimama na nguo zake zenye viraka kama vile alivyompatia Mola wake na kama alivyotaka mwenyewe. Huzungumza na wafalme wa Kirumi na wa Kiajemi kwa maneno yake yenye kutetemesha anawaelekeza maisha haya na maisha ya akhera. Alikuwa anajua uwezo wa Nafsi yake, alikuwa ni mtu mwenye kupitisha azma yake, hacheleweshi kazi ya leo hadi kesho."

Thomas Carlyle

Mwandishi na Mwanahistoria wa Scotland.

https://www.path-2-happiness.com/sw

UTUME WA MWISHO

Hekima ya Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) imepelekea kumtuma Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) kwa ujumbe wake kwa watu wote wa ardhi, yenye kunasibiana na zama na mahala pote, Allah amesema: {Na hatukukutuma ila kwa watu wote, uwe mbashiri, na mwonyaji. Lakini watu wengi hawajui.} [34:28],

Na akauhifadhi (ujumbe huo) kutokana na kubadilishwa na kugeuzwa; ili ujumbe wake ubakie hai watu wanaishi nao, ikaepushwa na upotofu na kubadilishwa na kwa ajili hiyo Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) akaufanya kuwa ni ujumbe wa mwisho, na akamhusisha nao Muhammad, kwa sababu yeye ndie mtume wa mwisho, hakuna nabii baada yake; kwa kuwa Allah amekamilisha kwake ujumbe (utume), na akahitimisha kwake sheria na akatimiza jengo lake.

Dini ni Moja.

"Dini ya Manabii wote ilikuwa ni moja tu: Wao ni wamoja katika mwendo wao tokea Adam hadi Muhammad, vilishuka vitabu vitatu toka mbinguni navyo ni: Zaburi, Torati na Qur-aan. Mfano wa Qur-aan kwa torati ni mfano wa torati kwa Zaburi. Muhammad kwa mtazamo wa Issa ni kama vile Issa kwa mtazamo wa Mussa, lakini jambo la muhimu kulifahamu ni kuwa Qur-aan ni kitabu cha mwisho kutoka mbinguni imeteremka kwa watu na mwenyewe (Muhammad) ni Mtume wa mwisho. Hakuna tena kitabu baada ya Qur-aan wala Nabii baada ya Muhammad."

Henri de Castriesry
Luteni wa zamani katika jeshi la Ufaransa.

Kitabu cha Mwisho Kuteremka.

"Hapo kabla Torati ndio iliokuwa muongozo kwa watu na msingi wa tabia zao. Hadi alipodhihiri masihi Wakristo walifuata mafundisho ya Injili. Kisha ikaja Qur-aan na kuchukua nafasi zao. Qur-aan ilikuwa ni pana zaidi na yenye maelezo zaidi kuliko vitabu viwili vilivyoitangulia kama Qur-aan ilivyoweza kusahihisha uzushi yaliyoingizwa kwenye vitabu vilivyotangulia. Qur-aan imekusanya kila kitu, imekusanya sheria na kanuni zote. Kwani hicho ndicho kitabu cha mwisho kutoka mbinguni."

Washington Irving

Mustashrik wa Kimarekani.

Kwa ajili hiyo Allah amekifanya kitabu alichokuja nacho Muhammad kuwa ni mtawala juu ya vitabu vilivyotangulia na kinachovifuta, kama vile ambavyo sheria aliyokuja nayo Muhammad (Swala Llahu'alayhi wasallam) kufuta sheria zilizomo kwenye vitabu vilivyotangulia, Allah mwenyewe amedhamini kuhifadhi ujumbe wake; na hivyo ikawa inanukuliwa na kupokewa hali ya kuwa ni tawaatur; na hivyo ndivyo ilivyonukuliwa na kupokewa Qur-aan ikiwa ni tawaatur kwa sauti (jinsi isomavyo) na kwa kuandikwa jinsi iandikwavyo, kadhalika sheria ya dini hii na ibada zake zimenukuliwa jinsi ilivyokuwa ikitendwa kunukuliwa kwa njia ya tawaatur na sunnah zake na hukumu zake mbali mbali.

Mwenye kuangalia katika vitabu mbali mbali vilivyonukuliwa Sira na Sunnah za Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) ataona kuwa sahaba zake

(Radhiya LLahu 'anhum) waliweza kuwahifadhia watu hali za Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam), maneno yake yote, na matendo yake, na hivyo basi wakanukuu ibada zake kwa Mola wake na dhikri zake, istighfaar, jihadi zake, ukarimu wake, ushujaa wake, namna alivyokuwa akiishi na sahaba zake na wanaomtembelea, kama walivyonukuu furaha yake ilivyokuwa, huzuni yake, safari zake na kutosafiri kwake, wasifu wa kula na kunywa kwake, na kuvaa kwake, kuamka na kulala kwake,utakapojua hilo utayakinisha kuwa dini hii imehifadhiwa kwa Allah kuuhifadhi,na wakati huo utajua kuwa yeye ni hitimisho la mitume na manabii; Allah amesema: {Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na Mwisho wa Manabii, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.} [33:40].

Mwalimu wa Wanadamu

"Mwenendo wa Mtume wa Waarabu umechukua (umeshika) akili za wafuasiwake; na haiba yake ikapanda kwao juu zaidi. Waliamini ujumbe wake kwa imani ambayo imewafanya wakubali Wahyi ulivyokuwa ukiteremka kwake. Kama ambavyo matendo yake (kama yalivyorekodiwa na Sunnah) ilikuwa ni chanzo cha kanuni. Kanuni ambazo haziishi katika kupanga maisha ya Kiislamu peke yake, bali yaliambatana vile vile na mahusiano ya Waislamu Wafunguzi (kwa nchi nyingi) na raia zao na wasio Waislamu."

Arnold J. Toynbee

Mwanahistoria wa Uingereza.

Mwisho wa Utume

"Mimi ni mmoja miongoni mwa waliofurahishwa na Nabii Muhammad aliyechaguliwa na Mwenyezi Mungu mmoja, ili ujumbe wa mwisho uwe juu ya mikono yake, na pia yeye awe Mtume wa mwisho."

Tolstoy

Mwanafasihi wa Kirusi.

Muabuduni Mwenyezi Mungu.

"Muhammad alikuwa Mtume wa mwisho Mtukufu ambae ametumwa na Mwenyezi Mungu ili awalinganie watu katika kumuabudu Mwenyezi Mungu."

Washington Irving

Mustashrik wa Kimarekani

REHEMA KWA WALIMWENGU

Allah amemtuma Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) kuwa rehma kwa walimwengu wote wanaume kwa wanawake, watoto kwa wakubwa, bali Allah amemtuma kuwa rehema hata kwa wasiomuamini, na rehema hii inaonekana wazi katika misimamo ya Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) maisha yake yote, na mingi inaonekana alipokuwa akilingania watu wake (akiwahurumia) walimkadhibisha na kumfukuza kutoka katika mji wake Makkah na kujaribu kumuua, Allah akawa ndiye anayemtosha kwa kila kitu akawarejeshea vitimbwi vyao Allah amesema: {Na walipo kupangia mpango walio kufuru wakufunge, au wakuuwe, au wakutoe. Wakapanga mipango yao, na Mwenyezi Mungu akapanga yake. Na Mwenyezi Mungu ndiye mbora wa mipango.} [8:30]

Na yote hayo hayakumzidishia isipokuwa rehema, huruma na kujali zaidi katika kuwaongoa, Allah Ta'ala amesema: {Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayo kutaabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma.} [9:128],

Uislamu wa Kilimwengu.

"Kwa hakika aya za Qur-aan ambazo zinaashiria kwenye Uislamu wa Ulimwengu kwa wasifu wake kuwa ni dini ambayo Mwenyezi Mungu amemteremshia Nabii wake kuwa (Rehema kwa Walimwengu): Huo ni mwito wa moja kwa moja kwa Ulimwengu wote. Hii ni dalili ya wazi kuwa Mtume alijua kwa yakini yote kuwa ujumbe wake umekadiriwa kuvuka mipaka ya Ummah wa Kiarabu, na kuwa ni juu yake kufikisha neno jipya kwa watu wanaonasibika na jinsi tofauti wenye kuzungumza lugha tofauti."

Laura VecciaVaglieri

Mustashrik wa Italia

Na baada ya kuwashinda katika siku ya ukombozi wa Makkah aliwasamehe, na Allah alipomtuma Malaika ili awabamize Makafiri kwa milima miwili mikubwa ili waangamie, Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) alisema: "Bali nitasubiri huenda Allah akatoa ndani ya migongo yao wenye kumuabudu Allah peke yake"

Allah Ta'ala amesema: {Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote.} [21:107],

Yeye ni rehema kwa Walimwengu, kwa watu wote pamoja na tofauti walizonazo za rangi zao, lugha zao, mitazamo yao, fikra zao, itikadi zao na sehemu zao.

Rehema hii haijaishia kwa wanadamu tu, bali imefika hadi kwenye wanyama na vitu visivyo na uhai. Kwa mfano yule ngamia wa mmoja wa wakazi wa Madina ambaye aliadhibiwa na mwenye ngamia akawa anamtesa kwa njaa kali, kwa hiyo moyo wa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) ukamhurumia na kuamuru mwenye ngamia kumfanyia wema ngamia wake na kutomtumikisha zaidi ya uwezo wake.

Mara moja Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) alipoona mtu amechukua vitoto vya njiwa alimhurumia njiwa yule na

kuamrisha kurejeshewa vitoto vyake, naye Mtume ndie aliyesema: «Na mnapochinja chinjeni vizuri.» (Muslim).

Kama ambavyo huruma ya Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) ilivyoenea kwa vitu visivyo na roho, alilihurumia lile gogo ambalo lilisikitika na kulia kwa kuachana na Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) hivyo akalihurumia na akateremka (kutoka mimbarini) na kukikumbatia hadi kiliponyamaza na kutulia.

Huruma yake haikuwa kwenye mitazamo na matukio peke yake, bali ni amri, sheria, mfumo na tabia njema ambayo ameifanya kwa ajili ya watu.

Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) amenukuliwa akisema katika kuhamasisha huruma, wema na ulaini kwa watu, na akaonya na kutahadharisha atakayefanya ugumu juu yao, akasema: «Ewe Mola wangu atakayetawalia jambo katika Ummah wangu akawafanyia watu ugumu, mfanyie ugumu, na atakayetawalia jambo katika umma wangu akawahurumia basi mhurumie.» (Muslim).

Hivyo basi rehema (huruma) ni tabia njema katika tabia njema za Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam), na msingi muhimu katika dini ya Kiislamu ni kuwa dini hii ni ya huruma na amani.

Ni Rehema iliyozawadiwa watu

"Maisha ya Kihistoria ya Muhammad hayawezi kupata wasifu mzuri zaidi ya ule alioueleza Mwenyezi Mungu pale aliposema: "Na hatukukutuma isipokuwa rehema kwa Walimwengu." Yatima Mtukufu ametoa rehani Nafsi yake kuwa yeye ni rehema kubwa kwa kila mnyonge na kila mhitaji. Muhammad alikuwa rehema kweli ya yatima, wapita njia (wasafiri), waliopatwa na maafa, fukara wote na wafanyakazi wa kima cha chini wenye tabu na usumbufu."

Jan Lake

Mustashrik wa Hispania

https://www.path-2-happiness.com/sw

FURAHA YA MWANADAMU KWA KUTUMWA KWAKE (Swala Llahu 'alayhi wasalaam)

Mwenye kuwatoa wanadamu kutoka kwenye kiza hadi kwenye nuru.

"Nabii Muhammad aliwafikisha viumbe kwenye kiwango cha juu zaidi cha furaha kwa haraka sana. Na atakayeangalia kwa jicho la busara na uoni wa kina katika hali za wanadamu kabla ya hapo na upotofu waliokuwa nao, na akaangalia hali zao baada ya hapo na yaliyowakuta katika zama zao katika maendeleo makubwa utaona tofauti kubwa kati ya hali mbili hizo kama ilivyo kati ya mbingu na ardhi."

Abdullah Quilliam
Mwanafikra wa Uingereza

Utume wake Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) umekuja kwa hiyo watu wakaongoka kwa baraka za utume wa Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam), na ubainifu na uongofu, aliyokuja nayo (hidaya). Uongofu ambao uko wazi kuliko maelezo ya wanaousifia na kuwa juu ya maarifa ya wajuzi.

Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) alikuja na elimu yenye manufaa, matendo mema, tabia tukufu kabisa, mwenendo ulionyooka, ambao lau zingekusanyika hekima zote na elimu za watu wote na Ummah zote na matendo yake kulinganisha na hekima aliyotumwa nayo Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) basi zingetofautiana na tofauti kubwa, kuhimidiwa ni kama apendavyo mola wetu na kuridhia.

Kwa upande wa akida; shirki ilikuwa imeenea kwa wanadamu na kumuabudu asiyekuwa Allah, kutokana na watu waliopewa kitabu kutoka mbinguni ambavyo vilipotoshwa.

Kwa hiyo Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) akaja na tawhidi halisi na kumuabudu Allah peke yake

na kutomshirikisha na chochote, na kuwatoa watu katika kuabudu watu na kuelekea kumuabudu Mola wa waja, hivyo kutakasa nafsi zao kwa tawhidi na kuondosha uchafu wa ushirikina na uchafu wa kuabudu asiyekuwa Allah. Hivyo Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) akamtuma kwa yale aliyowatuma nayo Mitume kabla yake, Allah amesema: {Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia ya kwamba hapana mungu isipo kuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu.} [21:25],

Na akasema Allah vilevile: {Na Mungu wenu ni Mungu mmoja tu, hapana mungu ila Yeye. Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.} [2:163].

Kwa upande wa kijamii, Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) alitumwa zama ambazo dhuluma, udikteta na kuabudiwa watu kulikuwa kumetawala, utabaka unaochukiza ulikuwa umewagawa wanadamu katika tabaka nyingi, kila tabaka linatumikisha tabaka lingine na yanadhulumiana, Mtume Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) akaja na kuwafanya watu wote kuwa sawa, Muarabu kwa Muajemi, mweupe kwa mweusi, hakuna mbora ila kwa ucha-Mungu na amali njema, Allah amesema: {…Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamngu zaidi katika nyinyi...} [49:13]

Na akaamrisha uadilifu, wema, kushikamana kijamii na kukataza dhulma, munkari na uadui, Allah amesema: {Hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha kufanya uadilifu, na hisani, na kuwapa jamaa; na anakataza uchafu, na uovu, na dhulma. Anakuwaidhini ili mpate kukumbuka.} [16:90]

Dini ya watu wote.

"Aya mbili: "Bila ya shaka Dini mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu…." (3:19) na "Na hatukukutuma ila kwa watu wote, uwe mbashiri, na mwonyaji" (34:28) zimeacha athari kubwa sana Katika nafsi yangu: Kwani ndani yake kuna dalili ya ile sifa ya kielmu ambao Uislamu umepambauka nao mbali na zile sifa unazosifika nazo Uislamu za nidhamu na sheria nyingine na ubainifu wake kamili wa ukweli wa Nabii Issa. Je, kuna ukweli wenye nguvu zaidi kuliko mafundisho yale huru ambayo yanatuusia kuheshimu kila walichokuja nacho Mitume na manabii?! Hapana shaka yoyote kuwa dini ya Kiislamu ni dini ya haki, dini ya kweli na dini yenye hoja na dalili."

Wagner

Mtafiti wa Kidachi (Uholanzi).

Bali akahifadhi haki za watu, na kukataza kundi moja kudharau kundi lingine, Allah amesema: {Enyi mlio amini! Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao, wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao. Huenda hao wakawa bora kuliko wao. Wala msivunjiane hishima, wala msiitane kwa majina ya kejeli. Ni uovu kutumia jina baya baada ya kwisha amini. Na wasio tubu, hao ndio wenye kudhulumu.} [49:11].

Upande wa tabia; Allah amemtuma Mtume wake na tabia za watu zilikuwa duni, chafu na mbaya sana, hakukuwa na maadili mema wala tabia njema, Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) akaja kuwarudisha watu kwenye maadili mema na adabu tukufu; ili maisha yao yafurahi kwa miamala mizuri, Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) amesema: "Kwa hakika nimetumwa kutimiza mazuri ya tabia." (Al-Bayhaqi).

Bali Allah amesifu tabia yake kuwa ni tukufu; Allah amesema: {Na hakika wewe una tabia tukufu.} [68:4],

Nae alikuwa ndie kiigizo chema katika tabia na adabu, na mfano mzuri katika kuipa nyongo dunia, Ucha-Mungu na muamala – mzuri na maneno mazuri bali Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) alikuwa ni kigezo kizuri katika kila kitu kizuri, Allah Ta'ala amesema: {Hakika nyinyi mnayo ruwaza njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anaye mtaraji Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na akamkumbuka Mwenyezi Mungu sana.} [33:21].

Mafunzo kutoka katika Hijja ya kuaga.

"Muhammad alihiji Hija ya kuaga kutoka Madina kwenda Makkah kabla ya kifo chake kwa mwaka mmoja. Wakati huo alitoa mawaidha makubwa kwa watu wake. Sentensi ya kwanza tu aliondosha mbele yake yote waliyokuwa nayo Waislamu kama vile unyang'anyi, uizi, kulipiza kisasi, na umwagaji wa damu, na paragrafu ya mwisho alisisitiza usawa kati ya muumini wa Kihebeshi na Khalifa wa Waislamu. Kwa hakika aliweka msingi mkubwa Ulimwenguni kwa ajili ya kuamiliana kwa uadilifu na ukarimu."

H. G. Wells.

Mwandishi na Mwanafasihi wa Kiingereza.

Ama mwanamke alikuwa anasumbuka kwa mengi kabla ya Allah kumtuma mtume wake, wakati huo mwanamke akidhalilishwa na hana haki yoyote, watu walitofautiana kuhusu mwanamke; Je, ni mwanadamu au la? Je, ana haki ya kuishi au huuawa na kuzikwa akiwa mdogo?! Watu walikuwa kama vile walivyosifiwa na Allah (Subhaanahu wa Ta'ala): {Na mmoja wao akibashiriwa kwa msichana, uso wake unasawijika, naye kajaa chuki. Anajificha asionekane na watu kwa ubaya wa aliyo bashiriwa! Je, akae naye juu ya fedheha hiyo au amfukie udongoni? Tazama uovu wa wanavyo hukumu!} [16:58-59],

Alikuwa ni mdoli tu anachezewa na watu na kustarehesha, akiuzwa na kununuliwa, kiumbe kinachodharauliwa, hivyo Allah hivyo Allah akamtuma Mtume wake kwa ajili ya kumtukuza, kumkirimu mwanamke, Allah Ta'ala amesema:

{Na katika Ishara zake ni kuwa amekuumbieni wake zenu kutokana na nafsi zenu ili mpate utulivu kwao. Naye amejaalia mapenzi na huruma baina yenu. Hakika katika haya bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanao fikiri.} [30:21],

Tabia ya Nabii wa Allah Muhammad.

"Muhammad alikuwa ni mtukufu mno na maadili mema, alikuwa mwingi wa haya mwenye hisia kali. Alikuwa ni mwenye ufahamu mkubwa na akili nyingi, mpole na mwenye heshima."

Abdullah Quilliam

Mwanafikra wa Uingereza



Njia ya Ulimwengu.

"Nimesoma vizuri maisha ya Muhammad Mtume wa Uislamu mara nyingi, sikupata ndani yake ila matukufu ya tabia kama kinavyotakiwa kuwa.Ni mara ngapi nimetamani Uislamu kuwa ndio njia ya Ulimwengu."

Sir George Bernad Shaw

Mwandishi wa Uingereza.



Hadhi ya Mwanamke.

"Uislamu umemnyanyua mwanamke katika nchi za Kiarabu, na hivyo ukamaliza desturi ya kuua mabinti na akaweka usawa baina ya mwanaume na mwanamke katika taratibu za kisheria na uhuru wa matumizi ya mali, na akajaalia miongoni mwa haki yake ni kufanya kazi yoyote ya halali. Na kuhifadhi mali na mapato yake, kurithi na uhuru wa kutumia mali yake atakavyo, na hivyo kufuta ada waliokuwa nayo Waarabu katika zama za Ujahilia ya wanawake kurithiwa na baba zao au watoto wao kama vile zinavyorithiwa mali na mizigo, na ukafanya fungu la mirathi ya mwanamke ni nusu ya fungu la mwanaume na akakataza kuozeshwa bila ya matakwa yao."

Will Durant

Mwandishi wa Kimarekani

Bali aliamrisha afanyiwe wema kama mama, Allah amesema: {Na Mola wako Mlezi ameamrisha kuwa msimuabudu yeyote ila Yeye tu, na wazazi wawili muwatendee wema….} [17:23],

Na wema kwake ukatangulizwa kuliko wema wa mwanaume, wakati mmoja mtu alikwenda kwa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) na kusema: «Ewe Mtume wa Allah, ni nani mwenye haki zaidi ya kusuhubiana nae? (Mtume) akajibu: "Ni Mama yako", akasema: kisha nani? Akasema: "Mama yako".

Akasema: "kisha nani?" Akasema: "Mama yako". Akasema kisha nani? Akasema: "Baba yako.» (Al-Bukhari).

Kadhalika Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) «ametaka akirimiwe akiwa ni msichana, akasema (Swala Llahu 'alayhi wasalaam): "Aliye na wasichana watatu anawalea, kisha akawahurumia, na kuwatunza, mtu huyu imempasa pepo kabisa amesema: ilisemwa: Ewe Mtume wa Allah, Je, akiwa na wawili (Mtume) akasema: "Na wawili:» (Imepokewa na Ahmad).

Vile vile mwanamke huyo akiwa ni mke ameamrishwa apewe hadhi yake kwa kuunganishwa na wema wake, hivyo Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) akasema: «Mbora wenu ni Mbora wenu kwa familia yake, na mimi ni Mbora wenu kwa familia yangu.» (Imepokewa na Ibn Majah).

Jeuri na Dhuluma!!

"Vikao vya Wanafalsafa huko Ulaya vilikuwa vikijadili: Je, mwanamke ana roho kama roho ya mwanamume? Je, ana roho ya mwanadamu au mnyama? Na wakahitimisha mjadala wao kuwa mwanamke ana roho. Lakini roho hiyo ni duni sana kuliko roho ya mwanamume."

NI UPI UJUMBE ULIOBAKIA?

Dini zote zimejiita kwa jina la mwanzilishi wake au kwa jina la taifa alilotumwa, hivyo basi kunasibishwa jina "Zoroaster" kwa dini ya uzorosti (Zoroastianism) na "Budha" kwa ajili ya dini ya Ubudha, na kwa sababu Uyahudi ulitokeza kwa kabila la Yahudha (Jehova), ndio maana ukaitwa Uyahudi na Ukristo kutokana na Kristo, tofauti na Uislamu ambao haujafungamanishwa na mtu au taifa fulani, bali kila mwenye kujisalimisha kwa Allah Mtukufu, na kutekeleza maamrisho yake na kukatazika na makatazo yake, mwenye kunyenyekea kwake peke yake, basi mtu huyo atakuwa amejisalimisha nafsi yake kwa Allah Ta'ala.

Yule ambaye atamfuata Mtume wa mwisho Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) na akaelekea katika dini ya haki ambayo amekuja nayo, na kuamini na kumfuata; huyo ndie Muislamu wa kweli, vyovyote awavyo katika zama zozote au mahala popote, na katika rangi yoyote au jinsia yoyote ile.

Mwenyezi Mungu hana Mshirika.

"Hakuna Mungu isipokuwa Allah peke yake hana mshirika. Yeye haki na kila asiyekuwa yeye ni batili, ametuumba na ameturuzuku. Uislamu ni kujisalimisha kwa Mungu, kumnyenyekea yeye, kutulia kwake na kumtegemea yeye tu–na kuwa nguvu yote iko katika (istiqama) kunyooka katika hekima yake, na kuridhika kwa mgawo wake kadiri itakayokuwa katika dunia hii na katika akhera. Na kwa kadiri yoyote Allah atakavyotupa mtihani (na hata ikiwa ni mauti) basi inatakiwa kupokea hayo nyuso kunjufu na nafsi zenye ghera, zenye kuridhia vile vile na kujua kuwa hayo ni kheri na kuwa hakuna kheri zaidi ya hayo, kwani ni upumbavu mtu kuweka ndani ya akili yake dhaifu mizani ya Ulimwengu na hali zake, bali ni juu yake kuamini kuwa Ulimwengu una sheria adilifu, na hata kama itapotea katika ufahamu wake, na ya kuwa kheri ndio msingi wa ulimwengu, na kutengeneza (Islahi) ni roho ya ulimwengu…ni juu yake kufahamu hayo na kuamini na kufuata katika utulivu na Ucha-Mungu."

Thomas Carlyle

Mwandishi wa Mwanahistoria wa Scotland.

Hakuna tofauti kati ya Muarabu na Muajemi.

"Waislamu, hawaonani wageni vyovyote vile watakavyotofautiana mataifa yao, vivyo hivyo katika miji ya Waislamu (Daarul Islam) hakuna tofauti kati ya Mchina Muislamu na Muarabu Muislamu katika kufaidi haki zao. Kwa sababu haki za Kiislamu zinatofautiana na haki za wazungu (Ulaya) na hii ni tofauti ya msingi kabisa."

Gustaf Lubon
Mwanahistoria wa Kifaransa.

UJUMBE ULIOBAKIA NDILO UMBILE LA ULIMWENGU

Uislamu ndio mwendo unaokwenda nao ulimwengu huu, Allah amesema: {Je, wanataka dini isiyo kuwa ya Mwenyezi Mungu, na hali kila kilichomo mbinguni na katika ardhi kimesilimu kwa kumt'ii Yeye kikipenda kisipende, na kwake Yeye watarejeshwa?} [3:83],

Kwa hiyo inafahamika kuwa kila kitu hapa ulimwenguni kinafuata kanuni maalumu, na mwendo maalumu thabiti; hivyo basi jua, mwezi, nyota, ardhi na sayari nyingine zipo chini ya kanuni za kudumu (zisizobadilika) haziwezi kujiondosha au kutembea nje ya mzunguko wake walau kwa kadiri ya unywele, hata mwanadamu kama utazingatia hali yake itakubainikia wewe kuwa ananyenyekea utaratibu wa Allah unyenyekevu kamili.

Mwanadamu huyu hapumui wala hahisi haja yake ya maji, chakula, mwanga, joto ila kulingana na makadirio ya Allah yaliyopangilia maisha yake kwa utaratibu maalumu, na makadirio haya ndiyo yanayoongoza viungo vyake vyote; hivyo basi wadhifa na kazi mbali mbali zifanywazo na viungo hivi havisimami vyenyewe ila kulingana na alichokadiriwa yeye na Allah.

Makadirio hayo ya jumla yenye kukusanya ndio ambayo mwanadamu anajisalimisha kwake wala hakiondoki kitu katika utiifu wake katika

https://www.path-2-happiness.com/sw

ulimwengu huu, kuanzia sayari kuwa mbinguni hadi punje ndogo ya mchanga ardhini, yote ni katika makadirio yake Mwenyezi Mungu Mfalme Mtukufu mwenye kukadiria mambo; ikiwa vitu vyote mbinguni na ardhini na yaliyo baina yake huongozwa na makadirio haya, inatubainikia kuwa; Uislamu ni dini ya Ulimwengu wote; kwa sababu Uislamu una maana ya kufuata amri ya mwenye kuamrisha na kuacha makatazo yake bila ya kupinga. {Na amefanya vikutumikieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi, vyote vimetoka kwake. Hakika katika hayo zimo Ishara kwa watu wanao fikiri.} [45:13].

Ama mwanadamu ambaye hamjui Mola wake na anakana uwepo wake pamoja na dalili zake, au kuabudu asiyekuwa Yeye na kumshirikisha na asiyekuwa Yeye, apende asipende mtu huyo anakuwa amejisalimisha kwake kwa maumbile yake aliyoumbiwa nayo.

Ama mwanadamu anashindana na mambo mawili:

Jambo la Kwanza:

Ni maumbile ambayo Allah amewaumbia nayo wanadamu kama vile kujisalimisha, kunyenyekea, na mapenzi ya kumuabudu Yeye Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) na kujikurubisha kwake.

Kadhalika kupenda anavyopenda Allah kama vile haki, kheri, ukweli, kuchukia anachokichukia Allah ikiwemo batili, shari, jeuri, dhuluma na yanayofuata hayo katika nyenzo za maumbile ya mwanadamu kama kupenda mali, familia, watoto, hamu ya kula na kunywa, kuoa na yanayohitajiwa katika hayo ili viungo vya mwili kufanya kazi zake.

https://www.path-2-happiness.com/sw

Jambo la Pili: Matakwa ya mwanadamu na Uchaguzi wake, wakati ambapo Allah amekwisha mtumia Mtume na kumteremsha vitabu; ili apambanue baina ya haki na batili, uongofu, upotevu, kheri na shari, na akampa akili na ufahamu ili awe na uoni katika uchaguzi wake; akipenda atafuata njia ya kheri ambayo itampeleka katika haki na uongofu, na akipenda kufuata njia ya shari ambayo itamwongoza katika shari na maangamizi: {Na sema: Hii ni kweli itokayo kwa Mola wako Mlezi. Basi atakaye, aamini. Na atakaye, akatae. Hakika Sisi tumewaandalia wenye kudhulumu Moto ambao utawazunguka kama khema. Na wakiomba msaada watasaidiwa kwa kupewa maji kama mafuta yaliyo tibuka. Yatayo wababua nyuso zao. Kinywaji hicho ni kiovu mno! Na matandiko hayo ya kupumzikia ni maovu mno!} [18:29].

Kwa hiyo ukimuangalia mwanadamu kwa mazingatio ya jambo la kwanza utaona kuwa ameumbwa juu ya kujisalimisha, umbile lake linampelekea katika kufuata na kulazimika, wala hawezi kwenda kinyume nayo hali yake ni kama hali za viumbe wengine.

Ukimuangalia kwa kupitia muono wa pili utamuona ni mwenye hiari; anachagua anayoyataka, kwa hali hii ni kuwa ima awe ni Muislamu au awe ni Kafiri, Allah Ta'ala amesema: {Hakika Sisi tumembainishia Njia. Ama ni mwenye kushukuru, au mwenye kukufuru.} [76:3];

Kwa hiyo utakuta watu wanagawanyika sehemu mbili:

Mwanadamu mwenye kumjua Mola wake, anamuamini kuwa ni Mola wake, Mfalme wake na mola wake anayemuabudu Peke Yake, na anafuata sheria yake katika maisha yake ya uchaguzi, kama vile ambavyo yupo katika maumbile ya kujisalimisha kwa Mola wake, ambapo hawezi kwenda nayo kinyume, akifuata makadirio yake, na huyu ndie Muislamu aliyekamilika ambae ameukamilisha Uislamu wake, na hapo ndipo elimu yake ilipokuwa sahihi; kwani amemjua Mola na Muumba wake ambae amemtumia Mitume na kumpa uwezo elimu na kujifunza, na hivyo akili yake ikawa sahihi na

rai yake kuwa nzuri, kwa sababu ameitumia fikra yake, kisha akaamua kutomuabudu yeyote ila Allah ambae amemkirimu kipawa cha ufahamu na rai katika mambo, hivyo basi ulimi wake ukawa sahihi wenye kutamka haki kwa sababu hakiri isipokuwa uwepo wa Mola mmoja tu ambaye ni Allah Ta'ala ambaye amemneemesha uwezo wa kuzungumza na kutamka.

Ni kama kwamba maisha yake yaliyobakia hayakubaki isipokuwa ukweli tu kwani anafuata sheria ya Allah katika mambo ambayo mwenyewe ana hiari nayo, na ukaenea baina yake na viumbe wengine ulimwenguni mtangamano wa kufahamiana na kuliwazana pamoja.

Kwa sababu hamuabudu isipokuwa Allah mwingi wa hekima, mjuzi, ambaye wanamuabudu na kunyenyekea na kufuata makaridio yake viumbe wake wote, na Allah amewadhalilisha kwa ajili yako ewe mwanadamu, Allah Ta'ala amesema: {Na mwenye kuuelekeza uso wake kwa Mwenyezi Mungu, naye akawa anafanya wema, basi huyo hakika amekwisha kamata fundo lilio madhubuti. Na mwisho wa mambo yote ni kwa Mwenyezi Mungu.} [31:22].

Kamwe Havipo pamoja

"Sikuwa na hiari katika kulinganisha kati ya msingi wa tawhidi ya Allah katika taswira ya Qur-aan pamoja na itikadi ya utatu kama Mkristo. Nikaona kuwa msingi huu wa pili upo duni sana kulinganisha na msingi wa Uislamu. Na kutokea hapo kwa dhati kubwa nikaanza kupoteza imani ya Ukristo kwa kuzingatia kuwa kumuamini kwangu Allah ndio mwanzo na muhimu zaidi katika dini yoyote: Kwa hiyo Ikiwa kumuamini kwangu Allah nimekosea katika ufahamu wa dini sahihi, maana yake ni kuwa kila kitu kinakuwa ni mchezo ambao hauna maana."

Najimu Ramoni

Mhubiri wa Ghana

UJUMBE ULIOBAKIA NI DINI YA MANABII NA MITUME WOTE:

Uislamu ni dini ambayo Allah ameiteremsha kwa wanadamu wote, Allah amesema: {…Basi Mungu wenu ni Mungu Mmoja tu. Jisalimishieni kwake tu, na wabashirie wanyenyekevu} [22:34],

Nayo ni dini ya manabii na Mitume wote, Allah amesema: {Semeni nyinyi: Tumemuamini Mwenyezi Mungu na yale tuliyo teremshiwa sisi, na yaliyo teremshwa kwa Ibrahim na Ismail na Is-hak na Yaakub na wajukuu zake, na waliyo pewa Musa na Isa, na pia waliyo pewa Manabii wengine kutoka kwa Mola wao Mlezi; hatutafautishi baina ya yeyote katika hao, na sisi tumesilimu kwake.} [2:136]

Mitume wa Allah wameiamini, na kutangaza Uislamu wao kwa Allah, na kuulingania, Allah amesema kuhusu Nuhu: {Wasomee khabari za Nuhu alipo waambia watu wake: Enyi watu wangu! Ikiwa kukaa kwangu nanyi na kukumbusha kwangu kwa Ishara za Mwenyezi Mungu kunakutieni mashaka basi mimi namtegemea Mwenyezi Mungu. Nanyi tengezeni mambo yenu pamoja na washirika wenu, na wala mambo yenu yasifichikane kwenu. Kisha nihukumuni, wala msinipe muhula. Lakini mkigeuka, basi mimi sikukuombeni ujira. Ujira wangu hauko ila kwa Mwenyezi Mungu. Na nimeamrishwa niwe miongoni mwa Waislamu.} [10:71-72],

Na kuhusu Ibrahim ('Alayhi Salaam) amesema: {Na Mola wake Mlezi alipo mwambia: Silimu, Nyenyekea! Alinena: Nimesilimu, nimenyenyekea kwa Mola wa walimwengu wote.} [2:131],

Bali Ibrahim aliwausia hayo wanawe baada yake, Allah amesema kuhusu hilo: {Na Ibrahim akawausia wanawe, na pia Yaaqub: Enyi wanangu! Hakika Mwenyezi Mungu amekuteulieni Dini hii; basi msife ila nanyi mmekuwa Waislamu, wanyenyekevu. Je! Mlikuwapo yalipo mfikia Yaaqub mauti, akawaambia wanawe: Mtamuabudu nani baada yangu? Wakasema: Tutamuabudu Mungu wako na Mungu wa baba zako, Ibrahim na Ismail na Is- hak, Mungu Mmoja tu, na sisi tunasilimu kwake. } [2:132-133]

Na kuhusu Musa ('Alayhi Salaam) Allah amesema: {Na Musa alisema: Enyi watu wangu! Ikiwa nyinyi mmemuamini Mwenyezi Mungu, basi mtegemeeni Yeye, ikiwa nyinyi ni Waislamu.} [10:84]

Na amesema katika habari za Masihi ('Alayhi salaam): {Na nilipo wafunulia Wanafunzi kwamba waniamini Mimi na Mtume wangu, wakasema: Tumeamini na shuhudia kuwa sisi ni Waislamu.} [5:111].

Uislamu ni ujumbe wa mwisho kutoka mbinguni kwa ajili ya wanadamu ambao amemtuma nao Mtume wake Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) kwa watu wote, ambao Allah ameukamilisha na kuuridhia kwa waja kuwa ndio dini yao. Allah Ta'ala amesema: {…Leo nimekukamiliishieni Dini yenu, na nimekutimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni UISLAMU uwe ndiyo Dini….} [5:3].

Katika aya hii tukufu Allah anaelezea kuwa amewaridhia wanadamu Uislamu kuwa ndio dini yao, na Allah akatangaza kuwa ndio dini ya haki, na ya kuwa hatokubali kwa yeyote dini isiyokuwa hiyo, Allah amesema: {Bila ya shaka Dini mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu….} [3:19],

Na akasema vile vile: {Na anaye tafuta dini isiyo kuwa Uislamu haitakubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa katika wenye kukhasiri.} [3:85].

Katika aya ya kwanza anasisitiza kuwa dini anayoitambua ni Uislamu tu, na katika aya ya pili kuwa Allah hatokubali kwa yeyote dini isiyokuwa Uislamu, na kuwa watakaofaulu wakiwa na furaha baada ya mauti ni Waislamu peke yao, na ambao watakufa bila ya Uislamu watakuwa wamepata hasara katika akhera, na wataadhibiwa motoni; na kwa hili Mitume wote walitangaza Uislamu wao kwa Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) na wakatangaza kuwa mbali na wale ambao hawakusilimu, atakayetaka kuongoka miongoni mwa Mayahudi na Manasara na kupata furaha basi asilimu na aingie katika Uislamu amfuate Mtume wa Uislamu Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) ndipo awe mfuasi wa kweli wa Musa, Issa ('Alayhima salaam); kwani Musa, Issa, Muhammad na Mitume wote ni Waislamu, wote walilingania Uislamu, kwani ndio dini ya Allah aliowatuma kuifikisha kwa wanadamu, hivyo haifai kwa yeyote aliyepatikana na kuzaliwa baada ya Muhammad hadi mwisho wa dunia kuwa yeye amejisalimisha kwa Allah, wala Allah hatokubali madai hayo ila tu baada ya kumuamini Muhammad kuwa ni Mtume kutoka kwa Allah, na amfuate, na atende kulingana na Qur-aan ambayo Allah ameiteremsha kwake, Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) amesema: «Naapa kwa ambae nafsi ya Muhammad ipo mikononi mwake, atayenisikia yoyote katika Ummah huu, awe Myahudi au Mnasara, kisha akafa na hakuniamini nilichoshushwa nacho, isipokuwa atakuwa katika watu wa motoni.» (Muslim).

Uislamu ni Mwepesi.

“Hakika wepesi mkubwa wa Uislamu unatokana na tawhidi halisi. Katika wepesi huu ndio kuna siri ya nguvu ya Uislamu. Uislamu na ufahamu wake ni mwepesi umeepukana na yale tunayo yaona katika dini nyingine na akili iliyosalimika inakataa migongano na utata. Hakuna kitu kilicho wazi zaidi kuliko misingi ya Uislamu inayoeleza uwepo wa Mungu mmoja na usawa wa wanadamu wote mbele ya Allah.”

Gustaf Lubon

Mwanahistoria wa Ufaransa.

https://www.path-2-happiness.com/sw



UKAMILIFU WA UJUMBE ULIOBAKIA:

Uislamu huu ambao Allah amemtuma nao Mtume wake Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) kwa watu wote ni Dini ya kumuamini Allah na kumpwekesha, Allah Ta'ala amesema: {Yeye ndiye aliye Hai - hapana mungu isipo kuwa Yeye. Basi muabuduni Yeye mkimsafishia Dini Yeye. Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote. Sema: Mimi nimekatazwa kuwaabudu hao mnao waomba badala ya Mwenyezi Mungu, zilipo nijia hoja zilizo dhaahiri kutokana na Mola wangu Mlezi. Na nimeamrishwa nisilimu kwa Mola wa walimwengu wote.} [40:65-66].

Ni dini ambayo waja humsafishia ibada Yeye Peke yake, Allah Mtukufu amesema: {Je, mabwana wengi wanao farikiana wao kwa wao ni bora au Mwenyezi Mungu Mmoja Mwenye nguvu? Hamuabudu badala yake ila majina tu mliyo yapanga nyinyi na baba zenu. Mwenyezi Mungu hakuyateremshia hayo uthibitisho wowote. Hapana hukumu ila ya Mwenyezi Mungu tu. Yeye ameamrisha msimuabudu yeyote isipo kuwa Yeye tu.} [12:39-40],

Nayo ni dini ya akili zilizosalimika lau ingedhihirishwa ukweli na usafi wake nafsi zingefuata kwa kutii na kujisalimisha, Allah Mtukufu amesema: {…Hiyo ndiyo Dini Iliyo Nyooka. Lakini watu wengi hawajui.} [12:40],

Ni dini ya dalili, hoja na uthibitisho: {…Sema: Leteni hoja zenu kama nyinyi ni wasema kweli.} [27:64],

Ni dini ya raha na furaha na utulivu: {Mwenye kutenda mema, mwanamume au mwanamke, naye akawa ni Muumini, tutamhuisha maisha mema…} [16:97].

Ndani ya dini ya Uislamu ambayo Allah amemtuma nayo Mtume Muhammad, Allah amehalalisha vizuri vyenye manufaa, na akaharamisha machafu yenye kudhuru, na akaamrisha kila mema na akakataza kila maovu na munkari. Uislamu ni dini nyepesi, hakuna mashaka ndani yake, wala taklifu, wala mzigo ambao watu hawawezi kuubeba, Allah Mtukufu amesema:

{Ambao kwamba wanamfuata huyo Mtume, Nabii, asiye soma wala kuandika, wanaye mkuta kaandikwa kwao katika Taurati na Injili, anaye waamrisha mema na anawakanya maovu, na anawahalalishia vizuri, na ana waharimishia viovu, na anawaondolea mizigo yao na minyororo iliyo kuwa juu yao. Basi wale walio muamini yeye, na wakamhishimu, na wakamsaidia, na wakaifuata nuru iliyo teremshwa pamoja naye - hao ndio wenye kufanikiwa.} [7:157].

Ni dini kamilifu, iliokusanya yenye kufaa kwa zama na mahali pote hadi pale Allah atakapoirithi ardhi na vilivyomo. Imekuja na mahitaji yote ayahitajiayo mwanadamu katika dini na dunia yao.

Uislamu ni njia ya furaha na utulivu, njia ya elimu na ustaarabu, njia ya uadilifu na wema, ni njia ya karama na uhuru, njia ya kheri zote na wema.

Ni utukufu wa dini hii na ukamilifu wake!! Na ni dini ipi ni bora kuliko ile ambayo mja amejisalimisha kwa Allah Mtukufu? Allah amesema: {Na nani aliye bora kwa dini kuliko yule aliye usilimisha uso wake kwa Mwenyezi Mungu, naye akawa mwema, na anafuata mila ya Ibrahim mwongofu?...} [4:125].



Hakuna kumuabudu asiyekuwa Allah.

"Navutika sana na Imani ya Uislamu ya Mungu mmoja. Hakuna kama Yeye. Imani hii ya Mungu Mmoja pekee inamuepusha mtu na kuwa mtumwa wa binadamu yeyote na huu ndio uhuru wa kweli. Ule uhusiano wa moja kwa moja kati ya Mungu na watumwa wake (waumini) ulinivutia vile vile."

Ibrahim Khalil (Philobus)
Padri na Muhubiri wa Misri.

Dini na Dunia Viko Pamoja

"Umoja huu wa kipekee ambao hauna mfano wake kwa taathira ya kidini na ya kidunia kwa pamoja, inamfanya Muhammad aonekane kuwa ni mtu mwenye haiba kubwa ya pekee yenye taathira katika historia ya wanadamu."

Michael Hart

Mwandishi wa Kimarekani

Kwanini Isiwe Hivyo.

"Ikiwa huu ndio Uislamu. Kwa nini basi sote tusiwe Waislamu."

Goethe

Mwanafasihi wa Kijerumani

Huu wito kutoka kwa Mola wako ambaye yeye ni Mwenye kukuhurumia wewe zaidi kuliko hata nafsi yako uliyo nayo. Anakulingania, kutoka kwenye kiza kwenda kwenye Mwanga, Allah Mtukufu amesema:

{Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Njooni kwenye neno lilio sawa baina yetu na nyinyi: Ya kwamba tusimuabudu yeyote ila Mwenyezi Mungu, wala tusimshirikishe na chochote; wala tusifanyane sisi kwa sisi kuwa Waola Walezi badala ya Mwenyezi Mungu. Na wakigeuka basi semeni: Shuhudieni ya kwamba sisi ni Waislamu.} [3:64].

Katika mkabala wa hilo mja ambae amejisalimisha kwa Allah kuna mtu Mwingine amekataa na kufunika umbile lake la Uislamu ambalo Allah amemuumba nalo kwa pazia la kupinga na kukanusha pamoja na mfululizo

wa dalili na miujiza inayoonesha usahihi wa dini hii.

Hivyo mtu huyu akajichagulia nafsi yake ushirikina kinyume na Tawhidi, kiza cha dhana, uzushi badala ya mwanga wa haki, yakini na uongofu, na kuridhia nafasi yake kuwa ni mtumwa wa waja mfano wake, kama vile watawa na wanazuoni wa kiyahudi, bali na Mitume badala ya kuwa ni waja wa Allah mmoja Peke yake; na hivyo basi fitra yake ikapotea na akili kupotea na kunyenyekea katika matamanio na utata huku akiacha fitra ya Allah ambayo Allah amemuumba nayo, hakuzaliwa mtoto yoyote ila katika fitra ya Uislamu:

{Basi uelekeze uso wako sawasawa kwenye Dini - ndilo umbile la Mwenyezi Mungu alilo waumbia watu. Hapana mabadiliko katika uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo Dini iliyo nyooka sawa. Lakini watu wengi hawajui.} [30:30].

Sasa ni juu yako kukadiria ndani ya nafsi yako kilichomtumbukiza kafiri kwenye upotevu wa wazi: {Yeye ndiye aliye kufanyeni manaibu katika ardhi. Na anaye kufuru, basi kufuru yake ni juu yake; na kufuru za makafiri haziwazidishii kwa Mola wao Mlezi ila kuchukiwa. Wala kufuru za makafiri haziwazidishii ila khasara.} [36:39]

Imani ya Muhammad juu ya Ujumbe Wake.

"Huenda wale wafalme na watawala ambao walipokea barua waliingiwa na mshangao kutokana na mtu huyu asiye na makuu ambae aliwaita kwenye utii. Kutuma barua hizi kunatupa picha ya kiasi cha kujiamini kwa Muhammad mwenyewe na ujumbe wake. Aliuandalia Umma wake kwa kujiamini huku na imani hii ni nguvu, utukufu na ulinzi, pembezoni mwake ni wakazi wa majangwani kubadilika kuwa mabwana waliofungua nusu ya Ulimwengu uliokuwa ukijulikana katika zama zao. Muhammad alifariki baada ya kuyafanya makabila yote ya Kiarabu yaliyotawanyika kuwa Ummah mmoja wenye ghera na hamasa."

Jawaharlal Nehru

Waziri Mkuu wa Kwanza India.

Ni ipi misingi na rejea na sifa za Ujumbe huu?

MISINGI YA UWEKAJI SHERIA

Uwekaji sheria wa Kiislamu umesimama katika misingi na nguzo za aina yake ambazo zinamfaa mwanadamu yeyote wa zama na mahala pote, na misingi ile muhimu ni hii ifuatayo:

Kwanza: Kurahisisha (Kufanya wepesi) na kuondosha Uzito.

Majukumu yote ya kisheria hayatoki nje ya uwezo wa wale waliokalifishwa na nafasi yao, wala haimbebeshi mtu mzigo au kumtoa katika mazoea katika kazi za kawaida, kwani dini ni nyepesi, Allah Mtukufu amesema:

{…Mwenyezi Mungu anakutakieni yaliyo mepesi wala hakutakieni yaliyo mazito…} [2:185],

Na Allah tena akasema: {Mwenyezi Mungu anataka kukupunguzieni taabu, na mwanaadamu ameumbwa dhaifu.} [4:28],

Na tena Allah Mtukufu akasema: {Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi yoyote ila kwa kadiri ya iwezavyo…} [2:286].Mama Aisha



Ujumbe wa Utume wa Muhammad.

"Muhammad alitumia muda wake wote kufanikisha ujumbe wake katika kudhamini hizi mandhari mbili katika mazingira ya jamii yake ya kiarabu, hayo mawili ni Umoja katika Fikra ya dini, kanuni na nidhamu ya utawala na hukumu. Yote yalitimia kwa fadhila za nidhamu ya Uislamu ambayo ulibeba mgongoni mwake umoja na utawala wenye mamlaka kwa pamoja. Uislamu ukawa na nguvu kwa fadhila hiyo, nguvu yenye msukumo na utisho imewahamisha waarabu kutoka kwenye umma wa kijahili na kuwa ulioendelea."

Arnold J. Toynbee

Mwanahistoria wa Uingereza

(Radhiya LLahu 'anha) amesema: «Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) hakukhiyarishwa kati ya mambo mawili ila alichagua jepesi zaidi, madamu si dhambi, ikiwa ni dhambi alikuwa mbali nayo sana, Wallahi hakulipa kisasi kwa ajili ya Nafsi yake jambo aliloletewa katu, hadi pale ambapo Sheria ya Allah itakapovukwa, hivyo kulipa kisasi kwa ajili ya Allah» (Al-Bukhari).

Miongoni mwa kuondoa uzito (Mashaka) katika sharia ya Kiislamu ni majukumu machache; kiasi cha kumuwezesha mwenye kukalifishwa kusimamia majukumu yake bila ya uchovu au taabu; kwani katika uchovu kuna mashaka na dhiki, na mashaka huondoshwa, Allah Mtukuka amesema: {...Wala hakuweka juu yenu mambo mazito katika Dini...} [22:78],

Kama ambavyo malengo ya majukumu ya kisharia ni kumpelekea mwenye kutekeleza majukumu yake katika maisha ya furaha duniani na akhera, hivyo basi sharia haileti jukumu ila kulingana na kinachowezekana kwa maumbile na tabia ya mwanadamu, Allah Mtukuka amesema:

Akida iliyokita.

"Katika nguzo tano za Uislamu hakuna kitu kinachochukiwa na asiyekuwa Muislamu. Pamoja na wepesi wa faradhi hizi na uchache wa idadi yake, hakukuwa na haja ya kuingiza marekebisho yatakayoingoza kwenye kuithibitisha imani ya Kiislamu katika nafsi ya kila Muislamu. Hakika ubobezi wa kielimu kwa imani ya Kiislamu ina dalili ya dhati kutokana na nguvu yake, kubakia na kuenea kwake."

George Sarton

Muhadhiri wa Vyuo Vikuu vya Washington na Harvard.

Dini Kwanza.

"Misingi ya tabia ya Kiislamu, sheria na serikali yao. Vyote vimesimama juu ya misingi ya dini: Uislamu ni dini nyepesi zaidi na ya wazi kuliko dini nyingine. Na msingi wake ni kushuhudia kuwa hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Allah na Muhamad ni Mtume wa Allah."

Will Durant

Mwandishi wa Kimarekani

{Enyi mlio amini! Msiulize mambo ambayo mkidhihirishiwa yatakuchukizeni. Na mkiyauliza inapo teremshwa Qur'ani mtabainishiwa. Mwenyezi Mungu amesamehe hayo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye maghfira Mpole. Waliyauliza hayo watu wa kabla yenu, kisha wakawa wenye kuyakataa.} [5:101-102].

PILI: KUCHUNGA MASLAHI YA WATU:

Mwenye kufuatilia hukumu za sheria ya Kiislamu itamdhihirikia kuwa muradi wake ni kufanikisha maslahi ya watu; kiasi cha kuwafanikishia watu kheri na wema, na hivyo basi kuondosha shari, ufisadi duniani na akhera, kwa mtu binafsi na kwa jamii yote katika zama na mahali pote, Allah Mtukuka amesema: {Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote.} [21:107],

Kwa hiyo rehema ni kwa ajili ya kufanikisha maslahi, vinginevyo kama rehema isingekuwa ndio makusudio yake, basi Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) asingesifika kuwa Nabii mwenye rehema, na majukumu yote yanarejea katika maslahi ya waja duniani na katika akhera yao; kwa sababu Allah anajitosha kwa

waja wake wote, hivyo basi utii haumnufaishi wala maasi hayamdhuru.

Sharia yote ni adilifu, ina kila aina ya huruma, maslahi na hekima; na suala lolote lililotoka kwenye uadilifu kwenda kwenye dhuluma, kutoka kwenye dhuluma na rehema kwenda kinyume chake, na kutoka kwenye maslahi kwenda kwenye uharibifu na ufisadi, na kutoka kwenye hekima kwenda kwenye upuuzi hayo si katika sharia.

TATU: KUTIMIZA UADILIFU KWA NJIA ZOTE:

Maandiko mengi yameshirikiana kuthibitisha nafasi ya Uadilifu kama mfumo wa jumla kwani tunapata maandiko yenye kulingania kusimamisha uadilifu, na mengine yenye kukataza dhuluma, hata ikiwa ni pamoja na mtu mwenye kuhalifu, Allah Mtukuka amesema: {Enyi mlio amini! Kuweni wasimamizi madhubuti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu mkitoa ushahidi kwa haki. Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutofanya uadilifu. Fanyeni uadilifu. Hivyo ndio kuwa karibu mno na uchamngu. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda.} [5:8].

NNE: KUENEA NA KUKAMILIKA.

Kwa hakika miongoni mwa yanayoonesha kusihi dini hii ni kule kujipambanua kwa upana na ukamilifu wake, Allah Mtukuka amesema: {…Hatukupuuza Kitabuni kitu chochote…} [6:38],

Na akasema vile vile: {…Na tumekuteremshia Kitabu hiki kinacho bainisha kila kitu, na ni uwongofu, na rehema, na bishara kwa Waislamu.} [16:89],

Na kuenea huku kunaonekana katika akida na taswira, na katika ibada na kujikurubisha, na katika Akhlaki na fadhila, (ubora katika maeneo yote) na katika uwekaji sheria, oganaizesheni na hukumu mbali mbali, si hivyo, bali katika maisha yote.

TANO: USAWA NA ULINGANIFU:

Dini ya Uislamu ni dini ya usawa na ulinganifu: {Na vivyo hivyo tumekufanyeni muwe Umma wa wasitani…} [2:143],

Na kila kitu katika hukumu zake zimetayarishwa katika mizani makini: {Na mbingu ameziinua, na ameweka mizani} [55:7]

Na Allah amewaamrisha Waislamu kusawazisha kila kitu, miongoni mwa hayo kauli yake Allah Mtukuka: {Na wale ambao wanapo tumia hawatumii kwa fujo wala hawafanyi ubakhili, bali wanakuwa katikati baina ya hayo} [25:67],

Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) amekataza Ghuluu (kupetuka mipaka): Akasema:

"Tahadharini kuzidisha katika dini kwani (ghulu) kuzidisha imewaangamiza waliokuwa kabla yenu."

Na akaamrisha usawa na kumpa kila mwenye haki, haki yake. Amesema Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam): "Hakika Mola wako ana haki juu yako, na Nafsi yako ina haki juu yako, na kwa familia yako ina haki juu yako, hivyo mpe kila mwenye haki haki yake."

Uislamu… Ni amani na salama.

"Mayahudi chini ya bendera ya Uislamu walipata amani na uadilifu ambayo iliwazuia na shari ya uadui na kukandamizwa, na Karne nyingi zilipita wakiwa katika kheri nyingi."

Naseem Souza
Mhadhiri wa Kiiraqi, Myahudi

SIFA ZA UWEKAJI SHARIA WA KIISLAMU:

KWANZA: INATOKA KWA MUNGU:

Chanzo cha dini ya Kiislamu ni Muumba Mtukufu Aliyemuumba mwanadamu na Ulimwengu na vilivyomo ndani yake, na kuwa kwake imetoka kwa Mwenyezi Mungu ina ipa hadhi nyingi, miongoni mwake ni kuwa Allah ndie Muumba na ndie mtoa riziki, yeye pekee ndiye mwenye kumiliki haki ya uwekaji sheria.

Mitume wote na wafuasi wao wakitegemea mwekaji sheria kutoka kwa Allah pekee, na hubatilisha kila sheria isiyotoka kwake, Allah akimuelezea Mtume wake wa mwisho kuhusu sheria yake na muelekeo wake: {Sema: Mimi si kiroja miongoni mwa Mitume. Wala sijui nitakavyo fanywa wala nyinyi. Mimi nafuata niliyo funuliwa tu kwa Wahyi, wala mimi si chochote ila ni mwonyaji mwenye kudhihirisha wazi.} [46:9]

Kwa hiyo Mtume wa Allah pamoja na utukufu wa hadhi yake na nafasi yake ya juu kwa Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) anafuata sheria ya Allah anayoshushiwa yeye wahyi, yeye sie mwanzilishi, bali hufuata mfumo wake na wala haendi kinyume nao, na kuwa Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) ndie Muumba anajua aliowaumba: {Asijue aliye umba, naye ndiye Mjua siri, Mwenye khabari?} [67:14]

Yeye anajua maumbile ya waja wake na yanayowafaa na yanayowaharibu, anajua zaidi yanayowanufaisha na yanayowadhuru, hakuna mwingine anayewafahamu zaidi ya aliyewaumba, na hakuna zaidi ya mtengezaji anajua zaidi yake alichokitengeneza. Allah Mtukufu amesema: {…Sema: Je, nyinyi mnajua zaidi au Mwenyezi Mungu?...} [2:140].

Na kwa sababu Allah ndie aliyeweka sheria, hii inaipa sheria yenyewe uadilifu na ukweli wake. Kamwe haiwezekani Allah ampendelee mja miongoni mwa waja wake kwa ajili ya hesabu ya mja mwingine, kama ambavyo adhabu ilivyo katika Uislamu basi Yule ambaye hakuchukua haki yake duniani kwa sababu yoyote au ambaye hajaadhibiwa duniani kwa ubaya wa matendo yake, basi atakuta malipo yake akhera.

PILI: UHUSIANO WA UWEKAJI SHERIA NA MAADILI:

Lengo la kanuni yoyote ni kuwa kanuni haifikiwi malengo yake kwa maumbile yake bali hutegemea mwitikio wa watu wa kutekeleza kanuni na sharia ile kwa ridhaa yao na kukinai kwao, kama vile ambapo lengo la kanuni husika halifikiwi kwa uzuri wa hukumu zake pekee, lakini hufikiwa pamoja nayo kwa utekelezaji wa wale waliowekewa sheria ile, kwa sharti ya kuwa utekelezaji huu uwe unatoka ndani ya Nafsi zao na mioyo yao.

Hisia hii hutokana na imani yao ya kuwa kanuni yenyewe ni ya uadilifu na kuiridhia kwao, na itikadi ya kulipwa na mtunga sheria nao wakiridhia sheria zake na hukumu zake mbali mbali. Sheria ya Kiislamu imesimama katika kuridhiwa na kukinai kwa watu wenyewe, Allah ameamrisha kufundishwa Uislamu: {…na uwaambie maneno ya kuathiri na kuingia katika nafsi zao.} (4:63), {Basi kumbusha! Hakika wewe ni Mkumbushaji. Wewe si mwenye kuwatawalia.} [87:21 – 22],

Dini ya Utulivu.

"Kwa mara ya kwanza katika maisha yangu nimehisi amani na utulivu na kuwa ndani ya maisha yangu kuna thamani. Nimefahamu maana ya kuwa Mungu (Allah) ambae humuoni yeye anakuona popote uwapo na huangalia matendo yako na huyapima kwa vipimo vya uadilifu ili upate malipo yako ya haki Siku ya Kiama."

Anatoli Andrbush
Jenerali wa Kirusi

ndio maana Allah akaufunga Ujumbe wa Muhammad na kutumwa kwake kwa sababu hii; Amesema Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam): "Kwa hakika nimetumwa kutimiza tabia njema."

TATU: UHUSIANO WA DUNIA NA AKHERA:

Miongoni mwa sifa zinazopambanua sharia ya Kiislamu dhidi ya sheria ziliotungwa na wanadamu ni kuwa (Sharia ya Kiislamu) humlipa mwanadamu katika maisha ya hapa duniani na katika akhera vile vile, malipo ya akhera ni makubwa kuliko ya dunia; kwa ajili hiyo daima muumini anahisi hili na

https://www.path-2-happiness.com/sw

kumsukuma ndani ya Nafsi yake katika ulazima wa kutekeleza hukumu zake, kufuata maamrisho na makatazo yake na kama atakwepa malipo katika maisha ya duniani hujua fika kuwa macho ya Allah hayaghafiliki wala kulala, na kuwa watu watachukuliwa kwa wayatendayo hapa duniani mbele ya Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) Allah Aliyetukuka amesema: {Ati anadhani hapana yeyote ataye muweza?} [90:5]

Na akasema vile vile: {Ati anadhani ya kuwa hapana yeyote anaye mwona?} [90:7]

NNE: SIFA YA KIJAMII KATIKA HUKUMU ZAKE:

Sheria ya Kiislamu haipendelei maslahi ya sehemu moja zaidi ya sehemu nyingine wala haimpendelei mtu mmoja dhidi ya mwingine, imeweza kutatua tatizo hilo kubwa ambalo jamii zingine mbali mbali linasumbuka nalo.

Tatizo la mgongano kati ya maslahi ya mtu binafsi na maslahi ya Ummah katika jamii kama tuonavyo katika mfumo wa Kibepari wakati ambapo katika mfumo wa Kijamaa kupendelea masilahi ya jamii na kupuuza masilahi ya mtu binafsi na kupoteza na kuvunja haki ya mtu binafsi na hivyo kutupa haki ya mtu binafsi na uhuru wake na haki ya kumiliki, na hivyo basi vipaji vyake kutojitokeza na kupotea kwa utu wake na kupelekea kutotumika kwa uwezo wa mtu binafsi.

Lakini Uislamu umeweka haki kwa msingi wa usawa baina ya haki hizi za kijamii (haki) ambayo inaisimamisha; Uislamu umechunga maslahi ya jumla ya jamii ya Kiislamu, hata hivyo wakati huo huo haujaghafilika

https://www.path-2-happiness.com/sw



na matakwa ya Muislamu binafsi.

Katika upande wa kisiasa tunaona kuwa haki ya mtawala na kiongozi ni kupata kusikilizwa na raia zake na kutiiwa, lakini kwa sharti la kufuata sheria katika kuhukumu kwake huku akichunga maslahi ya Ummah.

Vinginevyo Uislamu unamnyang'anya haki hii; hivyo basi itapasa kumtii mtawala au kiongozi katika yasiyokuwa kumuasi Allah (Subhaanahu wa Ta'ala).

TANO: UTHIBITI KATIKA KANUNI NA ULAINI KATIKA UTEKELEZAJI:

Uislamu umesimama juu ya misingi thabiti isiyobadilika inachukuwa vyanzo vyake kutoka katika misingi yake ya mwanzo:

Qur-aan iliyohifadhiwa na Allah: {Hakika Sisi ndio tulio teremsha Ukumbusho huu, na hakika Sisi ndio tutao ulinda.} [15:9],

Ambayo haingiliwi na batili yoyote: {Hautakifikia upotovu mbele yake wala nyuma yake. Kimeteremshwa na Mwenye hikima, Msifiwa. } [41:42].

Sunnah tukufu imerikodiwa nakuhifadhiwa kwa undani na umakini mkubwa na maandiko yake (nususi) mara nyingi hukusanya hukumu za uwekaji sheria bila ya kubainisha vipengele vinavyohusiana na utekelezaji wa

hukumu hizo; na hivyo kuacha uwezo mkubwa wa utawala na kukadiria kwa Mujtahidi akichunga tofauti za hali na mazingira, hata hivyo utekelezaji wa hukumu hizi bado umebaki katika kuangalia wasaa na kutokakamaa katika jambo.

Kwani lililo la msingi ni kutekeleza malengo haya bila ya kujali njia zitakazotumia au maumbo yaliyosimamia madamu hayaendi kinyume na andiko la kisheria au msingi miongoni mwa misingi ya kisheria ya Kiislamu, kwa hiyo utekelezaji wa makusudio ya jumla ya sheria ya Kiislamu kwa daraja ya juu ya wepesi na uwezekano wa kuendelea (kukua) kadhalika hakuna kizuizi katika kutokea kwa hukumu mpya ambayo haikujulikana hapo kabla kwa kuangalia kuzuka mazingira yanayoafikiana nayo.

Dini ya Utukufu na Ukarimu

"Uislamu ni dini ya amani, usawa, uhuru, udugu, ukarimu na utukufu, yote hayo yanaonekana wazi kwenye hukumu zake, misingi yake na taratibu zake, kwa mfano Saumu katika Uislamu si kama saumu katika dini nyingine, kwa sababu matatizo ya mwanadamu si (mtu) kukandamiza mahitaji ya mwili wake kama vile wafanyavyo watawa kiasi kwamba kiwiliwili cha mmoja wao kinakuwa kama vile hekalu la mifupa inayotembea. Uislamu umenyoosha matamanio ya kiwiliwili na haujayakandamiza; Saumu katika Uislamu unazoesha nafsi ya mfungaji kusubiri na Jihadi dhidi ya matamanio maovu yaliyoharamishwa, na kumchunga Allah katika siri na dhahiri na kujitambuza ladha ya kukosa na njaa, ili mfungaji awaonee huruma waliokosa, kama ambavyo Saumu ni fursa ya kuupa mwili raha dhidi ya kuvimbiwa. Saumu humfaidisha mtu afya yake, roho yake na akili, na katika yote kuna kujiburudisha kwake, na umoja wake."

Berisha Pennekmrt

Mwanataaluma wa Kithailand aliyetoka kwenye Ubudha na kuingia Uislamu.

SHERIA YA KIISLAMU NA KANUNI ZA WANADAMU… TOFAUTI ZILIZOPO:

Kuna tofauti na kuhitilafiana Sharia ya Kiislamu na sheria zilizowekwa na wanadamu.

1. Haiba, Utukufu na kuheshimu Nafsi za watu:

Sharia ya Kiislamu inasifika kwa kuwa na haiba na utukufu wa kujali utu wa mwanadamu, na hivyo inatokana na sifa ya kidini iliyoshikamana nayo na kwa sababu muwekaji wake ni Allah ambaye yeye nafsi za wanadamu zinanyenyekea kwake na kutukuzwa.

2. Sharia kukubaliana na maumbile (fitra) kwa zama zote na mahala pote:

Sharia ya Kiislamu ni kwa ajili ya Ummah na mataifa yote kwa tofauti zao zilivyo, tabia, mazingira na lugha-wanayozungumza; kwa sababu muwekaji wake (sharia hii) ni Allah (Subhaanahu Wa Ta'ala), naye ni mjuzi wa yaliyopo na yajayo kwa maumbile yao na silika ya tabia zao na kila chenye kuhusiana nao pamoja na kutakasika kwake kutawaliwa na matamanio, Allah amesema: {Basi uelekeze uso wako sawasawa kwenye Dini - ndilo umbile la Mwenyezi Mungu alilo waumbia watu. Hapana mabadiliko katika uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo Dini iliyo nyooka sawa. Lakini watu wengi hawajui.} [30:30],

Ama sharia hizi za wanadamu zimewekwa na mwanadamu nao pamoja na elimu kubwa waliyofikia elimu yao hiyo ina upungufu na hata wakijua ya jana yao na mambo yao ya leo, hawawezi kujua ya kesho yalivyo, na hata wakijua tabia za baadhi ya watu hawawezi kujua yote, katika hali hii. Sheria za wanadamu hazilingani na maumbile yote ya mwanadamu wala hazilingani na mazingira yote, na ikiwa sheria hiyo imefaa kutumika kwa watu fulani haifai kutumika kwa wengine….

3. Sharia ya Kiislamu kuafikiana na haki na uadilifu.

Sharia ya Kiislamu inaafikiana na usawa, haki na uadilifu na hiyo ni kutokana na kutowezekana kutokea makosa, au dhuluma au kutawaliwa na matamanio na hamasa za watu, Allah Mtukuka amesema: {Na yametimia maneno ya Mola Mlezi wako kwa kweli na uadilifu. Hapana awezaye kuyabadilisha maneno yake. Na Yeye ndiye Mwenye kusikia na Mwenye kujua.} [6:115],

Allah pekee ametakasika kuepukana na malengo (matamanio), mwenye kujua mambo yaliyofichikana na yaliyodhihiri, yeye ndie amezunguka mambo ya waja, hawezi kuamrisha ila lenye maslahi yao, wala hakatazi ila lenye kuwadhuru. Ama kanuni na sheria waliyojitungia wanadamu hukumbwa na makosa, usahaulifu, na kufuata matamanio ya watu, hivyo ni vigumu kusalimika na makosa, upungufu na mabadiliko, Allah Mtukuka amesema: {… Na lau kuwa imetoka kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu bila ya shaka wangeli kuta ndani yake khitilafu nyingi.} [4:82].

4. Sharia kujali utu wa mwanadamu:

Sharia ya Kiislamu sio kanuni tu zilizowekwa na fikra za watu, lakini muwekaji wake ni Allah Aliyetukuka katika yale yaliyo mnasaba na mwanadamu na tabia yake na maumbile yake, Aliyeumba watu anafahamu zaidi yenye kunasibiana nao, {Asijue aliye umba, naye ndiye Mjua siri, Mwenye khabari?} [67:14],

Naye anajua zaidi anachomrahisishia: {Mwenyezi Mungu anataka kukupunguzieni taabu, na mwanaadamu ameumbwa dhaifu.} [4:28].

Ama sheria za wanadamu zimewekwa kulingana na matakwa ya aliyeiweka, na kulingana na umuhimu na mazingira yake.

5. Uhusiano wa Sharia ya Kiislamu na upande wa kiroho:

Sharia ya Kiislamu inahusiana na matendo ya dhahiri na matendo ya ndani ya mwanadamu; Allah Mtukuka amesema: {…Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu anajua yaliyomo katika nafsi zenu. Basi tahadharini naye….} [2:235].

Kinyume na sheria za mwanadamu ambazo zinajihusisha na matendo ya nje ya mwanadamu tu na hayajali upande wa kiroho hata kidogo, ama adhabu zinazotolewa na sharia hizi za mwanadamu ni za kidunia tu.

Jamii (Safi) yenye furaha.

"Jamii ya Kiislamu ambayo inajilazimisha kufuata hukumu na adabu zake, ni jamii nadhifu yenye furaha, ni jamii ambayo ndani yake hakuna jinai kwa rangi zake zote."

Berisha Pennekmrt

Mwanataaluma wa Kithailand aliyebadilisha Ubudha na kuwa Muislamu.

VYANZO VYA UISLAMU.

Dini ya Kiislamu inapokea sheria yake, akida zake na hukumu katika ufunuo (Wahyi), kutoka kwa Mwenyezi Mungu (Qur-aan na Sunnah) hizo ndizo vyanzo vikuu viwili vya msingi vya Uislamu, na kutoka katika vyanzo hivyo ndio imepatikana sheria yake, itikadi zake na hukumu zake, ifuatayo ni taarifa zake kwa ufupi.

A. QUR-AAN TUKUFU:

Allah ameteremsha Qur-aan kwa Mtume wake Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) kuwa muongozo kwa wamchao Mungu, desturi ya Waislamu, tiba ya nyoyo ambayo Allah ametaka kuwapa uongofu na taa kwa yule ambaye Allah amemtakia kufanikiwa na mwangaza.

Nayo inakusanya misingi ambayo kwa ajili yake Allah ametuma Mitume, na Qur-aan sio kitabu kilichozushwa miongoni mwa vitabu kama ambavyo hakuwa Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) Mtume miongoni mwa Mitume aliyezuka tu; Allah alishateremsha kwa Ibrahim Suhufi (maandiko), na akamkirimu Musa Taurati na Dawuud Zaburi na Issa akaja na Injili.

Vitabu hivi ni Ufunuo (Wahyi) kutoka

Qur-aan ....Kitabu cha Mwisho cha Mbinguni.

"Nilipoamini tawhidi nikaanza kutafuta hoja na dalili mbali mbali ambazo zinathibitisha kuwa Qur-aan ni kitabu cha Mwenyezi Mungu Aliyetukuka na kuwa Qur-aan ni kitabu cha Mwisho. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kutatua mas-ala haya: Qur-aan Tukufu ni kitabu pekee ambacho kinakubali na kutambua vitabu vyote kutoka mbinguni, wakati ambapo vitabu vyote vinapinga vitabu vingine. Kwa hakika hii ndio moja ya sifa kubwa inayopambanuka Qur-aan Tukufu."



Bashir Shaad
Muhubiri wa India.

kwa Allah amewafunulia Mitume wake, na kinachothibitisha kuwa Qur-aan hii ni Wahyi kutoka kwa Allah, ni kuwa inathibitisha imani ya kila Mtume wa Allah wala haitofautishi kati yao, Allah amesema: {Hakika wale wanao mkataa Mwenyezi Mungu na Mitume wake, na wanataka kufarikisha baina ya Mwenyezi Mungu na Mitume wake, kwa kusema: Wengine tunawaamini na wengine tunawakataa. Na wanataka kushika njia iliyo kati kati ya haya, Hao ndio makafiri kweli. Na tumewaandalia makafiri adhabu ya kudhalilisha. Na walio muamini Mwenyezi Mungu na Mitume wake, wala wasimfarikishe yeyote kati yao, hao atawapa ujira wao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghfira, na Mwenye kurehemu. } [4:150-152],

Isipokuwa vitabu hivi vilivyotangulia vingi vimepotea na kuharibika sehemu yake kubwa na vikaingiliwa na kubadilishwa na kugeuzwa.

Ama Qur-aan Tukufu Allah amedhamini hifadhi yake Allah Mtukufu amesema: {Hakika Sisi ndio tulio teremsha Ukumbusho huu, na hakika Sisi ndio tutao ulinda.} [15:9],

Na akaifanya iwe ufunuo na kufuta vitabu vilivyotangulia katika vitabu, Allah amesema: {Na tumekuteremshia wewe, kwa haki, Kitabu hichi kinacho sadikisha yaliyo kuwa kabla yake katika Vitabu na kuyalinda…} [5:48],

Na yule aliyeiteremsha akaisifu kuwa ni ubainisho wa kila kitu; kwa hiyo Allah akasema: {…Na tumekuteremshia Kitabu hiki kinacho bainisha kila kitu, na ni uwongofu, na rehema, na bishara kwa Waislamu.} [16:89].

Nafasi ya Qur-aan na fadhila zake.

"Qur-aan imebakia karne kumi na nne imehifadhiwa katika kumbukumbu ya Waislamu ikihamasisha fikra zao, kutengeneza tabia zao, na kuchochea hamasa za mamia ya milioni ya watu, Qur-aan inaweka katika nafsi za watu imani nyepesi zaidi yenye utata mchache ambao ipo mbali na vifungo vya rasimu na mafundisho ya Kikristo.
Qur-aan imekuwa bora katika kunyanyua viwango vya tabia za Waislamu na elimu. Na ndio iliyosimamisha ndani yao kanuni za mfumo wa kijamii na umoja wake, na kuwahimiza kufuata kanuni za afya na kufungua akili zao kutokana na dhana potofu na dhuluma na ususuavu (wa nyoyo) na kutengeneza vizuri hali za watumwa na kuingiza katika nafsi za wanyonge heshima na utukufu."

Will Durant
Mwandishi wa Kimarekani

Ni muongozo na rehema; Amesema Allah: {…Basi imekufikieni bayana kutoka kwa Mola wenu Mlezi, na uwongofu, na rehema….} [6:157]

Na kuwa huongoza kwa yaliyonyooka (madhubuti), Allah amesema: {Hakika hii Qur'ani inaongoa kwenye ya yaliyo nyooka kabisa, na inawabashiria Waumini ambao wanatenda mema ya kwamba watapata malipo makubwa.} [17:9]

Humuongoza mwanadamu katika njia iliyonyooka katika kila jambo katika maisha yake,

Qur-aan imekusanya kila kitu anachokihitaji mwanadamu; kwani inakusanya misingi ya kanuni, itikadi, hukumu, miamala, maadili, adabu zake na mengineyo, Allah amesema: {…Hatukupuuza Kitabuni kitu chochote….} [6:38].

Kitabu Chenye Kukusanya

"Kwa hakika Qur-aan ni kitabu cha elimu, malezi na utamaduni, haina maana kwamba yote yaliyomo ndani yake ni maneno kuhusu faradhi za Swala na Ibada. Mambo mema ambayo Qur-aan inahamasisha Waislamu mambo mema kabisa katika mizani ya maadili mema. Muongozo wa kitabu hiki unaonekana zaidi katika makatazo yake, kama yalivyo wazi katika maamrisho yake pia."

Sydney Fisher

Profesa katika Chuo Kikuu cha Ohio-Marekani.

https://www.path-2-happiness.com/sw

SUNNAH ZA MTUME (Swala Llahu ʻalayhi wasallam)

Allah amemteremshia Mtume wake Qur-aan Tukufu na akampa Wahyi wa Sunnah ya Utume, Allah amesema: {Hayakuwa haya ila ni ufunuo ulio funuliwa} [53:4]

Nayo ni kama Qur-aan Mtume (Swala Llahu ʻalayhi wasallam) amesema: "Jueni mimi nimepewa Kitabu (Qur-aan) na mfano wake pamoja nao, jueni, mimi nimepewa Kitabu (Qur-aan) na mfano wake pamoja nao" (Ahmad). Ni Wahyi kutoka kwa Allah kwa Mtume wake Muhammad (Swala Llahu ʻalayhi wasallam) kwa sababu Mtume (Swala Llahu ʻalayhi wasallam) hazungumzi kwa matamanio, Yeye hufikisha kwa watu aliyoamrishwa, Allah amesema: {…Mimi nafuata niliyo funuliwa tu kwa Wahyi, wala mimi si chochote ila ni mwonyaji mwenye kudhihirisha wazi.} [46:9].

Kwa hiyo Sunnah ni chanzo cha pili katika vyanzo vya Uislamu, nayo ni yote yaliyopokewa kutoka kwa Mtume (Swala Llahu ʻalayhi wasallam) kwa sanadi sahihi inayoungana hadi kwa Mtume (Swala Llahu ʻalayhi wasallam) nayo ni maneno yake, kauli, kukiri au wasifu, nayo ni yenye kusherehesha na

Sunnah Tukufu

"Hakika Sunnah ing'aayo ya Muhammad imebakia hadi leo hii. Ikifunikwa na ikhlasi sahihi ya kidini, nafsi za mamilioni ya wafuasi wa Sunnah yake wametapakaa kwenye mgongo wa dunia."

Etienne Denier

Mchoraji na Mwanafikra wa Kifaransa

https://www.path-2-happiness.com/sw

kubainisha kwa ajili ya Qur-aan Tukufu; Allah amemuidhinisha yeye abainishe yaliyo ndani ya Qur-aan katika mambo ya jumla, au mahususi, Allah amesema: {…Nasi tumekuteremshia wewe Ukumbusho ili uwabainishie watu yaliyo teremshwa kwao, wapate kufikiri.} [16:44];

Kwa hiyo Sunnah inabainisha Qur-aan na kufafanua ayah zake, na hupambanua hukumu zake za jumla, kama vile Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) alivyokuwa akipambanua yaliyokuwa yakiteremka mara nyingine kwa maneno, wakati mwingine kwa vitendo, na wakati mwingine kwa njia zote pamoja.

Huenda Sunnah ikajitegemea bila Qur-aan Tukufu kwa kubainisha baadhi ya hukumu na sheria zake.

Sunnah iliotoharika ndiyo utekelezaji wa vitendo vya Uislamu kwa hukumu, itikadi, ibada, miamala na taratibu zake.

Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) alikuwa anatekeleza aliyoamrishwa, na kuyabainisha kwa watu na anawaamrisha kufanya mfano wa matendo yake, Allah amewaamrisha waumini kumfuata yeye (Swala Llahu 'alayhi wasallam) katika matendo yake na katika maneno yake ili imani yao ikamilike, Allah amesema: {Hakika nyinyi mnayo ruwaza njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anaye mtaraji Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na akamkumbuka Mwenyezi Mungu sana.} [33:21].

Qur-aan na Hadithi bega kwa bega.

"Qur-aan ina kamilishwa na hadithi ambazo ni mtiririko wa maneno yanayofungamana matendo ya Mtume Muhammad (Swala Llahu 'Alayhi Wasallam) na maelekezo yake. Katika hadithi mtu anapata yale yote yaliyokuwa yakitokea kwa Mtume (Swala Llahu 'Alayhi Wasallam). Ni kipengele cha msingi katika tabia zake mbele ya hakika zenye kubadilika katika maisha. Hivyo basi Sunnah ndio yenye kubainisha Qur-aan wala haijitoshi peke yake."

Jack Rislow

Mustashrik wa Kifaransa

https://www.path-2-happiness.com/sw

Masahaba wamenakili na kupokea kutoka kwa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) matendo ya Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) hadi wale waliokuja baada yao, nao wamepokea hadi kwa waliokuja baada yao kisha wakasajili katika Rejesta (diwani) za Sunnah.

Wapokezi wa Sunnah walikuwa wakishadidia (wakiweka mkazo na msisitizo mkubwa) katika yale waliyokuwa wakipokea kutoka kwao, na wakitaka wale wanaopokea kwao wawe watu walioishi zama moja na wale wanaopokea kutoka kwao, ili isnadi iungane kutoka kwa Rawiy (Mpokezi) wa Hadithi hadi kwa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) na kuwa wapokezi wote (walio katika mtiririko wa ile sanadi) ni watu madhubuti (wenye kuaminiwa) na waadilifu, wakweli na waaminifu.

Inapasa kuamini Qur-aan na Sunnah kuwa ndio vyanzo vikuu vya dini ya Uislamu ambavyo yapasa kuvifuata na kuvirejea na kufuata maamrisho yake, kuacha makatazo yake, kuamini habari zake na majina matukufu ya Allah yaliyo ndani yake, sifa zake na matendo yake, na yote aliyoandaa Allah kwa ajili ya mawalii wake waumini, na aliyokamia nayo adui zake makafiri, Allah amesema:

Muongozo wa Sunnah

"Kuitekeleza Sunnah ya Muhammad ni kuhifadhi kiini cha Uislamu na kuuendeleza, na kuacha Sunnah ni kuangusha Uislamu. Sunnah ndio msingi wa chuma ambalo juu yake Uislamu umesimama na ukiondoa muundo wake usishangae kuona jengo lile likianguka kama vile nyumba ya vikaragosi."

Leopold Weiss

Mwanafikra wa Austria.

https://www.path-2-happiness.com/sw

{La! Naapa kwa Mola wako Mlezi! Hawataamini mpaka wakufanye wewe ndiye muamuzi katika yale wanayo khitalifiana, kisha wasione uzito katika nyoyo zao juu ya hukumu utayo toa, na wanyenyekee kabisa.} [4:65]

Na akasema vile vile Allah: {…Na anacho kupeni Mtume chukueni, na anacho kukatazeni jiepusheni nacho.…} [39:7]

Ni furaha iliyoje kwa atakayefuata njia hii nayo ni njia ya Furaha!!!

Kukusanywa kwa Sunnah za Mtume.

"Hadithi hizi ambazo mkusanyiko wake unatengeneza Sunnah zimeandikwa kutokana na yaliopokewa kutoka kwa Masahaba au kunakiliwa kutoka kwao kwa umakini mkubwa katika kuzichagua kwake; na kwa namna hii kiasi kikubwa cha Hadithi kilikusanywa."

Jack Rislow

Mustashrik wa Kifaransa.

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw

الطريق إلى السعادة
The Path to Happiness

NJIA YA FURAHA

https://www.path-2-happiness.com/sw

Yaliyomo

NJIA YA FURAHA

- Maana ya furaha na uhakika wake.

- Furaha sio ladha..

- Sivyo kabisa – furaha si katika Raha

- Furaha chini ya kivuli cha hakika kuu za uwepo

- Njia ya furaha …suluhisho la mtu na nafsi yake, maisha na ulimwengu wake.

- Alama za Njia ya Furaha:

Sababu za furaha katika maisha ya Dunia katika Uislamu.

Tabu na mateso ni kuwa mbali na Njia ya Furaha.

NJIA YA FURAHA

MAANA YA FURAHA NA HAKIKA ZAKE

Neno furaha ni miongoni mwa maneno ambayo watu wametofautiana; kuna miongoni mwao wanaona kuwa ni mwenza wa neno ladha au raha au mali au cheo au umaarufu na kadhalika.

Na kwa sababu hiyo watu wengi hupoteza maisha yao katika njia mbali mbali wakitafuta furaha, ndio…furaha ni hisia inayotoka ndani ya nafsi ya mwanadamu anapohisi hali ya kuridhika na utulivu, hata hivyo mtazamo wa watu kuhusu furaha umetofautiana na hii ni kutokana na tofauti tabia zao, mapenzi yao, na matarajio yao, na hata jamii zao, baadhi ya watu wanaiona ipo kwenye mali au makazi au cheo na afya, na wengine wanaiona ipo kwenye mke, au watoto au kazi au masomo na huenda wengine wakaiona ni kuwa ukaribu na mpenzi au katika kuondokana na mtu mwenye kero au katika hisia nzuri ya kiroho au kumsaidia masikini na fukara, ama jambo la kushangaza ni kuwa utakapo wauliza wengi miongoni mwa watu hawa: Je, wewe ni mwenye furaha? Jibu lake litakuwa ni kwa kukataa!!!

Kwa hiyo utaona kuwa taarifu zina tofautiana baina ya mtu na kwa mwingine na jamii moja hadi jamii nyingine, kiasi cha kufanya jumuia ya kimataifa kuweka daraja

Dini ya furaha na Utulivu

"Nilikuwa nikijiuliza: Kwa nini Waislamu wanahisi furaha imetawala katika maisha yao pamoja na ufukara wao na kukosa kwao maendeleo?! Na kwanini Wasweden wanahisi dhiki na huzuni pamoja na maisha mazuri, starehe na maendeleo makubwa wanayoishi nayo?! Hata nchini mwangu Uswisi nilikuwa nikipata hisia zile zile za Wasweden pamoja na kuwa ni nchi yenye maendeleo makubwa na kiwango cha juu cha maisha!! Mbele ya yote haya nimekuta kuwa nafsi yangu ina haja ya kusoma dini za Mashariki, na nikaanza kuusoma Uhindu, sikukinaishwa nayo sana, hadi nilipoanza kusoma Uislamu uliponivuta na kuona kuwa haugongani na dini zingine bali imebeba dini zote; nayo ni dini ya mwisho inayohitimisha, ukweli huu kwangu ukawa (umoja wa katiba ya wananchi) unapanuka kwa kupanuka kusoma kwangu hadi ikazama kwa ukamilifu akilini mwangu."

Roger Du Pasquier

Mwanafikra na Mwandishi wa Kiswisi

Furaha kwa Wanadamu.

"Inatupasa kupotea kwenye fikra kuwa maendeleo ya Magharibi kwa sasa yamefeli kwa sababu ya kuridhisha nafsi za watu na na kushindwa kushughulikia katika kuleta furaha ya kibinadamu kwa hiyo ikawatupa watu katika shimo la kuangamiza na kumaliza kila kitu. Ni mbali hali hii kusifika kwa ukamilifu, au iwe nyenzo ya kumtumikia mwanadamu kama ilivyokuwa katika zama za Uislamu."

Naseem Souza
Mhadhiri wa Kiyahudi wa Iraqi



jina lake daraja la furaha miongoni mwa mataifa, walitaka kujua ni taifa gani lenye furaha zaidi, na hivyo basi kuzipa alama daraja hizi na wakasimamia ufuatiliaji na tafiti mbali mbali, Lakini matokeo yaliwa shangaza wote; hivyo Wamerekani wakawa ndio wenye matatizo zaidi na si furaha, na hawakupata isipokuwa alama za chini kabisa, pamoja na kuwa tunajua hali ya starehe na mas-ala ya anasa kwa watu wake.

Cha kushangaza mno ni kuwa watu wa Nigeria ndio waliopata alama kubwa zaidi na ndio walioonekana ni watu wenye furaha zaidi pamoja na ufukara wa watu hawa!!!

Hayo ndio yaliyokuwa matokeo ya mwisho ya utafiti huo uliofanywa na jarida la Newsweek la Marekani kuhusu taifa gani lenye furaha duniani, ambapo Nigeria nchi fukara yenye wakazi wengi Waislamu kuwa juu ya orodha miongoni mwa nchi sitini na tano, na kufuatiwa na nchi za Mexico, Venezuela, Salvador, wakati ambapo nchi zilizoendelea sana zimepata daraja za chini.

Katika majibu yao Waamerika wengi walikiri katika ripoti hii kuwa suala la furaha halihusiani na utajiri na mali , na hili ndilo linaloonekana kuwa jambo la kushangaza katika jamii inayofuata programu maalum ambayo imeasisiwa katika misingi ya Kibepari uliopetuka mipaka; jambo lililoisukuma jarida hilo hilo baada ya hapo kuangalia suala linaloenea kwa Wamarekani kurudi kwenye dini huko Marekani jambo ambalo linafanya maswali yarejee tena upya kuhusu hamu kubwa ya Wamarekani ya kutafuta furaha, kupitia njia za tafakuri za juu juu tu, ambayo mtu anapewa kama dozi ya tiba ya Nafsi kwa watu wenye matatizo hayo.

https://www.path-2-happiness.com/sw

Matatizo haya yanaonekana katika maana ya furaha na jinsi ya kuipata kwa wengi wenye kuijua; Plato aliona furaha kuwa ni fadhila za Nafsi. (Hekima, ushujaa, kujitunza na uadilifu) na akazingatia kuwa mwanadamu hawezi kupata furaha iliyo kamili ila baada ya roho kurejea katika ulimwengu mwingine (akhera).

Ama Aristotle alizingatia kuwa furaha ni hiba kutoka kwa Allah, na akaigawa katika vipengele vitano; navyo ni: Afya ya kiwiliwili na usalama wa milango ya fahamu na kupata utajiri na namna nzuri ya kutumia, na kufanikiwa katika kazi na kufanikisha ndoto za mtu na usalama wa akili na usahihi wa itikadi ya mtu; sifa nzuri na kuwafanyia hisani watu.

Katika Saikolojia tunaweza kufahamu furaha kwa wasifu wa kuakisi kuridhia na maisha au kuakisi kurudia mara kwa mara kwa hisia za mambo yenye kufurahisha, hata hivyo Swali linalobakia katika tofauti hizi katika ufahamu wa furaha, Ni nini maana ya furaha? Na vipi naweza kuwa mwenye furaha? Na je furaha hufikiwa kwa kufanikiwa kwa kuthibitisha ladha fulani?

FURAHA SIO LADHA (STAREHE):

Mara nyingi watu huwa nyuma ya ladha mbalimbali, hawaachi ladha ila wataiendea na wataiendea na anadhani kama akipata ladha zote basi atakuwa amepata furaha, lakini hushtukizwa na kuwa mbali kabisa na mtu mwenye furaha, ladha zilizopo duniani ni nyingi sana na za kila namna na hubadilika maumbo, na wasifu lakini sio kila ladha ina furaha ndani yake, hivyo basi watu huchanganya maana ya furaha na maana ya ladha, kilichokuwa sahihi ni kuwa zinakutana upande mmoja mahali na kuachana upande mwingine, kukutana ambako kila kimoja humuingizia mtu furaha ndani ya nafsi yake, lakini huachana na kutengana, na tofauti baina yao ni kuwa ladha huchumwa na utamu wake huondoka mara moja baada ya kuondoka sababu zake, huenda baada ya hapo yakawepo majuto, na mashaka ambayo hakuna mfano wake, ama furaha huendelea kuwepo kwa mtu kwa muda mrefu.

Huku kuchanganya baina ya maana ya furaha na mtazamo wa ladha mara nyingi humuweka mtu katika utata kutoka kwa mtu mwenyewe na hivyo kudhania kuwa kila starehe ni furaha.

Umaarufu ni ladha isiyo na mfano wake, mtu kuwa mashuhuri na maarufu mbele za watu, watu humtanguliza mabarazani na humsifu –yote hayo ni aina za ladha, lakini ni watu hao hao maarufu na mashuhuri au wenye mali au vyeo au uzuri, pamoja na hayo lakini ni wenye huzuni, wenye kutibiwa na tabibu nafsi, au maisha yake yakaishia kujiua na hivyo basi kero, huzuni na tabu!!! Yakamuondoka.

Mara ngapi tumewasikitia watu mashuhuri maarufu ambao maisha yao yaliishia katika kujiua ili amalize maisha ya shida na tabu aliyokuwa akiishi na hivyo kuamua kuyaondoa kwa kujiua!!

Mara nyingi tunamuona mtu aliyeizamisha nafsi yake katika starehe za jinsia na kubadilisha mwanamke mmoja hadi mwingine na baada ya muda utakapomuulizia baada ya hapo utakuta ni mhanga wa maradhi ya AIDS!!

Mahusiano yaliyoharamishwa ni matamu lakini yanavunja familia, nyumba na kuangamiza jamii na kuchanganya nasaba za watu, na kuangalia filamu za jinsia kuna aina ya ladha na raha lakini kunavunja nafsi ya mtu mwenyewe, na kuvunja mahusiano matukufu, na kuifanyia uadui staha ya jamii, na katika aina zingine za ladha ni chakula; tunawaona walio na mapenzi ya kula kuliko vile yalivyo mapenzi yao ya ibada au zaidi ya hapo, na huenda akavimbiwa

kwa kula kwake nyama kwa wingi au kula kwake vyakula vyenye sukari, lakini muda si mrefu mtu huyo tuna muona hospitalini kwa madaktari.

Wakati mwingine hii inakuwa ni kuingiliana kwa maana ya furaha na maana ya ladha, iliokusudiwa kutoka pande fulani hivyo basi pande nyingi zinajaribu kutangaza ladha mbali mbali kuwa ndio furaha yenyewe na kiini cha furaha, na malengo yao katika hilo ni kutawala akili za watu na kuzipeleka katika mielekeo tofauti, kwa mfano kijana mwenye kutumia madawa ya kulevya, mwanzoni hutumia ili apate ladha iliyokuwemo ndani yake, lakini baada ya hapo hubadilika kuwa ni mdoli katika mikono ya mwenye kumpa au kumuuzia!!

Matangazo mbali mbali ya biashara huwahadaa watu kwa bidhaa zake zinazotangazwa; utawaona sokoni wakitafuta bidhaa mpya au nguo mpya.

Furaha si kwa mwanadamu kupata kila akitakacho! Na kama ingekuwa hivyo basi matajiri wote pamoja na maraisi wangekuwa ni watu wenye furaha, ila tunachokiona katika tafiti mbali mbali za kisomi pamoja na hali halisi linapinga hilo, na huenda hilo ni kutokana na ukamilifu wa uadilifu wa Allah katika ulimwengu huu, Je, huoni furaha kwa fukara wengi pamoja na kuwa hawafahamiki! Basi kwani huoni furaha kwa matajri kutamani mambo mengi yalio kwa fukara ambayo yeye hana! Huenda basi furaha ikawemo kwenye raha!!

HAPANA.. FURAHA HAIPO KWENYE RAHA!!

Watu wengi hudhania kuwa raha ndio furaha hivyo wakaanza kutafuta raha ambayo huenda ikawaletea kero nyingi na huzuni pamoja na upweke na tabu na hivyo husahau kuwa mara nyingi huhisi furaha wakati mwili wake ukitaabika, bali wakati mwingine tabu na mashaka ayapatayo mtu ndio furaha yenyewe.

Utakapoamua kujitupa ndani ya kisima ili kumuokoa mtoto aliyetumbukia utakuwa ni mwenye furaha pamoja na majeraha na maumivu utakayoyapata wakati ushukapo kwenye kisima.

Ama tabu na mashaka wayapatao wanazuoni na watafuta elimu wakati wa kutafuta kwao elimu huwapelekea katika furaha na huwanyanyua katika vyeo vya juu pamoja na maumivu wayapatao na mashaka makubwa!!

Vivyo hivyo mwanariadha hufurahi kwa michezo yake pamoja na jasho linalotiririka mwilini mwake, na yule mwenye kuhudumia wanyonge na wenye kuhitaji hufurahi katika kufanya kwake hivyo pamoja na kutoa kwake na kujituma na kutumia mali aipendayo kwa fukara na masikini, hivyo kutoa mtu ni sehemu ya raha yake na anachokipenda ili apate furaha ndani ya nafsi yake.

Hivyo matokeo ya maingiliano haya na mitazamo mbali mbali na taarifu za aina nyingi za furaha (bado) mwanadamu anabaki akiwa hajui katika kivuli cha utafiti wake wenye kuchosha maana na jinsi gani atakapopata furaha ya kweli.

FURAHA CHINI YA HAKIKA KUU ZA UWEPO

Hapana shaka ya kuwa mwenye akili yoyote au mwadilifu yeyote ana yakini kuwa ili mtu aweze kufikia njia ya furaha hapana budi afahamu hakika kuu za uwepo; baada ya hapo ni juu yake atarajie kupata furaha kupitia njia ya amani ya kuamiliana na misingi mikuu ya uwepo huu, nayo ni binadamu, Maisha na Ulimwengu.

Maisha Hayavumiliki!!

"Kabla ya kujiua aliandika barua yake ya mwisho. Alisema ndani yake:Maisha hayavumiliki!! Nisameheni."

Dalida
Mwimbaji mashuhuri Ulimwenguni

1. MWANADAMU:

Ameumbwaje?!

Allah Aliyetukuka anasema: {Yeye ndiye aliye kuumbeni kwa udongo, kisha kwa tone la manii, kisha kwa pande la damu, kisha akakutoeni katika hali ya mtoto mchanga, kisha mpate kufikilia utu uzima, kisha mpate kuwa wazee. Na kati yenu wapo wanao kufa kabla, na ili mfikie muda ulio kwisha wekwa, na ili mpate kufahamu. [41:67],

Ndio …asili yake ni kutokana na udongo, maji dhalili na mwisho wake ni mzoga usio na roho na ndani yake anabeba najisi tumboni mwake na huhisi uchafu kila kinapotoka katika kiwiliwili chake, na baada ya yote haya huwa hasimu kwa Mola wake, ni kiasi gani ukanaji wake!! Allah Ta'ala anasema: {Ameangamia mwanaadamu! Nini kinacho mkufurisha?Kwa kitu gani amemuumba? Kwa tone la manii, akamuumba na akamkadiria. Kisha akamsahilishia njia. Kisha akamfisha, akamtia kaburini. Kisha apendapo atamfufua. } [80:17-22],

Pamoja na hayo bali amekirimiwa kuliko viumbe wengine, Allah ameamrisha Malaika kumsujudia babu yake Adam, na akamdhalilishia ardhi na wanyama, na kumkirimu kwa akili ambayo kwayo alimtengenezea miujiza mingi, Allah Mtukuka amesema: {Na hakika tumewatukuza wanaadamu, na tumewapa vya kupanda nchi kavu na baharini, na tumewaruzuku vitu vizuri vizuri, na tumewafadhilisha kwa fadhila kubwa kuliko wengi miongoni mwa tulio waumba.} [17:70]

Hivyo kiini cha mwanadamu hakiwezi kufahamika isipokuwa kwa taswira ya hakika hizi mbili pamoja, na kwa taswira hii ulinganisho unasimama katika imani utanyooka na kuwa yote yatakayomfikisha mwanadamu katika utukufu, mali na elimu na yasiyokuwa hayo si chochote ila ni katika neema ya Allah Mtukuka juu yake, Allah Mtukuka amesema: {Na neema yoyote mliyo nayo inatoka kwa Mwenyezi Mungu. Kisha yakikuguseni madhara mnamyayatikia Yeye.}

[16:53]. Ama mwanadamu mwenyewe hakuwa yeye isipokuwa ni mkusanyiko unaotokana na nyama na mifupa, nafsi yake inatukuka kwa (vitu) hivyo, ambayo anapenda kuinyoosha na kuilea kwa elimu yenye manufaa na matendo mema na ya kuwa pamoja na unyonge wake na udhaifu alionao ila ni kuwa Allah amemkirimu kwa sifa ambazo zitamuwezesha kubeba amana ambazo viumbe vingine vilivyo mzunguka haiviwezi, Allah Mtukuka amesema: {Kwa hakika Sisi tulikadimisha amana kwa mbingu na ardhi na milima; na vyote hivyo vikakataa kuichukua na vikaogopa. Lakini mwanaadamu akaichukua. Hakika yeye amekuwa dhaalimu mjinga.} [33:72]

Na atakapoharibu mwanadamu imani yake kwa sharti la lingano kati ya hakika mbili ima akili yake iondoke na kuelekea katika hakika ya mwanzo, na hivyo basi asiione nafsi yake isipokuwa ni kiwiliwili kichafu chenye matamanio kisichokuwa na malengo yoyote, hivyo kudhalilisha matamanio yake kama mnyama hadi imalize nafsi yake, Allah Mtukuka amesema: {…Na walio kufuru hujifurahisha na hula kama walavyo wanyama, na Moto ndio makaazi yao.} [47:12],Au avuke mpaka juu ya fikra ya hakika ya pili; ambayo humpelekea kuwa na kiburi na kufanya dhuluma akighafilika kuwa yeye atarejea kwa Mola wake, Allah Mtukuka amesema: {Kwani! Hakika mtu bila ya shaka huwa jeuri Akijiona katajirika. Hakika kwa Mola wako Mlezi ndio marejeo.} [96:6-8].

Ni juu ya mwanadamu kujua hadhi ya nafsi yake na kuitengeneza; kwani hiyo imekuwa ni sababu muhimu ya matatizo, kwani mwanadamu hajui sehemu yake katika jamii, wala hajui yeye ni nani na ni ipi nafasi yake na anaweza kufanya nini.

Jibu Toshelevu

"Katika kutekeleza mafundisho ya dini ya Kiislamu mwanadamu anagundua tabia yake na haiba yake ya kweli ya kibinadamu na atajua dhati yake. Uislamu ni dini pekee iliyonipa majibu yenye kukinaisha kwa maswali yangu yenye kutatanisha."

Rosemary Howe

Mwandishi wa habari wa Uingereza



Fahamu uwezo wako.

"Hata kama hadhi yake ni ndogo na matendo yake ni machache kwa mtazamo wa watu, lakini (Edison ambaye alifukuzwa shuleni) aliipata Nafsi yake katika uvumbuzi: Fadhila zake kwa wanadamu zilikuwa ni kubwa sana, la msingi ni wewe kutengamana na Nafsi yako, ili uwe na furaha na kufahamu nafasi na uwezo wako."

Thomas Edison

KWANINI AMEUMBWA?!

Allah Mtukuka ameumba yote yaliyomo, wala kuumba kwake hakukuwa kwa mchezo, upuuzi au bila ya maana. Allah Mtukuka amesema: {Je! Mlidhani ya kwamba tulikuumbeni bure na ya kwamba nyinyi kwetu hamtarudishwa? Ametukuka Mwenyezi Mungu, Mfalme wa Haki, hapana mungu ila Yeye, Mola Mlezi wa A'rshi Tukufu.} [23:115-116],

Bali ameumba viumbe ili vimuabudu kwa maana pana ya ibada ambayo inakusanya maisha yote ya mja hadi kazi zake michezo yake, na upuuzi wake na maisha yake yote, sio tu vile vipengele maalumu vya ibada pekee, amesema Mtukuka: {Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi.} [51:56].

Ama asiyejua hayo mtu huyu ataendelea kuadhibika kwa ujinga huu, na ataendelea kuwa na shaka na babaiko ambalo atapata nalo shida katika maisha yake, na hivyo basi ibada yake itajitenga na furaha, ibada na maisha yake ya hapa duniani, na dunia itajitenga na akhera, Allah Mtukuka amemhalalishia mwanadamu yote yaliyomo mbinguni na ardhini, amesema Mtukuka; {Na amefanya vikutumikieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi, vyote vimetoka kwake. Hakika katika hayo zimo Ishara kwa watu wanao fikiri.} [45:13],

Ni juu ya mwanadamu kujua kuwa yeye ni khalifa katika ardhi hii kutoka kwa mmiliki wake wa kweli na mmiliki wa mwanadamu ili kumpa mitihani, amesema Mtukuka: {Naye ndiye aliye kufanyeni makhalifa wa duniani, na amewanyanyua baadhi yenu juu ya wengine daraja kubwa kubwa, ili akujaribuni kwa hayo aliyo kupeni. Hakika Mola Mlezi wako ni Mwepesi wa kuadhibu, na hakika Yeye ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.} [6:165].

https://www.path-2-happiness.com/sw

2. MAISHA:

Baada ya mwanadamu kujua ukweli wa kuwepo kwake nafsi yake inatarajia kuzingatia katika maisha yake ya ndani ambayo ameumbwa kwa ajili yake, huo ni msingi ambao unasimamia ladha zote na yenye kufurahisha hapa duniani, na juu yake husimama matarajio ya kupata nafsi ya mwanadamu kinachotamani na kuelekea kwake, Ni nini basi lengo la maisha haya?! Kwa hakika lengo la kuumba mauti na uhai ni kumpa mtihani mwanadamu ni yupi atatenda matendo mazuri, amesema Mtukuka: {Ambaye ameumba mauti na uhai ili kukujaribuni ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi. Na Yeye ni Mwenye nguvu na Mwenye msamaha.} [67:2].

Huo ndio ukweli, lakini watu wengi hawafahamu!! Naam hiyo ndio hekima ya hii dunia, amesema Aliyetukuka: {Hakika mfano wa maisha ya dunia ni kama maji tuliyo yateremsha kutoka mbinguni, kisha yakachanganyika na mimea ya ardhi wanayo ila watu na wanyama. Mpaka ardhi ilipo kamilika uzuri wake, na ikapambika, na wenyewe wakadhani wamesha iweza, iliifikia amri yetu usiku au mchana, tukaifanya kama iliyo fyekwa - kama kwamba haikuwapo jana. Namna hivi tunazipambanua Ishara zetu kwa watu wanao fikiri.} [10:24]

Akasema Ta'ala: {Na wapigie mfano wa maisha ya dunia. Hayo ni kama maji tunayo yateremsha kutoka mbinguni, yakachanganyika na mimea ya ardhi, kisha hiyo mimea ikawa vibuwa vinavyo peperushwa na upepo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.} [18:45].

Kwa hiyo maisha yetu ambayo tunaishi ni mapito na sio ya kudumu, na hilo ni daraja lenye kufikisha katika nyumba ya akhera, maisha hayaishi kwa kuisha dunia bali kuna maisha ya hakika yenye kubakia Akhera, hivyo basi maisha ya duniani ni mchezo na pambo na kujifakharisha kama alivyosema Allah Mtukuka: {Jueni ya kwamba maisha ya dunia ni mchezo, na pumbao, na pambo, na kujifakhirisha baina yenu na kushindana kwa wingi wa mali na watoto. Mfano wake ni kama mvua ambayo huwafurahisha wakulima mimea yake, kisha hunyauka ukayaona yamepiga manjano kisha yakawa mabua. Na akhera kuna adhabu kali na maghfira kutoka kwa Mwenyezi Mungu na radhi. Na maisha ya dunia si chochote ila ni starehe ya udanganyifu.} [59:20];

Hivyo basi Aya hii inatoa taswira ya maisha haya ya dunia kwa sura ya udhalili inadunisha hadhi yake, na huzinyanyua nafsi na kuzitundika na akhera na kuzipa thamani.

Pindi maisha ya dunia yanapopimwa kwa vipimo vyake na kuangaliwa uzito wake katika macho na hisia za watu huonekana ni kitu kikubwa sana, lakini pindi inapopimwa na kuangaliwa uzito wake kwa vipimo vya akhera inaonekana kuwa ni kitu kidogo kisichokuwa na thamani; ni mchezo na upuuzi na pumbao na watu kujifakharisha na kutaka wingi (wa mali), huu ni ukweli ambao moyo unaujua pindi moyo huo unapotafuta ukweli, ukweli ambao Qur-aan hailengi kumtenga mwanadamu na maisha yake ya hapa duniani, wala kupuuza kuijenga kwake na kuiongoza, bali inalenga katika kusahihisha vipimo vya kihisia na kuinua thamani ya Nafsi kuliko kiburi au jeuri ya starehe fupi zenye kuondokana na mvuto wake na kuufunga na dunia.

https://www.path-2-happiness.com/sw

Kwa hakika maisha ni daraja ambalo viumbe hupita njiani katika njia yao ya kuelekea akhera, na dunia hii ni ufupi wa maisha yake si kitu ambacho kinaweza kufananishwa na maisha ya milele yanayofuatia. Kadhalika akhera na upana usio na mwisho inategemea hali atakayokuwa nayo binadamu katika maisha haya ya mwanzo, yeye atakuwa katika awamu ya mitihani ya kudumu, na kila akionacho pembezoni mwake katika starehe mbali mbali au katika tabu na balaa na maumivu mengi yote haya muda wake ni mdogo sana wenye kupita haraka, yatawekwa katika mkono wa mizani ili kumweka mwanadamu huyo katika marejeo yake ya milele, Je, utachukua nini kwenda nacho kaburini? Mtukuka amesema: {Nanyi mlitujia wapweke kama tulivyo kuumbeni mara ya kwanza. Na mkayaacha nyuma yenu yote tuliyo kupeni, na wala hatuwaoni hao waombezi wenu, ambao mlidai kuwa ni washirika wa Mwenyezi Mungu kwenu. Yamekatika makhusiano baina yenu, na yamekupoteeni mliyo kuwa mkidai.} [6:94].

Watu wengi wameghafilika na ukweli huu na hili ndilo alilosema Allah: {Wanajua hali ya dhaahiri ya maisha ya dunia, na wameghafilika na Akhera.} [30:7]

https://www.path-2-happiness.com/sw

Hali itakuwa vipi kwa aliyeridhia maisha haya duniani wala hataraji kukutana na Mola wake?! Mtukuka amesema: {Hakika wasio taraji kukutana nasi, na wakaridhia maisha ya dunia na wakatua nayo, na walio ghafilika na Ishara zetu, Hao, makaazi yao ni Motoni kwa sababu ya waliyo kuwa wakiyachuma.} [10:7-8],

Ni ipi hali ya aliyeitanguliza dunia, Allah amesema: {Na akakhiari maisha ya dunia, Kwa hakika Jahannamu ndiyo makaazi yake! Na ama yule anaye ogopa kusimamishwa mbele ya Mola wake Mlezi, na akajizuilia nafsi yake na matamanio, Basi huyo, Pepo itakuwa ndiyo makaazi yake! } [79:37-41].

Ndio, kwa sababu wamechukua dini yao kuwa ni upuuzi na mchezo na maisha haya duniani yakawahadaa, Allah amesema:

{Ambao waliifanya dini yao kuwa ni pumbao na mchezo, na maisha ya dunia yakawadanganya. Basi leo Sisi tunawasahau kama walivyo usahau mkutano wa Siku yao hii, na kwa sababu ya kule kuzikataa Ishara zetu.} [7:51],

Ndio; kwa sababu wanataka kuipotosha, Allah amesema: {Wale wanao fadhilisha maisha ya dunia kuliko Akhera, na wanawazuilia watu wasifuate Njia ya Mwenyezi Mungu, na wanataka kuipotosha. Hao wamepotelea mbali.} [14:3].

Hii haina maana ya kudharau maisha ya dunia kwa mtazamo wa mwanadamu na aache kujenga ardhi na dunia kwa elimu na matendo na ajitenge na kuwa mbali kabisa na dunia na kusubiri mauti tu.

Hii haina maana ya kudharau maisha ya dunia kwa mtazamo wa mwanadamu na aache kujenga ardhi na dunia kwa elimu na matendo na ajitenge na kuwa mbali kabisa na dunia na kusubiri mauti tu.

Hasha …bali njia nzuri inayofaa ya kutangamana pamoja na dunia ni ile aliyoisema Allah Mtukuka: {Na utafute, kwa aliyo kupa Mwenyezi Mungu, makaazi ya Akhera. Wala usisahau fungu lako la dunia. Nawe fanya wema kama Mwenyezi Mungu alivyo kufanyia wema wewe. Wala usitafute kufanya ufisadi katika ardhi. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi mafisadi.} [28:77]

Na amesema tena Allah: {Na chochote mlicho pewa ni matumizi ya maisha ya dunia na pambo lake. Na yaliyoko kwa Mwenyezi Mungu ndio bora na yatakayo baki zaidi. Basi je, hamfahamu?} [28:60].

Kwa mtazamo huu uliokamilika maisha kwa mtazamo wa mwanadamu yatakuwa ni Hazina yenye thamani ambayo inampasa mwanadamu kuwekeza; kama ilivyo yenyewe haimpasi mwanadamu kuipupia zaidi ya kuona kuwa ni daraja la kufikia furaha ya milele. Ama furaha, na aina ya mapambo na starehe ambayo mtu anakumbana nayo kwenye daraja hilo si chochote isipokuwa ni starehe za dunia na pambo lake kwani ni vizuri sana kuzitumia. Allah amesema: {Watu wamepambiwa kupenda matamanio ya wanawake, na wana, na mirundi ya dhahabu na fedha, na farasi asili, na mifugo, na mashamba. Hayo ni starehe ya maisha ya duniani; na kwa Mwenyezi Mungu ndio kwenye marejeo mema.} [3:14],

Na akasema Aliyetukuka: {Mali na wana ni pambo la maisha ya dunia. Na mema yanayo bakia ni bora mbele ya Mola wako Mlezi kwa malipo, na bora kwa matumaini.} [18:46]

Wala haichukizi vile vile kwa dhati yake ikiwa itatumiwa vizuri, Allah amesema: {Sema: Ni nani aliye harimisha pambo la Mwenyezi Mungu alilo watolea waja wake, na vilivyo vizuri katika riziki. Sema hivyo ni kwa walio amini katika uhai wa duniani, na Siku ya Kiyama vitakuwa vyao wao tu. Namna hivi tunazieleza Ishara kwa watu wanao jua.} [7:32],

Uliza na Qur-aan itakujibu.

"Nimesoma Qur-aan nikakuta ndani yake kuna majibu ya kila swali kuhusu maisha."

Mike Tyson.
Bondia Maarufu.

Na kwa ufahamu huu Muislamu anaingia katika msongamano wa maisha na utamu wake akiwa mwenye imani na hatua madhubuti baada ya kuyakinisha kuwa kila anachomiliki hakibakii, naye yupo daima katika kutafuta starehe bila ya kufanya israfu, pamoja na imani ya ndani kuwa alichokimiliki humo (duniani) katika miliki ya mkono wake na sio katika moyo wake. Aliyoyakosa humo hayamdhuru au aliyoyapata katika dunia yake, Allah Aliyetukuka amesema: {Hautokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila umekwisha andikwa katika Kitabu kabla hatujaauumba. Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi. Ili msihuzunike kwa kilicho kupoteeni, wala msijitape kwa alicho kupeni. Na Mwenyezi Mungu hampendi kila anaye jivuna akajifakhirisha.} [57:22-23]

Na hivyo basi anastarehe kwa starehe na mapambo, naye ni mwenye kupata ujira na malipo kutoka kwa Allah, na kwake dunia inaungana na akhera na furaha za viwiliwili pamoja na furaha za kiroho, na furaha kwa mapambo ya dunia, na furaha kwa kuridhika na utulivu ndani yake.

3. ULIMWENGU:

Muislamu anahama katika kufikiria kwake katika kipengele cha tatu na cha mwisho katika kufahamu kwake uwepo; nao ni Ulimwengu ambao unakusanya viumbe vyote ulimwengu ambao unakusanya viumbe vyote vinavyomzunguka, fikra yake inaanzia katika kauli yake Allah Aliyetukuka:

{Sema: Angalieni yaliomo mbinguni na kwenye ardhi! Na Ishara zote na maonyo hayawafai kitu watu wasio amini.} [10:101] Kisha anaendelea kusoma makumi ya aya ambazo zinamuita kwenye kufikiria kuumbwa kwake na uzuri wa sanaa yake ili atoke na matokeo yanayofanana na yale aliyoyapata mwanzoni kuhusu kufikiri kwake kulikotangulia kuhusu uhakika wa uwepo wake na maisha yake, na kugundua kuwa kufahamu kwake ulimwengu inapasa vile vile kuanzia pale alipofahamu ukweli ule uliokamilika ambao upo katika namna mbili:

Kwanza: Ukweli wa kuwa Allah Aliyetukuka amemdhalilishia vingi vinavyomzunguka katika viumbe; ya kuwa ubora na kutangulizwa kwake hakukuwa ni kwa sababu ya kuwa na sifa tu ya baadhi ya vipambanuzi, bali ni kule kumpelekea kudhalilishwa viumbe hivi kumhudumia ili lengo la maendeleo lifikiwe, Allah Aliyetukuka amesema: {Kwani hamwoni ya kwamba Mwenyezi Mungu amevifanya vikutumikieni viliomo mbinguni na kwenye ardhi, na akakujalizieni neema zake, za dhaahiri na za siri? Na miongoni mwa watu wapo wanao bishana juu ya Mwenyezi Mungu pasipo ilimu, wala uwongofu, wala Kitabu chenye nuru.} [31:20],

Na akasema: {Na amefanya ukutumikieni usiku na mchana, na jua na mwezi, na nyota zikutumikieni kwa amri yake. Hakika katika hayo zipo ishara kwa watu wenye akili.} [16:12],

Na akasema tena: {Yeye ndiye aliye idhalilisha ardhi kwa faida yenu, basi tembeeni katika pande zake, na kuleni katika riziki zake. Na kwake Yeye ndio kufufuliwa.} [67:15],

Muislamu atapata katika aya nyingi dalili kubwa ya kudhalilishwa ulimwengu huu na kumthibitisha yeye ndani yake, na katika hilo ni ishara nzuri ya umuhimu wa kujiliwaza na ulimwengu huu, na kujizuia kufadhaika pindi tatizo au balaa litakapompata, maumbile daima hayapo katika kupingana na mwanadamu dhaifu, na hivyo hivyo mwanadamu huyo hayupo katika kushindana na maumbile.

Pili: Ama ile hakika ya pili: ambayo ni kuwa ulimwengu haukumfichulia mwanadamu siri zote; pamoja na kumdhalilishia, na kumuwezesha (kumthibitisha) lakini kundi lingine katika ulimwengu huu bado ni siri iliyofichika kwa mwanadamu na zipo nje ya utawala wake.

Ulimwengu huu una Malaika, majini na huenda kuna viumbe vingine ambao bado hawajafahamika na mwanadamu au hata elimu ya kufahamu kuwepo kwao na uwepo wa mwanadamu katika ulimwengu huu ni sehemu ndogo tu ya atomi ambayo huwezi kuitaja mbele ya ukubwa na upana wa ulimwengu huu.

Dini ya Ubinadamu.

"Dhati yangu niliyoikosa kwa muda mrefu katika maisha yangu nimeipata ndani ya Uislamu na kwa mara ya kwanza, wakati huo nilihisi kuwa mimi ni binadamu. Uislamu ni dini inayomrejesha mtu katika tabia yake (asili yake) kwani inaafikiana na maumbile ya mwanadamu."

Martin Lings

Mwanafikra wa Kiingereza.

Kwa hakika hizi mbili ule mtazamo wa Muislamu unakamilika kwa ulimwengu unaomzunguka; yeye kujua kwa ukamilifu nafasi yake maalumu iliyopambanuliwa kati ya viumbe, kiasi cha Allah Aliyetukuka kumfanya kuwa yeye ni kilele cha uwepo ambao viumbe vingi vimedhalilishwa kwa ajili yake, na wakati huo huo akijua ukweli wa kuwa baadhi ya milango kufungwa kwake, na kuwa uwezo wake wa kustaajabisha vyovyote iwavyo hauwezi kugonga milango ile.

Ama uhusiano wa mwanadamu na wanaomzunguka ni uhusiano unaodhibitiwa na hisia (heshima) ya hali ya juu na adabu kubwa, watu wenye kuishi katika hali ya fujo katika mahusiano yao huishi kwa shida na tabu nyingi kwa sababu mahusiano yao hayana uwiano na hayapo katika udhibiti mzuri hivyo basi mahusiano yao yanasimama katika ubinafsi, hasadi, dhana mbaya na kulipizana visasi na kuviziana.

Yote hayo yanamfanya mwanadamu kutokuwa na furaha na kutoridhika na kumfanya kuwa na wasiwasi mara kwa mara na kuwa katika hali ya dhiki muda wote, katika hali hiyo mtu huyu atapata wapi raha na furaha?! Allah Aliyetukuka amesema: {Mema na maovu hayalingani. Pinga uovu kwa lilio jema zaidi. Hapo yule ambaye baina yako naye pana uadui atakuwa kama rafiki jamaa wa kukuonea uchungu. Lakini hawapewi wema huu ila wanao subiri, wala hawapewi ila wenye bahati kubwa. } [41:34-35]

Ama mtu ambae amepangilia maisha

yake katika misingi ya haki na majukumu mbali mbali mtu huyo hutekeleza wajibu wake na huwarahisishia wenye haki zake na husamehe mahasimu wake, mwisho wa yote hayo huwa ni mtu mwenye furaha bila ya shaka.

Mapenzi ni ngazi ya juu kabisa ya mtu kutangamana na nduguye mwanadamu, upole, urafiki una maana ya mapenzi kuzoeana nayo ni maumbile ya asili ya mwanadamu yalio sawa.

NJIA YA FURAHA..UZURI WA MWANADAMU NA NAFSI YAKE PAMOJA NA MAISHA NA ULIMWENGU:

Kwa imani hii mwanadamu anafanya suluhu pamoja na Mola wake pamoja na Nafsi yake na ulimwengu unaomzunguka, yeye hufahamu kwanza kabisa ukweli wa uja wake kwa Mola wake Aliyetukuka, husimamia majukumu yake ipasavyo na kadhalika hujua thamani ya nafsi yake kama kiumbe ambae Allah amemkirimu kwa kumdhalilishia viumbe, na kuwa aliteremka ardhini ili apewe mtihani ndani yake kabla ya kurejea peponi, pepo ambayo imeumbwa kwa ajili yake, amekalifishwa kuijenga ardhi

Dini ya Karama na Tabia Njema.

"Ni kwa sababu hii ndio nimechagua Uislamu ili ndani yake nipate raha. Na nimeukumbatia Uislamu ili nipate hisia na kufahamu kuwa nimechagua dini ambayo haitofautishi baina ya kiwiliwili, roho, na nafsi, inanitosha kuwa Uislamu ni dini nadhifu inasukuma kwenye tabia njema na kujipamba nayo na kwenye karama na kushikamana nayo. Kwa ajili hiyo nimeshuhudia kuwa hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Allah na Muhammad ni Mtume wake na juu ya hilo nitakutana na Mola wangu."

F. Mosey

Mwanafikra wa Kifaransa.

hii, Allah Aliyetukuka amesema: {…Yeye ndiye aliye kuumbeni katika ardhi, na akakuwekeni humo. Basi mwombeni msamaha, kisha mtubu kwake. Hakika Mola wangu Mlezi yupo karibu, anaitikia maombi.} [11:16],

Na amekalifishwa vile vile kuilea na kuizoesha nafsi yake katika kujizuia matamanio na kuwa chini ya mipaka ya kisheria kulingana na mahitaji yake.

Tukiwa na ufahamu huu kamili kuhusu Muumba Mtukuka, pamoja na nafsi na ulimwengu sasa ni haki kwetu kujiuliza kuhusu matokeo ya kimatendo baada ya kutekeleza ufahamu na mtazamo huu.

Baada ya mwanadamu kujua ukweli ule atajua kuwa furaha ipo katika nyumba zote–Dunia na Akhera na zote hutegemea radhi za Allah kwa kutekeleza maamrisho yake na kusimama katika mipaka yake.. yote haya huja katika kulinganisha baina ya matakwa ya kiwiliwili na kiroho; na baina ya matakwa ya mtu binafsi na matakwa ya kundi baina ya kujenga dunia na kujenga akhera na hivyo kubaki furaha duniani – vyovyote itakapokuwa ni furaha yenye upungufu, kwa sababu dunia ni nyumba ya kujitahidi na kufanya matendo na mitihani na akhera ni nyumba ya hesabu na atakayefuzu atapata furaha kamili ya milele, Allah Aliyetukuka amesema: {Mola wao Mlezi anawabashiria rehema zitokazo kwake, na radhi, na Bustani ambazo humo watapata neema za kudumu. Watadumu humo milele. Hakika kwa Mwenyezi Mungu yapo malipo makubwa.} [9:21-22]

Ili mwanadamu apate furaha na kuhisi utulivu na maisha mazuri yalio bora duniani na akhera hapana budi awe na imani na matendo mazuri, Allah amesema: {Mwenye kutenda mema, mwanamume au mwanamke, naye akawa ni Muumini, tutamhuisha maisha mema; na tutawapa ujira wao kwa bora ya waliyo kuwa wakiyatenda.} [16:97].

Neema ya Uislamu.

"Hakuna neema kubwa miongoni mwa neema za dunia ambavyo mwanadamu ananeemeka nayo mtu kuliko Allah kumfungulia mtu kifua chake kwa ajili ya Uislamu, na akaongoka kwa nuru yake hadi akaona hakika za duniani na akhera hivyo mtu akaweza kutofuatisha baina ya haki ya batili, na baina ya furaha na huzuni na mashaka. Nami namsujudia Allah na kushukuru neema hii tukufu aliyonipa, neema ambayo imejaza furaha ndani ya nafsi yangu na kunipa fursa kuwa chini ya kivuli cha mti huu mkubwa wenye matawi yenye vivuli na matunda (mengi), nayo ni mti wa familia ya Kiislamu na udugu katika Uislamu."

Marshila Michelangelo

Mwanadada wa Kitaliano aliyesilimu

ALAMA ZA NJIA YA FURAHA:

Ili kufahamu njia ya furaha katika hakika yake, ambayo ndio njia ya kumuamini Allah Aliyetukuka, ni vizuri kwetu tubainishe baadhi ya alama na Njia hii, ili tuwe watulivu na wenye hima za juu katika safari yetu hii.

1. HIYO NI NJIA YA ALLAH ALIYETUKUKA:

Allah amesema:

{Na kwa hakika hii ndiyo Njia yangu Iliyo Nyooka. Basi ifuateni, wala msifuate njia nyingine, zikakutengeni na Njia yake. Haya amekuusieni ili mpate kuchamngu.} [6:153],

Hivyo basi njia ya furaha ni njia ya Allah na wasia wake aliousia waja wake kuufuata (naye ndie mjuzi wa yanayowafaa).

Hapana shaka yoyote kuwa mtu muovu ndie ambaye anaacha njia ya Allah na anatarajia furaha katika njia nyingi tofauti; hivyo hakuna furaha kwa hali yoyote ile bila ya kufuata njia yake, Allah Aliyetukuka amesema: {… basi atakaye ufuata uwongofu wangu, hatapotea wala hatataabika. Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu.} [20:123-124].

Imani na Afya ya Nafsi

“Kwa muda wa miaka thelathini iliyopita nimewapa ushauri watu wa mataifa mbali mbali yaliyostaarabika ulimwenguni, nikatibu mamia ya wagonjwa. Sijapata tatizo moja katika matatizo ya wale wenye umri zaidi ya miaka thelathini na tano au mfano wake ila tatizo lao wote lilikuwa linarejea katika msingi wa kukosa kwao imani na kutoka katika mafundisho ya dini. Na ni sahihi kusema kuwa: Kila mgonjwa katika wagonjwa wale walikuwa ni mhanga wa maradhi: Kwa sababu wamenyimwa utulivu wa nafsi ambao unaletwa na dini. Hakupona hata mmoja miongoni mwao ila aliporejesha imani yake na kujisaidia kwa kufuata maamrisho ya dini na kuacha makatazo yake na kukabiliana na maisha yao.”

Carl Jung

Mtaalamu maarufu wa tiba na Magonjwa ya akili Ulimwenguni.

Furaha ni kwa aliyefuata njia na kufuata uongofu, na dhiki ni kwa yule aliyeupa mgongo na kukengeuka (kupotoka) hata idhihiri kuwa ni miongoni mwa watu maarufu au wenye nyota katika jamii.

2. Ni njia inayokusanya kati ya furaha ya kiroho na furaha ya kiwiliwili:

Kinachofahamika ni kuwa mwanadamu ni mkusanyiko wa roho na kiwiliwili, na kila kimoja kina chakula chake, na baadhi ya njia na falsafa dhaifu ambazo zimeshughulika na kujali upande wa kiroho tu na kukataa matakwa ya kiwiliwili ikawa ni tatizo ni kurejea tena, na wanaojali maada ya kisasa ni kinyume chake nao wamefuta na kuondoa mzizi wa mambo ya kiroho na kukipa kiwiliwili kila linachokitamani; hivyo kuondosha kundi kubwa la utu na ubinadamu kuelekea kwenye uhayawani wa ladha na matamanio! Au kuwafanya watu kuwa mashine zisizoweza kuzalisha.

Ama njia ya Uislamu roho yake imelishwa na mianga ya mbinguni na kuhifadhi kiwiliwili, na kushibisha hoja zake na matamanio yake kwa vitu vizuri vya halali: {Na utafute, kwa aliyo kupa Mwenyezi Mungu, makaazi ya Akhera. Wala usisahau fungu lako la dunia. Nawe fanya wema kama Mwenyezi Mungu alivyo kufanyia wema wewe….} [28:77];

Mtume (Swala llahu 'alayhi Wasallam) alithibitisha yale aliyoyasema Salman Al-Farisy (Radhiya Llahu 'anhu):

«Kwa Mola wako una haki na nafsi yako ina haki na familia yako ina haki, mpe kila mwenye haki haki yake.»(Al-Bukhari).

3. Ni Njia ya Furaha na Ujasiri:

Atakayeonja utamu wa imani hatopenda kabisa kuachana nayo hata kama atawekewa upanga shingoni mwake, waangalie wachawi wa Firauni walipoamini na kufuata njia ya furaha, Firauni aliwatisha, na akawaambia kama ilivyo kuja katika Qur-aan Tukufu: {…Basi kwa yakini nitakukateni mikono yenu na miguu yenu kwa kutafautisha. Na nitakutundikeni misalabani katika vigogo vya mitende, na hapo kwa yakini mtajua ni nani katika sisi aliye mkali wa kuadhibu na kuiendeleza adhabu yake.} [20:71]

Na jibu lao likawa la imara kabisa: {Wakasema: Hatutokukhiari wewe kuliko ishara waziwazi zilizo tujia, na kuliko yule aliye tuumba. Basi hukumu utavyo hukumu; kwani wewe unahukumu haya ya maisha ya duniani tu.} [20:72]



Na kilichothibitika kuhusu hilo baada ya muda mdogo tu kutokana na imani yao, na hiyo ni baada ya kuonja utamu wa imani hii ambayo imewafanya wakawa watulivu zaidi katika rai zao na maamuzi yao, bali hata katika hali ya kutishiwa kuuawa.

4. Furaha ni utulivu moyoni:

Hakuna furaha isiyokuwa na utulivu, wala utulivu usiokuwa na imani, Allah Aliyetukuka amesema: {Yeye ndiye aliye teremsha utulivu katika nyoyo za Waumini ili wazidi Imani juu ya Imani yao. Na Mwenyezi Mungu ndiye mwenye majeshi ya mbingu na ardhi. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye ujuzi, Mwenye hikima} [48:4].

Imani humpa mtu furaha pande zote mbili:-

Kwanza: Inamzuia mtu kutumbukia katika shimo la uovu na jinai, nayo ni sababu hatari zaidi za tabu na mashaka, hakuna kitu kinachompa dhamana mwanadamu ili asivutwe na matamanio yake kufanya maovu yaliyokatazwa ila ni pale ambapo moyo wake unapokuwa ni mtupu wa imani kwa Mola wake.

Pili: Hiyo inatoa umuhimu mkubwa katika sharti miongoni mwa masharti ya furaha, nayo ni utulivu; katika wimbi la matatizo hakuna kitu kitakachoweza kumuokoa mtu zaidi ya imani bila ya imani khofu na wasi wasi humkumba mwanadamu.

Ama mtu akiwa na Imani hakuna chenye kustahiki kuhofiwa zaidi isipokuwa ni mtu

Majibu Toshelevu.

"Nimepata katika Uislamu majibu yenye kutosheleza kuhusu mas-ala tata ya roho na maada: Nikafahamu kuwa kiwiliwili kina haki kwetu kama ilivyo roho. Na kuwa mahitaji ya kiwiliwili katika mtazamo wa Uislamu ni silika asilia ambazo zinapaswa kushibishwa ili mwanadamu aishi akiwa ni mwenye nguvu na mwenye uwezo wa kuzalisha.
Isipokuwa Uislamu umeweka kanuni za msingi ili kushibisha hoja hizi katika misingi ya amani ambayo itahakikisha ridhaa ya nafsi na kufuata maamrisho ya Allah. Kwa mfano ndoa katika Uislamu ni njia pekee ya kisheria ya kushibisha matamanio ya kijinsia. Na Swala, Saumu, kufanya ibada na kumuamini Allah ni njia nyingine ya kushibisha upande wa kiroho kwa mwanadamu, na kwa sababu hiyo hapo ndipo itakapothibitika mizani ya sawa ambayo hapana budi kwa maisha mema ya mwanadamu."

Rosemery Hawe

Mwanahabari wa Uingereza.



https://www.path-2-happiness.com/sw

kuwa mbele ya Allah (Subhaanahu wa Ta'ala)

Katika Moyo wa muumini kila kigumu kinakuwa chepesi; kwa sababu humtegemea Allah na moyo mtupu usiokuwa na imani ni kama vile jani lililokatwa kutoka kwenye tawi lake, ambayo inachezewa hata na upepo mdogo upitao, Je! ni kitu gani kinachomtisha mwanadamu zaidi ya kifo na kuondoka katika ulimwengu huu?! Kwa muumini haswa sio jambo la kuhofia, bali ni jambo ambalo anatulizana nalo vile vile, mauti yana manufaa kwa yule ambaye moyo wake umejaa imani na ucha-Mungu!!

Kwa hakika imani inasukuma hisia ya utulivu kwa mtu; mtu aliyekuwa muumini hupita katika njia ya Allah kwa amani na utulivu; kwa sababu imani yake ya kweli daima humpa matarajio mema na kusubiria msaada wa Allah na ulinzi wake katika nyakati zote, nae huhisi mara zote kuwa Allah Aliyetukuka yupo nae kila wakati, Allah amesema: {…Kwani hakika Mwenyezi yu pamoja na Waumini. { [8:19].

Muda wowote muumini atakapokabiliana na matatizo, na wakati wowote muumini matatizo yatakapomuelekea, na wakati wowote atakapopambana na mitihani basi Allah na maneno yake yanayong'aa kwa mwangaza wa Nuru ya uongofu hutosha kumuondoshea yote aliyonayo ndani ya Nafsi yake, kama vile wasi wasi na maumivu katika kiwiliwili chake na



Imani na Babaiko Havikutani.

"Mawimbi makali ya bahari kamwe hayaathiri utulivu wa chini ya bahari. Wala kuathiri amani yake, vivyo hivyo mtu ambae imani yake imezama kwa Mungu kikweli ameepukana na babaiko na atahifadhi mizani yake, na atajiandaa wakati wote kupambana na matatizo yoyote yanayoweza kuletwa na masiku huko baadae."

William James

Mwanafalsafa wa Kimarekani.

ugonjwa hivyo khofu yake kubadilika kuwa amani na salama kwake, na tabu zake, mashaka na huzuni kuwa furaha na uchangamfu, na hivyo basi huongozwa katika kufanikisha utulivu wa nafsi na furaha ya kiroho ambayo haikabiliani na furaha yoyote nyingine hata kama mtu huyo atamiliki hazina za dunia na vilivyomo.

5. Safari ya Furaha kutoka Duniani kuelekea Peponi:

Kuwa maisha ya mwanadamu yapo katika hatua tatu: Ya kwanza ni hapa duniani, na ya pili ni Kaburini baada ya kifo na ya tatu ni Siku ya Kiama.

Njia ya furaha hupita katika hatua zote hizi tatu; hapa duniani Allah amesema: {Mwenye kutenda mema, mwanamume au mwanamke, naye akawa ni Muumini, tutamhuisha maisha mema; na tutawapa ujira wao kwa bora ya waliyo kuwa wakiyatenda.} [16:97] ;

Yaani tutamhuisha hapa duniani maisha ya furaha yenye utulivu na amani hata kama atakuwa na mali kidogo; na hiyo ni kwa kuridhisha nafsi na hali yake ya kiroho na ya kinafsi na hivyo kupata utulivu, na yakini yake kwa Allah Aliyetukuka na utulivu wake kwake (Allah).

Ama suala la furaha ya mwanadamu kaburini kwake; tunaliona katika aliyopokea Abu Hurairah (Radhiya Llahu 'anhu) kuwa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) amesema: "Hakika muumini ndani ya kaburi lake yupo katika bustani ya kijani, na kaburi lake hupanuka kwa dhiraa sabini na huingizwa mwanga kama vile usiku wa Badri." (Al-Albany amesema kuwa ni Hadithi Hassan).

Ama kuhusu furaha yake Akhera Allah amesema:

Wema wa Amani



"Kila Muislamu anaposoma Qur-aan kwa undani zaidi na akasimamisha kutekeleza alama za Uislamu kwa ukweli, basi mtu huyu atakuwa amepanda wema wa amani katika msafara wa Uislamu. Na hivyo atakuwa amepanda vile vile treni ya utulivu na kuwa mbali na uchafu wa shetani."

Casius Clay
Bondia wa Zamani wa Marekani.

Dini ya Dunia na Akhera



"Mwanadamu msomi anaelekea kwa tabia yake katika Uislamu. Kwa sababu ni dini pekee ambayo inaangalia mambo ya duniani na akhera kwa usawa."

Sir George Bernard Shaw
Mwandishi wa Kiingereza

{Na ama wale walio bahatika, wao watakuwamo Peponi wakidumu humo muda wa kudumu mbingu na ardhi, isipo kuwa apendavyo Mola wako Mlezi. Hicho ni kipawa kisio na ukomo.} [11:108]

Na hapo atakuwa amefaulu kupata furaha duniani na neema zisizokwisha Akhera.

Kwa hivyo Uislamu umeleta furaha ya milele; furaha ya mwanadamu katika maisha anayoishi sasa, na furaha katika nyumba ya akhera na kilicho kwa Allah ni kheri na ndicho kinachobakia zaidi na Allah amefanya furaha hii ya mwanadamu na furaha yake akhera ni vitu viwili vilivyo pamoja, bila ya mvutano kati yake wala mgongano.

Maisha haya ya dunia si chochote bali ni njia ya kuelekea akhera na kwenye furaha kuu zaidi Siku ya Kiama, zote ni njia moja, ni njia ya furaha milele duniani na akhera, Allah Aliyetukuka amesema:

{Anaye taka malipo ya dunia, basi kwa Mwenyezi Mungu yapo malipo ya dunia na Akhera. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia na Mwenye kuona.} [4:134].

SABABU ZA FURAHA DUNIANI KATIKA UISLAMU

Furaha katika maisha ambayo tunayaishi katika Uislamu yana vyanzo vingi na sababu mbali mbali, miongoni mwa hizo ni:-

1. Furaha kwa Tawhidi na Kumuamini Allah:

Hakuna furaha wala raha wala utulivu kama ilivyokuwa raha na utulivu wa Tawhidi, Allah Aliyetukuka amesema: {Wale ambao wameamini, na hawakuchanganya imani yao na dhulma - hao ndio watakao pata amani na wao ndio walio ongoka.} [6:82]



Hivyo basi hupimwa ukamilifu wa tawhidi na utimilifu wake kwa jinsi amani, utulivu, furaha inayopatikana duniani na akhera, ambapo Allah humuingizia mtu mwenyewe furaha ndani ya Nafsi yake.

Ama Shirki (Allah atulinde) ambao inamfanya mtu mwenyewe kuwa na dhiki, tabu na mashaka ndani ya kifua cha mtu mwenyewe kama kwamba anapaa mbinguni. Allah amesema: {Basi yule ambaye Mwenyezi Mungu anataka kumhidi humfungulia kifua chake kwa Uislamu. Na anaye taka apotee hukifanya kifua chake kina dhiki, kimebana, kama kwamba anapanda mbinguni. Namna hivi Mwenyezi Mungu anajaalia uchafu juu ya wasio amini.} [6:125],

Hivyo bali hawalingani kati ya yule ambaye Allah amekunjua kifua chake kwa Uislamu; yeye yupo kwenye nuru ya Mola wake, na aliye katika kiza cha ushirikina kuwa mbali na dhikri ya Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) moyo wake umekuwa mgumu; naye yupo kwenye upotevu ulio wazi: Allah Aliyetukuka amesema: {Je! Yule ambaye Mwenyezi Mungu amemfungulia kifua chake kwa Uislamu, na akawa yuko kwenye nuru itokayo kwa Mola wake Mlezi (ni sawa na mwenye moyo mgumu?) Basi ole wao wenye nyoyo ngumu zisio mkumbuka Mwenyezi Mungu! Hao wamo katika upotofu wa dhaahiri.} [39:22]

Itikadi Nyepesi

"Itikadi ya Kiislamu ni itikadi moja ambayo ni nyepesi ambayo imani inakata nayo njia ya kila mwenye hofu na babaiko, na kufufua utulivu katika kila nafsi. Mlango wa akida hii upo wazi kwa mwanadamu yeyote. Haufungiwi dhidi ya yoyote (kuzuiwa kuingia) kwa sababu ya jinsia au rangi yake. Hivyo basi kila mtu hupata nafasi yake chini ya kivuli cha itikadi ya Mungu kwa misingi ya usawa na uadilifu ambao haimfadhilishi yoyote pamoja nayo ila kwa ucha-Mungu. Ucha-Mungu kwa Allah Mola wa Walimwengu."

Nazm Luka
Mwanafalsafa na Mwanafikra wa Misri

https://www.path-2-happiness.com/sw

Amani ya Kweli.

"Ninapata hisia kama wapatavyo Waislamu wanaposwali; Hisia tamu inapochanganyika na furaha na hilo ndilo nililokuwa nikihisi na kushukuru kwa sababu yake. Kama ambavyo watoto wangu wapo katika amani. Kwa hakika sitaki zaidi ya hayo."

Lauren Booth

Mwana harakati wa kutetea haki za Binadamu wa Uingereza.

Na hawi sawa yule aliyekuwa maiti katika kiza cha ushirikina kisha akaongozwa na Allah kwa fadhila zake na rehema zake kama yule aliyebakia katika kiza cha ushirikina hatoki humo, Allah Aliyetukuka amesema:

{Je, aliye kuwa maiti kisha tukamhuisha, na tukamjaalia nuru inakwenda naye mbele za watu, mfano wake ni kama aliyoko gizani akawa hata hawezi kutoka humo? Kama hivyo makafiri wamepambiwa waliyo kuwa wakiyafanya.} [6:122].

2. Dhikrullah na kunong'ona naye na kujikurubisha kwake:

Vyovyote mwanadamu atakavyopewa katika mapambo ya dunia na maisha yake, na vyote atakavyomiliki na kupata sababu za furaha; hatoweza kupata furaha muda wa kuwa yupo mbali na njia ya Allah.

Mwanadamu hatopata utulivu ila atakapokuwa karibu na Allah na katika kivuli chake cha harufu nzuri ya dhikri yake Allah amesema: {Wale walio amini na zikatua nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndio nyoyo hutua!} [13:28];

Na hiyo ni kwa sababu: "Ndani ya moyo wake mambo yameparaganyika ambavyo hayakusanyiki ila kwa kuwa karibu na Allah Ta'ala, na hiyo ni kwa sababu: "Ndani yake kuna ambayo haliondoshwi isipokuwa kwa kujiliwaza

kwake katika faragha yake (kumkumbuka Allah) na kadhalika kuna huzuni ambayo haiondoki isipokuwa kufurahi kwa kumjua Allah na ukweli wa kuamiliana nae na ndani yake kuna babaiko ambalo halitulii isipokuwa kwa kukusanyika kwa ajili yake na kumkimbilia yeye tu.

Vivyo hivyo ndani ya moyo wa mtu kuna moyo wa majuto na wenye hasara hauzimwi isipokuwa kwa kuridhia maamrisho yake, makatazo yake na hukumu zake na kuikumbatia subira juu ya hayo, hadi mtu atakapokutana na Mola wake, na kuna kutafuta sana ambayo hakuna chenye kumzuia isipokuwa matakwa yake kwa Mola wake yawe peke yake, na ndani yake kuna balaa ambalo haliondolewi isipokuwa kwa mapenzi na kumtegemea yeye tu na kudumu katika dhikri yake na ukweli wa kumsafishia nia, hata kama mtu huyo atapewa dunia yote na vilivyomo basi hiyo haja yake haitozibwa milele."

3. Matendo mema:

Allah Aliyetukuka amesema: {Wale walio amini na wakatenda mema watakuwa na raha na marejeo mazuri.} [13:29]

Walioamini kwa nyoyo zao–kuamini Mwenyezi Mungu, Malaika wake, vitabu vyake, Mitume yake na Siku ya Mwisho na imani hii ikasadikishwa na matendo mema–matendo ya nyoyo; kama vile kumpenda Allah, kumuogopa na kumtarajia, na matendo ya kiwiliwili, kama vile Swala na mfano wake wanakuwa katika hali nzuri ya ukamilifu wa raha na utulivu, na hiyo ni kwa sababu ya kupata kwao radhi za Allah na utukufu wake duniani na akhera, hivyo ni juu yetu matendo mema pamoja na imani, Allah Aliyetukuka amesema:



{Hakika walio amini, na Mayahudi na Masabii na Wakristo, walio muamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya mwisho, na wakatenda mema, basi hawatakuwa na khofu wala hawatahuzunika.} [5:69],

Na Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) alikuwa akipata raha na ladha yake ndani ya Swala na utii na alikuwa akisema: «Ewe Bilal kimu swala, tufurahishe nayo.» (Abu Dawuud).

4. Utoaji ni Siri ya Furaha:

Hili ni jambo lililokwisha jaribiwa na kushuhudiwa, sisi tunawaona wale wenye kuwafanyia wema wengine kuwa ni watu wenye furaha zaidi na ni miongoni mwa watu wanaokubalika duniani, Allah Aliyetukuka amesema: {KABISA HAMTAFIKIA wema mpaka mtoe katika vile mnavyo vipenda. Na kitu chochote mnacho kitoa basi hakika Mwenyezi Mungu anakijua.} [3:92],

Na utoaji una mifumo mingi sana; kwani Allah amefanya utoaji wa mali kuwa ni sehemu ya nguzo ya Uislamu; akafaradhisha na akawajibisha Zakkah kutoka kwa tajiri kwenda kwa masikini, na Allah akaamrisha kuwa utoaji huu unapasa kuwa uzuri wa Nafsi na (Ikhlas) kwa Allah kwa yale mazuri na ayapendayo mwanadamu na kutosimbulia watu, Allah amesema: {Enyi mlio amini! Msiharibu sadaka zenu kwa masimbulizi na maudhi…} [2:264],

Bali amepanua utoaji ili mali ifikie kila utoaji, ni sawa uwe ni mali au chakula au juhudi, au amali, Allah amesema: {Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini, na yatima, na wafungwa. Hakika sisi tunakulisheni kwa wajihi wa Mwenyezi Mungu. Hatutaki kwenu malipo wala shukrani.} [76:8-9],

Bali hata ikiwa utoaji huo ni kutabasamu kutupu, Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) amesema: «Tabasamu lako mbele ya ndugu yako ni sadaka» (Al-Tirmidh).

Akasema vile vile: «Mwenye kuwa na hoja ya nduguye basi Allah atakuwa kwenye haja yake, na atakayemuondolea Muislamu tatizo Allah atamwondolea matatizo yake Siku ya Kiama, na mwenye kumsitiri Muislamu Allah atamsitiri Siku ya Kiama.» (Abu Dawuud).

Bila shaka utoaji huu ndio ambao unapasisha furaha ya dunia, Ama utoaji ili mtu apate chumo lakidunia au masimbulizi au maudhi hatopata chochote katika furaha hata kama hilo likidhihirika (kinyume) vinginevyo.

5. Kumtegemea Allah (Tawakul) ndio Ufunguo wa Furaha:

Mara nyingi mtu hujihisi mnyonge na kutokuwa na uwezo wa kufanya kitu; na hurudi kwa mwenye nguvu akaomba msaada wake na kumtegemea ili afikie analotaka, sasa ni nani aliye na nguvu kuliko Allah?!

Kwa hakika ufunguo wa furaha ni kumtegemea Allah, mwenye nguvu na muweza ambaye anamiliki falme (Malakuti) za mbingu na ardhi, ambaye akitaka kitu husema: 'kuwa na kikawa', Allah amesema: {Hakika amri yake anapo taka kitu ni kukiambia tu: Kuwa! Na kikawa.} [36:82];

Hivyo Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) ameamrisha kumtegemea Yeye peke yake, Allah amesema: {… Na mtegemeeni Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi ni Waumini.} [5:23];

Basi ni toshelezo gani analolipata mtu baada ya hilo, atatosheka na Allah Aliyetukuka kuwa ndie wakili wake, Allah amesema: {…na umtegemee Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mtegemewa wa kutosha.} [4:81],

Bila ya shaka hilo litampa utulivu, raha, furaha na kutosheka na kutekeleza mambo ambayo mtu hafahamu isipokuwa yule aliye yajaribu, Allah amesema: {…Na anaye mcha Mwenyezi Mungu humtengezea njia ya kutokea. Na humruzuku kwa jiha asiyo tazamia. Na anaye mtegemea Mwenyezi Mungu Yeye humtosha. Hakika Mwenyezi Mungu anatimiza amri yake. Mwenyezi Mungu kajaalia kila kitu na kipimo chake.} [65:2-3],

Mbali na ulinzi wake Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) anaowapa wanaomtegemea dhidi ya shetani, Allah Aliyetukuka amesema: {Hakika yeye hana madaraka juu ya walio amini na wakamtegemea Mola wao Mlezi.} [16:99],

Na maadui vile vile, Allah amesema: {Walio ambiwa na watu: Kuna watu wamekukusanyikieni, waogopeni! Hayo yakawazidishia Imani, wakasema: Mwenyezi Mungu anatutosha, naye ni mbora wa kutegemewa. Basi wakarudi na neema na fadhila za Mwenyezi Mungu. Hapana baya lilio wagusa, na wakafuata yanayo mridhi Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila kuu. Hakika huyo ni Shet'ani anawatia khofu marafiki zake, basi msiwaogope, bali niogopeni Mimi mkiwa nyinyi ni Waumini.} [3:173-175]

Na siri ya kumtegemea Allah na ukweli wake ni moyo wa mtu kumtegemea Allah peke yake, na hakutomdhuru kuvaana na sababu wakati ambapo moyo wa mtu humtegemea yeye, kama ambavyo kauli ya kusema kwake kuwa nimemtegemea Allah wakati ambapo anamtegemea asiyekuwa yeye, hivyo basi kutegemea kwa ulimi ni sehemu moja na kutegemea kwa moyo ni sehemu nyingine.

6. Furaha ipo kwenye Yakini na Kumtegemea Allah:

Kwa hakika imani inampa muumini yakini na kumtegemea Allah kwa ukamilifu, jambo linalompa mtu kujiamini; hivyo haogopi lolote katika maisha haya, kwa hiyo atajua wakati wake kuwa mambo yote ni ya Allah Aliyetukuka, Allah amesema: {Na ikiwa Mwenyezi Mungu akikugusisha madhara, basi hapana wa kukuondolea hayo ila Yeye. Na ikiwa akikugusisha kheri, basi Yeye ndiye Mwenye uweza wa kila kitu.} [6:17],

Kama ambavyo ana yakini kuwa riziki yake ni kutoka kwa Allah peke yake, Allah

amesema: {Hakika nyinyi mnaabudu masanamu badala ya Mwenyezi Mungu, na mnazua uzushi. Hakika hao mnao waabudu badala ya Mwenyezi Mungu hawakumilikiini riziki yoyote. Takeni riziki kwa Mwenyezi Mungu, na mumuabudu Yeye, na mumshukuru Yeye. Kwake Yeye ndio mtarudishwa.} [29:17],

Na ya kuwa hakuna mnyama aliyepo ardhini ila Allah anadhamini riziki yake, amesema Aliyetukuka: {NA HAKUNA mnyama yoyote katika ardhi ila riziki yake iko kwa Mwenyezi Mungu. Naye anajua makao yake na mapitio yake. Yote yamo katika Kitabu chenye kubainisha.} [11:6],

> “Kuna utafiti unaothibitisha kuwa mtu kuwasaidia wengine ni tiba ya babaiko la nafsi, wataalamu katika saikolojia wanathibitisha kwamba kuwasaidia wengine hupunguza wasiwasi na msongo wa mawazo ambapo kushughulika kwa hima katika kuwasaidia wengine huhamasisha kutoa Homoni aina ya hormone endorphins nayo ni homoni yenye kumsaidia mtu kuhisi raha ya kinafsi na hisia za juu za furaha, Alan Leeks Mkuu wa zamani wa chuo cha “Kukuza Afya” (institute for health promotion) huko Marekani anathibitisha kwamba kuwasaidia wengine husaidia katika kupunguza msongo wa mawazo ambapo mtu kuwasaidia wengine hupunguza mawazo yake yeye mwenyewe binafsi na matatizo yanayomkabili mwenyewe: Na mwisho hupata mwenyewe hisia za raha na utulivu wa nafsi.”

Hata kama hatoweza kuleta riziki yake Allah amesema: {Na wanyama wangapi hawawezi kujimilikia riziki zao! Mwenyezi Mungu anawaruzuku hao na nyinyi pia. Na Yeye ndiye Mwenye kusikia Mwenye kujua.} [29:60],

Na akawa na yakini kuwa riziki yake itamjia bila ya shida na hilo ni jambo la haki lisilokuwa na shaka ndani yake, Allah amesema: {Na katika mbingu ziko riziki zenu na mliyo ahidiwa. Basi naapa kwa Mola Mlezi wa mbingu na ardhi, hakika haya ni kweli kama ilivyo kweli kuwa nyinyi mnasema.} [51:22-23]

Na ya kuwa Yeye Subhaanahu Aliyetukuka amegawa riziki yake kwa watu na akamkadiria, Allah amesema:

{Sema: Hakika Mola wangu Mlezi humkunjulia riziki na humdhikisha amtakaye. Lakini watu wengi hawajui.} [34:36]

Na ataamini imani ya kweli yenye kukata kuwa Allah anampa mtihani daima katika kheri na katika shari, Allah amesema:

{Kila nafsi itaonja mauti; na tunakujaribuni kwa mtihani wa shari na kheri. Na kwetu Sisi mtarejeshwa.} [21:35]

Na kama sio upole wa Allah Subhaanahu basi angeangamia maangamivu makubwa.

Kama ambavyo anajua kuwa yeye ni mgeni katika dunia hii vyovyote umri utakavyokuwa urefu au ufupi, bila shaka yeye atahamia katika ulimwengu mwingine; hivyo basi yeye anatembea katika dunia hii kwa msingi huu, haogopi misiba ya dahari, wala hamuogopi yoyote isipokuwa Allah, hata kama adui yake atakuwa karibu kiasi cha ncha mbili za upinde au zaidi;

Allah amesema:

{Na yalipo onana majeshi mawili haya, watu wa Musa wakasema: Hakika sisi bila ya shaka tumepatikana! (Musa) akasema: Hasha! Hakika yu pamoja nami Mola wangu Mlezi. Yeye ataniongoa! Tulimletea wahyi Musa tukamwambia: Piga bahari kwa fimbo yako. Basi ikatengana, na kila sehemu ikawa kama mlima mkubwa. Na tukawajongeza hapo wale wengine. Tukawaokoa Musa na walio kuwa pamoja naye wote. Kisha tukawazamisha hao wengine. Hakika bila ya shaka katika hayo ipo Ishara; lakini wengi wao si katika wenye kuamini.} [26:61-67].

Hapa tunamuona bwana wa wenye yakini Muhammad (Swala Llahu ‘alayhi wasallam), lau adui yake angeangalia chini ya miguu angemuona, lakini kwa imani na yakini ya Mola wake na wakati huo washirikina wakimuandama ili wamuue - anamwambia sahibu yake Abu Bakr (Radhiya Llahu ‘anhu) akiwa nae pangoni:

{…Usihuzunike. Hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja nasi. Mwenyezi Mungu akamteremshia utulivu wake, na akamuunga mkono kwa majeshi msiyo yaona, na akalifanya neno la walio kufuru kuwa chini, na Neno la Mwenyezi Mungu kuwa ndilo juu. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye nguvu Mwenye hikima.} [9:40].

Kama ambavyo ameyakinisha kuwa Allah ndie ambae amemkadiria mauti hivyo hayaogopi mauti, Allah amesema: {MWENYEZI MUNGU huzipokea roho zinapo kufa. Na zile zisio kufa wakati wa kulala kwake, huzishika zilizo hukumiwa kufa, na huzirudisha nyengine mpaka ufike wakati uliowekwa. Hakika katika hayo bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanao fikiri.} [39:42],

Bali ameyakinisha kuwa huo ndio ukweli halisi ambao hakuna kukimbilia, Allah amesema: {Sema: Hayo mauti mnayo yakimbia, bila ya shaka yatakukuteni. Kisha mtarudishwa kwa Mwenye kuyajua yaliyo fichikana na yanayo onekana. Hapo atakwambieni mliyo kuwa mkiyatenda.} [62:8],

Na kuwa mauti hayaji isipokuwa wakati ule ulioandikwa, Allah amesema:{Na lau kuwa Mwenyezi Mungu angeli wachukulia watu kwa mujibu wa dhulma zao, basi asingeli mwacha hapa hata mnyama mmoja. Lakini anawaakhirisha mpaka muda ulio wekwa. Na unapo fika muda wao hawatakawilia hata saa moja wala hawatatangulia.}[16:61].



Imani na Maisha.

“Imani ni nguvu ambayo hapana budi ipatikane ili iweze kumsaidia mtu maishani. Kukosa kwake ni ilani ya kushindwa kukabiliana na maisha na changamoto zake.”

Ernest Renan
Mwanahistoria wa Kifaransa

Basi Zianguke Staarabu za Vitu

"Imekwisha bainika kuwa Uislamu na misingi yake humletea mtu utulivu katika nafsi yake. Ama ustaarabu wa Maada (vitu) humpelekea mtu kukata tamaa: Kwa sababu wao hawaamini chochote, kama ambavyo imebainika kuwa watu wa Ulaya hawakufahamu Uislamu: Kwani wanapima kwa vipimo vyao vya kimaada."

Roger Du Pasquier

Mwanafikra na Mwanahabari wa Kiswisi.

7. Kuridhika ni mlango wa Njia ya Furaha:

Furaha ni ile hali ya Nafsi ya mtu kuishi kwa kuridhika; kwa hiyo chuki, inda humkaba mtu maisha yake, roho yake na hisia zake, ama kuridhia ni mlango wa furaha, utulivu, ghera na furaha. Kwa hiyo utulivu katika moyo hadi kwenye uchaguzi wa Allah kwa mtu. Kwa hiyo utulivu huu unamfanya mtu kila kinachotokea katika maisha yake kuwa ni kheri kwa mwanadamu, furaha na raha, hivyo hamuangalii mwingine isipokuwa Mola wake tu, wala haoni hasara kwa chochote cha duniani, humfanya mja kufanya kazi kwa bidii na kumuomba Mola wake, kisha huridhika kwa yale Mola wake aliyomgawia; ili aishi maisha ya hali ya kuridhika na mwenye furaha. Kuridhika kuna aina nyingi; miongoni mwa hizo ni:-

Kuridhia kuwa Allah ni Mola na Uislamu ndio dini na Muhammad ni Nabii na Mtume, na ambae hatoridhia kwa hilo basi ataishi katika babaiko daima na maswali tata kila mara, amesema Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam): "Ameonja utamu wa imani atakayemridhia Allah kuwa ni Mola wake na Uislamu kuwa ni dini yake na Muhammad kuwa ni Mtume." (Al-Bukhari).

Na yule ambae hakuonja utamu wa imani basi hajaonja utamu wa furaha, bali ataendelea kuwa katika babaiko na wasiwasi na tabu na kumridhia Allah ina maana kuamini uwepo kwa Allah na kuhisi ukubwa wake, hekima yake, uwezo wake, elimu yake na majina yake mazuri, na imani na kuridhia ibada yake, vinginevyo itakuwa ni shaka, wasiwasi, maradhi na huzuni na sononeko Mwenyezi Mungu utulinde na hayo.

Kuridhia hukumu za Allah na sheria zake, Allah amesema: {La! Naapa kwa Mola wako Mlezi! Hawataamini mpaka wakufanye wewe ndiye muamuzi katika yale wanayo khitalifiana, kisha wasione uzito katika nyoyo zao juu ya hukumu utayo toa, na wanyenyekee kabisa.} [4:65],

Na binadamu amejaribu njia za mashaka mengi, tabu na dhiki nyingi katika maisha yake hapa duniani kwa kutegemea sheria na hukumu na mifumo yenye dhuluma yenye mapungufu; kwa sababu ni katika matengenezo ya mwanadamu na sio katika sheria za Muumba wa watu, mwenye kujua yenye kumfaa mtu, Allah amesema: {Asijue aliye umba, naye ndiye Mjua siri, Mwenye khabari?} [67:14].

Kuridhia hukumu za Allah na Kudura zake Subhaanahu: kwani ana yakinisha kuwa haiwezekani kupata msiba isipokuwa kwa matakwa ya Allah Aliyetukuka, na ya kuwa Allah Aliyetukuka atauongoza moyo wake, Allah amesema: {Haufiki msiba wowote ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu huuongoa moyo wake. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.} [64:11],

Kuwa yeye anaridhika na hukumu ya Allah na kudura zake; kwa sababu anajua (kwa elimu ya yakini) kuwa yoyote haondoshi madhara isipokuwa Mwenyezi Mungu Aliyetukuka, Allah Ta'ala amesema: {Na Mwenyezi Mungu akikugusisha madhara, basi hapana wa kukuondolea ila Yeye. Na akikutakia kheri, basi hapana awezaye kurudisha fadhila yake. Huifikisha kwa amtakaye katika waja wake, na Yeye ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.} [10:107].

Hakika miongoni mwa ajabu ya mambo ya imani ni kuwa muumini anachuma radhi kwa yale Allah aliyomgawia, na hivyo kusubiri juu ya misiba na matatizo, na kushukuru neema na anavyopata, na hili linamungizia ndani mwake kuridhika yale Allah aliyomgawia na hili halipati mwingine asiyekuwa muumini.

Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) amesema: «Ni ajabu jambo la muumini, hakika mambo yake yote ni kheri na hilo haliwi kwa yoyote isipokuwa muumini, akipata yenye kufurahisha anashukuru na hivyo kuwa ni kheri kwake, na akipata lenye kudhuru anasubiri na hivyo kuwa ni kheri kwake.» (Muslim).

Bali Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) ametufundisha namna ya kuridhika hata kama tumemuona aliye juu yetu katika kupata neema na starehe za hapa duniani, amesema Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam): «Waangalieni walio chini yenu na wala msiwaangalie walio juu yenu, kwani hilo litawafanya msidharau neema ya Allah kwenu.» (Bukhari na Muslim).

Roho ya Uislamu.

"Mimi naamini kuwa Uislamu ni dini ambayo huingiza amani na utulivu ndani ya nafsi. Na humfundisha mwanadamu utulivu, kupumzisha akili katika maisha haya. Roho ya Uislamu imetambaa kwenye nafsi yangu: Nikahisi neema ya kuamini hukumu ya mungu na kutokujali athari za Ki-Maada kama vile utamu na uchungu."

Rex Ingram

Muandaaji Sinema maarufu Ulimwenguni.

Huzuni ya kuwa mbali na Njia ya Furaha:

Uislamu umekuja ukiwa ni wenye kufaa mahala na zama zote, unakwenda pamoja na maumbile ya mwanadamu, ukichunga mabadiliko ya maisha, ukienda pamoja na maendeleo na ustaarabu wa mwanadamu.

Uislamu huu ukijishughulisha na kutibu matatizo ya Ummah na mataifa na ukishughulikia uchumi, siasa, hali zao za kijamii na kivita na mengineyo; isipokuwa ni kwamba watu wengi wamepotea njia hii yenye mwanga, na wengine wakaupiga vita na wakaamua kuchafua sura yake ili wawaweke watu mbali nayo.

Hili ndilo ambalo limewasababishia watu wengi matatizo miongoni mwa watu na jamii mbali mbali ulimwenguni; Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) amemdhamini atakayefuata uongofu wake na kushikamana na sheria yake kupata furaha ya nyumba zote mbili na akawahukumia tabu na mashaka na udhalili na unyonge kwa atakayeupa mgongo na kuwa na kiburi.

Uislamu huu ndio ambao Allah amemkalifisha nayo mwanadamu ili mambo yake yanyooke, ili afurahi hapa duniani na huko akhera na asipate tabu na mashaka ya kuwepo duniani na kupata malipo mema akhera, hata hivyo nafsi ya mwanadamu (kwa tabia yake) haipendi majukumu na kufungwa kwa matamanio yake na vitu avipendavyo, hata kama majukumu haya ni kwa maslahi yake mwenyewe; na ndio maana Allah amewafaradhishia watu wa haki kulingania kheri na haki waliyoongozwa kwayo, na waibebe haki hiyo kwa walimwengu wote. Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) alitumwa ili afurahi na awafurahishe kaumu yake na watu wote ulimwenguni, Allah Aliyetukuka amesema: {Hatukukuteremshia Qur'ani ili upate mashaka. } [20:2]

Na akasema vile vile: {Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote.} [21:107],

Hivyo basi kumfuata Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) na kushikamana na njia yake ni chanzo cha furaha na njia ya kuokoka, na ni njia ya maisha ambayo Allah ametuamrisha tuyaishi katika jumla ya kushikamana na maamrisho yake na kukatazika na makatazo yake hayo matunda yake ni furaha katika nyumba zote mbili (duniani na akhera), na kutoka katika mipaka hii matokeo yake ni tabu na mashaka duniani na akhera, amesema kweli Allah pindi aliposema: {Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu. Aseme: Ewe Mola wangu Mlezi! Mbona umenifufua kipofu, nami nilikuwa nikiona? (Mwenyezi Mungu) atasema: Ndivyo vivyo hivyo. Zilikufikia ishara zetu, nawe ukazisahau; na kadhaalika leo unasahauliwa. } [20:124-126].

Mwanga wa Uislamu

“Ni vizazi vingapi ambavyo vitapambana na hofu na tabu, kabla kuibuka tena kwa mwanga mpya wa Uislamu mtukufu ambao inadhihirika kuwa Historia nzima inaelekea upande wake. Wakati huo amani itafunika dunia na nyoyo za watu.”

H. G. Wells

Mwandishi na Mwanafasihi wa Kiingereza.

Tofauti kubwa iliyopo kati ya muumini ambaye Allah amesema juu yake: {… tutamhuisha maisha mema….} [16:97]

Na mwenye kuupa mgongo ukumbusho wa Allah ambae Allah amesema juu yake: {…basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki} [20:124],

Hivyo basi maisha mazuri yanakuwa kwa mtu kushikamana na maamrisho ya Allah na kukatazika na makatazo yake kwa siri na dhahiri, na moyo kutulia kwa hukumu za Allah; kwa sababu anaishi kwa stara yake Allah na uangalizi wake Allah Aliyetukuka amesema: {Wale walio amini na zikatua nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndio nyoyo hutua!} [13:28]

Na hivyo basi utulivu ule wa moyo ukaakisi katika matendo ya mwanadamu katika mambo yote yanayokwenda kinyume kabisa na yule anayeishi maisha ya dhiki na tabu kama ilivyo katika kauli yake Allah Aliyetukuka: {Basi yule ambaye Mwenyezi Mungu anataka kumhidi humfungulia kifua chake kwa Uislamu. Na anaye taka apotee hukifanya kifua chake kina dhiki, kimebana, kama kwamba anapanda mbinguni. Namna hivi Mwenyezi Mungu anajaalia uchafu juu ya wasio amini.} [6:125],

Hivyo basi dhiki na tabu yake ya maisha yake sio kwa sababu ya ufukara na sio kwa sababu ya maradhi, lakini hali ya wasiwasi katika matendo yake au katika maamrisho yoyote yanatokana na kupupia kwake dunia kwa mtu aliye na huzuni au kuupa kwake mgongo hakumuondoshi katika duara lake la mashaka na tabu zake, na sio sababu za mashaka aliyonayo, bali sababu yenyewe ni namna anavyofikiri na njia ya kufikiri kwake, hivyo basi ziada ya mali yake au upungufu wake na siha yake au maradhi yake huenda ikawa ni sababu ya kuongezeka kwa mashaka yake Allah Aliyetukuka amesema: {Yasikufurahishe mali yao wala wana wao. Hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwaadhibu kwayo hapa duniani, na zitoke roho zao na hali wao ni makafiri.} [9:55],

Na akasema vile vile: {Wala zisikushitue mali zao na watoto wao. Mwenyezi Mungu anataka kuwaadhibu kwa hayo katika dunia; na zitoke roho zao na hali wao ni makafiri.} [9:85].

Tabu na mashaka ayapatayo mwanadamu hayahusiani na utajiri au umasikini, wala maradhi au mitihani, bali tabu na mashaka ni mtu kuwa mbali na Allah na kupotoka na njia yake, na mja kukata kabisa mahusiano yake na Allah, Zakaria ('Alayhi Salaam) alipomuomba Mola wake alisema: {…sikuwa mwenye bahati mbaya kwa kukuomba Wewe.} [19:4]

Hapo kabla alinikirimu kwa kuitikia dua yangu na kunifanya ni mwenye furaha kwa kunijibu.

Jambo hili halimuhusu Zakaria ('Alayhi Salaam) pekee bali Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) ametujulisha aliposema Subhaaanahu: {Na waja wangu watakapo kuuliza khabari zangu, waambie kuwa Mimi nipo karibu. Naitikia maombi ya mwombaji anapo niomba. Basi na waniitikie Mimi, na waniamini Mimi, ili wapate kuongoka.} [2:186].

Madamu kuna kamba inayomuunganisha mja na Mola wake moja kwa moja, basi furaha ataipata na kufanikiwa, na mashaka na tabu atapata pindi akikata kamba hii, na kwa kadiri mwanadamu atakapokuwa na mapungufu katika kuihukumu nafsi yake kwa dini hii ndio kadiri inapoangukia tatizo na wasiwasi katika nafsi na maisha yake. Kwa hili ndio maana Allah anaambatanisha baina ya Uongofu na rehema, upotofu na tabu, ya kwanza ni kauli yake: {Hao wapo juu ya uwongofu utokao kwa Mola wao Mlezi, na hao ndio walio fanikiwa. } [2:5].

Na kauli yake : {Hao juu yao zitakuwa baraka zitokazo kwa Mola wao Mlezi na rehema. Nao ndio wenye kuongoka.} [2:157]

Na kauli yake: {….Na ukikufikieni uwongofu kutoka kwangu basi atakaye ufuata uwongofu wangu, hatapotea wala hatataabika.} [20:123],

Na uongofu: kumkataza na upotofu, na Rahma: kumkataza au kumuepusha mashaka na tabu, na hili ndilo alilolitaja Allah mwanzoni mwa Surat Twaha katika kauli yake Allah: {T'AHA! Hatukukuteremshia Qur'ani ili upate mashaka.} [20:1-2].

Hivyo akakusanya kati ya kumteremshia Qur-aan na kuondosha mashaka kwake, kama alivyosema mwisho wa sura kuhusu wafuasi wake: {…hatapotea wala hatataabika.} [20:123],

Hivyo basi uongofu na ubora na neema na rehema ni yenye kulandana hazitengani, kama ambayo upotofu, mashaka ni yenye kulandana na hayatengani, Allah amesema: {Hakika wakosefu wamo katika upotofu na wazimu.} [54:47],

Na su'ur ni wingi wa sa'iyr; nayo ni adhabu ambayo ni kilele cha tabu na mashaka na kwa mkabala wake ni mwisho mbaya wa waovu

Allah amesema kuhusu marejea ya wacha-Mungu katika sura hiyo hiyo: {Hakika wachamngu watakuwa katika Mabustani na mito. Katika makalio ya haki kwa Mfalme Mwenye uweza.} [54:54-55]

Hii ndio njia ya furaha ikiwa utataka kuifuata na kujipamba nayo, ni njia ambayo haisimami kwa upotofu na uzushi katika dini, kiroho au fikra tupu, ni njia ya Furaha, nayo ni njia vile vile ya elimu na ustaarabu.

Mwokozi wa Binadamu

"Kwa hakika ni katika Uadilifu Muhammad kuitwa, "Mwokozi wa Wanadamu". Naamini kuwa mtu mfano wake lau angetawala ulimwengu huu leo hii angefanikiwa kutatua matatizo yake na hivyo furaha na amani ingechukua nafasi yake."

Sir George Bernard Shaw

Mwandishi wa Kiingereza.





https://www.path-2-happiness.com/sw

الطريق إلى السعادة
The Path to Happiness

NJIA YA ELIMU NA USTAARABU

https://www.path-2-happiness.com/sw

Yaliyomo

NJIA YA ELIMU NA USTAARABU

Njia ya Elimu na Ustaarabu

Uislamu na Elimu

Njia ya Ustaarabu

Vipengele vya Njia ya Ustaarabu

Miujiza ya Qur’an na Sunnah

https://www.path-2-happiness.com/sw

NJIA YA ELIMU NA USTAARABU

UISLAMU NA ELIMU

Hapana shaka kuwa Njia ya Furaha hapana budi kupita katika njia za elimu na ustaarabu, haiwezekani kwa hali yoyote kupita katika mabonde ya ujinga, na haipatikani dini wala fikra ambayo imenyanyua hadhi ya wanazuoni na kuheshimu miamala yao na kuhimiza kutafuta elimu na kuitumia akili na kulingania katika mazingatio na kufikiria kama mfano wa dini ya Uislamu aliokuja nao Mtume Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) ambae alijenga ustaarabu mkubwa ulioenea mashariki ya ardhi na magharibi yake.

Kwa hali hiyo kutumwa kwake Swala Llahu 'alayhi wasallam kunahesabiwa kuwa ni mapinduzi ya kweli ya kielimu katika mazingira ambayo roho ya kielimu imeyazoea, Kwa hiyo Uislamu ukaja ili elimu ianze, na dunia ing'are kwa nuru ya uongofu wa Mwenyezi Mungu, Akasema Aliyetukuka: {Je, wao wanataka hukumu za Kijahiliya? Na nani aliye mwema zaidi katika kuhukumu kuliko Mwenyezi Mungu kwa watu wenye yakini?} [5:50].

Hakuna nafasi ya ujinga kwenye dini hii au dhana au shaka, aya ya kwanza kushuka kwa Nabii Umiyyi (Swala Llahu 'alayhi wasallam): {Soma kwa jina la Mola wako Mlezi aliye umba, Amemuumba binaadamu kwa tone la damu, Soma! Na Mola wako Mlezi ni Karimu kushinda wote! Ambaye amefundisha kwa kalamu. Kamfundisha mtu aliyo kuwa hayajui.} [96:1-5].

Ikawa wazi kuwa maudhui ya kwanza ni ufunguo wa kufahamu dini hii, na ni ufunguo wa kufahamu dunia hii, bali kufahamu akhera ambayo ni marejeo ya watu wote.

https://www.path-2-happiness.com/sw

Atakayeangalia jinsi Qur-aan ilivyojali kadhia ya elimu haimdhihirikii katika mazingatio ya mwanzo kuteremshwa kwake tu, lakini ilikuwa tokea kuumbwa kwa mwanadamu mwenyewe, kama Qur-aan yenyewe ilivyolieleza hilo katika aya zake; Allah amemuumba Adam na kumfanya khalifa katika ardhi, akaamuru Malaika kumsujudia, akamkirimu na kumtukuza na kumnyanyua, kisha akatutajia sisi na Malaika sababu ya heshima, utukufu na kunyanyuliwa huku; akaainisha kuwa ni elimu Allah, Aliyetukuka amesema: {Na pale Mola wako Mlezi alipo waambia Malaika: Mimi nitamweka katika ardhi Khalifa (mfwatizi), wakasema: Utaweka humo atakaye fanya uharibifu humo na kumwaga damu, hali sisi tunakutakasa kwa sifa zako na tunakutaja kwa utakatifu wako? Akasema: Hakika Mimi nayajua msiyo yajua. Na akamfundisha Adam majina ya vitu vyote, kisha akaviweka mbele ya Malaika, na akasema: Niambieni majina ya hivi ikiwa mnasema kweli. Wakasema: Subhanaka, Wewe umetakasika! Hatuna ujuzi isipokuwa kwa uliyo tufunza Wewe. Hakika Wewe ndiye Mjuzi Mwenye hikima. Akasema: Ewe Adam! Waambie majina yake. Basi alipo waambia majina yake alisema: Sikukwambieni kwamba Mimi ninajua siri za mbinguni na za duniani, na ninayajua mnayo yadhihirisha na mliyo kuwa mnayaficha?} [2:30-33].

Soma… Huu Ndio Mwito wa Uislamu

"Hapana shaka kuwa Uislamu (ambayo ni dini ya elimu na maarifa) inawalingania wenye kuikumbatia katika kutafuta elimu na kuitumia, wala hakuna ajabu katika hilo. Kwani Ayah ya mwanzo katika Qur-aan Tukufu ni kauli yake Allah Ta'ala: "Soma kwa jina la Mola wako Aliyeumba."

Robert Pierre Joseph

Profesa wa Falsafa katika Vyuo Vikuu vya Ufaransa.

Kinachoashiria umuhimu wa elimu na thamani yake katika Uislamu ni kuwa si tu kuwa tokea mwanzo katika Qur-aan imezungumzia masuala ya elimu katika kauli yake Allah {Soma}

bali huu ndio mfumo uliothibiti katika katiba hii ya milele, hivyo hakuna sura yoyote miongoni mwa sura zake zenye kuzungumzia elimu, iwe ni kwa njia ya moja kwa moja au isiwe ya moja kwa moja, Allah ameamrisha elimu katika jambo kubwa lenye kushuhudiwa nalo ni kumpwekesha Allah Aliyetukuka; katika kauli yake Allah Ta'ala: {Basi jua ya kwamba hapana mungu ila Mwenyezi Mungu, na omba maghufira kwa dhambi zako na za Waumini wanaume na Waumini wanawake. Na Mwenyezi Mungu anajua mahali penu pa kwenda na kurudi, na mahali penu pa kukaa.} [47:19],

Kwa hiyo ikaonyesha juu ya ukubwa wa ubora wa elimu na watu wake, imekana kulinganisha kati ya mwenye kujua na asiye jua: {…Sema: Ati watakuwa sawa wale wanao jua na wale wasio jua? Hakika wanao kumbuka ni watu wenye akili.}[39:9].

Bali Allah amewanyanyua ambao wamepewa elimu daraja la juu duniani, mbali na thawabu huko akhera. Allah amesema:{…Mwenyezi Mungu atawainua walio amini miongoni mwenu, na walio pewa ilimu daraja za juu. Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda.} [58:11],

Msikiti…Chuo Kikuu

"Ndivyo misikiti ilivyokuwa hapo kabla (hata leo hii baadhi yake) imekuwa ni vyuo vikuu vya Kiislamu: Ni mshangao mkubwa kwa wanafunzi waliojawa na hamu katika elimu. Wanafunzi ambao wamekuja kusikiliza mihadhara ya wanazuoni katika elimu za dini, sheria, falsafa, tiba na hesabu. Na kwa hakika wanazuoni wenyewe wamekuja kutoka pande zote za Ulimwengu ambao walikuwa wakizungumza lugha ya Kiarabu, nao walikuwa wakimkaribisha kila mwanafunzi bila kujali utaifa wake."

Stanley Lane-Poole

Mwanazuoni wa Uingereza.

https://www.path-2-happiness.com/sw

Ikutoshe kuwa haipatikani katika Qur-aan kusisitizwa juu ya kuomba ziada ya kitu chochote isipokuwa katika elimu, Allah amesema: {…Na sema: Mola wangu Mlezi! Nizidishie ilimu.} [20:114],

Wala haikuwa amri ni kwenye mlango wa kuzidisha pindi Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) aliposema: «Atakayefuata njia ya kutafuta elimu Mwenyezi Mungu atamrahisishia njia ya peponi, na kuwa Malaika wanaweka mbawa zao kwa kuridhia mtafuta elimu, na kuwa mtafuta elimu wanamuombea msamaha waliomo mbinguni na ardhini, hata nyangumi baharini, na kuwa ubora wa mwanazuoni juu ya mshika ibada (mwenye kuabudu) ni kama ubora wa mwezi kwa sayari nyinginezo, kwa hakika wanazuoni ni warithi wa Mitume, kwani Mitume hawarithiwi dinari wala dirhamu bali hurithiwa elimu, kwa hiyo atakayeichukua amechukue hadhi kubwa.» (Muslim). Na hivyo basi baada ya kutumilizwa kwake misikiti ikawa ndio kasri ya elimu na wanazuoni.

Jambo kubwa la kushtua ni pale utakapohesabu idadi ya neno "Elimu-'Ilmu" na vitoheo vyake tofauti vilivyokuja kwenye kitabu cha Allah; unapata idadi yake kufikia mara mia saba na sabini na tisa (779); kwa wastani wa mara saba kwa kila sura ya Qur-aan! Hii ni kuhusu neno elimu,

Qur-aan na Sayansi

"Qur-aan imekusanya ndani aya bainifu katika elimu ya mazingira (sayansi) zilizotolewa na Pro Yusuf Marwa katika kitabu chake, "Sayansi katika Qur-aan." Na ikafikia aya mia saba na sabini na nne. Na maelezo yake ni kama ifuatavyo: Hesabu aya sitini na moja, Fizikia aya mia mbili na sitini na nne, atom aya tano, Kemia aya ishirini na tisa, Vipimo vya mwendo aya sitini na mbili. Hali ya hewa aya ishirini, maji aya kumi na nne, elimu ya anga aya kumi na moja, elimu ya wanyama aya kumi na mbili, kilimo aya ishirini na moja, elimu ya viumbe hai aya thelathini na sita, Jiografia aya sabini na tatu, elimu ya nasaba za watu aya kumi, elimu ya tabaka za ardhi aya ishirini na elimu kuhusu ulimwengu na historia ya matukio yake aya thelathini na sita."

Maurice Buccaile

Mwanazuoni na tabibu wa Kifaransa.

hata hivyo kuna maneno mengi yenye kuashiria maana ya elimu lakini hayakutajwa kwa tamko lenyewe; mfano: Yakini, uongofu, akili, kufikiri, kuangalia, hekima, fiqhi (kujua), Burhani, dalili, hoja, aya (alama) ubainifu na mengineyo yasiyokuwa hayo katika maana yanayotokana na elimu na kuhimiza elimu yenyewe, ama sunnah ya Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) kuhesabu neno hili ni vigumu kwa wingi wa ilivyoelezwa.

Qur-aan sio kitabu cha Physics, Chemistry, Biology au hesabu, bali ni kitabu cha Uongofu pamoja na hayo haukusaza chochote kulichothibitishwa na sayansi ya kisasa.

Hayo yalikuwa na athari kubwa katika dola ya Kiislamu baada ya hapo; kwani kulikuwepo na harakati kubwa kabisa za kielimu katika nyanja zote za elimu na mataifa, harakati na nguvu ambazo hazijawahi kuwepo mfano wake katika historia; jambo ambalo lilifanya ustaarabu na maendeleo makubwa kufikiwa katika mikono ya wanazuoni wa Kiislamu, na kumpa urithi binadamu kwa silaha nzuri za elimu ambayo dunia nzima inadaiwa na Uislamu.

MarxMarhaaf anasema: "Maendeleo ya Chemistry Ulaya yanarejewa kwa Jabir bin Hayyan moja kwa moja, na dalili kubwa ya hilo ni kuwa Istilahi nyingi alizozigundua bado hutumika katika lugha mbali mbali za Ulaya."

Ama Aldo Mieli anasema: "Na tukihamia katika elimu ya sayari (astronomy), tokea mwanzo tutawaona wanazuoni wa sampuli ya kwanza, na miongoni mwa wanazuoni hao maarufu ni Abu Abdullah Muhammad bin Musa Al-Khawarizmy.(Mwanzilishi wa elimu ya Aljebra na kujua mfumo wa idadi ya kihindi na ameweka misingi ya tafiti za hesabu, elimu za unajimu (astronomy) na Jiografia.)

Al- Khawarizmy alikuwa ndie mfunguzi wa mnyororo wa wanazuoni wakubwa wa mahesabu, na vitabu vyake viliendelea kusomeshwa katika vyuo vikuu vya Ulaya hadi karne ya kumi na sita."

Zaghrid Honka amesema katika juzuu maalumu kuhusu operesheni katika kitabu: "Ubainifu kwa aliyeshindwa kutunga." Cha mwandishi: Az-Zahrawy; (Ni kitabu kinachokusanya maarifa yote ya tiba katika mijaladi thelathini. Kina picha mbali mbali, na maumbo ya vyombo na vifaa alivyokuwa akitumia mwandishi wake Az-Zahrawiy katika operesheni zake, kimefasiriwa na Gerald Al-Karmuni juzuu maalumu inayohusiana na mas-ala ya operesheni katika kitabu hiki kwa lugha ya kilatini katika karne ya kumi na mbili Miladiy. Chapa mbali mbali zilishatoka hapo zamani, ya kwanza huko Bundukia (Venice) mwaka 1497 AD. Na ya pili ni huko Bazli mwaka 1541 AD na ya tatu Oxford mwaka 1778 AD kama ambavyo Dr. Lucklirk alifasiri katika lugha ya kifaransa katika karne ya kumi na tisa.) (sehemu ya tatu ya kitabu hiki kimekuwa na nafasi muhimu sana Ulaya ambapo paliwekwa misingi ya operesheni Ulaya, tawi hili la tiba likawa lipo kileleni, hivyo masuala ya opereseniyakawa yanajitegemea katika misingi yake katika elimu za upasuaji."

Kitabu cha Az-Zahrawy kilikuwa na athari kubwa katika kuinyanyua Ulaya kwa muda wa karne tano, ambapo kilikuwa kikifundishiwa katika vyuo vikuu vya Ulaya, kama ambavyo wapasuaji wengi wa Ulaya wakidondoa humo na kuchukua.

Bado wanazuoni wa Kiislamu waliendelea kutoa michango yao kwa wanadamu wote; Ahmad Zuwayl (Huyu ni mwanakemia wa Kimisri, aliwahi kupata zawadi ya Nobel mwaka 1999AD kwa ugunduzi wake wa Camera ya kuchambua spectra (mpangilio maalum wa taswira zinazotokana na miali ya mnunurisho), Kamera ambayo inafanya kazi kwa spidi ya Femtosecond (Femtosecond Spectroscopy). Na utafiti wake kuhusu maingiliano na kikemia kwa matumizi yake. Hii imesaidia ulimwengu kuingia katika mas-ala ambayo mwanadamu hakuweza kutaraji kuyafahamu, ili kuweza kuona na kufahamu harakati za vitu vidogo sana wakati wa muingiliano wa kikemia kwa njia ya Teknolojia ya Laser kwa njia ya haraka zaidi. Dr. Ahmad Zewail aligundua mfumo wa upigaji picha wa haraka zaidi inatumika kwa njia ya laser, yenye uwezo wa kufuatilia harakati za protons wakati wa kukua kwake na wakati wa kukutana pamoja, na unit ya muda ambayo picha inapiga ni hiyo Femtosecond, nayo ni sehemu ya Bilioni ya sehemu ya sekunde.) anasema: katika kitabu chake, Zama za Elimu: (kazi yangu kubwa ilikuwa ikiangukia kwenye sehemu maalum

Mapenzi ya kuelimika.

"Haikuwahi kutokea katika Historia ya maendeleo Ulimwenguni harakati yenye kufurahisha kuliko mapenzi ya ghafla ya utamaduni. Kama ilivyotokea katika sehemu zote za ulimwengu wa Kiislamu: Ikawa kila Muislamu kwa khalifa kuwa ni msanii (mtengenezaji) kama kwamba ghafla tu amekumbwa na shauku ya elimu na kiu ya safari (kutafuta elimu). Haya yakawa ni mambo ya kheri Uislamu ulioyaleta kutoka pande zote. Wanafunzi walisongamana katika vituo kama vile Baghdad. Na baada ya hapo katika vituo vingine ambavyo vilikuwa ni mbeleko ya adabu na elimu, mfano wake ni harakati mpya za wanazuoni wa ulaya ambao walifurika katika vyuo vikuu kuchukua elimu mpya. Bali kwa hakika lilikuwa ni jambo zuri."

Stanley Lane-Poole

Mustashrik wa Uingereza.

katika moyo wa atoms, ambapo kuna kukutana na kuna kuachana kwa vitu katika milango ya fahamu, kama ambavyo muda ulivyo ndani ya sekunde; ambapo sekunde huwa ni muda mkubwa."

Wala hakuna ubishi kuwa elimu hii, uongofu, na nuru aliyokuja nayo Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) imemtoa mwanadamu kutoka katika makutano ya maji ya Asina (yaliyobadilika rangi), hivyo akainyanyua kwa elimu, ustaarabu na utamaduni kwa muda wote wa historia.

Uislamu ukaja kwa mfumo wa kielimu na kisayansi, kwa mfano Uislamu unahadharisha kuiga kibubusa bila kutumia akili; anasema Subhaanahu kuhusu washirikina: {…wao husema: Bali tutafuata tuliyo wakuta nayo baba zetu. Je, hata ikiwa baba zao walikuwa hawaelewi kitu, wala hawakuongoka?} [2:170],

Na kufuata dhana bila kufuata mfumo wa kielimu; Allah Aliyetukuka amesema: {… Hawa hawafuati ila dhana tu, na hawakuwa ila ni wenye kusema uwongo tu.} [6:116]

Na kuhusu matamanio ambayo yanakwenda kinyume na elimu, mantiki, akili na utafiti; Allah amesema: {…Na hakika wengi wanapoteza kwa matamanio yao bila ya kuwa na ilimu….} [6:119],

Na kuhusu bughudha na chuki ambayo inamuweka mtu mbali na uadilifu amesema: {…Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutofanya uadilifu. Fanyeni uadilifu. Hivyo ndio kuwa karibu mno na uchamngu. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda.} [5:8],

Ustaarabu wa Elimu

"Kila tunapoangalia kwa kina ustaarabu wa Waarabu, vitabu vyao vya kielimu. Uvumbuzi wao, fani zao, inadhihiri kwetu ukweli mpya na upeo mpana. Na kwa haraka tumewaona Waarabu kuwa ndio watu bora katika karne za kati (Middle age) kuwa na maarifa kwa ajili ya elimu za waliotangulia.
Kwa muda wa karne tano vyuo vikuu vya Magharibi (Ulaya) vilitegemea vyanzo vya elimu na machapisho ya Waarabu. Nao ndio ambao waliiendeleza Ulaya kwa akili na tabia njema. Historia haijawahi kufahamu Ummah uliozalisha kama walivyozalisha Waarabu (Waislamu) kwa muda mfupi na hakuna watu wengine waliowafikia katika uvumbuzi na fani zingine."

Gustaf Lubon

Mwanahistoria wa Ufaransa.

https://www.path-2-happiness.com/sw

Qur-aan ni Miujiza

"Kwa hakika nimefuatilia aya zote za Qur-aan ambazo zina uhusiano na sayansi na mazingira nikazikuta kwamba aya hizi zinakubaliana na elimu zetu mpya.
Nimeyakinisha kuwa Muhammad (Swala Llahu 'alayhi Wasallam) amekuja na ukweli ulio wazi kabla ya miaka elfu moja, na kabla ya kuwepo mwalimu yoyote miongoni mwa wanadamu. Lau kila mwenye elimu au fani angelinganisha vizuri aya zote za Qur-aan zinazohusiana na alichokisoma, kama nilivyolinganisha bila shaka angetii Qur-aan, ikiwa ana akili ameepukana na hisia za chuki."

Rene Guenon

Mwanafalsafa wa Kifaransa

Na kuhusu uwazi wa usio na upendeleo kuhusu elimu; Allah Ta'ala amesema kuhusu Mayahudi: {Miongoni mwa Mayahudi wamo ambao hubadilisha maneno kuyatoa mahala pake, na husema: Tumesikia na tumeasi…} [4:46]

Na kuhusu kutofanya dhuluma na uharibifu amesema Aliyetukuka: {Bali lawama ipo kwa wale wanao wadhulumu watu, na wanafanya jeuri katika nchi bila ya haki. Hao watapata adhabu iliyo chungu.} [42:42]

Na kuhusu amana ya kielimu pamoja na uadilifu baina ya watu; amesema: {…Na mnapo hukumu baina ya watu mhukumu kwa uadilifu….} [4:58],

Na uadilifu, unyoofu na kushuhudia haki; Amesema: {Enyi mlio amini! Kuweni wenye kusimamisha uadilifu, mtowao ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, ijapo kuwa ni juu ya nafsi zenu…} [4:135],

Ama kuhusu umuhimu wa utafiti wa dalili na hoja amesema: {Sema Leteni hoja zenu kama nyinyi ni wasema kweli.} [27:64]:

Na mengi yasiyokuwa hayo yenye kujenga na kutengeneza mfumo wa kisomi kwa njia ya sayansi na ustaarabu.



NJIA YA USTAARABU

Hakuna umma, kundi, taifa iwe ni la kijima au la kisasa, ambalo litakuwa na utamaduni ambao unawaunganisha na kuwapa tabia pambanuzi, utamaduni ni njia katika kuishi, ni sehemu ya maisha na uwepo, ni mfumo wa maadili na kijamii ambayo yanahukumu mandhari ya maisha na vipengele vyake vyote, hili linaakisiwa katika mambo ya nguvu na tabia zote na kuipa jamii kitambulisho chake na kuhifadhi mshikamano wake.

Mfumo Bora

"Uislamu ulifanikiwa: Kwa sababu ulikuwa ni mfumo bora wa Kijamii na kisiasa ambao siku ziliweza kuutanguliza (mbele). Nao ulisambaa. Kwa sababu kila ulipokwenda ulikumbana na mataifa yaliyokuwa nyuma kisiasa. Mataifa ambayo yalikuwa yakinyang'anya raia zake, yakidhulumu na yakiwahofisha wala hayakusoma wala kuwa na utaratibu wowote, vile vile ulikuta serikali hizo zina ubinafsi na ugonjwa hazina uhusiano baina yake na watu wake. Hivyo Uislamu ukabaki ndio fikra safi zaidi ya kisiasa na utendaji mzuri ulimwenguni hadi muda ule ulikuwa ukiwatumikia watu kwa mfumo bora kuliko nidhamu yoyote nyingine. Ama mfumo wa Kibepari ulikuwa ukiwafanya watu kuwa ni watumwa katika ufalme wa Roma. Elimu, fasihi na taratibu na ada na kijamii huko Ulaya zilikwisha anguka kabla ya Uislamu kuibuka."

H. G. Wells
Mwandishi

Ama ustaarabu huu ni wasifu wa ziada wa uwepo kwa utamaduni wa kijamii ambao unabeba maana ya maendeleo, na kupanda (kuendelea) kwa pande zote mbili ya aina na idadi, na hivyo kupata mafanikio katika uhalisia wa mambo, ni hatua inayoonekana katika athari ya mazingira katika historia yenye uwezo wa kutengeneza matukio yake na kuyaelekeza, harakati zinaweza kufikia kiasi cha kutengeneza bonde linatotenganisha zama na mahali.

Na hivi ndivyo ambavyo ustaarabu unavyowakilisha hakuna mfano wake katika tabia na mazingira, siasa na dini, utamaduni na sayansi na Akhlaqi, vipengele vyote hivi tunaviona vikitoka katika chombo kimoja nacho ni ustaarabu wa watu hawa au wale kwa tabia zao za kipekee.

Uislamu umefanikiwa kubadilisha nafsi za kundi la mwanzo lililoamini kutoka katika maisha ya kibedui ambayo ilikuwa yakitawaliwa na kasumba na kuwa nyuma na kuwafanya kupambika kwa tabia tukufu na kwa muda mfupi maendeleo na ustaarabu ukasambaa duniani na watu wengi wakaitikia kwenye ustaarabu huu wakati ule kwa wepesi wa dini aliyobashiriwa nayo Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam), uadilifu, udugu na usawa, ustaarabu huu ulikuja wakati ambapo binadamu alikuwa amekwisha choshwa na mfumo wa zamani uliosimamishwa kutokana na

utumwa na udikteta, kwa hiyo wakaukumbatia mfumo mpya ambao ndani yake waliona utukufu na utu wao baada ya kuonja dhulma na ukandamizaji chini ya wafalme, makuhani na utawala wa kidikteta wa mtu mmoja.

Kwa hiyo Uislamu ukawa ndio fursa yao ya dhahabu, kwani Uislamu huo ulitengeneza mambo yao mengi na ndani yake wakaona maisha matukufu ambayo walikuwa wakiyatamani, na wakati huo huo ikawaondoshea dhuluma, ujinga na ujima.

Ustaarabu wa Kiislamu umeheshimu mtazamo wa binadamu; haukuwahi kumtofautisha hata siku moja kati ya mtu na nduguye, kwa misingi ya ubaguzi wa rangi au lugha, bali umewapa wote muamala mmoja na haki sawa kwa wote, na hivyo Ustaarabu ukachangia maendeleo ya wanadamu baada ya kubadilisha mfumo wa kikabila ambao unasimama katika uhusiano wa damu na nasaba kuelekea katika mfumo wa kundi unaoshirikiana katika itikadi na fikra ambayo inasimama katika mashirikiano ya kijamii kwa misingi ya udugu na usawa.

Lengo la kwanza la Ustaarabu kwa mtazamo wa Uislamu ni kufanikisha utulivu, usalama na amani na kusimamisha jamii bora na kuwafurahisha wanadamu katika yaliyokuwa ya kheri, kadhalika kupiga vita matendo yote ya shari; ambapo maendeleo yote, ustaarabu na tamaduni zote lengo lake sio ustaarabu wenyewe kwani malengo halisi ya ustaarabu sahihi ni kufikia katika furaha ndani ya nafsi ya mwanadamu na utulivu katika moyo wake na kwenda pamoja katika kufikia amani na maendeleo ya jamii pamoja na mataifa, na



Miongoni mwa Alama za Kughurika.

“Hakika ni wakati muafaka kufanya utafiti kuhusu athari za Kiislamu juu ya Ulaya kwa wakati huu ambapo uhusiano kati ya Waislamu na Wakristo Waarabu pamoja na Wazungu wa Ulaya unaongezeka katika ulimwengu huu mmoja. Kwani imewahi kuonekana wakati fulani kabla katika karne za kati waandishi Wakristo wa Ulaya walitengeneza sura chafu kuhusu Uislamu katika maeneo mengi: Hata hivyo kwa fadhila za jaribio la watafiti katika karne iliyopita sura sahihi zaidi ya kuangalia mambo kwa mtazamo usio na upendeleo imeanza kutengenezwa katika akili za watu wa Magharibi: Na kwa sababu ya kuwepo mahusiano mzuri na Waarabu na Waislamu basi ni juu yetu kutambua fadhila zote tulizofanyiwa na Waislamu. Ama jaribio letu la kukana hayo ni alama miongoni mwa alama za uongo za kudanganyika.”

W. Montgomery Watt

Mustashrik wa Uingereza.

hilo kupitia kufikia katika yaliyokuwa ya kheri na yenye manufaa na kuwa mbali na kila yaliyokuwa ya shari na yenye kudhuru

ambayo ni kinyume na ustaarabu wa kisasa ambayo umemuongezea mwanadamu khofu na wasi wasi na kumswaga mwanadamu katika upotofu wa kimaada unaoangamiza na kuwa mbali na tabia njema, fadhila na dini na mfano wake katika thamani za utu wa mwanadamu, hali ambayo (kwa ustaarabu mambo leo) umemfanya mwadamu kuwa ni chombo (mashine) kisichokuwa na roho ambayo mwenye nguvu humsaga mnyonge.

Kuanguka kwa Ulimwengu.

"Magharibi kwa sasa wana haja ya Uislamu kuliko muda wowote uliopita ili kuyapa maisha maana na historia makusudio yake, hadi Wamagharibi waweze kubadili tabia yao ya kutenganisha kati ya elimu na imani. Uislamu hauweki kizuizi kati ya elimu na imani, bali kinyume chake unaunganisha baina yake kwa kuzingatia kuwa hicho ni kitu kimoja kisichowezakugawanyika. Kama ambavyo inawezekana kwa Uislamu kurejesha uhai wa matarajio ya jamii yetu mpya iliyoathirika na upweke (ubinafsi) wa njia ambayo inaupeleka ulimwengu kwa ujumla wake kuanguka."

Marmaduke Picthall

Mwanafasihi na Mwanafikra Mwingereza

Mafanikio ya Kielimu

"Uislamu umepata mafanikio makubwa ya kielimu zaidi ya karne nane: Hivyo basi ni makosa kudhania kuwa Uislamu ni kunakili Ustaarabu tu. Au kuwa ustaarabu mpya ni wa Magharibi kwa vile umekamilika. Uislamu una fadhila kubwa katika kuweka kanuni za awali ambazo zimepelekea mafanikio hayo."

Prince Charles

Mwanamfalme wa Uingereza

VILINZI VYA NJIA YA FURAHA

Ustaarabu wa Kiislamu una vidhibiti bainifu na wasifu uliokuwa wazi ambao unatengeneza haiba ya mtu mkamilifu vidhibiti vyenye alama zenye kujitegemea na nyinginezo kwa misingi ya ustaarabu, malengo yake na misingi yake pamoja na kuwepo kiasi cha ushirikiano kati yake na tamaduni nyingine.

Misingi ya ustaarabu wa Kiislamu sio tu kutukuza akili kama ilivyokuwa kwa Wagiriki, wala kutukuza nguvu na utawala kama ilivyokuwa kwa Waroma, au kuupa umuhimu matamanio ya kiwiliwili na nguvu za kijeshi na siasa kama ilivyokuwa kwa wafursi au kujenga nguvu za kiroho kama walivyofanya Wahindu na baadhi ya Wachina au nguvu na utawala wa 'watu wa dini' pamoja na upotofu ambao ulipelekea kwenye kiza katika karne ya kati huko Ulaya.

Kadhalika sio kama ilivyo hivi sasa ambapo fitna ya sayansi na elimu na maada na kiasi binadamu kufaidika na silaha na hazina zilizokuwepo ulimwenguni kwa maada yenye kuangamiza kama tunavyoona leo hii katika mfumo wa ustaarabu huu uliorithiwa kutoka kwa Wagiriki na Warumi.

Ama misingi ya Ustaarabu wa Kiislamu una Tawhidi, kufikiri, elimu, matendo, roho, kujenga, kuheshimu akili na kuheshimu mwanadamu, yaani kwa vile inavyokusanya sehemu zote za maisha ya mwanadamu, na hili ndilo lililofanya Ustaarabu huu wa Kiislamu uwe unajitegemea kwa ukamilifu yenye desturi pana maalumu inatofautiana kwa tofauti kubwa na misingi ya staarabu nyinginezo.

Ustaarabu wa Kiislamu upo juu ya staarabu nyingine kwa kuwa na nguvu ya kiroho, kijihadi, kujitahidi, usawa, uadilifu, msamaha pamoja na wenye kutofautiana nao, na kadhalika kupenda kheri na kueneza sayansi ulimwenguni kote, na kwa hilo basi ustaarabu huu unapendekezwa kwa mara nyingine tena kuwaongoza wanadamu kwa hoja ya kumiliki vidhibiti hivi.

Karne ya Kati

"Lau Musa bin Nasir angewafikisha kuichangua Ulaya; Basi angeifanya Ulaya nzima kuwa ni ya Kiislamu, na angeiokoa Ulaya (bila ya shaka) katika duru ya karne ya Kati ambayo Uhispania haikuweza kujua na kusimama ila kwa fadhila za Waarabu."

Gustaf Lubon
Mwanahistoria wa Kifaransa

Uislamu unajipambanua kwa vipambanuzi vingi katika hivyo ni:

1. Imani na Tawhidi:

Imani inahesabiwa kuwa ni kiini cha njia ya furaha na linganio kubwa kwenye kutafuta elimu na kujenga ustaarabu, na kila ustaarabu ambao hautosimama katika imani ya Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) na tawhidi yake ni ustaarabu wenye mgogoro ndani yake, wenye kupigana vita kati ya sehemu



Arnold J. Toynbee

Mwanahistoria Mwingereza.

Ushindi wa Mateka.

"Uislamu uliziteka nchi zilizoishinda katika vita vya msalaba na hivyo kuingiza fani mbali mbali na ustaarabu katika maisha ya ulimwengu wa Wakristo. Maisha ya walatini yalikuwa na kutu katika baadhi ya makonde ya harakati ya mwanadamu, kwa mfano kama vile uhandisi wa ujenzi. Athari za Uislamu ziliingia katika ulimwengu wa Kikristo muda wote wa karne ya kati. Ama Sicily na Andalusia (Hispania) athari ya ufalme mpya wa Waarabu ulidhihirika zaidi na kupanuka."

zake, baadhi yake kuangamiza zingine, ambapo huwafanya asiyekuwa Allah kwa miungu mingine kwa kutofautiana majina, ambayo hupelekea kwenye ufisadi wa maisha ya mwanadamu na uovu wake!! Allah amesema: {Lau wangeli kuwamo humo miungu wengine isipo kuwa Mwenyezi Mungu basi bila ya shaka hizo mbingu na ardhi zingeli fisidika. Subahana 'Llah Ametakasika Mwenyezi Mungu, Bwana wa A'rshi (Kiti cha Enzi), na hayo wanayo yazua.} [21:22],

Na akasema Aliyetukuka: {Mwenyezi Mungu hana mwana yeyote, wala hanaye mungu mwengine. Inge kuwa hivyo basi kila mungu angeli chukua alivyo umba, na baadhi yao wangeli washinda wengine. Mwenyezi Mungu ameepukana na sifa wanazo msifu.} [23:91]

Na Akasema tena Aliyetukuka, {Sema: Lau kuwa wangeli kuwa pamoja naye miungu mingine kama wasemavyo, basi wangeli tafuta njia ya kumfikia Mwenye Kiti cha Enzi.} [17:42]

Na kinachoakisi haya ni kile kilichotokea na kinachoendelea kutokea sana katika tamaduni nyingine, na hivyo kupoteza malengo yake, na kupotoka kilichoelekezwa kwake; na hivyo kumpa mwanadamu uovu hata kama ilikusudia kumpa kheri, Allah amesema: {Wamewafanya makuhani wao na wamonaki wao kuwa ni marabi badala ya Mwenyezi Mungu, na pia Masihi bin Maryamu. Na wala hawakuamrishwa isipo kuwa wamuabudu Mungu Mmoja, hapana mungu ila Yeye. Subhanahu, Ametakasika na hayo wanayo mshirikisha nayo} [9:31].

K. Lal Gaba

Mwanasiasa na Mwanahabari wa India.

Unaingia katika Maisha

"Uislam ndio dini bora kwa mwanadamu: Uislamu ndio ambao unaingia ndani ya maisha ya Muislamu katika vipengele vyake vyote, bali ndio kipambanuzi cha mwisho katika kila shughuli anayofanya Muislamu. Hakuna dini nyingine zaidi ya Uislamu ambayo ina uwezo wa kutatua matatizo yote ya watu katika Ulimwengu huu leo hii. Na huu ndio ubora pekee wa Uislamu."

2. Sifa ya Kilimwengu:

Uislamu ni dini ya ulimwengu, imekuja iwe ni kwa zama na mahali pote na kwa kila lugha na watu wote, kwa kila rangi na taifa, Allah Aliyetukuka amesema:{Na hatukukutuma ila kwa watu wote, uwe mbashiri, na mwonyaji. Lakini watu wengi hawajui.} [34:28],

Na Allah akasema: {Ametukuka aliye teremsha Furqani kwa mja wake, ili awe mwonyaji kwa walimwengu wote.} [25:1],

Na akasema tena: {Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume kwenu nyinyi nyote, niliye tumwa na Mwenyezi Mungu Mwenye ufalme wa mbingu na ardhi….} [7:158]

Na akasema tena Aliyetukuka, {Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote.} [21:107].

Hivyo basi Uislamu ukaja na itikadi thabiti ambayo haibadiliki kwa kubadilika hali, na sheria iliyosimama kwa misingi ya uadilifu, haki na kheri inayowiana na tabia ya mwanadamu katika kila zama na mahali na sababu yake ni kuwa inatoka kwa Allah ambae hufahamu yenye kufaa viumbe vyake, Allah amesema: {Asijue aliye umba, naye ndiye Mjua siri, Mwenye khabari? } [67:14],

Kama ambavyo Uislamu sio dini mahususi kwa kundi au rangi au taifa maalumu la watu, Uislamu ni kwa ajili ya weupe, weusi, watu wa manjano, wekundu, nayo ni kwa ajili ya zama zilizopita na zama zilizopo na zama zijazo, wala mtafiti vyovyote atakavyopewa uwezo mkubwa wa kielimu hataona aliyokuja nayo Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) hisia yoyote ya kimajimbo, au ya kikundi



Yuko wapi Kiongozi Afaae?

"Akipatikana kiongozi anayefaa ambaye atazungumza maneno yanayofaa kuhusu Uislamu. Basi kuna uwezekano wa dini hii kuibuka tena kama ni moja ya nguvu kubwa za msingi za kisiasa ulimwenguni kwa mara nyingine."

W. Montgomery Watt

Mustashrik wa Uingereza.

au kitabaka, na hiyo ni alama ya wazi kuwa Da'wah yake ni ya Kilimwengu haitegemei kwa kundi maalumu au taifa maalumu; kwani ibada za Kiislamu, sheria zake, hukumu zake, tabia zake zote zinafaa kwa watu wote katika zama zote;

hivyo basi haiwezekani kusema kuwa uadilifu au tabia njema haifai watu fulani au zama fulani, na hili ni maalumu kwa Uislamu.

Ama katika baadhi ya dini zile hisia za kimajimbo au za kitaifa au za kujuana zipo wazi sana; kwa mfano Mayahudi wanapoamiliana na wasio katika dini yao Mwenyezi Mungu anawaelezea: {Na miongoni mwa Watu wa Kitabu yupo ambaye ukimpa amana ya mrundi wa mali atakurudishia, na miongoni mwao yupo ambaye ukimpa amana ya dinari moja hakurudishii isipo kuwa ukimsimamia kumdai. Haya ni kwa kuwa wakisema: Hatuna lawama kwa ajili ya hawa wasio jua kusoma. Na wanamzulia uwongo Mwenyezi Mungu, hali nao wanajua.} [3:75].

Injili ya Mathayo

"Akajibu, akasema, "Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea katika nyumba ya Israeli."
Na alipowachaguwa watu kumi na wawili ili wakawalinganie mayahudi aliwausia: "Hao Yesu aliwatuma, akawaagiza, akisema, katika njia ya mataifa msiende, wala katika mji wowote wa Wasamaria msiingie. Afadhali shikeni njia kuwaendea kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli. Na katika kuenda kwenu, hubirini mkisema, Ufalme wa mbingu umekaribia."

https://www.path-2-happiness.com/sw

3. Ustaaabu wa Elimu, Kuimarisha na Kujenga:

Mtazamo wa Uislamu kwa mwanadamu ni kuwa Allah amemuumba kwa ajili ya Ukhalifa na kuimarisha Ulimwengu, Allah amesema: {…Yeye ndiye aliye kuumbeni katika ardhi, na akakuwekeni humo….} [11:61],

Na akasema Aliyetukuka: {Yeye ndiye aliye kufanyeni manaibu katika ardhi. Na anaye kufuru, basi kufuru yake ni juu yake; na kufuru za makafiri haziwazidishii kwa Mola wao Mlezi ila kuchukiwa. Wala kufuru za makafiri haziwazidishii ila khasara.} [35:39],



Kujenga na Kuimarisha

"Uislamu unatambua kuimarisha vipaji; uzamifu na upembuzi binafsi: ni dini ya kujenga na kuimarisha na sio dini ya kubomoa. Kama kwa mfano mtu anamiliki ardhi na yeye kwa upande mwingine ana utajiri ambao hataki kulima ardhi ile na akaiacha tupu, baada ya muda fulani ardhi ile itahamia katika ardhi za Ummah katika hali ya kawaida. Sheria ya Kiislamu inathibitisha kuwa miliki ya ardhi hiyo itahamia katika mkono wa mtu wa kwanza ambae atalima ardhi ile."

Sir Charles Edward Archibald.

Mwanasiasa wa Uingereza.

Kunyoosha Nafsi

"Uislamu ni dini ambayo ina afikiana na ugunduzi wa elimu, na kubwa katika hayo ni kuzinyoosha kuzipeleka kwenye Uadilifu, wema na kusameheana."

Gustof Lubon
Mwanahistoria Mfaransa.

Hivyo ndani ya dini ya Kiislamu watu hupata dhambi watakapoacha elimu yoyote inayomfaidisha mwanadamu na kuimarisha ulimwengu, wakati ambapo Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) ametumwa wakati watu wakiishi katika shimo la ujima wa ustaarabu na elimu, na watu kushughulishwa na falsafa, majadiliano kinyume na kujenga, kutenda na kuimarisha ardhi; hivyo Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) akawanyanyua wanadamu kwa dini ya Uislamu, dini ya Ustaarabu na dini ya kujenga bila ya kuwepo mgongano kati yake na kuimarisha ardhi, na kati yake na kunawirisha roho, hivyo hamna migongano ndani ya nafsi ya Muislamu baina ya ibada na matendo, na kuimarisha ardhi na kati yake na maisha ya kiroho na kutenda katika kumridhisha Mola wake, yote hayo ni kwa ajili ya Allah na katika njia yake, Allah Aliyetukuka amesema: {Sema: Hakika Sala yangu, na ibada zangu, na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote.} [6:162].

Juu ya Vichwa vya Mashahidi.

"Nyote mnafahamu kuwa mimi ni "Heral" mtoto wa kiongozi mkubwa wa Kipagani, "Ghandi". Mimi natangaza mbele ya vichwa vya mashahidi na katikati ya kundi kubwa hili la Waislamu kuwa mimi nimeupenda Uislamu, nimeipenda Qur-aan na nimemuamini Allah Peke Yake na Mtume wake mtukufu Sayidina Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) na kuwa yeye ni Mtume wa mwisho na kuwa hakuna nabii baada yake na Qur-aan ilichokileta ni haki na vitabu vyote viliyoteremshwa ni haki. Mitume na manabii wote ni haki. Na kwa Uislamu na Qur-aan nitaishi na kufa kwa ajili yake na nitautetea na kupigana kwa ajili yake na nitakuwa moja ya nguzo yake imara na nitaulingania kati ya jamaa na ndugu zangu. Dini hii tukufu ni dini ya elimu, utamaduni, uadilifu, uaminifu, rehema na usawa."

Abdullah Harlal Ghandi,
Mtoto wa Mahatma Ghandi

4. Ustaarabu wa Kimaadili:

Tabia njema katika Uislamu ni ibada, bali Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) ametujulisha kuwa lengo la kutumwa kwake ni kukamilisha Matukufu ya maadili; amesema Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam): «Nimetumwa kukamilisha matukufu ya tabia.» (Imepokewa na Malik), hivyo basi njia ya ustaarabu na furaha ni njia ya kimaadili inahimiza matukufu ya tabia na matendo mema, na maadili katika Uislamu ni mpana katika nyanya zote za maisha, mfano wa mtu kuamiliana na nafsi yake pamoja na Allah na wengine, kama inavyokusanya muamala wa Muislamu pamoja na kafiri na pamoja na mdogo na mkubwa na mwanamume na mwanamke na mtu na mtesi wake.

Hivyo basi Uislamu ukaamrisha ukarimu, ushujaa, na uadilifu, rehema na huruma, kutojikweza, adabu njema katika miamala na watu, ukweli, haya, uvumilivu, amani ya moyo na kupenda kheri na yasiyokuwa hayo, Allah Aliyetukuka ameelezea umuhimu na wajibu wa kufanya uadilifu hata ikiwa ni mtu na mtesi wake: {Enyi mlio amini! Kuweni wasimamizi madhubuti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu mkitoa ushahidi kwa haki. Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutofanya uadilifu. Fanyeni uadilifu. Hivyo ndio kuwa karibu mno na uchamngu. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda.} [5:8],

Na akasema kuhusu ujumbe wa Mtume Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) na kubainisha kuwa yeye ni rehema kwa walimwengu wote na sio mahsusi kwa waliomuamini peke yake tu, Allah aliyetukuka

https://www.path-2-happiness.com/sw

amesema: {Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote.} [21:107],

Tabia hizi ni sehemu muhimu katika ustaarabu wa Kiislamu na nguzo yake ya asili, ndani yake, wala haiwezekani kupotea tabia njema kwa Muislamu kwa sababu yoyote ile kwa ajili ya kujenga ulimwengu huu au kwa ajili ya maslahi yoyote au yasiokuwa hayo, Allah amemtengeneza Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) na kumpa adabu ili awe mfano katika adabu na maadili na kigezo chema katika kila kitu, Allah amesema: {Hakika nyinyi mnayo ruwaza njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anaye mtaraji Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na akamkumbuka Mwenyezi Mungu sana} [33:21],

Na Allah akaelezea sehemu ya rehema yake na pupa yake katika kuwaongoza watu kwenye uongofu katika njia ya furaha, Allah Aliyetukuka amesema: {Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayo kutaabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma.} [9:128].



5. Ustaarabu wa Akili na Kufikiri:

Katika dini ya Uislamu hakuna ukahanuti (siri zinazotawaliwa na makuhani na watu wa dini) ambao huwezi kuuliza au siri ambayo hauwezi kuzingatia, bali Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) ameamrisha kufikiria katika aya zake, katika viumbe na katika Ummah mbali mbali, Allah Aliyetukuka amesema: {Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayo kutaabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma.} [3:191],

Na Allah Aliyetukuka akasema tena: {…Namna hivi tunazipambanua Ishara zetu kwa watu wanao fikiri.} [10:24],

Na Allah Aliyetukuka akasema: {Kwa Ishara wazi na Vitabu. Nasi tumekuteremshia wewe Ukumbusho ili uwabainishie watu yaliyo teremshwa kwao, wapate kufikiri.} [16:44],

Na akasema Aliyetukuka: { Je! Hawajifikirii nafsi zao? Mwenyezi Mungu hakuumba mbingu na ardhi na viliomo ndani yake ila kwa Haki na kwa muda maalumu. Na hakika watu wengi bila ya shaka ni wenye kukataa kuwa watakutana na Mola wao Mlezi.} [30:8]

Na akasema tena Aliyetukuka, {…Na hiyo mifano tunawapigia watu ili wafikiri.} [59:21],

Bali Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) ametufundisha kuwa elimu sio dhana peke yake bali hapana budi elimu hiyo iwe na dalili inayosimamia, Allah Aliyetukuka amesema: {…Sema: Leteni ushahidi wenu kama nyinyi ni wasema kweli} [2:111]

Hivyo hakuna siri anayoifahamu mtu au kuhani au kiongozi wa dini ambaye hatoi siri hiyo kwa mtu.

https://www.path-2-happiness.com/sw

6. Ustaarabu wa Amani ya Ndani na Nje:

Amani ya ndani ina maanisha furaha ya ndani ya mwanadamu na kuokoka kwake na migongano ya ndani ambayo huwakumba watu wengi katika ustaarabu wa kisasa; kiasi cha kuwa dunia na akhera zikaishi katika fikra ya amani ya mwanadamu na hivyo ibada na matendo na ujenzi wa ardhi kuishi pamoja, roho na mada, elimu na dini, hakika amani ya ndani katika ustaarabu wa Uislamu ni alama ya wazi inayotokana na tawhidi ambayo inakusanya yote yaliyotangulia katika nafsi ya muumini kwa wepesi na urahisi.

Katika Uislamu dunia si lengo katika dhati yake, bali ni shamba la akhera, mapito na kivuko cha kuelekea huko, na hili lipo wazi katika kauli yake Allah Aliyetukuka:

{Na utafute, kwa aliyo kupa Mwenyezi Mungu, makaazi ya Akhera. Wala usisahau fungu lako la dunia. Nawe fanya wema kama Mwenyezi Mungu alivyo kufanyia wema wewe. Wala usitafute kufanya ufisadi katika ardhi. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi mafisadi.} [28:77];

Na, {Na itakapo kwisha Sala, tawanyikeni katika nchi mtafute fadhila za Mwenyezi Mungu, na mkumbukeni Mwenyezi Mungu kwa wingi ili mpate kufanikiwa} [62:10];

Yaani utakapomaliza Swala basi uende kwenye kazi zako za kidunia madamu ni halali na utafute kwenye kazi hizo ikhilasi, ukitarajia radhi za Allah; kama Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) alivyomwambia mmoja wa sahaba zake:

Akili na Mantiki

"Katika vivutio vya Uislamu ni kuwa kwake dini inayosimama kwa kutumia akili. Haumtaki kamwe mfuasi wake kufuta kipaji hiki alichopewa na Mungu. Kama ambavyo Uislamu unapenda utafiti na kuulizia mambo. Kadhalika inalingania wafuasi wake katika kusoma na kufanya utafiti, uchunguzi na kuangalia kabla ya imani. Uislamu unaunga mkono hekima isemayo: Thibitisha ukweli wa kila jambo kisha shikamana na kheri. Hili si jambo geni: Kwani hekima ni jambo lililompotea muumini popote alipatapo basi ni mwenye haki nayo zaidi. Uislamu ni dini ya matumizi ya akili na mantiki: Hivyo basi tunakuta kuwa neno la kwanza lililoshuka kwa Nabii Muhammad ni: "Soma", kama ambavyo tunaiona kauli mbiu ya Uislamu ni kulingania katika kuangalia na kutafakari kabla ya kuamini: Kwani Uislamu ni haki na silaha yake ni elimu, na adui yake mkubwa ni ujinga."

Profesa Haroon Mustapha Lion

Mwanazuoni wa Mambo ya Lugha huko Uingereza.

«Na wewe hutotoa matumizi yoyote ukitarajia nayo radhi za Allah isipokuwa utalipwa ujira hata kile ambacho utakiingiza katika mdomo wa mke wako.» (Imepokewa na Malik); Yaani katika mdomo wa mke wako unapata ujira, katika dini yetu hakuna kutenganisha kati ya dunia na akhera lakini kwa sharti ya kutoshughulishwa na dunia na kuacha akhera, kama alivyosema Allah Aliyetukuka:

{Enyi mlio amini! Yasikusahaulisheni mali yenu, wala watoto wenu, kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Na wenye kufanya hayo ndio walio khasiri} [63:9]

Na akasema vile vile: {Na utafute, kwa aliyo kupa Mwenyezi Mungu, makaazi ya Akhera. Wala usisahau fungu lako la dunia. Nawe fanya wema kama Mwenyezi Mungu alivyo kufanyia wema wewe….} [28:77],

Hivyo basi mapenzi ya matendo, mapenzi ya mke, kucheza na watoto na kuwajali, na mengine katika mipaka ya kisheria katika dini ni miongoni mwa uongofu wa Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) iwapo kutakusudiwa radhi za Allah, Allah amesema: {Sema: Hakika Sala yangu, na ibada zangu, na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote.} [6:162],

Suluhisho la Kiakili

“Qur-aan imeleta suluhisho la kiakili la matatizo ya zama hizi za Kiuchumi, kijamii na kimaadili: Kwa hili haiwezikani kutia shaka katika ile hekima ya Qur-aan kwa kuangalia mafanikio ya Muhammad katika kufikisha ujumbe ambao Mungu amemuarisha kuufikisha. Hivyo yapasa kwetu (kwa mtazamo wangu) kadiri ya misimamo yetu ya dini ilivyo kuzingatia ujumbe wa Qur-aan tangu kuchimbuka kwake huko Makkah.”

W. Montgomery Watt

Mustashrik wa Kiingereza



Kwa hiyo maisha yote ni kwa ajili ya Allah, hata kile ambacho ndani yake kuna hadhi ya nafsi basi hicho ni kwa ajili ya kumtii Allah Aliyetakasika na kutukuka madamu nia imenyooka.

Amani ya nje pamoja na watu wa karibu na wa mbali, mwenye kuafikiana nae na mwenye kutofautiana nae, bali salamu ya kwanza anayomsalimia mtu nduguye ni kauli yake kwa nduguye; Amani juu yenu na rehema za Allah na baraka zake, watu hawakufurahi na kuhifadhika kwenye dini zote kama walivyofurahi katika utawala wa Uislamu; ni kiasi gani ulimwengu ulivyopata hasara kwa kuanguka kwa baadhi yaWaislamu, Allah amesema: {…Wala kuwachukia watu kwa kuwa wali-kuzuilieni kufika Msikiti mtakatifu kusikupelekeeni kuwafanyia uadui. Na saidianeni katika wema na uchamngu. Wala msisaidiane katika dhambi na uadui. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu..} [5:2].

Maisha Mazuri

"Ikiwa tunataka kuwa waadilifu kuhusu Uislamu ni juu yetu kukubali kuwa katika mafundisho yake kunapatikana nguvu hii ambayo inawezekana ikawa maisha mazuri na haswa katika upande wa kimaadili. Mafundisho haya yanatakia rehema kwa viumbe vyote vya Mungu, na uaminifu katika mahusiano ya watu wenyewe kwa wenyewe, kadhalika mapenzi na ikhlasi na kuzuia silika zenye kuipelekea kwenye matamanio kama ambayo inavyowatakia mambo mengine mazuri.

Matokeo ya mambo yote haya ni kuwa Muislamu mwema anaishi maisha yenye uzalishaji mwingi kwa kadiri maadili yanavyohitajia."

Ignaz Goldziher

Mustashrik wa Kiyahudi.

7. Ustaarabu waUsawa na Mapenzi:

Ustaarabu wa Kiislamu unawajibisha Waislamu kuwa watu wenye nyoyo zilizosalimika na nafsi zilizo safi, amesema Allah Aliyetukuka kuhusu kisa cha dua ya Waumini: {Na walio kuja baada yao wanasema: Mola wetu Mlezi! Tughufirie sisi na ndugu zetu walio tutangulia kwa Imani, wala usijaalie ndani ya nyoyo zetu undani kwa walio amini. Mola wetu Mlezi! Hakika Wewe ni Mpole na Mwenye kurehemu.} [59:10]

Maadili ya Watu

"Kwa hakika Waislamu kama wanavyojulikana ni watu waliokamilika zaidi kuliko Wakristo: Walikuwa ni watu wenye kulinda ahadi zaidi, wenye kuwahurumia zaidi wanaowashinda. Na makosa machache sana waliyofanya katika historia yao kuliko unyama waliofanya Wakristo walipotawala Qudsi mwaka 1099.

Will Durant

Mwandishi wa Kimarekani.

Na, {Siku ambayo kwamba mali hayato faa kitu wala wana. Isipo kuwa mwenye kumjia Mwenyezi Mungu na moyo safi.} [26:88-89],

Na Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) akasema: «Msibughudhiane wala msihusudiane na kuweni waja wa Allah ni ndugu, haiwi halali Muislamu kumuhama nduguye zaidi ya siku tatu, hukutana huyu akampa mgongo huyu na mbora wao ni yule anayeanza kutoa salamu.» (Imepokewa na Muslim).

Na Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) akasema huku akihimiza mapenzi na kuzoeana: «Naapa kwa ambae nafsi yangu ipo mikononi mwake, hamtoingia peponi hadi muamini, na hamtoamini hadi mpendane, Je, nikujulisheni kitakachothibitisha hilo kwa ajili yenu? Enezeni salamu.» (Imepokewa na Tirmidhi).

Wakati fulani Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) aliulizwa: ni mtu yupi bora? Akasema: Kila mwenye moyo Makhmum, mkweli wa ulimi, wakasema: Mkweli wa ulimi tunamjua, basi ni nani Makhmumul-Qalbi? Akasema: «Huyo ni mcha-Mungu msafi, hakuna dhambi, wala uovu, wala kuvuka mipaka, wala husuda.» (Imepokewa na Ibn Majah).

8. Ustaarabu wa Kiroho na wa Kimada:

Ustaarabu wa Kiislamu umekuja kung'arisha roho za watu, na wakati huo huo haujasahau mada wala kuipuuuza, Allah amemuumba mwanadamu katika mada na roho, na kumpa sababu zote za maisha katika pande zake za kimada na kiroho; akatayarishia mwili mazingira yenye kufaa kuishi nayo katika uso wa ardhi, kadhalika Allah Aliyetukuka akaitayarishia chakula cha roho kutokana na wahyi wa mbinguni ambao Allah amemteremshia mwanadamu kupitia Mitume yake, Allah Aliyetukuka amesema: {Na Mola wako Mlezi alipo waambia Malaika: Hakika Mimi nitamuumba mtu kwa udongo unao toa sauti, unao tokana na matope yaliyo tiwa sura. Basi nitakapo mkamilisha na nikampulizia roho yangu, basi mumwangukie kumsujudia.} [15:28-29],

Dale Carnegie
Mwandishi wa Kimarekani



Starehe ya Kiroho.

“Kinachonishughulisha mimi sasa hivi ni ninachokipata katika neema za dini. Kama vile ambavyo ninajali neema tunayopata kutokana na umeme, chakula bora na maji safi. Haya yote hutusaidia kuishi maisha mazuri yenye neema. Ama dini hunipa mengi zaidi ya haya. Hunipa raha starehe ya kiroho, au hunipa (kama aliyozungumza William James) msukumo wa nguvu wenye kuunganisha maisha. Maisha yenye nafasi, yenye furaha maridhawa, kwa hakika inanipa imani, matarajio na ujasiri na huniondolea khofu, sononeko na wasiwasi. Vile vile hunielekeza kwenye malengo katika maisha na hukunjua mbele yangu upeo wa furaha na kunisaidia katika kujenga chemchem ya maji na rutuba katikati ya jangwa la maisha yetu.”

Nassry Salhab
Mwanafasihi wa Kilebanoni

Ukubwa wa Uislamu

“Uislamu hauhitaji kalamu zetu kwa ufasaha wowote ule kalamu zetu zitakaoufikia. Lakini kalamu zetu zinauhitajia Uislamu, kwa yale ambayo Uislamu unayo kama vile utajiri wa kiroho na kimaadili kutoka kwenye Qur-aan yake nzuri ambayo kwake tunaweza kujifunza mengi.”

Hivyo basi roho na kiwiliwili ni vitu viwili vyenye kulazimiana kimoja hakitoki kwa mwenzake ila kwa mauti ya mtu.

Roho na kiwiliwili kila kimoja kina mahitaji na matakwa yake; kiwiliwili kinaishi kwa kula, kunywa na kuvaa hata kama kutakuwa na mapungufu upande mmoja utaona athari ya upande mwingine, kama mtu atakuwa amefanya mapungufu katika chakula chake utamkuta kuwa ni dhaifu anayeangamia hawezi kuishi maisha yenye utulivu na mazuri, vivyo hivyo kwenye kunywa na kuvaa.

Kwa hakika upungufu wa matakwa yoyote katika kiwiliwili hiki kinaakisi yote katika maisha yake, hawezi kuishi vizuri wala kusaidia upande wake wa pili (kiroho) katika maisha ya utulivu.

Hali kadhalika roho ina matakwa yake, roho haiishi bila mapenzi kutoa, wala kujitolea basi vipi roho itaishi bila mola inayemuabudu, kumpenda, kumtarajia, kumuogopa na kumkimbilia? Vipi roho itaishi ikiwa kifua kitupu haipati inayomtegemea na kutulia kwake, au haipati amani, kutoa na kusalimika moyo na mahaba baina ya watu?!

Ama kwa hakika mwanadamu akifanya mapungufu katika kuipa roho haja zake basi yeye ni kama aliyefanya mapungufu katika chakula chake na kinywaji chake, mwanadamu atatulia vipi, vipi hali yake itakuwa na utulivu na nusu yake ya pili hulalama na jeraha?! Kwa bahati mbaya ustaarabu wa Kimagharibi umesahau furaha ya roho na ndio maana ikawa na huzuni katika maisha haya ya dunia wakati ambapo yeye yupo katika kilele cha maisha mazuri, Ustaarabu wa kisasa ni ustaarabu uliopambazuka kwa kuhudumia kiwiliwili na Mada lakini umesahau au kujisahaulisha kiwiliwili bila ya roho ambayo haina furaha wala mafanikio wala utulivu, bali sio ustaarabu wa kweli.

9. Ustaarabu unaomjali mwanadamu na haki zake:

Limekuwa ni jambo maarufu kuwa utekelezaji wa haki za mwanadamu kuhesabiwa kuwa ni kigezo cha kujua kiasi ambacho nchi husika inazingatia misingi ya uadilifu, usawa, kulinda haki za wananchi wake na uhuru wao.

Kama ambavyo huzingatiwa kuwa ni kipimo cha ufahamu na mwamko wa wananchi kuneemeka na haki na uhuru wao, bali ni kipengele muhimu sana katika mifumo ya Kidemokrasia ambayo ni kulinda haki za wanadamu.

Katika Ustaarabu wa Kiislamu imejaa mifano mingi na ya kipekee katika uhalisia kuhusu haki za binadamu, nayo ndio ukubwa na utukufu wa ustaarabu huu wa Kiislamu, na kuwa sio maneno matupu tu au alama au kauli mbiu tu.

Mambo yenye kupambanua haki za binadamu katika Uislamu ni haya yafuatayo:

1. Chanzo cha haki hizi zimejengwa katika msingi kuwa ubwana na utawala ni wa Allah Aliyetukuka, Allah Ta'ala amesema: {…Hapana hukumu ila ya Mwenyezi Mungu. Yeye anasimulia yaliyo kweli; naye ni Mbora wa kuhukumu kuliko wote.} [6:57].

Hivyo basi sheria ya Kiislamu kuhusu haki huangaliwa kwa mtazamo wa kiiungu kwa kiumbe huyu, na yale yenye kumfaa.

Aibu ipo Ndani Yetu

"Yapasa kuwa wazi kwetu kuwa Waislamu kupuuzia mambo (na sio upungufu katika mafundisho ya Uislamu) Hiyo ndio ambalo limesababisha matatizo tuliyonayo leo hii."

Leopold Weiss

Mwanafikra wa Austria.

2. Kuthibiti: Haibadiliki kwa kubadilika wakati na kubadilika mazingira na hali.

3. Kuchunga haki kulingana na msimamo wa hisani: Haki katika Uislamu zinaibuka kutokana na kisimamo ambacho ndani yake mja anakuwa chini ya kumuogopa Allah (Subhaanahu wa Ta'ala), nacho ni kisimamo cha hisani (wema) ambacho Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) ameielezea: «Kumuabudu Allah kana kwamba unamuona, na kama humuoni yeye anakuona.» (Muslim).

4. Kuchanganyika na ukamilifu kati ya haki za binadamu na tabia ya dini hii:

Kwa hiyo Uislamu haukuacha haki hivi hivi tu, bali imezitengenezea mazingira ya hukumu za kisheria na katika mtazamo wa makusudio ya kisheria, na ikazilinganisha na adabu na maadili yake, na ikafanya kuharibu adabu zile ni kuharibu haki hizi, na mwishowe ni kuziunganisha na dini, na kuzingatia vyanzo vyake vya kiungu, na hivyo basi huhesabiwa kuwa ni majukumu ya Muislamu binafsi, na sio haki hivi hivi tu, hivyo basi kujenga haki katika Uislamu ni kujenga kwa ukamilifu wenye kulandana na tabia ya kiungu ya dini hii.



Amani ya Ulimwengu.

"Taarifa ya Qur-aan kuhusu Muumba wa Ulimwengu ilinitingisha: Nimeufahamu Uislamu kupitia Qur-aan, na sio katika matendo ya Waislamu. Enyi Waislamu kuweni Waislamu wa kweli ili Uislamu uweze kuenea ulimwengu. Kwani huo ni amani kwa ulimwengu wote."

Cat Stevens.

Mwimbaji wa Uingereza.

5. Utawala wa mtu binafsi katika jamii ya kiislamu ndio msingi wa haki za binadamu katika Uislamu, na sio kinyume chake kama hali ilivyo katika sheria za wanadamu, Allah Aliyetukuka amesema:

{Kwa sababu ya hayo tuliwaandikia Wana wa Israili ya kwamba aliye muuwa mtu bila ya yeye kuuwa, au kufanya uchafuzi katika nchi, basi ni kama amewauwa watu wote. Na mwenye kumuokoa mtu na mauti ni kama amewaokoa watu wote. Na hakika waliwajia Mitume wetu na hoja zilizo wazi. Kisha wengi katika wao baada ya haya wakawa waharibifu katika nchi.} [5:32].

6. Uislamu kutangulia katika haki za binadamu kabla ya wengine.

Kwa hiyo haki hizi ambazo Uislamu umedhamini kwa mwanadamu hazikuja katika mapambano ya kififikra au ya kimapinduzi na matakwa yake kama ilivyo katika historia ya haki za binadamu katika mfumo wa kidemokrasia na sababu za kuanza kwake, kama vile ilivyokuwa hali ya Ufaransa na Marekani na kwingineko, bali (haki hizi ambazo Uislamu umezidhamini) misingi yake imetulia na hukumu zake kwa Wahyi kutoka kwa Allah Aliyetukuka bila kuwepo mazungumzo yake kabla ya hapo au kuyafuatilia au mapambano ya kufikia njia yake.

7. Kuwa inafuata hali halisi na inaungana na maisha, hugusa haja ya mwanadamu; kinyume na haki katika sheria za kigeni –ambazo zimewekwa na kupambwa katika hali ya kifalsafa zaidi.

8. Kuna sheria ambazo ni za Uislamu peke yake, miongoni mwa haki hizo muhimu ni: haki za wazazi wawili, haki za ndugu kwa watoto, haki za jamaa wenye ndugu, haki ya kichanga tumboni, haki ya mtu kupata malezi ya kidini na ya kidunia, haki ya chumo halali, makatazo ya riba, haki ya kulingania katika kheri, kuamrisha mema na kukataza maovu.

9. Suluhisho la Uislamu kuhusu kadhia za haki za binadamu inasimama katika asili ya utu wa mwanadamu na kuchochea hisia ya imani kwa Allah Aliyetukuka, kinyume na sheria zingine. Haki hizi zinaegemea katika ufahamu wa kuwa ulimwengu huu umedhalilishwa na Allah Aliyetukuka kwa maslahi ya binadamu kulingana na kanuni za kimaumbile. Historia ya mwanadamu haikuwa kushuhudia ustaarabu ambao umetekeleza haki za mwanadamu pasipo maslahi (ya watawala), vinginevyo tunaona kwa wepesi nembo zinazotolewa na wito mwingi na kunyanyuliwa kwa mabango, lakini ni ugumu ulioje kugundua hakika zilizojificha nyuma yake na nia zilizo funikwa nyuma yake pindi wale viongozi wake wanapokuwa chini ya viwango vya utata….

Pamoja na ustaarabu huu kuwaenea wanadamu kwa kutumwa kwake, ila ni kuwa baadhi ya watu wanaweza kujiuliza-kuhusu sababu za kurudi nyuma Waislamu na kuwa kwao katika hali waliyonayo leo hii pamoja na maendeleo haya ya Ustaarabu wa Kiislamu?!

Hata hivyo kushangazwa huku kunaondoka tukifahamu hali ya Waislamu leo hii haiwakilishi ukweli wa dini yao, wengi wao wamerudi nyuma pindi walipoacha misingi ya dini yao na yaliyokuja kwenye kitabu chao na katika Sunnah ya Mtume wao (Swala Llahu 'alayhi wasallam), vinginevyo dunia isingefahamu ustaarabu uliofurahisha walimwengu wote kuliko ustaarabu wa Kiislamu, inatosha kusoma historia na kusikiliza kauli za waadilifu hata wasiokuwa Waislamu ili tuone ni kwanini ulimwengu umepata hasara kwa kuparaganyika Waislamu?!

Ulimwengu Mtupu

"Inawezekana Waislamu wakasambaza ustaarabu wao katika ulimwengu kwa haraka ile ile ambayo walioisambaza hapo kabla: Kwani ulimwengu huu mtupu hauwezi kuthubutu mbele ya Roho ya Ustaarabu wao."

Marmaduke Pickthal
Mwandishi wa Uingereza

https://www.path-2-happiness.com/sw

MIUJIZA KATIKA QUR-AAN NA SUNNAH

Kila Mtume ana miujiza inayothibitisha ukweli wa utume wake na ujumbe wake, kwa mfano miujiza ya Musa ('Alayhi Salaam) ilikuwa ni ile fimbo yake, na miujiza ya Issa ('Alayhi Salaam) ilikuwa ni kuponya mbalanga na ukoma na kuhuisha mauti kwa idhini ya Allah. Ama miujiza ya Mtume wa mwisho inawiana kwa kila zama na mahali muda wote mwanadamu akiwepo na ndio hii Qur-aan Tukufu, na ikiwa Qur-aan Tukufu ni kitabu cha mwongozo; basi kitabu hiki kitukufu ni miujiza wa kila kitu, na miujiza yake ni kusadikisha ukweli na utume wa Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) na kuwa yeye ametumwa na Muumba, mwenye kutoa riziki Msimamia mambo yote milele, na kuwa ni kitabu alichotumwa nacho mwisho wa Mitume na Manabii, inayofaa kila zama na mahali na sehemu zake za miujiza yake ambazo tumezitaja huko nyuma; kwa hakika Qur-aan ni muujiza wa kisayansi na elimu mbali mbali kama ilivyokwisha oneshwa na watafiti wa kisasa katika kubainisha kuwa Qur-aan kugusa kwake mambo ya ndani ya kisayansi ambayo hayakuvumbuliwa isipokuwa katika karne hii, miongoni mwa hayo kwa mfano: awamu za kuumbwa mwanadamu na kitoto kilicho tumboni katika wasifu makini kabisa na wa ndani kabla watu hawajaweza kulijua hilo kwa mamia ya miaka, Allah Aliyetukuka amesema: {Na kwa yakini tumemuumba mtu kutokana na asli ya udongo. Kisha tukamjaalia awe tone ya mbegu ya uzazi katika kalio madhubuti. Kisha tukaiumba tone kuwa damu iliyo ganda, na tukaiumba damu kuwa pande la nyama, kisha tukaliumba pande la nyama kuwa mifupa, na mifupa tukaivika nyama. Kisha tukamfanya kiumbe mwengine. Basi ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbaji. } [23:12-14]



Na akasema Aliyetukuka: {Amekuumbeni kutokana na nafsi moja. Kisha akamfanya mwenziwe katika nafsi ile ile. Na akakuleteeni wanyama wa mifugo jozi nane. Anakuumbeni katika matumbo ya mama zenu, umbo baada ya umbo, katika viza vitatu. Huyu ndiye Mwenyezi Mungu Mola wenu Mlezi. Ufalme ni wake. Hapana mungu isipo kuwa Yeye. Basi nyinyi mnageuzwa wapi?} [39:6]

Na pindi madaktari waliporejea katika rejea zao na katika ugunduzi wao walipata kama alivyosema Mjuzi wa yote.

Kwa kuongezea kubainisha sehemu ya hisia ndani ya mwili, Allah amesema: {Hakika wale walio zikataa Ishara zetu tutawaingiza Motoni. Kila zitapo wiva ngozi zao tutawabadilishia ngozi nyengine ili waionje hiyo adhabu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima.} [4:56],

Na ubainifu wa upana wa anga, Allah Aliyetukuka amesema: {Na mbingu tumezifanya kwa nguvu na uwezo na hakika Sisi bila ya shaka ndio twenye uwezo wa kuzitanua.} [51:47],

Na kubainisha mzunguko wa jua katika mzunguko wake, Allah Aliyetukuka amesema: {Na usiku ni Ishara kwao. Tunauvua humo mchana, mara wao wanakuwa gizani. Na jua linakwenda kwa kiwango chake. Hayo ni makadirio ya Mwenye nguvu, Mwenye kujua. } [36:37-38].

Wasifu wa Kichanga

"Sipati tabu kukubali kuwa Qur-aan ni maneno ya Mwenyezi Mungu, kwani wasifu wa kichanga kilicho tumboni katika Qur-aan hauwezi kujengwa juu ya utaalamu wa kisayansi wa karne ya saba. Matokeo pekee yanayoweza kukubalika ni kuwa wasifu huu ni WAHYI (UFUNUO) alioupata Muhammad kutoka kwa Mungu."

Profesa Yushudi Kusan

Mkuu wa Kituo cha Anga Tokyo.

Hali kadhalika Sunnah Tukufu ya Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) haikujitenga na miujiza hiyo; kutoka kwa Ummul Muuminina bibi Aisha (Radhiya Llahu 'anha) amesema: amesema Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam); «Hakika kila mwanadamu ameumbwa kutokana na mwanadamu kwa viungo mia tatu na sitini, yule atakayesema takbira, atakayemhimidi Allah, na akasema: 'La illaha illa llah, akamsabihi Allah, akamuomba msamaha, na akaondoa jiwe kwenye njia za watu, au mwiba, au mfupa au kuamrisha mema au kukataza maovu akahesabu miaka ile miaka mia tatu na sitini mifupa na viungo vya mwili basi mtu huyo hufika jioni akiwa ameepushwa na moto.» (Muslim).

Kilichothibiti kisayansi leo hii ni kuwa bila ya viungo hivi katika mwili wa mwanadamu, asingeweza kuwepo katika maisha haya, wala kusimamia majukumu yake ya ukhalifa ardhini, na ndio maana inapasa mwanadamu kushukuru Allah Aliyetukuka kila siku kwa neema hii ambayo inathibitisha uwezo wa Muumba juu ya kila kitu.

Jambo la muujiza katika Hadithi hii ni kuainisha kuwa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) idadi ya viungo vya kiwiliwili cha mwanadamu ni ainisho la kina kabisa katika zama ambazo hakukuwepo elimu hiyo kwa yeyote aliyeumbwa.

Watu wengi leo hii katika karne hii ya Ishirini na moja hawajui hilo, bali hata baadhi ya walimu wa tiba hawafahamu hilo!!! Hadi walipovumbua hivi karibuni kuwa idadi ya viungo vya mwanadamu ni mia tatu sitini kama ilivyoainishwa na Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) kabla ya karne kumi na nne zilizopita ambazo ndani ya viungo hivyo, viungo mia moja arubaini na saba (147) vya uti wa mgongo na Ishirini na nne (24) viungo vya kifuani na themanini na sita (86) ni viungo vya nusu ya juu ya kiwiliwili na themanini na nane (88) ni viungo vya nusu ya chini, na kumi na tano (15) na viungo vya Hodhi.

Swali linalojitokeza hapa: Kama sio Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) Muumba Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) angewezaje kujua hakika hii ya kisayansi ya ndani zaidi, ambayo elimu ya mwanadamu haijaweza kuifikia ila mwishoni mwa karne ya Ishirini?!!

Nani ambaye anaweza kumlingania Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) kuzamia mambo ya ghaib kama haya?! Kama sio Allah Aliyetukuka anayejua kwa elimu yake iliyozunguka kila kitu kuwa mwanadamu atafikia siku moja kufahamu hakika hii ya kielimu ya

upasuaji kiwiliwili cha mwanadamu, na hivyo hili kuwa ni mng'ao wa nuru katika hadithi hii tukufu kuwa ni uthibitisho wa utume wa Mtume huyu wa mwisho kwa ukweli wa muungano wake na Wahyi wa mbinguni.

Hata hivyo njia ya elimu na ustaarabu madamu kama haitakuwa ni njia ya maadili basi ustaarabu huo utakuwa ni wenye kuangamiza na elimu yake itakuwa ya maangamizi na sio ya kuwafurahisha watu na kuwahudumia! Vivyo hivyo njia ya elimu na ustaarabu vile vile ni njia ya maadili, kama ambavyo njia ya furaha bila ya elimu na ustaarabu ni upotofu, na hali kadhalika njia ya elimu na ustaarabu bila ya maadili ni yenye kuangamiza watu, Umma na jamii za wanadamu.

Mtume Umiyi (Asiyesoma Yaliyoandikwa).

"Akili inashangaa! Iweje ayah zile zitoke kutoka kwa mtu asiyeweza kusoma yaliyoandikwa. Watu wote wa Mashariki wamekubali kuwa ni ayah ambazo fikra ya mwanadamu haiwezi kuleta mfano wake kwa lafudhi na maana."

Henri de Castriesry

Luteni wa Jeshi la Ufaransa

Miujiza ya Ulimwengu.

"Vipi aliweza Muhammad, mtu asiyesoma yaliyoandikwa, aliyeishi maisha zama za Ujinga aweze kujua miujiza ya Ulimwengu iliyoelezwa kwenye Qur-aan Tukufu, ambazo sayansi leo hii bado zinaendelea kushughulikia?! Bila shaka hapana budi basi maneno haya kuwa ni maneno ya Mwenyezi Mungu."

Deborah Potter

Mwanahabari wa Kimarekani.

https://www.path-2-happiness.com/sw

الطريق إلى السعادة
The Path to Happiness

NJIA YA MAADILI

Yaliyomo

NJIA YA MAADILI

Imani iliyoungana na tabia njema:i

Ibada na tabia njema:i

Maadili katika Uislamui

NJIA YA MAADILI

Njia ya furaha ni njia ambayo ndani yake inapelekea kwenye maadili hapana budi kwa mwenye kupita njia hiyo apate njiani mapenzi, usamehevu, ukarimu, haya, amani, kunyenyekea, kuwatanguliza wengine, uadilifu, ukweli na kushauriana; pamoja na yasiyokuwa hayo katika matukufu ya tabia.

Nayo pia ni njia ya kuiweka nafsi juu na matakwa yake kwenye tabia njema za juu na adabu kubwa, maadili mema sio mambo ya anasa ambayo mtu anaweza kuyaacha, bali nafasi yake huja mwanzo kabisa katika misingi ambayo yanasimamia juu yake muelekeo wa maisha, ikiwa maadili ya watu yatakuwa mazuri basi yatageuka kuwa mambo mazuri katika furaha ya maisha yao na maisha ya jamii zao, na ikiwa mbaya wataharibika na kudhalilika wote.

Kwa sababu hiyo Uislamu umefanya pupa kuotesha fadhila katika nafsi za wafuasi wake, na kuwahimiza kushikamana nayo, Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) ameainisha lengo la mwanzo la kutumwa kwake kwa kauli yake: «Hakika nimetumwa kukamilisha matukufu ya tabia.» (Imepokewa na Al-Baihaqi).

Ni kama kwamba ujumbe wa Uislamu ambao umepanuka na kuenea katika zama na maeneo mengi ili kujenga ustaarabu mkubwa kuliko ambao mwanadamu amewahi kuujua. Mwenye nao akatoa juhudi kubwa katika kufikisha nuru yake na kuwakusanya watu pembezoni mwake.

Haiiti zaidi ya kutengeneza maadili ya mwanadamu na kutakasa ubora wao na kuamsha ukamilifu wa upeo wa macho yao.

Hivyo basi kutumwa kwake (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) ilikuwa ni kwa ajili ya maadili na kuyakuza, na kuzitakasa nafsi na kuzitoharisha, watu hapo kabla walikuwa katika upotofu mwingi zaidi ya maadili haya, hawayajui wala hawajali, Allah Aliyetukuka amesema: {Yeye ndiye aliye mpeleka Mtume kwenye watu wasio jua kusoma, awasomee Aya zake na awatakase, na awafunze Kitabu na hikima, ijapo kuwa kabla ya haya walikuwa katika upotofu ulio dhaahiri.} [62:2]

Allah amesema vile vile; {Kama tulivyo mtuma Mtume kwenu anaye tokana na nyinyi, anakusomeeni Aya zetu na kukutakaseni na kukufundisheni Kitabu na hikima na kukufundisheni mliyo kuwa hamyajui.} [2:151].

Misingi ya Kimaadili

"Kwa hakika misingi ya kimaadili katika Uislamu ni ya juu kabisa, na kuwa maadili ya Ummah zingine, zilizofuata dini ile zilibadilika baada ya muda mfano wa mabadiliko yale ya wale waliofuata dini ya Issa.

Matokeo muhimu ambayo tunaweza kuyapata na athari ile ya Qur-aan Tukufu katika ummah ambazo zilifuata hukumu zake: Dini ambazo zina yalio kwenye Uislamu kwa jinsi unavyotawala nafsi ni chache sana, na pengine huwezi kupata dini iliyoafikiana na yalioafikiana na Uislamu na kutokana na athari ya kudumu. Qur-aan ni msingi wa maisha huko Mashariki na tunaona athari yake katika maisha ya watu.!!!!

Gustaf Lubon

Mwanahistoria wa Kifaransa.

UHUSIANO WA IMANI NA TABIA NJEMA

Imani ni nguvu inayomsukuma muumini kwenye mambo mazuri na humzuia na mambo duni na makosa, hivyo udhaifu wa mwendo mwema kuhesabiwa kuwa ni dalili ya udhaifu wa imani, kama ambavyo tabia njema huhesabiwa kuwa ni dalili ya nguvu ya imani ya mtu, Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) amebainisha kuwa imani yenye nguvu mwishowe huzaa maadili mema ndani yake, na kuwa kuanguka kwa maadili hurejewa kutokana na udhaifu wa imani au kukosekana kwake.

Hivyo asiyekuwa na imani hufanya maovu, hajali chochote kile wala haogopi lawama, wala hadhani kuwa atalipwa kwa uovu wake, Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) amesema: «Kwa hakika haya na imani vimeambatanishwa, kimoja iwapo kikiondolewa basi na kingine kitaondolewa hivyo hivyo.» (Al-Baihaqi).

Bali Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) amefananisha tabia mbaya unayomfanyia jirani wako ni dalili ya kuzimika kwa imani (kupotea).

Anasema Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam); «Wallahi! Haamini, Wallahi haamini, Wallahi Haamini, (Masahaba) wakauliza: Ni nani huyo Ewe Mtume wa Allah, (Mtume akasema:Jirani ambae jirani yake hatasalimika na Bawaiq yake, (Masahaba) wakauliza: Ewe Mtume wa Allah ni nini maana ya Bawaiq yake? (Mtume) akasema: Shari zake.» (Al-Bukhari).

Hivyo basi pindi Allah anapowalingania waja wake katika kheri au kuwakataza shari anafanya hayo katika muktadha wa imani iliyotulia katika mioyo yao na mara ngapi Allah Aliyetukuka amesema katika kitabu chake: {Enyi Mlioamini!},

kisha baada ya hapo hutaja majukumu yao, mfano kauli yake: {Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kuweni pamoja na wakweli.} [9:119].

Vivyo hivyo tunamuona Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) anapowafundisha sahaba zake maadili mema huunganisha hilo na imani vilevile, mfano wa kauli yake (Swala Llahu 'alayhi wasallam):

«Atakayekuwa anamuamini Allah na Siku ya Mwisho basi na amkirimu mgeni wake, na mwenye kumuamini Allah na Siku ya Mwisho basi na amuhifadhi jirani yake, na atakaye kuwa anamuamini Allah na Siku ya Mwisho basi na aseme kheri au anyamaze.» (Ahmad).

Hivi ndivyo Uislamu unavyotegemea ukweli wa imani na ukamilifu wake katika kuotesha Fadhila katika nafsi.

https://www.path-2-happiness.com/sw

IBADA NA TABIA NJEMA

Ibada katika Uislamu si kauli zilizofichika au harakati zisizo na maana, bali ni matendo na kauli ambazo zinatakasa nafsi na kufanya maisha yawe mazuri, faradhi katika Uislamu zina lenga katika kumhuisha Muislamu katika maadili mema, na aendelee kushikamana na maadili haya, vyovyote vile hali na mazingira yatakavyobadilika, Qur-aan Tukufu na Sunnah iliotoharika zimetubainisha hakika hizi; kwa mfano Swala ni wajibu ambao lengo lake ni kuondoa maadili mabaya, maovu na munkari, amesema: {SOMA uliyo funuliwa katika Kitabu, na ushike Sala. Hakika Sala inazuilia mambo machafu na maovu. Na kwa yakini kumdhukuru Mwenyezi Mungu ndilo jambo kubwa kabisa. Na Mwenyezi Mungu anayajua mnayo yatenda.} [29:45]

Desturi Mbovu

“Inatosha aliyofanya Muhammad kuuondoshea Ummah wake uliokuwa duni kwenye kutoka kwenye makucha ya shetani na desturi mbovu. Hivyo kufungua mbele yao njia ya kupenda maendeleo, na kuwa sheria ya Muhammad itatawala Ulimwengu kwa kuambatana kwake na akili na hekima.”

Tolstoy

Mwanafasihi wa Kirusi



Zakkah katika Uislamu sio kodi inayochukuliwa kutoka kwa matajiri kwenda kwa masikini tu, bali ni mche unaopanda hisia za wema kwa mtu na upole, na kuimarisha uhusiano na kufahamiana baina ya watu wa tabaka tofauti, mbali na kutoharisha nafsi kutokana na uchafu na aibu, maovu, kujamiiana na kuelekea kwenye kiwango cha juu na heshima katika kuamiliana.

Hiyo ni hekima ya kwanza ya Zakkah, kama alivyosema Allah Aliyetukuka: {Chukua sadaka katika mali zao, uwasafishe na uwatakase kwazo, na uwaombee rehema. Hakika maombi yako ni utulivu kwao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mwenye kujua.}[9:103];

Na kwa ajili hiyo sadaka si kutoa mali, bali inakusanya idadi ya maadili ya juu ambayo yanachangia furaha ya jamii na watu wake, na Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) akapanua maana ya neno sadaka ambayo yampasa Muislamu afanye juhudi kutoa, Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) amesema:

«Kumimina kwako ndoo yako katika ndoo ya ndugu yako ni sadaka, na kuamrisha kwako mema na kukataza kwako maovu ni sadaka.» Katika riwaya nyingine: «Na kutabasamu kwako mbele ya uso wa ndugu yako ni sadaka, na kutoa mawe, mwiba na mfupa katika njia za watu ni sadaka, na kumuelekeza mtu aliyepotea njia ni sadaka.» (Al-Baihaqi).

Na funga hali kadhalika, Uislamu hauangalii kuwa ni kujinyima na kula na kunywa tu, bali umezingatia kuwa ni hatua ya kufikia hisia za ndani za mafukara na walionyimwa, na wakati huo huo huielekeza Nafsi na kumiliki matamanio yake, Allah Aliyetukuka amesema: {Enyi mlioamini! Mmeandikiwa Saumu, kama waliyo andikiwa walio kuwa kabla yenu ili mpate kuchamngu. } [2:183].

Akasema Mtume: «Ambaye hatoacha maneno machafu na kuyafanyia kazi, basi Allah hana haja ya mtu Yule kuacha chakula chake na kinywaji chake.» (Ahmad)

Na akasema tena: «Funga si kuacha kula na kunywa tu, bali funga kuacha upuuzi na uchafu, ikiwa yoyote atakutukana au akakufanyia ujinga, basi na useme: Mimi nimefunga, mimi nimefunga.» (Ibn Khuzaima).

Ama Hijja, mtu anaweza kudhania kuwa safari tupu (rihla) kwa maana ya kimaumbile; kwa yaliyomo ndani yake katika ibada za ghaib, na hili ni kosa; ambapo Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) anazungumzia kuhusu ibada hii;

{Hija ni miezi maalumu. Na anaye kusudia kufanya Hija katika miezi hiyo, basi asiseme maneno machafu wala asifanye vitendo vichafu wala asibishane katika Hija. Na kheri yoyote mnayo ifanya Mwenyezi Mungu anaijua. Na jitengezeeni zawadi. Na hakika bora ya zawadi ni uchamngu. Na nicheni Mimi, enyi wenye akili!} [2:197],

Na yote yaliyotangulia hubainisha umadhubuti wa uhusiano kati ya dini na tabia njema kwa hiyo, nguzo muhimu za Kiislamu kama vile Swala, Saumu, Zakah, Hijja, na utiifu mwingine katika Uislamu.

Zote hizo ni njia zenye kumfikisha mtu kwenye ukamilifu wa utu unaolengwa kumnyanyua mtu katika maisha mazuri ambapo ataneemeka kwa furaha na utulivu katika kivuli cha maadili mema na misingi mitukufu, kwa kuwa hizo ni ibada zenye kutofautiana katika matendo na mandhari yake. Lakini zote hizo zinakutana katika malengo aliyoyaweka Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) katika kauli yake: "Nimetumwa kukamilisha matukufu ya tabia." (Baihaq); Hivyo basi njia ya furaha ni njia inayojikita kwenye maadili inazunguka kwenye sayari yake wala ndani yake maadili hayajitengi kabisa na ibada.

Kanuni na Maadili

"Akida ya Kiislamu haitofautishi kati ya wajibu wa kisheria na ule wa wajibu wa tabia njema. Kwa hakika mjumuisho huu ulioratibiwa vizuri kati ya sheria na tabia njema huthibitisha nguvu ya mfumo huu tokea mwanzo."

Marcel Boisard

Mwanafikra wa Kifaransa.

https://www.path-2-happiness.com/sw

Kanuni za Pambanuzi Muhimu

"Qur-aan ina suluhisho la kadhia zote na kuunganisha kati ya sheria za kidini na zile za kimaadili. Huweka na kutengeneza mfumo mmoja wa kijamii na kupunguza kukata tamaa, nyoyo ngumu na uzushi. Kwa hakika unashughulikia kwenye kuunga mkono wanyonge, na kuamrisha watu kuhurumiana. Ama katika uwekaji wa sheria imeweka kanuni katika pambanuzi muhimu ili kusaidiana kila siku na ikaratibu mikataba na mirathi na miamala, ama katika uwanja wa familia umemuwekea kila mtu mfumo wa kuamiliana na watoto na watumwa, wanyama, afya na mavazi…..n.k.

Jack S.Rislor
Mtafiti wa Ufaransa.

AKHLAKI KATIKA UISLAMU

Njia ya furaha misingi yake ya kisheria, kimaadili na kiakida inasimama katika msingi wa maadili katika kila kitu, kuanzia kwenye kumfanyia adabu Allah Ta'ala, kupitia kwenye tabia na kuifanyia adabu nafsi, pamoja na marafiki, jamaa, ndugu na majirani, tabia njema pamoja na adui na hata kwenye vita, hadi (adabu) pamoja na wanyama na viumbe wengine, bali tabia njema pamoja na mazingira, miti na mimea, yote hayo yanakusanywa kwenye tabia njema katika mazungumzo, tabia njema katika matendo, tabia njema katika nyoyo na fahamu; Allah Aliyetukuka anasema akithibitisha misingi ya tabia njema katika mazungumzo: {…na semeni na watu kwa wema…} [2:83]

Na akizungumzia asili ya misingi katika maadili mema ya kimatendo Anasema: {Kinga maovu kwa kutenda yaliyo mema zaidi. Sisi tunajua wayasemayo.} [23:96],

Na mwenye kuchunguza kitabu cha Allah atakuta kumejaa maamrisho ya

tabia, zingatieni aya hizi zifuatazo, Allah Aliyetukuka amesema: {Ati yaweza kuwa malipo ya ihsani ila ihsani? } [55:60],

Na akasema Aliyetukuka: {… Wala msisahau fadhila baina yenu…} [2:237],

Na akasema tena Aliyetukuka: {… Lakini subira ni njema; na Mwenyezi Mungu ndiye wa kuombwa msaada kwa haya mnayo yaeleza.} [12:18],

Na akasema tena Allah: {…Na hakika Kiyama kitafika. Basi samehe msamaha mzuri.} [15:85],

Na akasema tena Aliyetukuka: {Shikamana na kusamehe, na amrisha mema, na jitenge na majaahili. } [7:199],

Na tena: {Na wanapo sikia upuuzi hujitenga nao na husema: Sisi tuna vitendo vyetu, na nyinyi mna vitendo vyenu. Salamun Alaikum, Amani juu yenu! Sisi hatutaki kujibizana na wajinga.} [28:55]

Na, {Mema na maovu hayalingani. Pinga uovu kwa lilio jema zaidi. Hapo yule ambaye baina yako naye pana uadui atakuwa kama rafiki jamaa wa kukuonea uchungu.} [41:34].

Tabia yake (Swala Llahu 'alayhi wasallam) ilikuwa ni Qur-aan, na vipi tabia yake isiwe hivyo wakati Allah Ta'ala akimsifu katika kauli yake: {Na hakika wewe una tabia tukufu. }[68:4];Kwa ajili hiyo ametumwa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) kwa ujumbe ambao umeweka maadili mema katika nafasi ya juu ambayo haijawekwa na wengine, Mtume (Swala

Uzushi na Fedheha

"Wanadai wenye kasumba kuwa Muhammad hakutaka ila umaarufu wake binafsi na kujifakharisha na utawala.
Sivyo kabisa, naapa kwa Mungu ndani ya kifua cha bwana mkubwa yule mtoto wa jangwani, ni mwenye nafsi kubwa iliyojua huruma, kheri, wema, mapenzi na hekima, mwenye fikra zisizo kuwa na tamaa ya kidunia, na nia yake ilikuwa ni kinyume na kutafuta utawala na hadhi na kwa nini isiwe hivyo hali ya kuwa ile ni nafsi safi ya mtu miongoni mwa watu wenye uaminifu, ikhlasi na umakini mkubwa."

Thomas Carlyle

Mwanahistoria na Mkosoaji wa Scotland.

Uadilifu na Usafi

"Maandalizi ya mtu huyu kwa kuvumilia mateso kwa ajili ya itikadi zake na tabia zake tukufu kwa wale waliomuamini wakamfuata na kumzingatia kuwa bwana na kiongozi wao, kwenye upande wa mafanikio makubwa aliyoyapata, yote hayo yanaonyesha usafi wa uadilifu wa usafi wa asili katika haiba yake. Hivyo yale madai kuwa Muhammad anajidai ni jambo lenye kuashiria matatizo zaidi wala halitatui. Bali hakuna mtu katika watu wakubwa katika historia ya watu wa Magharibi aliyepata heshima kubwa mfano wa Muhammad."

W. Montgomery Watt

Mustashrik wa Uingereza.

Llahu 'alayhi wasallam) amesema:

«Ukamilifu wa waumini kwa imani ni ukamilifu wao wa tabia njema, na mbora wao ni mbora kwa wanawake wake.» (Baihaqi).

Na akasema tena (Swala Llahu 'alayhi wasallam) :

«Wema ni tabia njema, na dhambi ni kile chenye kuwasha kifuani mwako, na ukachukia watu kukiona.» (Muslim).

Kadhalika amesema:

«Kwa hakika uchafu na kujichafua havimo katika Uislamu kwa vyovyote vile, na mbora wa watu katika Uislamu ni mbora wao kwa tabia.» (Ahmad).

Katika hadithi nyingine amesema: «Hakuna kitu kizito katika mizani ya muumini Siku ya Kiama kuliko tabia njema, na ya kuwa Allah humchukia muovu mchafu.» (Baihaqi).

Na amesema tena:

«Hakika Mpendwa wenu zaidi kwangu ni wa karibu yenu zaidi kwangu ni mzuri wenu zaidi wa tabia, na ninayemchukia miongoni mwenu na aliye mbali nami zaidi miongoni mwenu akhera ni mbaya wenu na mwenye maneno mengi, wenye kujikalifisha katika mazungumzo, na wenye kujaza vinywa vyao maneno kwa kiburi.» (Ahmad)

Na maadili katika Uislamu ni jambo pana lililokamilika linaanza kwa:



KUMFANYIA ALLAH TABIA NJEMA

Kumfanyia Allah tabia njema inakusanya mambo matatu:-

Kwanza: Kumuamini na kupokea habari zake kwa kuziamini; Allah Aliyetukuka amesema kuhusu nafsi yake: {Mwenyezi Mungu, hapana mungu isipo kuwa Yeye. Kwa yakini atakukusanyeni Siku ya Kiyama. Halina shaka hilo. Na ni nani msema kweli kuliko Mwenyezi Mungu?} [4:87],

Kukubali maneno ya Allah kunampelekea mtu kumuamini Yeye, kumtetea, na kufanya jihadi katika njia yake, kiasi cha kutoingia shaka katika nafsi yake au utata katika habari zake Allah Aliyetukuka au habari za Mtume (Swala Llahu ʻalayhi wasallam).

Pili: Ni mtu kupokea hukumu za Allah kwa kuzikubali na kuzitekeleza, kwa hiyo hakatai chochote katika hukumu za Allah, na akikataa chochote katika hukumu za Allah basi huo ni ukosefu wa adabu kwa Allah Aliyetukuka; ndio maana Allah amekataza kutanguliza rai yetu au matamanio yetu juu ya maneno yake, Allah Aliyetukuka amesema: {Enyi mlio amini! Msitangulie mbele ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua.} [49:1].

Louis Saidou

Mustashrik wa Kifaransa

Dina ya Maadili

"Hakuna aya ambayo utaikuta katika Qur-aan ila ayah hiyo inapelekea katika mapenzi makubwa kwa Mungu na himizo kubwa katika mambo mema kupitia misingi hiyo mahususi kwa mfumo wa kimaadili, ndani yake kuna wito mkubwa wa kuhurumiana na makusudio mema na kupatana kutokana na kushutumiana. Hata hivyo ndani yake kuna kujiona na ghadhabu na ishara kuwa dhambi huenda ikawa ni kwa kufikiri na kuangalia na ndani yake kuna himizo katika kutimiza ahadi hata ikiwa ni pamoja na makafiri. Kuwa mpole na kunyenyekea. Maneno yote hayo yaliokusanya ambayo yamejaa yanatosha kuwa ni hekima na muongozo kwa kuthibitisha usafi wa misingi ya kimaadili katika Qur-aan. Kwa kuwa ndio yenye kuona kila kitu."

Tatu: Kupokea Kudura za Allah kwa kuridhika na kusubiri, kwani tabia njema kwa Allah kwenye kudura zake ni mwanadamu kuridhia, kujisalimisha na kutulia kwa ajili ya kudura za Allah na hukumu zake; kwa ajili hii Allah amewasifu wenye kusubiri. Amesema: {Wale ambao ukiwasibu msiba husema: Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake Yeye hakika tutarejea.} [2:156].

TABIA NJEMA PAMOJA NA WATU

Allah ameamrisha kila mtu afanyiwe wema, na haswa wazazi wawili, na ndugu wa karibu, nao ni ndugu wa nasaba ambao inapasa kuwaunga, na majirani, Allah Aliyetukuka amesema: {Na tulipo funga agano na Wana wa Israili: Hamtamuabudu yeyote ila Mwenyezi Mungu; na muwafanyie wema wazazi na jamaa na mayatima na masikini, na semeni na watu kwa wema, na shikeni Sala, na toeni Zaka. Kisha mkageuka isipo kuwa wachache tu katika nyinyi; na nyinyi mnapuuza.} [2:83]

Na akasema tena, {Sio wema kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi. Bali wema ni wa anaye muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii, na anawapa mali, kwa kupenda kwake, jamaa na mayatima na masikini na wasafiri, na waombao, na katika ugombozi, na akawa anashika Sala, na akatoa Zaka, na wanao timiza ahadi yao wanapo ahidi, na wanao vumilia katika shida na dhara na wakati wa vita; hao ndio walio sadikisha, na hao ndio wajilindao.} [2:177],

Na kadhalika katika aya zifuatazo: {Wanakuuliza watoe nini? Sema: Kheri mnayo itoa ni kwa ajili ya wazazi na jamaa na mayatima na masikini na wasafiri. Na kheri yoyote mnayo ifanya Mwenyezi Mungu anaijua.} [2:215],

Na, {Na walio amini wakahama na wakapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na walio toa mahala pa kukaa na wakanusuru, hao ndio Waumini wa kweli. Watapata msamaha wa Mwenyezi Mungu na kuruzukiwa kwema. Na watakao amini baadaye na wakahajiri, na wakapigana Jihadi pamoja nanyi, basi hao ni katika nyinyi. Na jamaa wa nasaba wanastahikiana wenyewe kwa wenyewe zaidi katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua kila kitu.} [8:74-75],

Na, {Muabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na chochote. Na wafanyieni wema wazazi wawili na jamaa na mayatima na masikini na jirani

wa karibu na jirani wa mbali, na rafiki wa ubavuni na mpita njia, na walio milikiwa na mikono yenu ya kulia. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wenye kiburi wanao jifakhiri} [4:36]

Vile vile amesema Aliyetukuka: {Hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha kufanya uadilifu, na hisani, na kuwapa jamaa; na anakataza uchafu, na uovu, na dhulma. Anakuwaidhini ili mpate kukumbuka.} [16:90],

Na, {Na Mola wako Mlezi ameamrisha kuwa msimuabudu yeyote ila Yeye tu, na wazazi wawili muwatendee wema. Mmoja wao akifikia uzee, naye yuko kwako, au wote wawili, basi usimwambie hata: Ah! Wala usiwakemee. Na sema nao kwa msemo wa hishima. Na uwainamishie bawa la unyenyekevu kwa kuwaonea huruma. Na useme: Mola wangu Mlezi! Warehemu kama walivyo nilea utotoni. Mola wenu anajua kabisa yaliyo nyoyoni mwenu. Ikiwa nyinyi mtakuwa wema, basi hakika Yeye ni Mwenye kuwaghufiria wanao tubia kwake. Na mpe aliye jamaa yako haki yake, na masikini, na msafiri; wala usitumie ovyo kwa fujo. Hakika wabadhirifu ni ndugu wa Mashet'ani. Na Shet'ani ni mwenye kumkufuru Mola wake Mlezi. Na ikiwa unajikurupusha nao, nawe unatafuta rehema ya Mola wako Mlezi unayo itaraji, basi sema nao maneno laini. } [17:23-28],

Na akasema Aliyetukuka: {Basi mpe jamaa haki yake, na masikini, na msafiri. Hayo ni kheri kwa watakao radhi ya Mwenyezi Mungu. Na hao ndio wenye kufanikiwa.} [30:38],

Na, {Enyi watu! Mcheni Mola wenu Mlezi aliye kuumbeni kutokana na nafsi moja, na akamuumba mkewe kutoka nafsi ile ile. Na akaeneza kutokana na wawili hao wanaume na wanawake wengi. Na tahadharini na Mwenyezi Mungu ambaye kwaye mnaombana, na jamaa zenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwaangalieni.} [4:1]

Na akasema vile vile : {Basi yanayo tarajiwa kwenu mkitawala ndio mfisidi katika nchi na mwatupe jamaa zenu?} [47:22]

Na, {Je! Anaye jua ya kwamba yaliyo teremshwa kwako kutoka kwa Mola wako Mlezi ni Haki ni sawa na aliye kipofu? Wenye akili ndio wanao zingatia, Wale ambao wanatimiza ahadi ya Mwenyezi Mungu, wala hawavunji maagano. Na wale ambao huyaunga aliyo amrisha Mwenyezi Mungu yaungwe, na wanaikhofu hisabu mbaya. Na ambao husubiri kwa kutaka radhi ya Mola wao Mlezi, na wakashika Sala, na wakatoa, kwa siri na kwa uwazi, katika tulivyo wapa; na wakayaondoa maovu kwa wema. Hao ndio watakao pata malipo ya Nyumba ya Akhera. Nayo ni Bustani za milele, wataziingia wao na walio wema miongoni mwa baba zao, na wake zao, na vizazi vyao. Na Malaika wanawaingilia katika kila mlango. (Wakiwaambia) Assalamu Alaikum! Amani iwe juu yenu, kwa sababu ya mlivyo subiri! Basi ni mema mno malipo ya Nyumba ya Akhera. Na wale wanao vunja ahadi ya Mwenyezi Mungu baada ya kuzifunga, na wanakata aliyo amrisha Mwenyezi Mungu yaungwe, na wanafanya fisadi katika nchi: hao ndio watakao pata laana, na watapata Nyumba mbaya.} [13:19-25].

Maadili mema katika Uislamu hayahusiani na rafiki jamaa wa karibu na jirani tu, bali inawavuka hao hadi kufika kwenye tabia njema pamoja na adui, hata ikiwa adui huyo ni anaepigana vita nawe! Maadili haya humuenea kila mtu, Allah Aliyetukuka amesema: {Mema na maovu hayalingani. Pinga uovu kwa lilio jema zaidi. Hapo yule ambaye baina yako naye pana uadui atakuwa kama rafiki jamaa wa kukuonea uchungu.} [41:34],

Allah ameamrisha kuwafanyia uadui wale ambao wanatupiga vita nao, amesema Ta'ala: {Na piganeni katika Njia ya Mwenyezi Mungu na wale wanao kupigeni, wala msianze uadui. Kwani Mwenyezi Mungu hawapendi waanzao uadui.} [2:190],

Angalia maadili ya Kiislamu pamoja na adui anayepigana nasi, katika amri zake (Swala Llahu 'alayhi wasallam) pamoja na jeshi lake linalotoka kwa ajili ya kupigana jihadi katika njia ya Allah kupigana na adui; amesema Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam):

«Msifanyiane hila, wala msipetuke mipaka, wala msiue kwa kutesa, wala msiuwe watoto wala watu wa mahekalu (wasiojishughulisha na vita).» (Ahmad).

Ajabu amri ya dini hii yenye kuamrisha maadili haya pamoja na maadui wanaotupiga vita, ama asiyekuwa mpiganaji (hata kama ni adui) Allah ameamrisha wafanyiwe wema na uadilifu, Allah Ta'ala amesema: {Mwenyezi Mungu hakukatazini kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakukupigeni vita, wala hawakukutoeni makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu.} [60:8]

TABIA NJEMA PAMOJA NA WANYAMA

Uislamu umeleta tabia njema hadi kwa wanyama, kwa sababu Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) amesema: «Mwanamke aliadhibiwa juu ya paka, alimfunga hadi akafa, kwa sababu hiyo akaingia motoni, hakumlisha wala kumyywesha alipomfunga, wala hakumuacha ale katika majani ya ardhi.» (Imepokewa na Al-Bukhari).

Bali Allah amewajibisha kufanyiwa wema hata katika kuchinjwa wanyama, amesema Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam): «Hakika Allah ameamrisha wema katika kila kitu, mkiua ueni vizuri na mkichinja chinjeni vizuri, na mmoja wenu anoe kisu chake, na akipe raha kichinjo chake.» (Imepokewa na Muslim).

Thomas Arnold.

Mustashrik wa Uingereza.

Hakika Waumini Wote ni Ndugu

"Mfano mzuri wa udugu kwa waumini wote katika Uislamu ndio uliowavuta watu wengi kwa kwa kuingia katika imani hii."

TABIA NJEMA PAMOJA NA MAZINGIRA

Pia Uislamu umeleta adabu hata pamoja na mazingira na mandhari yote; hivyo unalingania kutofanya ubadhirifu; na hivyo kutoharibu vyanzo vya asili, Allah Ta'ala amesema: {….Kuleni na mnywe riziki ya Mwenyezi Mungu, wala msiasi katika nchi mkafanya uharibifu.} [2:60]

Na akasema tena Aliyetukuka: {Wala msit'ii amri za walio pindukia mipaka, Ambao wanafanya ufisadi katika nchi, wala hawatengenezi.} [26:151-152],

Kadhalika vyanzo vingine vya asili kama vile maji na mfano wake ambao Uislamu umeupa nafasi kubwa, Allah Ta'laa amesema: {Je! Hao walio kufuru hawakuona kwamba mbingu na ardhi zilikuwa zimeambatana, kisha Sisi tukazibabandua? Na tukajaalia kwa maji kila kilicho hai? Basi je, hawaamini?} [21:30]

Na akasema vile vile: {Na Mwenyezi Mungu ameteremsha maji kutoka mbinguni na kwa hayo akaihuisha ardhi baada ya kufa kwake. Kwa hakika katika hayo imo Ishara kwa watu wanao sikia.} [16:65].

Mbali na Qur-aan Tukufu, Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) amehimiza umuhimu wa kulinda mazingira na vilivyomo ambapo tunaona katika Sunnah yake lingano linalokaririwa mara kwa mara la kuhifadhi mazingira; hivyo basi kuweka mipaka katika kulinda mazingira mfano: mmomonyoko wa ardhi, ukame na kuzuia kupanuka kwa majangwa; na mfano wa hayo Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) amesema:

«Epukeni vitatu vyenye kulaani: kujisaidia kwenye mapito ya maji na katikati ya njia, na kivuli.» (Imepokewa na Abu Dawuud).

Amesema tena Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam):

«Hakuna Muislamu yoyote anapanda mmea au anaotesha mche, akala kwenye huo ndege au mwanadamu au mnyama, ila hiyo itakuwa ni sadaka yake.» (Imepokewa Muslim).

Katika hadithi nyingine Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) amesema: «Kitakaposimama kiama na mmoja wenu akawa na mmea akiweza kabla ya kiama kusimama na kuupanda basi na afanye.» (Imepokewa na Ahmad).

Wakati mmoja Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) alipita na Sa'ad alikuwa akitawadha; Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) akasema:

«Ni Israfu gani hii? (Sa'ad) akasema: Je, katika udhu kuna Israfu?! (Mtume) akasema: Ndio na hata ingekuwa katika mto unaotembea.» (Imepokewa na Ibn Majah).

Uislamu na Mazingira

"Katika Qur-aan Tukufu hakuna kutenganisha kati ya mwanadamu na mazingira. Ulimwengu wa Kiislamu unalea hazina zilizojazana kutokana na hekima na maarifa aliyozawadiwa mwanadamu."

Prince Charles
Mwanafalme wa Uingereza

https://www.path-2-happiness.com/sw

Na haya ndio waliyoyafanya wenyewe katika kutendea wema mazingira hata katikati ya vita dhidi ya adui yao, Abu Bakr (Radhiya Llahu 'anhu) alimuusia jemedari wa vita kwa kumwambia: "Msiue watoto, wala mwanamke, wala mzee, wala msikate mti wenye matunda, wala msichinje mbuzi au ng'ombe ila kwa ajili ya kula wala msivunje jengo wala msikate mtende wala msichome moto." (Imepokewa na Malik).

MIONGONI MWA USIA WA KIMAADILI

Tunapendelea hapa kuonesha idadi ya wasia wa kimaadili zilizokuja katika kitabu cha Allah na Sunnah ya Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) miongoni mwa hizo ni:

Kutoka katika Qur-aan Tukufu;

Allah amesema: {Hakika Mwenyezi Mungu anakuamrisheni mzirudishe amana kwa wenyewe. Na mnapo hukumu baina ya watu mhukumu kwa uadilifu. Hakika haya anayo kuwaidhini Mwenyezi Mungu ni mazuri sana. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kusikia, Mwenye kuona.} [4:58]

Na akasema tena Aliyetukuka: {Sema: Njooni nikusomeeni aliyo kuharimishieni Mola wenu Mlezi. Nayo ni kuwa, msimshirikishe Yeye na chochote. Na wazazi wenu wafanyieni wema. Wala msiwauwe watoto wenu kwa sababu ya umasikini. Sisi tunakuruzukuni nyinyi na wao. Wala msikaribie mambo machafu, yanayo onekana, na yanayo fichikana. Wala msiuwe nafsi ambayo Mwenyezi Mungu ameharimisha kuiuwa, ila ikiwa kwa haki. Hayo amekuusieni ili myatie akilini. Wala msiyakaribie mali ya yatima ila kwa njia ya wema kabisa, mpaka afikilie utu-uzima. Na timizeni vipimo na mizani kwa uadilifu. Sisi hatumkalifishi mtu ila kwa kadiri ya uwezo wake. Na msemapo semeni kwa uadilifu ingawa ni jamaa. Na ahadi ya Mwenyezi Mungu itekelezeni. Hayo amekuusieni ili mpate kukumbuka. Na kwa hakika hii ndiyo Njia yangu Iliyo Nyooka. Basi ifuateni, wala msifuate njia nyingine, zikakutengeni na Njia yake. Haya amekuusieni ili mpate kuchamngu.} [6:151-153]

Tena akasema: {Wala msifanye uharibifu katika nchi baada ya kuwa imekwisha tengenezwa. Na muombeni kwa kuogopa na kwa kutumai. Hakika rehema ya Mwenyezi Mungu iko karibu na wanao fanya mema.} [7:56],





Akasema Aliyetukuka: {Na subiri, kwani Mwenyezi Mungu hapotezi ujira wa wanao fanya wema.} (11:115),

Akasema Aliyetukuka: {Wala usiufanye mkono wako kama ulio fungwa shingoni mwako, wala usiukunjue wote kabisa, utabaki ukilaumiwa muflisi. Hakika Mola wako Mlezi humkunjulia riziki amtakaye, na humpimia amtakaye. Hakika Yeye kwa waja wake ni Mwenye kuwajua na kuwaona. Wala msiwauwe wana wenu kwa kuogopa umasikini. Sisi tunawaruzuku wao na nyinyi. Hakika kuwaua hao ni khatia kubwa. Wala msikaribie uzinzi. Hakika huo ni uchafu na njia mbaya. Wala msiuwe nafsi ambayo Mwenyezi Mungu amekataza isipo kuwa kwa haki. Na aliye uliwa kwa kudhulumiwa basi tumempa madaraka mrithi wake. Lakini asipite mpaka katika kuuwa. Kwani yeye anasaidiwa. Wala msiyakaribie mali ya yatima, isipo kuwa kwa njia iliyo bora, mpaka afike utuuzimani. Na timizeni ahadi. Kwa hakika ahadi itasailiwa. Na timizeni kipimo mpimapo. Na pimeni kwa mizani zilizo sawa. Hayo ni wema kwenu na khatimaye ndio bora. Wala usiyafuate usiyo na ujuzi nayo. Hakika masikio, na macho, na moyo - hivyo vyote vitasailiwa. Wala usitembee katika ardhi kwa maringo. Hakika wewe huwezi kuipasua ardhi wala kufikia urefu wa milima. Haya yote ubaya wake ni wenye kuchukiza kwa Mola wako Mlezi. Haya ni katika hikima alizo kufunulia Mola wako Mlezi. Wala usimweke pamoja na Mwenyezi Mungu mungu mwengine, usije ukatupwa katika Jahannamu ukilaumiwa na kufurushwa.} [17:29-39],

Na akasema Aliyetukuka: {Na yakimbilieni maghfira ya Mola wenu Mlezi, na Pepo ambayo upana wake ni mbingu na ardhi, iliyo wekwa tayari kwa wachamngu, Ambao hutoa wanapo kuwa na wasaa na wanapo kuwa na dhiki, na wanajizuia ghadhabu, na wasamehevu kwa watu; na Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao wema} [3:133-134]

Na kadhalika akasema Aliyetukuka: {Enyi mlio amini! Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao, wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao. Huenda hao wakawa bora kuliko wao. Wala msivunjiane hishima, wala msiitane kwa majina ya kejeli. Ni uovu kutumia jina baya baada ya kwisha amini. Na wasio tubu, hao ndio wenye kudhulumu. Enyi mlio amini! Jiepusheni na dhana nyingi, kwani baadhi ya dhana ni dhambi. Wala msipelelezane,

wala msisengenyane nyinyi kwa nyinyi. Je! Yupo katika nyinyi anaye penda kuila nyama ya nduguye aliye kufa? Mnalichukia hilo! Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea toba, Mwenye kurehemu. Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamngu zaidi katika nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye khabari.} [49:11-13].

Na akasema Aliyetukuka: {Ewe mwanangu! Shika Sala, na amrisha mema, na kataza maovu, na subiri kwa yanayo kupata. Hayo ni katika mambo ya kuazimiwa.. Wala usiwabeuwe watu, wala usitembee katika nchi kwa maringo. Hakika Mwenyezi Mungu hampendi kila anaye jivuna na kujifakhirisha. Na ushike mwendo wa katikati, na teremsha sauti yako. Hakika katika sauti mbaya zote bila ya shaka iliyo zidi ni sauti ya punda.} [31:17-19].

Na akasema tena: {Na waja wa Arrahman Mwingi wa Rehema ni wale wanao tembea ulimwenguni kwa staha, na wajinga wakiwasemeza hujibu: Salama!} [25:63],

Na akasema tena Aliyetukuka: {Muabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na chochote. Na wafanyieni wema wazazi wawili na jamaa na mayatima na masikini na jirani wa karibu na jirani wa mbali, na rafiki wa ubavuni na mpita njia, na walio milikiwa na mikono yenu ya kulia. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wenye kiburi wanao jifakhiri} [4:36]

Na, {Basi ni kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu ndio umekuwa laini kwao. Na lau ungeli kuwa mkali, mwenye moyo mgumu, bila ya shaka wangeli kukimbia. Basi wasamehe, na waombee maghfira, na shauriana nao katika mambo. Na ukisha kata shauri basi mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanao mtegemea.} [3:159].

KUTOKA KATIKA SUNNAH TUKUFU

Tukienda katika bustani ya hadithi tukufu za Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) tunapata kuwa ndani yake kuna miti mingi ya imani ambayo tunaweza kuchuma ndani yake kwenye matunda yaliyoiva ya maadili, mema na misingi bora, katika hiyo:

Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) amesema:

«Ameharamishwa motoni kila mnyonge, laini, mwepesi aliyekaribu na watu.» (Al-Tirmidhi).

Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) alimwambia mmoja wa maswahaba zake:

«Hakika ndani yako kuna tabia tukufu na upole na usubirifu.» (Ahmad).

Na akasema vile vile: «Kheri yoyote nilionayo sitoihifadhi dhidi yenu, (yaani kuwa nyinyi kwa nyinyi), na mwenye kujizuia (kuomba) Allah atamzuia, na mwenye kujihifadhi Allah atamtosheleza na mwenye kusubiri Allah atamsubirisha, na hakupewa yoyote kitu cha kheri na kikunjufu zaidi kuliko subira.» (Imepokewa na Muslim). Na akasema Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam): «Utajiri sio wingi wa mali, bali utajiri ni utajiri wa nafsi.» (Al-Bukhari).

Na akasema Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam): «Mkali sio kwa kukabana (na watu), lakini mkali ni ambaye anamiliki nafsi yake wakati wa ghadhabu.» (Al-Bukhari). Na akasema (Swala Llahu 'alayhi wasallam): «Hamshukuru Allah asiyewashukuru watu.» (Ahmad).

Katika hadithi zingine amesema: «Hakika Allah ameniteremshia wahyi kuwa muwe wapole, wala baadhi yenu wasiwadhulumu wengine.» (Imepokewa na Ibn Majah).

Akasema: «Kila jema ni sadaka, na miongoni mwa mema ni kukutana na nduguyo kwa uso mkunjufu, na kumimina kwenye ndoo yako katika ndoo ya nduguyo.» (Imepokewa na Al-Tirmidhi).

Mwishowe utaona kuwa uhusiano baina ya furaha ya kweli na tabia njema na uhusiano madhubuti ulioshikamana na kuambatana vizuri; hivyo basi tabia njema ni chanzo pekee cha furaha ya mwanadamu na bila hiyo hakuna furaha, na mwanadamu hatochuma katika maisha yake isipokuwa maovu na matarajio mabaya, hivyo basi furaha ni kichocheo muhimu kwa mwanadamu kuelekea kwenye tabia njema kwa sababu anajua kwa elimu ya yakini kuwa bila ya tabia njema hatofanikiwa furaha ya kweli na siku yenye furaha.

https://www.path-2-happiness.com/sw

NJIA YA REHEMA NA UTUKUFU

Yaliyomo

NJIA YA REHEMA NA UTUKUFU
Njia ya rehema
Njia ya rehema na utukufu

NJIA YA REHEMA NA UTUKUFU

NJIA YA REHEMA:

Sura nyingi katika Qur-aan zimeanza kwa kutaja majina mawili ya Allah (Rahmanir Rahiym) katika kila sura, na Mwenyezi Mungu akajiandikia mwenyewe rehema: {…Mola wenu Mlezi amejilazimisha rehema…}[6:54],

Na rehema yake imeenea kila kitu: {…Na rehema yangu imeenea kila kitu….} [7:156],

Na watu wakajipendekeza katika rehema yake na akawabashiria nayo na akawatahadharisha kutokata tamaa: {Sema: Enyi waja wangu walio jidhulumu nafsi zao! Msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu husamehe dhambi zote. Hakika Yeye ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.} [39:53];

Ni yeye Aliyetakasika ni mwingi wa rehema hupenda kusamehe; amesema (Swala Llahu ‘alayhi wasallam). «Hakika Allah Ta’ala hukunjua mkono wake usiku ili watubie mkosaji wa mchana, na hupanua mkono wake mchana ili watubie waliokosa usiku hadi linyanyuke jua kutoka Magharibi yake.» (Muslim).

Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) akatujulisha kuhusu Mola wake, kasema: «Hakika Allah ameandika kitabu (Qur-aan) kabla hajaumba viumbe kuwa rehema yangu imetangulia ghadhabu yangu.» (Bukhari na Muslim).

Amesema Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) kuhusu rehema ya Mola wake: «Allah amejaalia rehema katika sehemu mia moja, akashusha sehemu tisini na tisa, na akateremsha ardhini sehemu moja, katika sehemu hiyo moja ndio wanayohurumiana viumbe kiasi cha kumfanya farasi akanyanyua mguu wake kwa kuhofia kumkanyaga mwanae.» (Al-Bukhari).

Allah akamtuma Nabii wake (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) kuwa ni rehma (huruma) kwa walimwengu: {Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote.}[21:107];

Na akaipendezesha kwa tabia njema za juu; hivyo Allah

akasema: {Na hakika wewe una tabia tukufu.} [68:4],

Na hiyo ilikuwa ni katika tabia zake ziliopambanuliwa yeye Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) ni hiyo Rehema; vinginevyo wangetawanyika walio pembizoni mwake na kumuacha peke yake. Allah Ta'ala amesema: {Basi ni kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu ndio umekuwa laini kwao. Na lau ungeli kuwa mkali, mwenye moyo mgumu, bila ya shaka wangeli kukimbia….} [3:159],

Bali yeye Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) ni Mpole, mwenye huruma, hatakii tabu Ummah wake (Swala Llahu 'alayhi wasallam), Allah Ta'ala amesema: {Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayo kutaabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma.} [9:128].

Hivyo basi Uislamu uliokuja kutoka kwa mwingi wa Rehema Aliyetakasika na akatumwa nao Mwingi wa rehema kwa Ummah wake (Swala Llahu 'alayhi wasallam) na kuwa ni rehema kwa Walimwengu, kuwatoa katika uovu wa udhalimu na chuki, na kuwatoa kwenye aina za huzuni, wasiwasi, woga, katika njia ya kulipiana kisasi, makosa, ukandamizaji na udikteta, akaja kama rehema kwa Walimwengu: {Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote.}[21:107].

Ni rehema kwa Waislamu na rehema kwa wasiokuwa Waislamu, ni rehema kwa wanaotii na ni rehema kwa wenye inadi, ni rehema kwa wakubwa, wadogo, wanaume, wanawake, watoto, matajiri kwa masikini, ni rehema kwa Walimwengu.

Na hivyo Uislamu ukaja kwa kuomba rehema na kutamanisha na

https://www.path-2-happiness.com/sw

kuusiana, Allah amesema: {Tena awe miongoni mwa walio amini na wakausiana kusubiri na wakausiana kuhurumiana.} [90:17]

Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) amesema: «Allah hamrehemu asiyehurumia watu.» (Bukhari na Muslim).

Na akasema (Swala Llahu 'alayhi wasallam): «Wenye kuhurumia atawahurumia Rahmaan, Wahurumieni waliopo ardhini mtahurumiwa na Aliye mbinguni, Kizazi (udugu) ni huruma kutoka kwa Rahmaan atakayekiunga Allah atamuunga na atakayekikata Allah atamkata.» (Al-Tirmidhi).

Na akasema Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam), «Rehema haiondolewi isipokuwa kwa muovu.» (A-Tirmidhi); Kwa hiyo, Allah akaamrisha Rehma na akahimiza hilo kwa sifa ya ujumla, kama vile tabia na mfumo wa maisha na sheria ikahusisha aina maalumu za huruma miongoni mwa hizo:-

1. Huruma kwa watu wote: Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) akawa ni mwenye huruma kwa Ummah wake, Allah aliwaongoa kupitia Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) kutoka katika kiza kwenda kwenye nuru, na kutoka kwenye uovu hadi kwenye furaha lakini huruma yake Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) ilipita hayo na hadi akahimiza huruma kwa Makafiri ambao bado hawajasilimu, Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) alisema kuhusu watu wa Makkah ambao hawajasilimu: «…Bali natarajia Allah atoe migongoni mwao wenye kumuabudu Allah peke yake wala hatomshirikisha chochote.» (Bukhari na Muslim). Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) alipojeruhiwa katika vita vya Uhud, Maswahaba wake walimwambia, "(waapize) washirikina adhabu; Mtume (akaomba); «Ewe Mola wangu! waongoze watu wangu kwani hawajui», na katika riwaya: ikasemwa Ewe Mtume wa Allah; "Waombee adhabu Washirikina." Mtume akasema: «Sijatumwa kulaani, bali nimetumwa kuwa Rehema.» (Muslim).

2. Huruma kwa Wadogo; Mmoja katika Sahaba za Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) amesema:« Tuliingia pamoja na Mtume wa Allah kwa Ibrahim nae akiwa anaugulia, macho ya Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) yakawa yamelengwa na machozi, AbdurRahman bin Auf akasema, " Na wewe Mtume wa Allah? Akasema (Mtume), "Ewe Ibn Auf hiyo ni Rehma," Kisha akasema: "Kwa hakika macho yanatoka machozi, na moyo unahuzunika, wala hatusemi ila lile linalomridhisha Mola wetu, na kwa hakika kuachana nawe Ibrahim tunahuzunika sana.» (Bukhari na Muslim).

Bali Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) alikuwa akimkalisha Usama katika paja lake na Al-Hassan katika paja lake lingine, kisha huwakumbatia na kusema: "Ewe Mola wangu wahurumie kwani mimi ninawahurumia." Mtu mmoja alipoingia kwa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) akamuona Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) akimbusu Al-Hassan au Al-Hussein, akamwambia: "Je, mnawabusu watoto wenu?!, Mimi nina watoto kumi sijawahi kumbusu yeyote kati yao, Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) akasema: "Asiyehurumia hatohurumiwa."

3. Kuwahurumia Wanyonge; Wakati Fulani Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) alimtafuta mwanamke mmoja mweusi aliyekuwa akisimamia msikiti, akamuulizia wakasema: «Amekufa", akasema: "Kwanini hamkunijulisha? Nielekezeni lilipo kaburi lake." Wakamuonesha nae akamswalia.» (Al-Bukhari na Muslim). Mtumishi wa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) Anas bin Malik (r.a.) amesema: «Nimemtumikia Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) kwa muda wa miaka kumi hakuwahi kuniambia Aah, wala kwa nini umefanya, au kwa nini hukufanya.» (Al-Bukhari).

Sahaba Mtukufu Ibn Masuud anasema;"Nilikuwa nikimpiga kijana wangu nikasikia sauti kutoka nyuma yangu ikisema: "Fahamu Ewe Abu Masuud Allah ana uwezo zaidi juu yako kuliko uwezo wako juu yake, nilipogeuka nikamuona Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam), nikasema: «Ewe Mtume wa Allah yeye yupo huru kwa ajili ya Allah, Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) akasema: Kama usingefanya hivyo basi moto ungekubabua au ungekushika.» (Muslim).

Huruma kwa Wanyama: Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) alipita akamuona mnyama mgongo wake umekutana na tumbo lake, akasema: «Muogopeni Allah kwa wanyama hawa (wasioweza kuzungumza), wapandeni wakiwa wazima, na waleni wakiwa wazima.» (Abu Dawuud).

Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) alipoingia katika nyumba ya Mtu katika Answar alimuona ngamia, Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) alipomuona alianza kunung'unika na machozi kumtoka, Mtume akamuendea na kufuta machozi yake, akanyamaza, (Mtume) akasema: «Ni nani mwenye ngamia huyu?, Ni ngamia wa nani? Akaja kijana wa Kianswari, akasema: Ni wangu Ewe Mtume wa Allah, akasema: Je, humuogopi Allah kwa mnyama huyu aliyekumilikisha Allah, amenishitakia kuwa unamnyima chakula na unamtelekeza.» (Abu Dawuud).

Hii ni mifano ya kutumwa kwake Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) kuwa ni rehema kwa Walimwengu, vinginevyo ubainifu wa rehema na utekelezaji wake katika Uislamu ni mwingi sana ambao unabainisha njia ya dini hii, lakini rehma hii haina maana ya udhalili bali ni rehma ya utukufu.

Amani, Utulivu na Usalama

"Rukuu na Sijida katika Swala ya Waislamu hushibisha nafsi amani, utulivu na usalama. Kila mmoja huanza Swala yake kwa Bismillahir Rahmanir Rahym na humalizia kwa Asalaam Alaykum."

Lauren Booth

Mwanaharakati wa haki za Binadamu wa Uingereza

NJIA YA UTUKUFU

Allah alipomuumba Adamu aliwaamrisha (malaika) kumsujudia:

{Na hakika tulikuumbeni, kisha tukakutieni sura, kisha tukawaambia Malaika: Msujudieni Adam. Basi wakasujudu isipo kuwa Iblisi, hakuwa miongoni mwa walio sujudu.} [7:11],

Allah alimuumba mwanadamu na kumkirimu na kumfadhilisha juu ya viumbe vingine toka mwanzo;

{Na hakika tumewatukuza wanaadamu, na tumewapa vya kupanda nchi kavu na baharini, na tumewaruzuku vitu vizuri vizuri, na tumewafadhilisha kwa fadhila kubwa kuliko wengi miongoni mwa tulio waumba.} [17:70],

Nae ni kiumbe aliyekirimiwa na kufadhilishwa tangu mwanzo kwa haya yafuatayo:-

1. Utukufu na ubora kwa kuumbwa kwake:

Allah amesema:

{Bila ya shaka tumemuumba mtu kwa umbo lilio bora kabisa.} [95:4],

Kwa hiyo Akamuumba katika umbile ambalo ni umbile bora zaidi, kwa upande wa usawa wa kiwiliwili na kushikamana kwake, na kwa upande wa jinsi alivyompa akili na kufikiri, na akatamka na kusikia, na kumjaalia katika umbo lililo bora na umbile bora.

2. Utukufu na kufadhilishwa katika kudhalilishiwa bara na bahari kwa ajili ya mwanadamu:

Na hili linaingia kudhalilishwa kwa anga, nalo hili ni katika yanayohakikisha utukufu uliotajwa hapo mwanzo; kwa kuwa yeye Aliyetukuka amedhalilisha kila kitu kwa mwanadamu, na akafanya vitu hivyo kuwa ni vyake maalumu, tofauti na viumbe vingine; na hili linatoa dalili kuwa mwanadamu

katika Ulimwengu huu ni kama vile Raisi mwenye kufuatwa au mfalme mwenye kutiiwa, na kila kisichokuwa hicho ni raia wake na mfuasi wake, Allah Ta'ala amesema:

{Na hakika tumewatukuza wanaadamu, na tumewapa vya kupanda nchi kavu na baharini…} [17:70],

Bali Allah Aliyetakasika amefahamisha aliyoyadhalilisha kwa mwanadamu yaliyomo mbinguni na ardhini vyote:

{Na amefanya vikutumikieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi, vyote vimetoka kwake. Hakika katika hayo zimo Ishara kwa watu wanao fikiri.} [45:13].

3. Riziki ya vitu Vizuri

Allah amemfundisha mwanadamu kula anavyovitamani katika alivyoruzukiwa, na akajaalia katika chakula dalili za manufaa, na akafanya vyakula anavyokula mwanadamu ni vingi sana kuliko wanavyokula wanyama wengine, ambao hawali isipokuwa walichozoea, kama alivyomkirimu kwa kumdhalilishia yote hayo kwa fadhila zake na ukarimu wake yeye Subhaanahu:

{(Mwenyezi Mungu) ambaye amekufanyieni hii ardhi kuwa kama tandiko, na mbingu kama paa, na akateremsha maji kutoka mbinguni, na kwayo akatoa matunda yawe riziki zenu. Basi msimfanyizie Mwenyezi Mungu washirika, na hali nyinyi mnajua.} [2:22].

4. Kufadhilisha kuliko viumbe wake wote Subhanahu wa Ta'ala aliyowaumba.

Hivyo basi mwanadamu katika njia hii anahisi utukufu, hadhi na umbo lake linalotokana na ukarimu wa Mwenyezi Mungu, hivyo basi mwanadamu hakuhesabika kuwa ni nukta ndogo tu katika Ulimwengu huu hai wa Mada… nukta ndogo isiyo na maana ukilinganisha na kiasi cha Mada ambayo ndio Ulimwengu mzima, ni nukta ndogo ambayo bomu moja tu la Nyuklia linaweza kufuta roho laki mbili kama ilivyotokea Hiroshima, ukubwa wa mwanadamu kwa mtazamo wa Uislamu unatokana na utukufu aliopewa na Allah ambaye ametayarishiwa mwanadamu tu, pale tunapoona katika maelezo ya Qur-aan kuhusu kuumbwa kwa mwanadamu

na wote Ulimwenguni kumsujudia Adam, kisha Allah akamfukuza Ibilisi, kwa sababu ya kukataa kumsujudia Adam na sisi tunajua ni kiasi gani msingi huu muhimu katika kujenga na kumjenga mwanadamu wa Ulimwengu huu. Ni muhimu katika muda ambao mwanadamu hawezi kumaliza matatizo yake, kiasi cha kuvamia matakwa yake na nguvu ya mtu, ila kwa njia hii. Njia ya Qur-aan ambayo inampa mwanadamu uhuru wake, utukufu wake na rangi (aina) za uchaguzi wake wote.

Katika njia ya utukufu, ukarimu haifai kumdhalilisha mwanadamu au kumdharau, Allah Ta'ala amesema:

{Enyi mlio amini! Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao, wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao. Huenda hao wakawa bora kuliko wao. Wala msivunjiane hishima, wala msiitane kwa majina ya kejeli. Ni uovu kutumia jina baya baada ya kwisha amini. Na wasio tubu, hao ndio wenye kudhulumu.} [49:11].

Hakuna ubora katika kutukuzwa mwanadamu mweupe juu ya mweusi, au mwekundu juu ya manjano, au Muarabu juu ya Muajemi, au kabila fulani juu ya jingine au sehemu fulani juu ya nyingine, au tajiri juu ya masikini ila kwa ucha-Mungu, Allah Ta'ala amesema:

{Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamngu zaidi katika nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye khabari.} [49:13],

Na Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) amesema: "Hakika Allah haangalii sura zenu wala mali zenu, lakini anangalia nyoyo zenu na matendo yenu" (Muslim).

Mwanadamu anapata utukufu na ukarimu kwa kadiri atakavyoshikamana na njia hii na kufuata:

{Mwenye kutaka utukufu basi utukufu wote uko kwa Mwenyezi Mungu….} [36:10]

Na atadhalilika kwa kadiri ya kuwa mbali na njia hii ambayo wanakusanyika viumbe wote kumtii Allah (Subhaanahu wa Ta'ala), Allah Ta'ala amesema:

{Je! Huoni kwamba vinamsujudia Mwenyezi Mungu viliomo mbinguni na viliomo katika ardhi, na jua, na mwezi, na nyota, na milima, na miti, na wanyama, na wengi miongoni mwa watu. Na wengi imewastahiki adhabu. Na anaye fedheheshwa na Mwenyezi Mungu hana wa kumhishimu. Hakika Mwenyezi Mungu hutenda apendayo.} [22:18].

Pamoja na kuwa Allah amemkirimu mwanadamu, isipokuwa watu wengi wamechagua njia ya udhalili.

{Atakayedhalilishwa na Mwenyezi Mungu hana wa kumtukuza}

Na wakachagua kumuangalia mwanadamu kuwa ni wanyama au vyombo au kiasi cha mali alichonacho au mfano wa hayo katika mtazamo ambao inapingana na mantiki ya Allah kumkirimu mwanadamu huyu

https://www.path-2-happiness.com/sw



na kumfadhilisha. Utukufu wa mwanadamu ni kwa kuwa kwake mwanadamu, kwa hiyo Uislamu hautengenezi mgongano kati ya jinsia mbili, na huo si wa mwanaume dhidi ya mwanamke, au mwanamke dhidi ya mwanaume, watu wameumbwa, kwa Nafsi moja, Allah Ta'ala amesema:

{Enyi watu! Mcheni Mola wenu Mlezi aliye kuumbeni kutokana na nafsi moja, na akamuumba mkewe kutoka nafsi ile ile. Na akaeneza kutokana na wawili hao wanaume na wanawake wengi. Na tahadharini na Mwenyezi Mungu ambaye kwaye mnaombana, na jamaa zenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwaangalieni.} [4:1],

Kwa hiyo Anayetaka ukarimu na utukufu basi na afuate njia ya karama na utukufu, Allah amesema:

{…Hakika utukufu wote ni wa Mwenyezi Mungu...} [10:65].

Kusingebakia Mwenye Njaa.

"Sijaona dini iliyoweka sheria timilifu kwa ajili ya Zaka kama Uislamu. Na Jamii ya Kiislamu inayopupia kutoa Zaka huepukana na ufukara, mtu kunyimwa mahitaji yake na watu kukimbia. Mimi ninasawirisha lau Ulimwengu wote huu ungeelekea kwenye Uislamu basi kusingebakia katika mgongo wa ardhi mwenye njaa yoyote mwenye kunyimwa."

Berisha Pennekmrt

Mtaalamu wa Elimu Thailand aliyeingia Uislamu.

الطريق إلى السعادة
The Path to Happiness



HITIMISHO: NJIA YA FURAHA

Yaliyomo

HITIMISHO: NJIA YA FURAHA

Ewe Mwenye kutafuta furaha!

Hii ndio Njia

HITIMISHO: NJIA YA FURAHA

EWE MWENYE KUTAFUTA FURAHA!!

Kabla ya kuja kwako katika Ulimwengu huu ulikuwa haupo kama Allah alivyosema: {Je! Hakumbuki mwanaadamu ya kwamba tulimuumba kabla, na hali hakuwa chochote?} [19:67],

Kisha Allah akakuumba kwa udongo, kisha kwa tone la manii, kisha akakufanya msikivu na mwenye kuona, Allah Ta'ala amesema: {Hakika kilimpitia binaadamu kipindi katika zama ambacho kwamba hakuwa kitu kinacho tajwa. Hakika Sisi tumemuumba mtu kutokana na mbegu ya uhai iliyo changanyika, tumfanyie mtihani. Kwa hivyo tukamfanya mwenye kusikia, mwenye kuona.} [76:1-2].

Kisha ukatoka kwenye udhaifu hadi kwenye nguvu na kurudi tena kwenye udhaifu, Allah Ta'ala amesema: {Mwenyezi Mungu ndiye aliye kuumbeni kutokana na udhaifu kisha akajaalia nguvu baada ya unyonge, kisha akajaalia baada ya nguvu unyonge tena na ukongwe. Anaumba atakavyo. Naye ndiye Mjuzi, Mwenye uweza.} [30:54],

Kisha mwisho ambao hauna shaka yoyote ndani yake ni mauti.

Na wewe katika hatua hizo unahama kutoka kwenye udhaifu mmoja kwenda kwenye udhaifu mwingine huwezi kuondosha dhara katika nafsi yako, wala huwezi kujiletea manufaa ila kwa kuomba msaada wa Allah kwako, nawe ukiwa ni fukara mwenye kuhitaji kulingana na maumbile uliyoumbwa nayo, ni vingapi unavyohitaji ili maisha yako yabakie, ambayo huna uwezo nayo, wakati mwingine ukapata na wakati mwingine ukakosa, na mangapi ambayo yanakufaa na unayatamani, unaweza



kupata na wakati mwingine kukosa, na mangapi yenye kukudhuru na kuondosha matarajio yako na juhudi zako zikapotea na kukuletea mitihani na balaa na ukataka kuyaondoa katika nafsi yako hivyo ukayaondoa mara moja na kushindwa wakati mwingine. Je, hukuwahi kushitakia ufakiri na haja yako kwa Allah?, Na Allah anasema: {Enyi watu! Nyinyi ndio wenye haja kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kujitosha, Msifiwa.} [35:15].

Kirusi kidogo usichoweza kukiona kwa macho kinakusumbua na kukufanya mgonjwa usiyeweza kusimama, na huwezi kukizuia, na unakwenda kwa mtu dhaifu kama wewe ili akutibu, wakati mwingine hukupa dawa iliyokuwa sawa, na wakati mwingine hushindwa, na wote, mgonjwa na daktari msijue la kufanya…. Ni udhaifu ulioje kwako wewe Ewe mwanadamu!! Lau nzi akikunyang'anya kitu huwezi kukirudisha!! Amesema kweli Allah pole aliposema: {Enyi watu! Unapigwa mfano, basi usikilizeni. Hakika wale mnao waomba badala ya Mwenyezi Mungu, hawatoumba hata nzi ijapo kuwa watajumuika kwa hilo. Na nzi akiwapokonya kitu hawawezi kukipata kwake. Amedhoofika kweli huyo mwenye kutaka na mwenye kutakiwa.} [22:73].

Ikiwa huwezi kuokoa alichokunyang'anya nzi, Je, unamiliki nini katika jambo lako?! Utosi wako uko mkononi kwa Allah, nafsi yako ipo mkononi mwa Allah, moyo wako upo baina ya vidole vyake viwili katika vidole vya Rahman anavigeuza atakavyo, na maisha yako na mauti yako viko mikononi mwake, furaha yako na tabu yako vipo mkononi mwake. Harakati zako, utulivu wako, na kauli zako kwa idhini ya Allah, na matakwa yake, hivyo huwezi kutembea ila kwa idhini yake, wala hutofanya ila kwa matakwa yake, akikuwakilisha katika nafsi

yako basi atakuwa amekuwakilisha katika unyonge, udhaifu, kupetuka mipaka, madhambi na hatia, na akikuwakilisha kwa mwingine, atakuwa amekuwakilisha kwa asiyemiliki kwako madhara wala manufaa wala mauti wala uhai wala kufufuliwa, hujitosha dhidi yake, japo kwa pepeso la jicho, bali wewe unalazimika kwake kwa pumzi yako yote ndani na nje, anakuenezea, neema na wewe unambughudhi kwa maasi na kufuru pamoja na dharura yako kubwa kwake kwa njia zote, umechukua kuwa ndio hisa na marejeo yako kwako na msimamo wako mbele yake.

Ewe mwanadamu kutokana na udhaifu na unyonge wako katika kuvumilia matatizo ya madhambi yako:

{Mwenyezi Mungu anataka kukupunguzieni taabu, na mwanaadamu ameumbwa dhaifu.} [4:28].

Allah alituma Mitume na kuteremsha vitabu, na kuweka sheria na kusimamisha mbele yako Njia ilionyooka na kusimamisha hoja, ubainifu na ushahidi na mpaka amekufanyia katika kila kitu alama yenye kuthibitisha upekee wake (kuwa Yeye Mungu ni mmoja), Uungu wake na Uola wake, pamoja na yote hayo bado utawaona baadhi ya watu wakitetea batili na kupinga haki na wakimchukua shetani kuwa ni walii kwao badala ya Allah na kujadili kuhusu batili:

{Na bila ya shaka tumewaelezea watu katika hii Qur'ani kila namna ya mfano. Lakini mwanaadamu amezidi kuliko kila kitu kwa ubishi.} [18:54].

Je, neema za Allah ambazo zinageuka ndani yake zimekuliwaza mwanzo na mwisho wako?? Au hukumbuki kuwa umeumbwa kwa tone la manii? Na mwisho wako ni kwenye shimo, na utafufuliwa peponi au motoni! Allah Ta'ala amesema: {Kwani mwanaadamu haoni ya kwamba Sisi tumemuumba yeye kutokana na tone la manii? Kisha sasa yeye ndio amekuwa ndiye mgomvi wa dhaahiri! Na akatupigia mfano, na akasahau kuumbwa kwake, akasema: Ni nani huyo atakaye ihuisha mifupa nayo imekwisha mung'unyika? Sema: Ataihuisha huyo huyo aliye iumba hapo mara ya mwanzo. Na Yeye ni Mjuzi wa kila kuumba.} [36-77-79]

Na amesema vile vile: {Ewe mwanaadamu! Nini kilicho kughuri ukamwacha Mola wako Mlezi Mtukufu? Aliye kuumba, akakuweka sawa, akakunyoosha} [82:6-7]

Ewe mwanadamu kwa nini unajiharamishia Nafsi yako ladha ya Tawhidi na kumuadhimisha Allah Ta'ala, ladha ya kusimama mbele ya Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) na kutaka msaada wake akuepushe naufakiri na akuponyeshe maradhi na kuondosha matatizo yako na kusamehe madhambi yako na kuondosha madhara na kukunusuru unapodhulumiwa na kukuongoza unapobabaika na kupoteza, nakukufundisha usiyoyajua na kukupa amani utakapoingiwa na khofu na kukuhurumia wakati wa unyonge wako na kuwarudisha adui zako na kukupa riziki yako?!

Ewe mwanadamu kwa hakika neema kubwa ambayo Allah amemneemesha kwayo mwanadamu baada ya neema ya dini ni neema ya akili, ili mwanadamu aweze kupambanua baina ya yenye kumnufaisha na yenye kumdhuru na aweze kuifahamu maamrisho ya Allah na makatazo yake na aweze kujua lengo tukufu zaidi nalo ni uja wake kwa Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) peke yake bila ya mshirika, Allah Ta'ala amesema:

{Na neema yoyote mliyo nayo inatoka kwa Mwenyezi Mungu. Kisha yakikuguseni madhara mnamyayatikia Yeye. Na anapo kuondosheeni madhara mara kundi moja miongoni mwenu linamshirikisha Mola wao Mlezi} [16:53-54].

Ewe mwanadamu, kwa hakika mwanadamu mwenye akili hupenda mambo makubwa na kuchukia mambo ya hovyo, na kupenda kumwiga kila mwema na watukufu miongoni mwa manabii na waja wema, na kila mmoja hutamani awafikie pamoja na kuwa hawakuwadiriki, na njia ya kuelekea huko ni ile

https://www.path-2-happiness.com/sw

aliyoielekeza Subhaanahu kwa kauli yake: {Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakufutieni madhambi yenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kufuta madhambi na Mwenye kurehemu.} [3:31]

Na akijifananisha nayo basi Allah humfikisha kwa manabii na waliotumwa, Allah Ta'ala amesema:{Na wenye kumt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume, hao wa pamoja na wale alio waneemesha Mwenyezi Mungu miongoni mwa Manabii, na Masiddiqi, na Mashahidi, na Watu wema. Na uzuri ulioje kuwa pamoja na watu hao!} [4:69].

Ewe mwanadamu na kuaidhi kujitenga kisha zingatia na uwe katika tafakuri kwa yaliyokujia katika haki, angalia dalili zake na zingatia hoja zake; ukiona kuwa ni haki basi jikusanye katika kufuata, wala usiwe mtumwa wa desturi na mazoea, najua kwamba kuwa Nafsi yako ni utukufu kwako kuliko rafiki zako, ndugu zako, mali zako na mirathi ya babu zako, na Allah Akawawaidhi Makafiri kwa hili na akawatamanisha nayo akasema Aliyetukuka: {Sema: Mimi nakunasihini kwa jambo moja tu - ya kwamba msimame kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, wawili-wawili na mmoja-mmoja; kisha mfikiri. Mwenzenu huyu hana wazimu. Yeye si chochote ila ni Mwonyaji kwenu kabla ya kufika adhabu kali.} [36:46].

https://www.path-2-happiness.com/sw

Ewe mwanadamu utakapojisalimisha hatopoteza chochote, Allah Ta'ala amesema: {Na ingeli wadhuru nini wao lau wangeli muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na wakatoa katika aliyo waruzuku Mwenyezi Mungu? Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwajua vyema.} [4:39],

Yaani, kitawadhuru nini lau wakimuamini Allah na yote aliyoteremsha? Kitawadhuru nini lau wakimuamini Allah na wakitaraji ahadi yake nyumba ya akhera kwa yule atakayefanya kazi yake vizuri?! Kitawadhuru nini lau wakitoa yale ambayo Allah amewaruzuku katika wajihi ambao Allah atapenda na kuridhia, nae akiwa anajua nia zao njema na zilizo chafu, na ni mwenye kujua kwa anayestahiki kuwafikishwa miongoni mwao. Hivyo kumuwafikisha na kumpa uongofu wake, na kumuelekeza matendo mema ambayo atamridhia kwayo, na mwenye kustahiki udhalili, kufukuzwa kutoka kwenye uwanja wake mtukufu wa kiungu ambae atakayefukuzwa mlangoni mwake amepata hasara na kukosa dunia na akhera?!

Uislamu wako haukuzuii baina yako na chochote kila unachotaka kufanya au kupata katika yale aliyokuhalalishia Allah, bali Allah atakulipa kwa kila amali mfanyayo ambayo unataka kwayo wajihi wa Allah, hata ikiwa ni katika yanayotengeneza dunia yako na kukuzidishia mali yako au cheo chako au utukufu wako, bali hata unachokitumia katika yaliyoruhusiwa ikiwa

Ananijua Kuliko Ninavyoijua Nafsi Yangu

"Qur-aan, kitabu hiki kitukufu kimeniteka kwa nguvu na kumiliki moyo wangu na kunifanya nijisalimishe kwa Allah, na Qur-aan humsukuma msomaji wake kwenye upeo wa mbali ambapo humtanguliza (kujiona) anasimama peke yake mbele ya Muumba wake. Ukiichukulia Qur-aan kwa umakini zaidi basi huwezi kusoma kwa urahisi, kwani hukubeba kama kwamba ina haki juu yako! Nayo inajadiliana nawe, kukukosoa na kushindana nawe. Nilikuwa katika kipande cha mwisho ikadhihirika wazi kuwa aliyeshusha Qur-aan ananijua kuliko ninavyojijua mwenyewe. Kwa hakika Qur-aan siku zote inanitangulia katika kufikiri kwangu, ilikuwa inajibu maswali yangu na kila usiku nilikuwa ninaweka maswali yangu na pingamizi zangu, hata hivyo nilikuwa napata majibu siku inayofuatia. Nimekabiliana na nafsi yangu uso kwa uso katika kurasa za Qur-aan."

Jeffrey Lang
Mwanazuoni wa Hesabu Marekani.

utatosheka na ya halali na kuacha ya haramu.

Ewe mwanadamu hakika Mitume wamekuja kwa haki, na wametimiza matakwa ya Allah, na mwanadamu ni mwenye kuhitajia maarifa ya sheria ya Allah, ili apite katika maisha haya kwa uoni na awe katika akhera miongoni mwa washindi, Allah Aliyetukuka amesema: {Enyi Watu! Amekwisha kujieni Mtume huyu na haki itokayo kwa Mola wenu Mlezi. Basi aminini, ndiyo kheri yenu. Na mkikanusha basi hakika viliomo mbinguni na duniani ni vya Mwenyezi Mungu tu. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye hikima.} [4:170],

Na akasema tena Aliyetukuka: {Sema: Enyi watu! Haki imekwisha kukujieni kutoka kwa Mola wenu Mlezi. Basi anaye ongoka anaongoka kwa faida ya nafsi yake, na anaye potea anapotea kwa khasara ya nafsi yake. Na mimi si mwakilishi juu yenu.}[10-:108].

Ewe mwanadamu hakika wewe ukisilimu hutonufaisha isipokuwa Nafsi yako tu, na ukikufuru hutoidhuru isipokuwa nafsi yako tu, hakika Allah ni mkwasi wa waja wake, hivyo basi haimdhuru yeye maasi ya wenye kuasi, hivyo Yeye haasiwi isipokuwa kwa elimu yake, na hatiiwi ila kwa idhini yake, Allah Aliyetukuka amesema:

{Zimekwisha kukujieni hoja wazi kutoka kwa Mola wenu Mlezi. Basi anaye ona ni kwa faida yake mwenyewe, na anaye pofuka basi ni khasara yake. Nami si mtunzaji wenu.} [6:104],

Na Allah alishaeleza kama ambavyo Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) alivyojulisha:

«Enyi waja wangu hakika mimi nimejiharamishia dhuluma na nikajaalia baina yenu haramu, hivyo basi msidhulumiane. Enyi waja wangu nyote mmepotea ila yule niliyemuongoza ombeni uongofu wangu nitawaongoa. Enyi waja wangu nyote ni wenye njaa ila niliyemlisha, ombeni niwalishe nitawalisha. Enyi waja wangu nyote mko uchi ila niliyemvisha, ombeni kuvishwa nami nitawavisha.

https://www.path-2-happiness.com/sw

Enyi waja wangu, nyote mnakosea usiku na mchana, nami ninasamehe dhambi zote, niombeni msamaha nitawasameheni.

Enyi waja wangu, nyie hamuwezi kunifikia mkanidhuru, wala hamuwezi kunifikia mkaninufaisha.

Enyi waja wangu lau wa kwanza wenu na wa mwisho wenu, na watu wenu na majini yenu walikuwa katika moyo wa mcha-Mungu mmoja miongoni mwenu, hilo halinipunguzii kitu katika ufalme wangu.

Enyi waja wangu lau wa kwanza wenu na wa mwisho wenu, na watu wenu na majini yenu walikuwa katika moyo wa mcha-Mungu mmoja miongoni mwenu, hilo halinipunguzii kitu katika ufalme wangu.

Enyi waja wangu lau wa mwanzo wenu na wa mwisho wenu na watu wenu na majini yenu wamesimama katika wanga mmoja na wakaniomba na mimi nikampa kila mtu kwa mujibu alivyoomba, hilo halitonipunguzia chochote isipokuwa kama inavyopungua makamasi yanapoingia baharini.

Kina katika Ustaarabu wa Magharibi

Mwanadamu ambae ameingia ndani ya ustaarabu wa Kimagharibi na akadiriki undani wake na akaupima kwa kina kinadharia na kivitendo hana budi kufuata kwa nguvu ndani ya nafsi kwenye imani ya Kiislamu ili akate kiu yake."

Naseem Souza

Mhadhiri wa Kiyahudi huko Iraqi.

Enyi waja wangu, kwa hakika hayo ni matendo yenu ninawahesabia, kisha ninawalipa kwayo, atakayepata kheri basi namshukuru Allah, na atakayepata yasiyokuwa hayo basi asilaumu isipokuwa Nafsi yake.» (Muslim).

Enyi wanadamu… Hii ndio njia, wala hakuna njia isiyokuwa hiyo kwa ajili ya furaha duniani na akhera.

Ama njia zingine ni njia za tabu, upotovu na mashaka, Allah Aliyetukuka amesema: {Na kwa hakika hii ndiyo Njia yangu Iliyo Nyooka. Basi ifuateni, wala msifuate njia nyingine, zikakutengeni na Njia yake. Haya amekuusieni ili mpate kuchamngu.} [6:153]

Atakayefuata njia ya furaha ataifikia, na atakayefuata njia zingine atapotea na kuwa mbali na njia ya Allah, wala hatopita njia ya furaha.

Misingi ya Amani na Furaha

"Ulaya hivi sasa imeanza kuhisi hekima ya Muhammad na imeanza kutamani dini yake, kama ambavyo itikadi ya Kiislamu itasafishika na tuhuma chafu za karne ya kati kutoka kwa watu wa Ulaya. Dini ya Muhammad itakuwa ndio mfumo ambao juu yake kuna misingi ya amani na furaha, na falsafa yake inategemea katika kutatua matatizo na vifungo."

Sir George Bernard Shaw

Mwandishi wa Uingereza



HII NDIO NJIA

Kila mwenye akili linganifu anaijua njia hii hata kama ataipinga hadharani, hujua kuwa njia hii ndio njia ya furaha ya milele, yeye ni kama waliosemwa na Allah baada ya kukana utume wa Musa ('Alayhi Salaam) baada yakuwajia miujiza: {Na wakazikataa kwa dhulma na kujivuna, na hali ya kuwa nafsi zao zina yakini nazo. Basi angalia ulikuwaje mwisho wa mafisadi!} [27:14].

Wengi wanaotumia akili zao vizuri (hata kama hawajasilimu) hujua kuwa njia hii ni njia pekee ya furaha ya wanadamu wote katika nyumba zote mbili (duniani na akhera).

Hii ndio njia.... huikiri njia hii kila aliyekuwa huru, shujaa katika kubainisha rai yake pamoja na dhiki aliyokuwa nayo na kificho, khofu haimzuii au kuwaogopea watu au kuogopea jambo jipya, au propaganda na sura ya siku nyingi iliyokwisha jijenga akilini mwake kuhusu kuipokea na kuikubali dini hii na kusilimu, wangapi katika watu waliojizuia kufuata njia hii kwa kuhofia udugu na maingiliano yao ya kijamii na hofu yao katika kushikamana na njia ya furaha, Allah Aliyetukuka amesema: {...basi msiwaogope, bali niogopeni Mimi mkiwa nyinyi ni Waumini.} [3:175].

Hii ndio njia.. Naam ndio njia ya furaha, njia ya mambo matukufu, njia ya huruma na rehema, njia ya elimu, njia ya ustaarabu, njia ya tabia njema pamoja na mitihani ambayo ni sunnah ya maisha na kumjua mkweli miongoni mwa

waongo. Allah Ta'ala amesema: {Ambaye ameumba mauti na uhai ili kukujaribuni ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi. Na Yeye ni Mwenye nguvu na Mwenye msamaha.} [67:2].

Hii ndio njia waliyopita manabii na waliotumwa kabla yetu, na njia waliopita masahaba watukufu na waliofuata baada yao kwa wema katika kila kaumu, kabila na lugha, na ndio ambao itaenea kwa wote na kuongoza katika mustakbali hivi karibuni.

Anasema Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam):"Jambo hili (Uislamu) litafika ilipofika usiku na mchana, wala Allah hatoacha nyumba yoyote ila Mwenyezi Mungu ataingiza dini hii kwa utukufu wa mtukufu, au kwa udhalili wa mnyonge, ni utukufu ambao Allah anaupa nao nguvu Uislamu, na udhalili ambao Allah anawadhalilisha nao ukafiri." (Imepokewa na Ahmad).

Kuwa miongoni pamoja na msafara mtukufu katika njia hii ya furaha ya milele.

Hii ndio njia…huku ndiko kufaulu..na hii ndio furaha..ambayo inajaza moyo wa atakayepita ndani yake, usiinyime nafsi yako (fursa hii), Jihadhari, Ole wako na kudhulumu Nafsi yako, fuata njia ya furaha, Allah Aliyetukuka amesema: {Mwenye kutenda mema, mwanamume au mwanamke, naye akawa ni Muumini, tutamhuisha maisha mema; na tutawapa ujira wao kwa bora ya waliyo kuwa wakiyatenda.} [16:97].

Unateka Mioyo

"Baada ya kusoma dini mbali mbali ulimwenguni nimefikia kwenye matokeo kuwa Uislamu ndio dini pekee inayowaathiri wale ambao wameiamini. Hata wale ambao hawaiamini kwa usawa vile vile. Kitu kikubwa katika Uislamu ni kuwa kinateka nyoyo za watu kwa sura ambayo mtu hawezi kutambua. Kwa ajili hiyo tunaona katika Uislamu mvuto wa ajabu na msukumo mkubwa ambao unawavuta wenye akili zilizofunguka miongoni mwa wasio Waislamu."

Mary Oliver
Mshairi wa Kimarekani

Wahi Pamoja na Wasafiri

"Kuenea kwa Uislamu ni alama miongoni mwa alama zake kwenye mapito ya historia: Na hilo ni sababu hiyo ni dini ya maumbile iliyoshushwa katika moyo wa aliyechaguliwa (Mustafa)."

Dr.Murad Hoffman
Balozi wa Ujerumani.

Mradi wa Milele

"Uislamu ni maisha mbadala wa mradi wa milele usiooza (wala usioisha ubora wake). Na wanapouona baadhi ya watu kuwa ni wa zamani, basi huo ni wa sasa na vile vile wa baadae, hautenganishwi kwa nyakati wala mahali. Uislamu sio wimbi la fikra tu wala staili mpya ya mambo inayofaa kusubiri. Haiko mbali Mashariki kurudisha uongozi wa Ulimwengu kwa ustaarabu, bado ule msemo: "Mwanga utatoka Mashariki" ni msemo sahihi kabisa."

Dr.Murad Hoffman.
Balozi wa Ujerumani

Kuijaza Roho Tupu

"Katika kipindi fulani cha maisha yangu, Mwenyezi Mungu amenipa elimu kubwa na rehema nyingi baada ya adhabu na maumivu yaliyonipata baada ya kuwepo na matayarisho makubwa kwangu na kujaza roho tupu ndani ya nafsi yangu. Hivyo nikasilimu, na kabla ya kuwa Muislamu sikuwa ninajua ndani ya maisha yangu maana ya mapenzi lakini mimi baada ya kusoma Qur-aan nilihisi rehema nyingi pana na mapenzi yakinifunika. Nikaanza kuhisi mapenzi yaliyodumu ndani ya moyo wangu. Kilichoniongoza kwenye Uislamu ni mapenzi ya Mungu ambayo hayazuiwi."

Jeffrey Lang
Mwanazuoni wa Hesabu wa Marekani

Hii ndio njia…jilazimishe nayo, na uifurahie, na ishi maisha yako ya duniani kwa furaha iliojaa, utulivu, na raha, wala usisahau kuwa yaliyo kwa Allah ni bora na yenye kubakia, na raha ya akhera ni raha ya milele, Mola wetu ameifanya njia hiyo kuwa moja tu; furaha ya dunia na furaha ya akhera, na amekusanya katika njia (zingine) uovu wa dunia na adhabu ya akhera, Allah Aliyetukuka amesema: {Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu. Aseme: Ewe Mola wangu Mlezi! Mbona umenifufua kipofu, nami nilikuwa nikiona?} [20:124-125],

Na akasema vile vile: {(Mwenyezi Mungu) atasema: Ndivyo vivyo hivyo. Zilikufikia ishara zetu, nawe ukazisahau; na kadhaalika leo unasahauliwa.} [20:126],

Jihadhari kusahau au kujisahaulisha njia hii..nayo ni njia ya furaha.

Hii ndio njia … ni njia nyepesi inaanza kwa tawhidi ya Allah katika moyo na kusadikisha katika kiwiliwili, na imani kwa manabii na walioteremshwa na kuishia katika furaha ya milele katika akhera, ambayo inaanza kwa kutamka shahada mbili; nazo ni: Ash-hadu an-Laailaha Illa llaah wa-anna Muhammadan Rasuulu llaah..na

uishi maisha yake ukiwa na furaha, na ufe ukiwa na furaha, na uamke kutoka kaburini mwako ukiwa na furaha katika pepo ya milele yenye furaha…hii ndio njia…usipopita njia hii basi Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) hana wajibu juu yake isipokuwa kufikisha waziwazi, Amesema Allah (Subhaanahu wa Ta’ala): {Ilipo fika amri yetu, tulimwokoa Hud na walio amini pamoja naye, kwa rehema itokayo kwetu. Na tukawaokoa na adhabu ngumu.} [11:58].

La Ilaha Illallah Muhammad Rasulullah

“Utakapomjua Allah na kuamini uwepo wake: Hapo Uislamu utakuambia: “Hakika Allah yupo karibu yako zaidi kuliko mshipa wa koo. Hivyo basi hakuna haja ya kiunganishi baina yako na Muumba wako. Wala hapana haja ya kuwepo kuhani ambae utakiri makosa yako kwa hivyo atakubali toba yako au hekalu ambalo ibada haitotimia isipokuwa ndani yake tu.”

Donald Rickwell

Mshairi wa Kimarekani.

الطريق إلى السعادة
The Path to Happiness

Faharasi

Utangulizi **4**

NJIA IKO WAPI?! **6**
Watu wote wanatafuta furaha, njia iko wapi?! 8
Je, ni Njia ya Kumkana Mungu au Njia ya Dini? 9
KUNA MASWALI AMBAYO BADO YANAHITAJI MAJIBU 13
MAJIBU YAWE VIPI?! 14
DALILI NI ZIPI? 16
DALILI ZA UUNGU WA ALLAH TA'ALA 20

Kuumbwa kwa Ulimwengu na Mwanadamu... Hekima, Kukirimiwa na Lengo **30**
Je, umewahi kufikiria Umbile la Ulimwengu?! 32
Hekima ya kuumbwa kwa ulimwengu 35
Kuumbwa na kukirimiwa kwa mwanadamu 39
Mwanamke kukirimiwa sawa na mwanamume 46
HEKIMA YA KUUMBWA KWA MWANADAMU 52
BAADA YA HAPO EWE MWANADAMU... 55

JE, MWANADAMU ANA HAJA YA DINI? **58**
Je, ni lazima kuwa na Dini? 60
Haja ya dini kwa jamii mbali mbali 67
Vidhibiti vya dini ya haki 69
Ni dini ipi tunayohitajia? 79

MITUME NA MANABII **84**
JE, WATU WANA HAJA NA MITUME? 86
UKWELI WA UTUME NA UJUMBE WAKE 89
DALILI ZA UTUME 91
MISINGI YA DA'WAH YA MITUME 99
HISTORIA YA ULUL-'AZM 103
NI IPI HISTORIA YA MANABII NA MITUME 107
AMBAYO NDIO HISTORIA YA WANADAMU? 107
1. NUUH ('Alayhi salaam) 108
2. IBRAHIM ('Alayhi salaam) 115
3. MUSA ('Alahyi Salaam) 121
4. ISSA BIN MARYAM ('Alayhi salaam). 137
5. MUHAMMAD (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) 145

UJUMBE UNAOBAKIA **154**
UJUMBE UNAOBAKIA 156
MIONGONI MWA DALILI ZA UTUME WAKE (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) 161
UTUME WA MWISHO 171
REHEMA KWA WALIMWENGU 175
FURAHA YA MWANADAMU KWA KUTUMWA KWAKE (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) 178
NI UPI UJUMBE ULIOBAKIA? 184
UJUMBE ULIOBAKIA NDILO UMBILE LA ULIMWENGU 185
UJUMBE ULIOBAKIA NI DINI YA MANABII NA MITUME WOTE: 189
UKAMILIFU WA UJUMBE ULIOBAKIA: 193
MISINGI YA UWEKAJI SHERIA 197
SIFA ZA UWEKAJI SHARIA WA KIISLAMU: 202
SHERIA YA KIISLAMU NA KANUNI ZA WANADAMU…TOFAUTI ZILIZOPO: 207
VYANZO VYA UISLAMU. 210

NJIA YA FURAHA **218**
MAANA YA FURAHA NA HAKIKA ZAKE 220
FURAHA SIO LADHA (STAREHE): 223
HAPANA.. FURAHA HAIPO KWENYE RAHA!! 225
NJIA YA FURAHA..UZURI WA MWANADAMU NA NAFSI YAKE PAMOJA NA MAISHA NA ULIMWENGU: 237
ALAMA ZA NJIA YA FURAHA: 239
SABABU ZA FURAHA DUNIANI KATIKA UISLAMU 244
Huzuni ya kuwa mbali na Njia ya Furaha: 256

NJIA YA ELIMU NA USTAARABU **262**
UISLAMU NA ELIMU 264
NJIA YA USTAARABU 272
VILINZI VYA NJIA YA FURAHA 274
MIUJIZA KATIKA QUR-AAN NA SUNNAH 294

NJIA YA MAADILI **298**
NJIA YA MAADILI 300
UHUSIANO WA IMANI NA TABIA NJEMA 302
IBADA NA TABIA NJEMA 303
AKHLAKI KATIKA UISLAMU 306

NJIA YA REHEMA NA UTUKUFU **320**
NJIA YA REHEMA: 322
NJIA YA UTUKUFU 327

HITIMISHO: NJIA YA FURAHA **332**
EWE MWENYE KUTAFUTA FURAHA!! 334
HII NDIO NJIA 342

Faharasi **346**

https://www.path-2-happiness.com/sw

Ni nani miongoni mwetu hatafuti furaha.? Hapana shaka kuwa kila mwanadamu anahaha kuitafuta, lakini ni wangapi katika sisi wanaofanikiwa katika kufikia hii furaha? Si hivyo bali ni wangapi miongoni mwetu ambao wanajua njia ya kuifikia? Bila shaka sababu za furaha ni nyingi, lakini kwa mtazamo wangu ni kuwa la muhimu zaidi katika sababu hizi ni mtu kuhakiki dhati yake, na mtu hawezi kuhakiki dhati yake ila kwa kuhakiki utu wake kwanza. Utu wake ambao unamtofautisha mtu na mnyama na viumbe wengine. Ama kwa hakika tafakuri kwa maswali makubwa kuhusu ulimwengu, mwanadamu na maisha, na kufikia kwenye majibu sahihi ya maswali haya humfikisha mwanadamu katika utulivu, bali kuridhika na furaha. Majadiliano haya huchangia katika kuweka miguu yetu katika njia ya mwanzo ya furaha, kwa kuondosha dhana na kufikia kwenye hakika, na kumfikisha mtu kwenye majibu kuhusu maswali yenye kushughulisha fikra za wengi wetu, ambapo maudhui mengi yamewekwa kuhusiana na pande za utu wa mwanadamu, ambayo yamewekwa katika hali ya mvuto wenye kunasibiana na wasomaji wengi.

Tovuti rafiki

Imam Academy

AIA
African Islamic Academy

AIA
African Islamic Academy

Ibn Kathir International University
of Humanities and Islamic Sciences

[redacted].